# FAHAMU ZA KISIASA
# ZA
# HIZB-UT-TAHRIR

**CHAPA YA UHARIRI**
**1444H-2023M**

# UTANGULIZI

Siasa ni kusimamia mambo ya Ummah kindani na kinje, na hutekelezwa na serikali na Ummah, hivyo basi serikali ndio inayotekeleza usimamizi huu kivitendo, na Ummah ndio ambao huihesabu serikali kwayo.

Usimamizi wa mambo ya Ummah kindani na kinje kwa upande wa serikali, huwa ni kwa kuutekeleza mfumo ndani, na hii ndio sera ya kindani.

Ama usimamizi wa mambo ya Ummah kinje kwa upande wa serikali huwa ni mahusiano yake na serikali na mataifa na watu wengine, na kueneza mfumo ulimwenguni. Na hii ndio sera ya kigeni.

Na kufahamu sera/siasa ya kigeni ni jambo la kimsingi ili kuhifadhi muundo wa serikali na Ummah, na suala msingi ili kuwezesha kubeba ujumbe katika ulimwengu, na ni kitendo kisichokuwa na budi ili kuyapangilia mahusiano ya Ummah na Ummah nyenginezo kwa namna sahihi.

Na kwa kuwa Ummah wa Kiislamu umekalifishwa kuupeleka ujumbe wa Kiislamu kwa watu wote, basi imekuwa ni lazima kwa Waislamu wawasiliane na ulimwengu kwa kuelewa hali zake, na kujua matatizo yake, na kujua misukumo ya serikali zake na watu wake, na wawe wenye kufuatilizia matendo ya kisiasa yanayoendelea ulimwenguni, na wawe wenye kudadisi mikakati ya kisiasa za serikali katika mbinu ya utekelezaji wake, na namna serikali zinavyohusiana, na mashindano ya kisiasa yanayofanywa na nchi. Hivyo basi imekuwa ni lazima juu ya Waislamu kutambua msimamo wa kihakika katika ulimwengu wa Kiislamu kwa kufahamu msimamo wa kimataifa wa kiulimwengu, ili nao waweze wafahamu mbinu ya kufanya kazi ili kuisimamisha serikali yao na kueneza ujumbe wao katika ulimwengu.

Lakini yatakiwa iwe wazi kuwa, misimamo ya nchi huwa haibakii katika hali moja, kwani hubadilika kutokana na mabadiliko ya hali za kimataifa.

Na hakika msimamo wa kila taifa huwa haijilazimishi na hali moja tu kiupande wa kimataifa, bali huingiwa na mabadiliko ya hali tofauti tofauti kama nguvu na udhaifu, na katika upande wa kuwa na kuathiri sana au kutoathiri, na kwa upande wa utofauti wa mahusiano yaliyopo kati yake na nchi nyenginezo, na kutafautiana kwa mahusiano hayo. Hivyo basi haiwezekani kuweka michoro mipana ya kudumu kuhusu msimamo wa kimataifa, wala kupeana fikra ya kudumu kuhusiana na msimamo wa nchi yoyote duniani. bali kinachowezekana ni kutoa tu mchoro mpana kuhusu msimamo wa kimataifa katika wakati fulani, pamoja na kutia maanani uwezekano wa kubadilika kwa msimamo huo. Na pia yawezekana kupeana fikra maalumu kuhusu msimamo wa nchi fulani, katika dhurufu fulani, pamoja na kuelewa kuwa kuna uwezekano wa msimamo huo kubadilika. Hivyo basi mwanasiasa hana budi kufuatilizia matendo ya kisiasa yaliyo ulimwenguni, na kuyaunganisha na maalumati yake ya kisiasa yaliyotangulia, ili aweze kufahamu siasa ufahamu wa sawa, na ili pia aweze kujua msimamo wa kila nchi, na kutambua ikiwa huu msimamo umebakia vilevile ulivyokuwa, au umebadilika.

Mabadiliko ya msimamo wa kimataifa hufuata mabadiliko ya msimamo wa baadhi ya mataifa kutoka hali moja hadi hali nyengine, ima kwa nguvu zake, au ima kwa udhaifu wake, na ima kwa nguvu za mahusiano yake na mataifa mengine, au kwa udhaifu wa mahusiano hayo, basi wakati huo hutapatikana mabadiliko katika mizani ya kiulimwengu, kwa sababu ya kupatikana mabadiliko katika mizani ya nguvu zilizo ulimwenguni. Kwa hivyo basi, msingi wa kufahamu msimamo wa kiulimwengu ni kufahamu msimamo wa kila nchi miongoni mwa nchi zenye kuathiri katika msimamo wa kimataifa. Kwa hivyo, umuhimu unaelekezwa katika kuwa na maalumati kamili kuhusu kila nchi, kwa sababu hiyo ndio nguzo ya kwanza ya ufahamu wa kisiasa. Na kujua msimamo wa kila nchi, hakuna mahusiano na nafasi ya nchi hiyo katika msimamo wa kimataifa, bali kujua huko kunahusiana na kila kitu kilicho na mahusiano na sera zake za kindani na za kigeni. Hivyo basi ni lazima

kujua fikra ambayo juu yake zimesimama siasa za mataifa yaliyo katika ulimwengu, na ambayo yana umuhimu wa maana katika msimamo ambao Ummah wa Kiislamu watakiwa kuuchukua. Kama ambavyo pia ni lazima kujua mikakati na mbinu zinazotumiwa na hayo mataifa, na huko kujua mipango na mbinu lazima kuunganishwe na kufuatilizia daima, na kujua kiwango cha kubadilika kwake, na kujua misukumo iliyopelekea kubadilika kwake, au sababu zilizoyalazimisha haya mataifa kubadilisha mikakati na mbinu, pamoja na kujua vyema mambo ambayo huathiri haya mataifa, au kuyalazimisha kubadili mipango yake na mbinu zake.

****

## [1] SIASA: FIKRA NA TWARIKA

Ama fikra ambayo juu yake husimama sera za serikali, huwa ni fikra ambayo hujengwa juu ya msingi wake mahusiano ya taifa kwa mataifa na watu wengine. Hivyo basi nchi zisizokuwa na mfumo, fikra zake huwa tofauti na huwa kuna uwezekano wa kubadilika. Hivyo nchi aina hizi hufanyiwa utafiti katika mikakati na mbinu zake za kisiasa, na wala hazifanyiwi utafiti kuhusu fikra zake za kisiasa.

Ama nchi ambazo zinaamini mfumo fulani, basi firka yake huwa thabiti haibadiliki, nayo ni kuueneza mfumo wake ulimwenguni kwa *Twariqa*/njia thabiti isiyobadilika, hata kama mbinu zitatafautiana na kubadilika. Nchi hizi hufanyiwa utafiti fikra zake za kisiasa.

Ni wajibu zitizamwe nchi zilizo ulimwenguni zitizamwe juu ya msingi huu, kwa kuzingatia kuwa kila nchi ina fikra msingi ya mahusiano yake na mataifa na watu wengine, iwe ni fikra thabiti au isiyokuwa thabiti, na huwa na njia (*twariqa*) maalumu ya kutekelezea hii fikra, iwe ni thabiti au isiyokuwa thabiti, na juu ya msingi wa fikra yake na njia yake ndio nchi huchora mikakati na hufuata mbinu (*uslub*) ambazo zitasaidia kufikia malengo yake.

Lakini nchi zilizo ulimwenguni leo hujiachia huru katika kutumia mbinu (*uslub*), kwani hutumia mbinu yoyote itakayohakikisha kufikia lengo, hata kama itagongana na njia (twariqa) yake, na zinafuata qaida isemayo (lengo huhalalisha mbinu).

Vyovyote itakavyokuwa, hakika nchi zote huweka mikakati ya kisiasa, na ambayo hubadilika kulingania na haja, na hufuata mbinu tofauti tofauti zinazobadilika kulingania na hali.

Na nchi zote katika matendo yake ya kisiasa huchunga maslahi ya ummah wake, na huweka mahusiano yake na nchi zengine kulingana na hayo maslahi, isipokuwa hutafautiana pakubwa katika hilo. Hivyo basi nchi ambayo haibebi mfumo maalumu hufanya maslahi ndio kitu pekee kinachoathiri katika mahusiano yake ya kimataifa, lakini nchi yenye kubeba mfumo maalumu na kuubeba ulimwenguni, huufanya mfumo kuwa kiungo muhimu zaidi katika mahusiano yake ya kimataifa, na hufanya maslahi yanayobainishwa na mfumo kuwa ndio kitendakazi saidizi katika hii njia. Hivyo basi ni lazima nchi ijulikane kwa upande wa fikra inazoamini, je ni nchi inayobeba mfumo au haibebi mfumo wowote? Wakati huo vitajulikana vitu ambavyo vyaathiri katika mahusiano yake ya kimataifa. Na kwa kuwa mfumo ndio unaoathiri katika sera za nchi inayoubeba, na hivyo kuathiri katika mahusiano ya kimataifa na katika msimamo ya kiulimwengu, hivyo basi ni lazima kujua mifumo inayotawala ulimwengu leo, na ijulikane kiwango cha kuathiri kila moja yao katika siasa za kiulimwengu leo, na kiwango cha uwezekano wa kuathiri kwake katika siasa za kiulimwengu katika siku za usoni, wakati huo mahusiano ya kiulimwengu yatajulikana kwa uwazi kulingana na hii mifumo, na upeo wa kuathiri kwake kwa sasa na siku za usoni.

Tukiuangalia ulimwengu leo tutakuta unatawaliwa na mifumo mitatu pekee, nayo ni: Uislamu, ukomunisti, na uraslimali, na kila mfumo wabebwa na mamilioni ya wanadamu. Isipokuwa Uislamu hauna serikali kwa sasa, ndio maana hatuoni uwepo wake katika mahusiano ya kiulimwengu, na wala katika siasa za kimataifa, wala

katika msimamo wa kiulimwengu unaotawala ulimwengu leo. Ama yale matendo yanayotendwa na madola ya ulimwengu ili kuzuia kurudi kwa dola ya Kiislamu katika maisha, baada ya kuwa ni wenye kuonekana na vijana wa Ummah wa Kiislamu, matendo hayo hayana mahusiano na msimamo wa kiulimwengu, wala hayaathiri katika mahusiano ya kimataifa, kwa sababu ili kuathiri katika msimamo wa kiulimwengu na mahusiano ya kimataifa huhitaji kuwepo kwa serikali itakayoubeba mfumo wa Uislamu na kuendesha sera zake za kindani na za kigeni juu ya msingi wake.

Ama ule mwelekeo wa kisiasa za kiulimwengu unaoonekana khususan kutoka kwa Marekani, wa kujaribu kuyawekea maeneo ya Kiislamu miradi ya kuyakoloni, kwa mfano (mradi wa mashariki ya kati iliyo kubwa) katika mwaka wa 2003 miladiya: bila shaka mwelekeo huu ni katika natija za hofu na wasiwasi unaozidi kukuwa ndani ya hizo nchi kwa kutarajia ukaribu wa kusimama kwa serikali ya Waislamu, na wala sio eti Uislamu unaathiri katika siasa za kiulimwengu ile taathira inayojulikana kama vile lau kama Uislamu ungekuwa na dola ambayo ipo kihakika.

Ama mifumo mengine miwili, kila mmoja wapo una serikali yake, bali serikali kadhaa, ndio maana ikawa inaathiri katika mahusiano ya kimataifa, na katika msimamo wa kiulimwengu, na katika siasa za kiulimwengu, na hasa wakati umoja wa usovieti ulipokuwepo kabla ya kuvunjika kwake, na miongoni mwa athari za hiyo mifumo miwili ni kuwa ulimwengu uligawanyika katika kambi mbili: kukawa kuna kambi ya mshariki na kambi ya magharibi. Isipokuwa kwa kuanguka kambi ya kimashiriki na kusambaratika kwa muungano wa Warsaw, hapo siasa za kambi mbili zikamalizika ulimwenguni, na mfumo wa ukomunisti haukuwa unatabikishwa katika dola yoyote japo kwa muundo tu isipokuwa ndani ya Uchina na Korea kaskazini, na kwa hivyo ilo baada ya hapo ikawa mivutano sio ya kiulimwengu tena bali ikawa ni ya kimaeneo. Kwani kwa kuanguka kwa muungano wa kisovieti fikra yake haikuwa ni yenye kuathiri katika siasa za kimataifa, na sababu ya hili ni kuwa fikra

iliyokuwa imesimama juu yake siasa za kigeni, fikra ambayo ni kueneza ukomunisti haikuwa ikitekelezwa tena. Ama dola ambazo bado zabeba mfumo wa kikomonisti sera zake za kigeni hazisimami juu ya hii fikra. Kwani sera za kigeni za Uchina hazikusimama juu ya msingi wa kueneza ukomunisti ulimwenguni, na hili larudia uhalisia wa Wachina ambapo wao hutosheka na ushawishi katika ujirani ya Asia, na kihistoria katika maisha yao hawajawahi kuwa ari ya kuwa na ushawishi wa kiulimwengu. Na kwa sababu ya uhalisia huu wa Uchina, basi Uchina haijawahi kwenda mbio kujitayarisha na nguvu zake ili iwe na nafasi ya kuathiri katika siasa za kiulimwengu, na bado vitendo vyote vya Uchina vimeelekezwa katika kuathiri maeneo ya jirani zake.

Ama kambi ya kirasilimali, hakika fikra ambayo juu yake siasa zimesimama ni kueneza mfumo wa kirasilimali ulimwenguni, mfumo ambao (aqida yake) ni kutengamanisha dini na maisha. Na pamoja wingi na utofauti wa nchi zinazoubeba mfumo wa kirasilimali lakini zote zinaeneza fikra yao kiongozi ya kirasilimali ulimwenguni, na kuufanya mwelekeo wao wa mtazamo wa kimaisha ndio unaotawala ulimwengu.

Ama njia ambayo hufuatwa na kambi ya kirasilimali ili kutekeleza fikra yake: ni ukoloni, yaani kulazimisha utawala wa kisiasa, kijeshi, kithaqafa, na wa kiuchumi juu ya watu walioshindwa ili kuwanyanyasa. Na njia hii ya ukoloni ni thabiti wala haibadiliki vyovyote zitakazo badilika serikali, na namna zitavyotofautiana kanuni zao. Na ukoloni sio kama anavyosema Lenin kuwa ***“Ni hatua ya juu zaidi katika hatua za urasilimali”*** bali ukoloni ni sehemu ya mtazamo wa urasilimali, nao ndio njia ya kuenezea urasilimali katika mataifa na watu. Hivyo basi siasa ya kigeni ya kambi ya kirasilimali ni thabiti katika fikra yake na njia yake, na wala hayabadilishwi na mivutano ya mataifa na mashindano yao. Hivyo basi Uingereza ni mfano wa Marekani, na ni mfano wa Ufaransa, na ni mfano wa Italia, na mfano wa nchi yoyote miongoni mwa nchi za kirasilimali, msingi wa sera zake ni

kueneza mfumo wake na mtazamo wake maishani, kupitia kukoloni mataifa na watu.

Na wakati wa kufahamu njia ya kambi ya wamagharibi ni lazima ieleweke kuwa hii njia, hata kama ni thabiti katika asili yake (ukoloni) isipokuwa mbinu za huo ukoloni na mtazamo wake yameingiwa na mabadiliko fulani katika kambi ya mmagharibi kulingana na zama, katika upande wa kushikana kwake kama njia, na kwa urasilimali kama fikra. Na katika jumla ya kubadilika kwake ni zile mbinu tofauti za ukoloni na mtazamo tofauti juu ya kukoloni wenyewe. Ama kubadilika kwa mbinu zake: ni kuwa kilichoitwa ukoloni wa kale ilikuwa ni kukalia kimabavu kupitia jeshi, kisha ukoloni mambo leo umekuwa sasa unategemea mambo mengine. Ambapo Amerika ikawa inategemea upande wa kiuchumi kama vile: mikopo, na yale yanayoitwa miradi ya maendeleo, na kuwategemea wajuzi wake waliosambaa kote, na mambo nyenginezo. Pamoja na upande wa ukandamizaji wa kisiasa na kulazimishwa. Baadaye Amerika mbali na mbinu hizi ikarudia hadi mbinu ya ukaliaji wa kimabavu wa kijeshi juu ya mataifa na watu, ili kuzifanya chini ya ushawishi wake na matakwa yake, na ikawa inakimbilia kuweka kambi zake za kijeshi katika koloni zake ili kulinda ushawishi wake humo. Na Uingereza nayo ikawa inategemea mbinu ya kutengeneza watu watakao kuwa vibaraka wake, na watu wa ujasusi wa kienegereza, na watawala wa nchi katika vibaraka wake, na mikataba miovu ya kibiashara, na haina nguvu katika kutegemea mikopo kwa sababu ya udhaifu wa hali yake kimali. Vilevile imedhoofika katika kutegemea kambi za kijeshi, kwa sababu ya kudhoofika ushawishi wake kimataifa, hata hivyo bado inazuia kuwepo kwa kambi zake za kijeshi katika koloni zake kama ilivyo katika Kopras (Cyprus) au karibu na koloni hizi. Kwa hivyo basi, kubadilika kwa mbinu ni kiungo muhimu cha ukoloni.

Ama tofauti ya mtazamo wa ukoloni, katika upande wa kushikamana kwake (kama njia) na urasilimali (kama fikra), hayo

hurudia katika nguvu ya mshikamano huu, yaani kuwa ukoloni ni njia tu ya kueneza urasilimali, kwa maana kuwa kipaumbele kwanza ni kueneza urasilimali. Na baina ya udhaifu wa mshikamano huu, yaani kipaumbele kwanza ni ukoloni wenyewe, halafu umuhimu wa pili ni kueneza urasilimali, ni kana kwamba ukoloni umekaribia kuwa ndio lengo hasa. Na nguvu katika ushikamano huu au udhaifu wake hutegemea nchi inayolengwa kukaliwa na mataifa ya kirasilimali: je ni yenye hadhara? ili ivamiwe na kuingizwa hadhara mbovu ya kirasilimali, ili iwe sahali kuitawala na kupora utajiri wake? au ni nchi isiyo na hadhara inayohitaji uvamizi, bali wataikoloni tu ili wapore utajiri wake na kuitawala? Na hili labainika wazi katika uhalisia wa mivutano ya nchi za kimagharibi katika kukoloni kwake bara Afrika, ambapo umechukua upande wa kuliibia, na suala la kueneza fikra ya kirasilimali hili lakaribia kukosekanwa. Kwani vita vya wenyewe kwa wenyewe huko Uganda na Rwanda viliendelea kwa miaka, na waathiriwa wake wakawa ni mamia ya maelfu ya watu, na pia matukio ya Zaire (demokrasia ya Kongo) hakuna kilichodhihirika humo isipokuwa ulafi wa kimada na mivutano juu ya ushawishi baina ya Uropa na Marekani. Na Uingereza na wale waliokuwa pamoja naye ambao ni Uropa na Marekani hawakuwa wakiangalia kitu chengine katika Afrika isipokuwa manufaa ya kimada tu, hivyo basi ukoloni ndani ya bara Afrika umekaribia kuwa ndio lengo hasa kuliko kuwa twarika/njia.

Ama katika ulimwengu wa Kiislamu huko mashariki ya kati na kaskazini mwa Afrika au Asia ya kati na kaskazini na mashariki yake: hakika nchi za kikoloni zikiongozwa na Amerika zinakimbilia huko pamoja na kutawala kisiasa na kijeshi na kiuchumi katika ulimwengu wa Kiislamu kwa ajili ya maslahi ya kimada, lakini pia zinakimbilia huko ili kueneza urasilimali kwa pande nyingi, kwa mfano: juhudi zao kwa ***"warsha za uhuru wa mwanamke"*** na ***"kummakinisha mwanamke"*** na yale yaliyokuja katika mpango wa kiamerika kwa mashariki ya kati, na kulazimisha ushawishi wa kithaqafa ambao imekuwa yajulikana kama ***"kujenga upya***

***thaqafa”***, na midahalo kati ya dini, na makutano ya hadhara, na kutilia mkazo mabadiliko au marekebisho ya mifumo ya kielimu ili kuondosha mafungamano ya Waislamu na hadahra yao na thaqafa yao. Na hivi ndivyo twarika/njia ya urasilimali inavyopiga hatua pamoja na wakati, lakini pamoja na hayo, ukoloni bado ni nguzo msingi katika urasilimali, iwe ndio njia ya kueneza urasilimali au njia iliyo karibu zaidi na lengo.

****

## [2] MIKAKATI NA MBINU ZA KISIASA

Mikakati ya kisiasa na mbinu ambayo hutuekelezwa nayo mikakati hiyo hubadilika kulingania na maslahi, japo mikakati hubadilika kwa uchache kuliko mbinu. Na tofauti kati ya mikakati na mbinu - kama inavyoonekanwa katika kufuatilia siasa za kimataifa - ni kuwa mikakati ya kisiasa huwa ni jumla, huwekwa ili kufikia lengo miongoni mwa malengo yanayohitajika kueneza mfumo au njia ya kuueneza, ama mbinu: ni sera maalumu katika sehemu miongoni mwa sehemu zinazosaidia kutekeleza mikakati na kumakinishwa kwake.

Kwa mfano: mpango/mkakati wa Marekani kuhusu Iraqi ilikuwa ni kuikoloni kwa maazimio au bila ya maazimio ya kimataifa, baadaye kuweka serikali itakayohalalisha ukolini huo kisheria kupitia umoja wa mataifa, baada ya kuwa (umoja wa mataifa) ulipuuzwa mwanzoni wa kukoloni, na kuhalalisha kadhalika (kindani) kupitia uchaguzi au mfano wa uchaguzi, kisha serikali hiyo kwa niaba ya watu wa Iraq kutia sahihi mkataba utakao ruhusu kubakia kwa jeshi la ukoloni humo ili lipewe sifa ya kisheria, kwa kuwa (eti) kuwepo kwake ni kupitia makubaliano ya wananchi wenyewe na kutaka kwao, na ni kwa na maazimio ya kimataifa. Na hili litayaweka mbali mataifa mengine na baraza la amani kuingilia masuala ya Iraq, na litafanya Marekani ndio muendeshaji pekee wa mambo yote ya Iraq, na kwa hayo ukoloni utahalalishwa kwa sababu kilichofanya kuwepo na kubakia kwake ni serikali halali

(iliyochaguliwa). Na Iraq itapewa katiba mpya chini ya usimamizi wa mkoloni, na hapo mgawanyiko utapewa umuhimu na nchi kugawanywa kwa kisingizio cha majimbo, na kutawashwa moto wa kimadhehebu, na Waislamu watashughulishwa na wenyewe kwa wenyewe badala ya kushughulika kumtoa mkoloni. Na kwa sababu hiyo Amerika ilitumia kila iwezavyo katika mbinu na namna ili kuikoloni Iraq kulingaa na mpango/mkakati uliowekwa, na baadaye kuhalalisha ukoloni huu na kuupatia uhalali kwa sura ya kanuni za kimataifa na za nchi.

Na upande wa pili, mpango/mkakati wa ufaransa ulikuwa ni kuleta muungano kati ya madola makubwa chini ya uongozi wake ili kupambana na mpango wa kiamerika. Na mpango huu ukapelekea kuwekea pingamizi baraza la usalama ili lisiweze kutoa maazimio wazi ili kufunika miradi ya kiamerika ya kutumia baraza hilo ili kuivamia Iraq, hivyo basi Amerika ikashindwa kabisa kucheza na karata ya baraza la usalama, na ikaweza kufichuka wazi kiulimwengu kuwa ni taifa linalokiuka kanuni, hivyo basi Amerika ikadhihirika kuwa inakwenda kimabavu, kidhulma, na inakiuka kanuni badali ya kudhihirika kuwa ni mlinzi wa kanuni za kiulimwengu kama ilivyokuwa ikidhihirika hapo zamani. Na Ufaransa ikaweza kuamsha hisia za Ujerumani na kuziathiri, kiasi cha kumuudhi Amerika katika vitendo vyao, na Urusi pia ikasimama upande wa Ufaransa katika kumpinga Amerika kutumia baraza la amani ili limsaidie katika mipango yake. Hivi ndivyo ulivyofaulu mpango wa Ufaransa, sio katika kuzuia uvamizi wa Amerika lakini katika kufedhehi malengo ya Amerika katika uvamizi huu.

Ama mpango wa Uiengereza: ulikuwa ni wa kimatata na mchafu, kwani ilimuunga mkono Amerika kidhahiri ili naye apate chochote katika ngawira, na hujitokeza pamoja naye juu ya jukwaa la kiulimwengu iwapo upande wa Amerika ndio mzito, na kumdunga visu mgongoni kila anapoweza kumdunga. Kwa hivyo Uingereza ilimuandama Amerika kwa sababu upande wake ulikuwa na uzito katika msimamo wa kiulimwengu, lakini kwa upande

mwengine iliilazimisha kuchukua azimio kutoka kwa baraza la usalama kuhusu kuifanyia uadui Iraq, na tangu hapo awali (Uingereza) ilikuwa yajua kuwa haiwezekani kutolewa maazimio kutokana na msimamo wa Ufaransa na Urusi na Ujerumani, hivyo basi ikadhihirika kwa hilo aibu ya Amerika kuwa inataka kuifanyia uadui Iraq kupitia maazimio au bila maazimio. Na Uingereza ikatilia nguvu hilo katika mkutano uliohudhuriwa na Blair na Chirac na Shroeder katika 20/09/2003 miladi, ili kutumia uwerevu wa kisiasa wa kiengereza ili kumakinisha na kukitisha msimamo wa dola mbili hizi dhidi ya msimamo wa kiamerika, kwa kuchochea baadhi za rai zilizotolewa na muingereza au mfano wake, na litawafanya wao kukakamaa pasina muingereza kujitokeza wazi kwa hilo mbele ya muamerika. Na Uingereza iliendelea na siasa hiyohiyo hata baada ya kukoloni Iraq, na muamerika kuupeleka mpango wake kwa umoja wa mataifa ili kuhalalisha kisheria ukoloni.

Na mfano wa mpango wa Amerika uliowekwa ili kuzuia muungano wa Uropa kuwa wamoja na kuwa tishio kwa Amerika, mkakati huu ulisimama juu ya misingi mitatu:

1. Kuupanua muungano wa Uropa kwa nchi za mashariki ya Uropa, na hizi nchi ni vibaraka wa Amerika na vichwa vya silaha yake, ili kuingiza uathiri wa Amerika ndani ya muungano. Na hili lilidhihirika pindi nchi hizi zilipounga mkono maoni ya Amerika katika kuivamia Iraq, na ndicho kilichomfanya Ramsfield kuikejeli Uropa kwa kuiita ya kale na mpya. Na Chirac raisi wa Ufaransa alikasirishwa mno na kitendo hicho cha nchi hizi, na akajaribu kuwatishia kuwa kuchagua kwao kuwa upande wa Amerika kutakuwa ni kizuizi kwao mwisho kukubaliwa katika muungano, lakini pamoja na hayo alikubali kujiunga kwao katika mkutano wa muungano wa Uropa ulioweka kwa ajili ya kukubali wanachama wapya, na wala Ufaransa haikuweza kuwazuia kujiunga.

2. Kuendelea kuuwepo kwa muungano wa Atlantic (NATO) licha ya kuvunjika kwa muungano pinzani wa (WARSAW),

kisha kupanua muungano huu ki-istratijia ili uingilie matatizo ya kiusalama ndani ya Uropa badali ya kuihami kiinje kama ilivyokuwa asili ya shughuli zake mwanzoni. Na pindi Uropa ilipohisi hatari ya muungano wa (NATO) dhidi yake kwa kuongozwa na Amerika kivitendo, basi Ufaransa na Ujerumani na Ubelgiji na Luxemborg zikalingania kuundwa kwa nguvu makhsusi ya Uropa, Amerika ikapinga hilo, na bado inasaibabisha Uropa shida hata kabla ya hiyo nguvu maalumu za kiUropa kujitokeza kivitendo.

3. Amerika kufaidika kutokana na msimamo wa Uingereza. Kwani Uingereza kwa ujanja wake wa jadi unaojulikana, haitaki muungano wa Uropa kuwa ni nguvu moja, na baadaye Uingereza iyayuke humo na kuwa nchi ya kando kama Luxemborg, kwa sababu Uingereza bado ndani yake ina ubwenyenye wa kibepari, ambapo ilikuwa na milki zake kubwa ambazo jua halichwi juu yake! ndio maana twaiona kuwa kizuizi cha kuundwa kwa huo muungano, na wala haikujiunga nao ila pale ilipoona tiyari ishakuwa ni uhalisia, basi ikajiunga ili kuudhoofisha, na mpaka leo bado haijaungana katika sarafu moja za kiUropa (Euro). Na hii aqliya yake ya kiukubwa ndio inayoifanya kutafuta nafasi katika jukwaa la kimataifa kwa njia yoyote ile itakayoipata.

Na kinyume chake, mpango wa Ufaransa ulikuwa ni kuupatia nguvu muungano wa Uropa na kuufanya ni mwavuli unaofaa kupambana na mwavuli wa Amerika, na kukimbilia kulianzisha jeshi la Uropa lenye kujitegemea kando na muungano wa kaskazini mwa Atlantic (Nato), na iliweza kuvutia Ujerumani upande wake kuhusu hilo, na Ufaransa ikacheza mchezo wa kiuerevu mno kwa kuweka mkataba na Ujerumani, kwa kiasi ambacho iliifanya Uingereza kuungana nao ili isikose fungu katika ngawira iwapo juhudi za Ufaransa na Ujerumani zitafaulu. Na hivi ndivyo Ufaransa ilivyo faulu hivi karibuni pamoja na Uingereza na Ujerumani katika kuanzisha kiini cha hili jeshi, pamoja na mbano mkali kutoka kwa

Amerika juu ya Uingereza na Ujerumani kuzuia kulibuni. Vile vile ilifaulu mikakati ya nchi tatu katika kuweka sera za muungano wa Uropa zenye upeo wa mbali, mbali na kuingiliwa na nchi ndogo katika muungano, na nchi zenye tamaa ya kuathiri ndani yake kama Italia na Uhispania.

Na hivi ndivyo tunavyokuta namna Ufaransa ilivyofaulu katika kuweka njia, hata kama ni muanzoni mwake ili kuupatia nguvu muungano wa Uropa na kubuni kiini cha kijeshi huru ndani ya Uropa kwa kukubaliana na Ujerumani na Uingereza. Na lau kama nchi hizi hazikushikana na urasilimali ambao hufanya (masilahi binafsi) kuwa ndio maadili kipao-mbele ya kila nchi, basi wangeliweza kuunda muungano wa Uropa ulio na nguvu dhidi ya Amerika. Lakini pamoja na hayo, kule kufaulu tu kwa Ufaransa katika kuweka mpango juu ya nchi zilizo na nguvu ndani ya Uropa (Ujerumani na Uingereza) huchukuliwa kuwa ni kitendo cha athari mbele ya Amerika, na katu haitoweza kukipuuza.

Na mfano wa mpango ambao Amerika ulioweka ili kakanyagia Urusi na kuifanya kuwa ni nchi isiyo na itibari/ushawishi hata wa kieneo pia, na inatekeleza hayo kwa kuitoa katika sehemu za itibari/ushawishi wake huko Balkan, mashariki ya Uropa, na Asia ya kati. Na pia kufunga ngao yake ya silaha za nuclear ambazo ni kiungo muhimu katika viungo vya nguvu zake, na pia hadi kumshinda katika anga. Hivyo basi Amerika ikatumia mbinu kadhaa kufikia hayo, ikiwemo: kulipiga jeshi la Yugoslavia (Serbia na mlima mweusi) kule kuliko na mahusiano ya (kijamii ya Slavia) pamoja na Urusi, kwa kupatiliza mzozo wa Kosovo. Vilevile Marekani iliweka mahusiano ya kiuchumi na ya kijeshi pamoja na nchi za mashariki ya Uropa ili kupenyeza ushawishi wake humo, kisha ikaunganisha wengi wao kwenye muungano wa kaskazini mwa Atlantic (Nato). Kama ambavyo pia ilipatiliza fursa ya vita dhidi ya "Ugaidi" na ikaweka kambi zake za kijeshi ndani ya nchi za Asia ya kati, na hili ni baada ya kufanikiwa kuwavutia baadhi ya watawala wa hizo nchi kupitia misaada ya kiuchumi, na ikakoloni

Afghanistan na ikakimbilia kuendeleza mfumo wa kinga ya makombora ya Urusi yanayopita bara hadi bara yaliyo na uwezo wa kubeba vichwa vya nuclear. Vilevile iliweza kutumia suala la ufukara ndani ya Georgia na kuwaweka vibaraka wake katika kilele cha piramidi, kitu kilichofanya eneo kuanguka kwa sehemu iliyo wazi kati ya Urusi na muungano wa Nato huko Uturuki, na Marekani ilikuwa imeikinaisha Urusi kuachana na vituo vyake vya angani “MIR” na kushiriki katika Kituo cha anga cha kiulimwengu "ISS" na hili ni kumuwekea mipaka katika mashindano ya kuvamia anga. Na hivi ndivyo inavyoendelea Amerika katika mipango yake ya kumzingira Urusi ili ibakie kuwa ni nchi isiyo na itibari (ushawishi) wa kimaeneo, baada ya kukata itibari yake kiulimwengu kwa kuanguka kwa muungano wa Usovieti.

Na hali kadhalika kwa Uchina, kwa sababu Amerika inaona uwajibu wa kuipigisha magoti Uchina, na kuifanya ni nchi ya kawaida tu, haswa kwa kuwa haimiliki vigezo vya kuwa dola kubwa, lakini imekuwa ni dola kubwa ya kimaeneo tangu nusu ya miaka ya tisaini, kwa nguvu inazomiliki na ina kura ya turufu katika baraza la usalama, na kuwa ina malengo na tamaa za kimaeneo, na hili ndilo lisilomridhisha Amerika. Hivyo basi Uchina katika jicho la Amerika ni soko kubwa la kibiashara na ni lazima ifaidike nalo, na jitu kubwa ambalo ni wajibu lichungwe ili lisije likawa ni hatari itakayotishia masilahi ya kiamerika katika eneo la mashariki ya Asia. Hivyo basi ilikuwa juu ya Amerika kuweka mikakati baada ya kumalizika kwa vita baridi ili kuikanyagia Uchina, na kuifungia katika sehemu hai ndogo, iwapo haitoweza kuikata kikamilifu kiameneo, hivyo basi umuhimu wake ilikuwa ni kusawazisha mahusiano na Vietnamu ili aifanye kuwa ni kizingiti mbele ya Uchina wakati yatakapotengenezeka mahusiano kati ya Amerika na Vietnam. Vilevile inajaribu kukifanya mfano wa kisiwa cha Korea kuwa ndio kituo cha hatari ubavuni mwa Uchina, kwa kuzidi kuikandamiza Korea kaskazini kwa hoja kuwa ni dira ya shari, na wakati huo huo inaendelea kubakisha kambi zake za kijeshi huko karibu na mipaka ya Uchina na mlangoni mwake. Vilevile inajaribu

kuifanya India kuwa mpinzani wa Uchina, na pia inafanya bidii ya kuleta miungano ya kistratejia na miungano ya kijeshi ya kieneo katika Asia ya kati na mashariki ya kati, vilevile imeweka kambi za kijeshi katikati ya Asia katika mipaka ya magharibi ya Uchina kwa upande mwengine wa Himalaya.

Hivyo basi, mikakati na mbinu ya kisiasa huwekwa kwa ajili ya kitendo cha papo hapo, lakini pamoja na hayo serikali haichukui muda kubadilisha mbinu zilizoko, na kutafuta mbinu zengine iwapo itadhihirika kuwa mbinu zile hazitoweza kufikisha kwenye malengo, na vilevile pia yaweza kubadilisha mikakati iwapo haisaidii, au iwapo kubakia kwake kutaipatia serikali taabu na wala kuwepo kwake hakuna masilahi, lakini pindi serikali inapobadilisha mkakati basi huweka mkakati mwengine badali yake, na pindi inapobadilisha mbinu huweka mahala pake mbinu nyengine, na wala haiwachi kuweka mpango na mbinu isipokuwa iwapo itashuka na kuporomoka hadhi yake katika msimamo wa kiulimwengu, kama hali ilivyokuwa kwa nchi zilipoteza ushawishi wake wa kisiasa tangu zamani, kwa mfano: Japan, Italia, Uholanzi, Ubelgiji, Uhispania, na Ureno.

Na mfano wa kubadilisha mikakati: ni yale yaliyofanywa na Amerika katika mikakati yake ambayo iliweka kuhusu Ujerumani, kwani mipango yake ilikuwa ni kulituma jeshi la kijerumani, na kuisimamisha jamuhuri ya kijerumani ya magharibi, na baadaye mpango wake ukawa ni kudhoofisha Ujerumani ya magharibi na kuleta muungano baina yake na Ujerumani mashariki, na kuiwekea Ujerumani mipaka ya silaha, kisha katika mwaka 1990 miladi ikaiunganisha ili kuunda nchi ya kiuropa yenye nguvu, itakayo shindana na Ufaransa na Uingereza, na ili ishindane nazo katika uongozi wa muungano wa Uropa, na kwa hilo utadhoofika uwezekano wa Uropa kuungana kama nguvu moja.

Vilevile mpango ambao Amerika iliuweka kwa ajili ya Uchina, baada ya kuona kuisaidia na kuifanya kuwa ni mchezaji wa

kiulimwengu, na kutengeneza mahusiano nayo, na vilevile kutengeza mahusiano kati ya Uchina na Japan, ili kuifanya kuwa ni nguzo miongoni mwa nguzo za nidhamu za kimataifa, na hilo ni kupitia kuudhoofisha msimamo wa muungano wa kisovieti wa kiulimwengu wakati huo, na ili kuzidisha mpasuko baina ya washirika waiwili wa kikomunisti walio maadui hatari kwa Amerika, baada ya hayo, baada ya kumaliza kwa vita baridi Amerika ikarudi na kubadilisha mpango wake, na ikaonelea kuwa suala sasa lahitajia kuweka mpango wa kumkanyagia Uchina na kumfungia ndani ya kuta zake kubwa, na ikalazimika kufanya haraka kuweka mkakati ili isije kuwa ni hatari kwa masilahi yake ndani ya mashariki ya Asia, haswa kwa kuwa Uchina sasa yamiliki viungo vitakavyo muezesha kufikia hilo.

Na mfano wa kubadilisha mbinu ni kama ilivyofanya Amerika katika nchi za ulimwengu wa Kiislamu, kwani baada ya kuwa ilikuwa inategemea mapinduzi ya kijeshi ili kuwafikisha vibaraka wake kwenye utawala, na misaada ya kiuchumi kama madeni na yale yaliyokuwa yanaitwa miradi ya maendeleo, na kama kuwatumia wajuzi, na mbinu nyenginezo, na baada ya kuwa ikitumia mbinu ya vivutio na vitisho au fimbo na karoti, badala ya mbinu hizo sasa imekuwa inategemea masuluhisho ya kijeshi na vitisho, na imerudi katika kutegemea washirika wake na makambi ya kijeshi baada ya kuwa imeachana nayo, jambo lililorudisha mabangoni zama za ukoloni wa kijeshi na ubeberu wa kimagharibi.

Na Uingereza pia ilishabadilisha mbinu zake kwa kuachana na mikataba na kambi za kijeshi, na kutegemea viongozi vibaraka na mikataba ya kiuchumi na mikataba ya silaha, na inavyoonekana sasa ni kuwa nayo yafuata mkumbo wa Amerika kwa kurudia kutumia kambi za kijeshi kama mbinu mpya na ya kale.

Hayo yalikuwa ni maelezo kuhusu mikakati na mbinu za kisiasa, hivyo basi ni wajibu juu ya Waislamu wajue kihakika kuwa kambi ya kimagharibi haibadilishi fikra yake ya kisiasa wala

Twarika/njia yake, lakini huweka mikakati mingine na kufuata mbinu mpya ili aweze kueneza mfumo wake. Na iwapo mbinu zake zitavunjwa na mipango yake kuharibiwa basi na malengo yake ambayo ameyawekea mipango na mbinu hizo pia nayo yataharibika, hivyo basi mapambano ya kisiasa ni lazima yaelekezwe kwenye mipango na mbinu, kwa kuifichua na kupambana nayo katika wakati wa kupambana na fikra ya kisiasa na njia yake. Kwa hivyo, ni lazima kwa Waislamu kujua mipango iliyowekwa ya kila nchi na kuzitambua mbinu zake.

****

## [3] MSIMAMO WA KIMATAIFA

Kufahamu msimamo wa kiulimwengu ni tofauti na kufahamu siasa ya kila nchi, na hili ni kwa sababu kufahamu siasa za nchi zinazoathiri inahusiana na kufahamu fikra na Twarika/njia ambazo husimama juu yake sera za nchi hiyo kama tulivyoelezea hapo awali. Ama msimamo wa kimataifa, ambao ndiyo msingi wa mahusiano ya kimataifa yenye athari, yaani ile hali inayokuwa juu yake nchi ya kwanza (super power) na nchi zinazoshindana nayo, msimamo huu hauhusiani na fikra wala Twarika/njia, bali huhusiana na mahusiano ya kiulimwengu na mashindano ya daima kati ya nchi mbali mbali ili kushika nafasi ya kwanza, na katika kuathiri siasa za kiulimwengu, hivyo basi hamna budi kufahamu msimamo wa kiulimwengu.

Lakini yapasa ieleweke wazi kuwa msimamo wa kimataifa haubaki katika hali moja, bali hugeuka na kubadilika kulingana na hali zake na matukio yake. Ila pamoja na hayo, yawezekana kuchora picha yake wazi, na kuweka misingi jumla kuhusiana nayo au kuelezea upambanuzi wake, lakini yote hayo hujulisha tu uhalisia wake wakati inapowadhihirikia watu wakati wa kuelezwa kwake, hivyo basi sifa huwa na uhakika katika uhalisia uliopo, na kipindi msimamo wa kimataifa unapobadilika basi ile sifa iliyopeanwa haisemwi kuwa ilikuwa ya makosa, bali husemwa ile ilikuwa ni sifa ya hali iliyokuwepo na sasa imeondoka/haipo na hubakia ni sehemu ya historia. Basi itakuwa ni lazima kuelezwa uhalisia wa

sasa, yaani msimamo mpya wa kimataifa. Kwa hivyo, sifa tutakayoelezea ya msimamo wa kimataifa kwa kuchora picha yake, au tutakayoelezea misingi yake jumla, au tutakayofafanua kiundani yote hayo ni sifa ya hali halisi iliyoshuhudiwa kitambo, au ni ule unaonekana sasa, au unaotarajiwa kutokea mbeleni, lakini pamoja na hayo msimamo wa kimataifa hauzingatiwi kuwa ni jambo thabiti, hivyo basi ni wajibu kwa mwanasiasa kuwa na maalumati kuhusu msimamo wa kiulimwengu na kuhusu siasa za kiulimwengu, na ayafungamanishe hayo na yale anayoyaona, ili aweze kuwa na bayana na mambo na kuyatolea hukmu yake.

Na ili kufahamu msimamo wa kiulimwengu, inawalazimu Waislamu kujua nafasi ya nchi nambari moja ulimwenguni na nafasi za nchi zengine kuhusiana nayo, na kuhusiana na siasa za kiulimwengu, pia inawalazimu kujua nchi zinazofuata na nchi ambazo zipo katika mzunguko na nchi huru.

Ama kuhusu nchi zinazofuata: ni nchi ambazo zimefungika na nchi nyengine katika sera zake za kigeni na hata katika masuala mengine ya kindani, kwa mfano Misri pamoja na Amerika, na Kazakhstan (kwa sasa) pamoja na Urusi. Ama nchi ambazo zipo katika mzunguko: hizi ni nchi ambazo sera zake za kigeni zimefungika na nchi nyengine, lakini mafungamano wa kimaslahi na wala sio mafungamano ya kufuata, kwa mfano Japani kwa Amerika, na mafungamano ya Australia kwa Amerika na Uingereza, na mafungamano ya Canada kwa Amerika, Uingereza, na Ufaransa. Na mafungamano ya Uturuki (kwa sasa) kwa Uingereza na Amerika. Ama kuhusu nchi huru: hizi ni nchi ambazo hutekeleza sera zake za kigeni na za kindani vile zinavyotaka kulingana na maslahi yake, mfano: Ufaransa, Uchina, na Urusi.

Na pia kuna hali ambazo haziingii chini ya siasa za kiulimwengu, bali ni matukio tu yaliyotokea kutokamana na kuondoka kwa dola za kikoloni katika nchi. Hivyo basi hali hizi na mifano yake hazifanyiwi utafiti katika siasa za kiulimwengu, na

wala hazitolewi misingi jumla kuhusiana nazo, bali kila hali husomwa kulingana na uhalisia wake na kisha kupewa hukmu yake. Kwa mfano: Iraq baada ya Muingereza kutoka humo, na kutokea kwa mapinduzi 14 /Julai/ 1958 miladi na kubatilishwa kwa mikataba yote na mafungamano, nchi ikawa ni huru kiulimwengu, mfano wake ni mfano wa Ufaransa na Uingereza na nchi yoyote ile iliyo huru, lakini kwa kuwa mtawala wake wakati huo alikuwa ni kibaraka wa Amerika, ndiposa Iraq katika uhalisia wake ikawa ni nchi inayofuata Amerika, japo katika upande wa kiulimwengu ni nchi huru, lakini pindi yalipotokea mapinduzi 17/ Julai/ 1968 na vibaraka wa Muingereza wakaja kwenye utawala, hapo Iraq ikawa ni nchi inayofuata Uingereza.

Na hivyo basi pindi nchi huru inapokuwa mtawala wake ni kibaraka au anayeiendesha serikali ni kibaraka, basi nchi inakuwa inafuata nchi ambayo huzingatiwa kiongozi wake ni kibaraka wake. Na hivi ndivyo zilivyo nchi zote zilizokoloniwa, hukumbwa na hali hizi, hutoka katika mkono mmoja hadi mikono mengine kwa kubadilishwa viongozi. Nchi hizi kwa upande wa kiulimwengu “kidhahiri” ni huru, Lakini “kiuhakika” zinafuata, lakini hali hizi huwa ni za nchi moja-moja na hutokamana na kukomboa koloni kutoka kwa mkoloni, na majaribio ya nchi za kikoloni kurudia katika koloni zake, au majaribio ya nchi nyengine kutaka kuchukua nafasi ya mkoloni katika nchi ambayo mkoloni mmoja ametoka humo.

Jambo ambalo ni lazima kulifahamu ni nafasi ya nchi ya kwanza katika ulimwengu, kwa sababu ya umuhimu wake katika kufahamu siasa za kiulimwengu na katika kufahamu msimao wa kiulimwengu. Kwani katika hali ya amani, nchi ya kwanza katika msimamo wa kiulimwengu huzingatiwa kuwa ndio yenye kauli kiulimwengu, na itajilinganisha katika hilo baada ya hapo nchi ya pili, na nchi yoyote nyengine yenye uwezo wa kuuathiri ulimwengu kisiasa.

Na kuathiri kwa nchi zengine huwa ni kwa nchi ambazo zina uzito wake katika kuiathiri nchi ya kwanza, na kuathiri huku hutofautiana kwa tofauti ya nchi katika nguvu/uwezo wa kujitegemea, na nguvu za kiulimwengu. Hivyo basi kwa kadri nguvu za nchi na upeo wa uzito wake kiulimwengu itakavyokuwa, basi ndivto itakavyoweza kuiathiri nchi ya kwanza, na pia kuathiri siasa za kiulimwengu kwa upande wa kimataifa.

Na mfano wazi zaidi leo wa kuathiri nchi ya kwanza na baadaye kuathiri siasa za kiulimwengu, ni mfano wa Uingereza siku hizi (2004 miladi) kwani kuathiri kwake katika siasa za kiulimwengu katika upande wa kimataifa imetokamana na baadhi ya ushawishi wake juu ya Amerika, ambayo ndio nchi ya kwanza ulimwenguni, na pia kutokana na ushawishi wake wa kuendelea katika koloni zake za kale. Na vilevile Ufaransa, Urusi, na Ujerumani, kwani hizi zilishirikiana pamoja baada ya vita vya Amerika na Uingereza dhidi ya Iraq na kuleta aina fulani ya athari kwa nchi ya kwanza, na kuathiri siasa za kiulimwengu katika upande wa kimataifa.

Ama mfano wa nchi ambazo haziiathiri nchi ya kwanza na vilevile zisizo na athari kipeke yake katika siasa za kiulimwengu ni nchi zinazofuata. Hizi haziwezi kuwa na athari juu ya nchi ya kwanza ila kwa kiasi cha nchi wanazozifuata. Na kadhalika nchi ambazo zipo katika mzunguko/mkumbo, kwani hizi pia kuathiri kwake inategemea zile nchi kubwa ambazo hizi zazunguka katika sayari yake.

Ama nchi zilizosalia zisizo futata, na zile zisizokuwa katika mzunguko wa nchi zengine, hizi ni zile nchi huru, kama vile: Uswizi, Uhispania, Uholanzi, Italia, na Uswidi, hizi zaweza kuathiri katika siasa za kiulimwengu katika upande wa kimataifa, iwapo zitalinda masilahi ya nchi ya kwanza au kutishia. Na mfano wa hayo ni Italia na Uhispania kulinda masilahi muhimu miongioni mwa masilahi ya Amerika, na hili ni kwa njia ya wao kuisaidia Amerika katika kuikoloni Iraq mwaka wa 2003 miladi.

Na kwa sababu hiyo, ni wajibu juu ya nchi yoyote inayotaka kuathiri katika siasa za kiulimwengu na kuziburuta kwa mujibu wa masilahi yake kufuata moja kati ya njia mbili: ima kutishia masilahi ya kihakika ya nchi ya kwanza katika msimamo wa kimataifa utishio wa kivitendo, au kulinda masilahi ya nchi ya kwanza kwa njia ya kutaridhilia kwa ajili ya masilahi yake.

Na njia ya kutishia kihakika kunako athiri ndio njia yenye matunda bila shaka, na ndio inayofaa kwa nchi sahihi ambayo yalenga kudhamini kuathiri kwake na kusikiwa sauti yake katika msimamo wa kimataifa. Ama njia ya pili ambayo kwa kuifuata kwake hulengwa kulinda masilahi, hii ni njia yenye kiza na wala haiaminiki, kwani huenda ikafikisha katika lengo na pia huenda ikapelekea katika maangamivu, hivyo basi ni kucheza kamari na muundo wa Ummah, na ni kamari ya kijinga kwa hatima ya nchi, kwa sababu nchi yoyote kulinda masilahi ya nchi kuu, hakutazuia kuridhia maslahi hayo pamoja na nchi yoyote iliyo chini yake kwa hadhi na uwezo. Kwani katika mwaka 2003 miladi Amerika ilifanya maridhiano juu ya marafiki zake wa kale katika nchi za Uropa ya magharibi, baada ya kuisifu kuwa ni Uropa ya kale, na ikaanza kutafuta katika nchi za mashariki ya Uropa ili kuweka badali yao katika kuungana naye katika suala la Iraq. Na kadhalika iliibeza Uingereza pale ilipojaribu kumzuia kusonga mbele na kuivamia Iraq pasina kurudia umoja wa mataifa ili ichukuwe uhalalisho wa kimataifa kutoka kwao, akasema Ramsfield aliyekuwa ni waziri wa ulinzi wa Amerika: “Amerika yaweza kwenda Iraq hata bila ya Uingereza”.

Na ili kutishia masilahi na kuleta athari ya kivitendo, ni lazima nchi iwe na uwezo wa kujihami, na iwe na sababu za udhibiti kamili wa kindani. Na njia sahihi ya kufikia hilo ni iwe yasonga mbele na kunyanyuka, yaani ni lazima iwe na mfumo, na ibebe ujumbe wa kiulimwengu, na ianze kwa majirani zake, ili iweze kujihami dhidi ya vita vya kuingiliwa mambo yake ya kindani, na wala isitosheke

na kuhami tu mipaka yake bali ijitanuwe kwa mfumo wake na ushawishi wake hadi iweze kushindana na dola ya kwanza katika msimamo wa kimataifa.

Na nchi yoyote ili iweze kuitingisha nchi ya kwanza katika kiti chake rasmi, basi ni lazima igeuze upepo wa kisiasa kuelekea upande wake na izivute nchi zengine kwenye siasa zake na fikra zake, kama ilivyofanya Ujerumani kabla ya vita vya pili vya dunia. Na wakati nchi yoyote itakapoweza kufanya hayo basi msimamo wa kimataifa utakuwa unayumbayumba, hadi pale nchi moja itakapochukuwa nafasi ya nchi ya kwanza, na mara nyingi hilo haliwezi kupatikana isipokuwa vitakapoibuka vita na kubalidilisha msimamo, viwe ni vita vya kiulimwengu jumla au vifungike na maeneo fulani, au iwapo hatari ya vita ipo dhidi ya dola ya kwanza na ni suala linalotarajiwa, na ikaihitajia nchi inayoshindana nayo ishiriki katika kambi yake katika hivi vita.

Na suala la kuwepo kwa nafasi ya nchi ya kwanza sio jipya ulimwenguni, kwani lilikuwepo tangu zamani. Kwani Misri katika historia ya kale ilikuwa ndio dola ya kwanza na Ashur huko Iraq ilikuwa ndio inayoshindana nayo katika nafasi hiyo, na dola ya Warumi ilikuwa ni dola ya kuanza na dola ya kifursi ilikuwa inashindana nayo juu ya nafasi hiyo, na dola ya Kiislamu tangu zama za makhalifa wema hadi vita vya kimsalaba ilikuwa ndio dola ya kwanza na wala hakuwepo wa kushindana naye katika nafasi hiyo, na Ufaransa ilikuwa ni dola ya kwanza na Uingereza ilikuwa inashindania hiyo nafasi, pia dola ya kiuthmaniya kwa sifa yake ya kuwa dola ya Khilafahh ya Kiislamu ilikuwa ni dola ya kwanza kwa muda wa takriban karne tatu, na wala haikuwa na mshindani katika nafasi hiyo hadi katikati ya nusu ya karne ya kumi na nane miladi. Na kabla ya vita vya kwanza vya dunia Ujerumani ilikuwa ndio dola ya kwanza na Uingereza na Ufaransa zilikuwa zinashindania nafasi hiyo. Kisha kidogo kabla ya vita vya pili vya dunia Uingereza ilikuwa ndio dola ya kwanza na Ujerumani ilikuwa inashindana nayo katika nafasi hiyo, hadi ikakaribia kuichukuwa nafasi hiyo, na

vikaibuka vita vya pili vya dunia, Amerika ikashiriki katika vita, na vita vilipomalizika Amerika ikawa ndio dola ya kwanza katika kuchora sera za kimataifa msimamo wa kimataifa, kwani kati ya nchi zote Amerika ilikuwa ndio nchi yenye uwezo zaidi katika kuzifanya sera za kimataifa kuwa upande wake, na ikaendelea kutawala msimamo wa kimataifa, ambapo hayatokei wala kutekelezwa ila matukio ya kisiasa inayotaka. Lakini pamoja na hayo, muungano wa kisovieti wakati huo, Uingereza, na Ufaransa zilijaribu kushindana nayo na zilikuwa zashiriki kuathiri katika siasa za kiulimwengu kwa kiasi fulani kulingana na nguvu za nchi hizi, na hasa muungano wa kisovieti kwa sura ya nguvu, kisha Uingereza kwa sura dhaifu.

Ama muungano wa kisovieti ulifaulu kusimama ubavuni mwa Amerika kama mshirika wake, lakini Uingereza ililegea na kurudi nyuma, na ikaendelea kushuka chini na chini zaidi hadi ikafika hivi ilivyo leo. Na ufafanuzi kuhusiana na hayo: ni kuwa Uingereza baada vita vya pili vya dunia, ilikuwa yaanza kuzinduka kutokana na kipigo cha vita, na ikaanza kujaribu kuitingisha Amerika katika nafasi yake ya kwanza, na ikawa yafanya matendo ya kisiasa ili kuiathiri Amerika, hivyo basi haikushiriki katika vita vya Korea isipokuwa kiishara tu, na ilikuwa ikipelekea Uchina habari za Amerika za kivita, na kihakika Uchina ndio ambayo ilikuwa yapigana vita vya Korea, na Uingereza kupitia mbinu zake chafu za kisiri ikaweza kuathiri nafasi ya Amerika kimataifa katika vita vya Korea, na ikatingisha nafasi yake. Na katika mkutano wa Geneva ambao uliwekwa kwa ajili ya India-Uchina, Uingereza ikasimama upande wa kambi ya mashariki, na ikatoka na maazimio yaliyokuwa na masilahi kwa upande wa mashariki. Pia Uingereza ilikuwa ikipelekea Urusi habari za Amerika za kijasusi na za kijeshi, na miongoni mwake ni ile iliyompelekea Urusi kuhusu Ndege (U2) na kupelekea kuangushwa kwake. Kisha msimamo wa Macmillan katika mkutano wa Paris kusimamia upande wa Khrushove dhidi ya Eisenhower na kujaribu kumdhalilisha Eisenhower kwa sifa yake ya kuwa raisi wa Amerika, na kupelekea kutofaulu kwa mkutano na

kudhoofisha nafasi ya Amerika. Na hivi ndivyo Uingereza ilivyokuwa, inafanya mambo mengi ili kuipiga Amerika na majaribio ya kuathiri nafasi ya nchi ya kwanza, lakini Amerika nayo ilitambua yote hayo. Baadaye katika mkutano wa Khrushove na Kennedy huko Vienne, na tangu tarehe hiyo Uingereza ikawacha kuihujumu Amerika na kuchukua msimamo wa kujihami, na hapo Urusi (muungano wa Usovieti) na Amerika kwa pamoja zikaanza kuisambaratisha Uingereza katika dunia.

Muungano wa usiovieti ulikuwa ukiwasha moto wa vita baridi dhidi ya kambi ya kimagharibi, na kuilenga haswa Amerika kwa kiasi kikubwa, kwani ulikuwa ukijaribu kuchukuwa hatamu za uongozi kutoka kwa kambi ya kimagharibi, na ukawa unafanya vitendo ili kumuondosha Amerika katika nafasi ya dola ya kwanza ili muungano huu uwe ndio dola ya kwanza duniani, na iliweza kufaulu katika vitendo kadhaa: kwani ulifanikiwa kuiondoa Amerika kwenye ngome yake kuu ambayo ni umoja wa mataifa katika kutatua matatizo ya kimataifa, na kuifanya iweke makongamano nje ya umoja wa mataifa, na huku ukiishajiisha Uingereza kuitingisha Amerika kwa lengo la kudhoofisha nafasi ya nchi ya kwanza, na kuzidi kupanua mwanya wa utesi ili kudhoofisha nafasi ya dola kwanza, na muungano huu ukapanua mwanya wa utesi baina ya Ufaransa na Amerika, na ukaathiri mno katika vitendo vya kimataifa. Pamoja na hayo, pia ukatangulia katika nyanja za anga na hatimaye ukamshinda Amerika, na ukaendelea katika silaha za nuclear na katika makombora yanayopita mabara, na ukaweka kambi yake ya kijeshi huko Cuba ili kumtishia Amerika, na ukafichua mbinu nyingi za Amerika huko Congo, Misri, na Algeria na kwengineko. Isipokuwa yote hayo, japo yaliiathiri sana Amerika tena kwa kiasi kikubwa, lakini muungano wa usovieti haukuweza kumuondosha katika nafasi ya kuwa nchi ya kwanza, bali hayo yalikuwa ni ushindi wa kivipande katika masuala fulani ya kisiasa za kimataifa, japo muungano wa usovieti haukuwacha kuihujumu Amerika kwa mbinu za vita baridi, hadi ukafanywa mkutano wa Khrushove na Kennedy mwaka 1961 miladi, walipokutana katika

mwezi wa Juni mwaka huo huko Vienna mji mkuu wa Austria, na wakakubaliana waugawanye ulimwengu baina yao. Na baada ya hiyo tarehe Uingereza na Ufaransa zote zikaanguka katika siasa za kiulimwengu, na muungano wa usovieti na Amerika zikawa ndizo pekee zinazochora siasa hizi. Na hayakufaulu majaribio yote yaliyofanywa na Uingereza ili nayo iwe na rai katika siasa za kiulimwengu, na Ufaransa vilevile pia haikufaulu hata katika zama za De Gall kupiga angalau hatua moja katika kuleta uwezekano wowote upande wake katika kuchangia kwenye siasa za kiulimwengu, na hali ikaendelea hivyo hadi mwaka 1989 miladi, wakati ukuta wa Berlin ulipoangushwa, na ikavunjika muungano wa Sovieti baada ya miaka miwili kwa sura rasmi, na vikamalizika vita baridi, na Urusi ikarithi rasmi mahala pa muungano wa usovieti mwanzoni mwa miongo ya tisaini katika karne iliyopita, lakini nayo iliangushwa katika nafasi ya pili katika siasa za kiulimwengu, na ikachipuka hali mpya ya kimataifa, na Amerika kwa mara ya kwanza ikawa haina mshirika wa kimataifa, na ulimwengu ukaingia katika hali ya kimataifa ambayo haijawahi kutokea, Amerika ikajaribu katika mwisho wa zama za Bush baba kuchora siasa za kiulimwengu kipekee, na akalingania kwa nidhamu mpya ya kiulimwengu (New world order) lakini hii nidhamu haikufaulu, na mwito huo ukabakia ni wenye utata, vilevile hali ya kimataifa kubakia ni yenye ukungu, hadi alipokuja Clinton katika kiti cha utwala mwaka 1992 miladia, naye akaweka nidhamu mpya ya kimataifa ambayo haitegemei upweke, bali inayotegemea nchi kuwa juu, na idara ya Clinton ikaanza kuweka misingi ya nidhamu hii mpya, ambayo miongoni mwa nguzo yake muhimu ilikuwa ni kufuata sera za ushirikiano pamoja na mataifa mengine makubwa, sera ambazo zilionekana katika kutatua matatizo ya Balkan katika Bosnia, Herzek, na Kosovo, na vilevile zikadhihirika katika kufaulu kuharibu silaha za nuclear huko Ukrain na Byelorussia kwa maelewano na Urusi, na pia kuwekwa sahihi mkataba wa uwiano kati ya Amerika na mataifa yaliyokuwa hapo awali ni sehemu ya nidhamu ya mashariki, na Uingereza na Ujerumani wakashiriki katika kuweka sahihi mkataba huu wa uwiano. Na pia Amerika

katika kipindi hiki - kupitia siasa ya ushirikiano - iliweza kupanua muungano wa Atlantic kaskazini (NATO) kwa kushirikiana pamoja na nchi za magharibi ya Uropa, ambapo pia nchi za muungano wa Uropa zilifaidika kwa upanuzi huu, na upanuzi huu ukatimia dhidi ya Urusi, na juu hisabu ya ushawishi wake.

Na kinachotofautisha kipindi hiki ni kupanda kwa nguvu za Ujerumani, kwani udhaifu ulipoingia katika muungano wa kisovieti, na kuangushwa kwa ukuta wa Berlin, na kuondoshwa kwa msaada wa Ujerumani ya mashariki, hapo kilichofuata ni kuunganishwa kwa Ujerumani mashariki pamoja na Ujerumani ya magharibi kwa haraka sana, na ikawa ni nguvu kubwa kabisa kiuchumi ndani ya Uropa, na ikabadilika kuwa ni nguvu ya kisiasa kivitendo na yenye athari, hadi Amerika na Uropa zikawa zajipendekeza kwake, hadi mazungumzo yakawa ni Ujerumani kuingia katika klabu ya nchi zenye uwanachama wa kudumu katika baraza la usalama ni suala la kuzungumzwa ndani ya Amerika, Uropa, na kiulimwengu.

Na hali hii mpya ya kisiasa iliandamana na hali mpya ya kiuchumi, ambapo ziliundwa sera za soko kwa kiasi kikubwa, na hili likadhihirika wazai katika sera za utandawazi ambayo ilijilazimisha yenyewe juu ya dunia, hivyo basi mashirika yakaungana na kuwa makubwa, na yakajitokeza kama mchezaji mkuu wa kiuchumi yanayolazimisha siasa zake juu ya madola, na mashirika yenye uraia wa nchi nyingi yakawa ndio mazungumzo ya wanauchumi, na maafikiano ya Gatt katika mwaka 1995 miladi yakabadilishwa kuwa ni muungano wa kimataifa wa kibiashara utakaolinda sera za utandawazi kwa sitara ya kanuni. Vilevile ilitendeshwa kazi dori ya sanduku la fedha la kimataifa (IMF) na benki ya kuu ya kiuliwemngu (World Bank) hapo haya matatu: muungano wa kimataifa wa kibiashara (WTO) na sanduku la fedha (IMF) na benki kuu ya kiulimwengu (World Bank) yakawa yanatumiwa na madola makubu kama vyombo vya kuingilia na kufinyilia sera za kiuchumi za mataifa mengine, na Lawrence Eagleburger aliyekuwa waziri wa mambo ya kigeni wa Amerika na Michael Kamdiso aliyekuwa raisi

wa sanduku la fedha la kiulimwengu wote hao walikiri kuwa walitumia (IMF) katika kuiangusha nidhamu ya Suherto kupitia kulazimisha sera za upataji wa fedha, na kumnyima mikopo iwapo hatakubali sera hizo, hivyo basi akalazimika kukubali matakwa, na akafanya upataji wa fedha na kwao akaangushwa.

Vilevile ilitendeshwa kazi dori ya (G7) nayo ni mataifa saba ya kiviwanda ikijumlishwa na Urusi, na haya mataifa manane: Amerika, Japan, Ujerumani, Uingereza, Ufaransa, Itali, Canada, na Urusi, mataifa haya yakatawala sera za kiulimwengu za kiuchumi na za kipesa. Na tukiongezea nchi ya Uchina kwa sababu ya uchumi wake mkubwa ulio nao, na kwa nguvu za kinuclear inayomiliki, na idadi kubwa ya wakaazi, na nafasi yake ya kiti cha kudumu katika baraza la usalama, iwapo tutaongezea Uchina kwa sababu ya nguvu hizi inazozimiliki, basi twaweza kusema kwa kufumba jicho, kwamba hakika mataifa makubwa duniani leo ni hizi nchi tisa, lakini kwa sababu ya utofauti wa nguvu za hizi nchi basi twaweza kuondosha nchi mbili miongioni mwao, nazo ni Itali na Canada, kwani hazimiliki nguvu zozote za kisiasa au za "jio-siasa" zinazowawezesha kucheza dori ya kiulimwengu. Kwa hivyo, itabaki kuwa nchi zinazoathiri katika siasa za kiulimwengu ni nchi saba: Amerika, Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Urusi, Uchina, na Japan. Pamoja na kuwa hizi nchi zatafautiana katika kuathiri kwenye siasa za kiulimwengu, kwani nchi tano za mwanzo zalenga kuathiri maeneo tofauti ulimwenguni, pamoja na kuwa Amerika imezizidi nchi nne kati ya hizo. Na nchi ya sita (Uchina) yalenga zaidi kuathiri katika maeneo yake ya kikanda. Na nchi ya saba (Japan) nayo yalenga kuathiri maeneo tofauti tofauti ulimwenguni lakini kwa msingi wa kiuchumi.

Anasema Hoper Vidrin aliyekuwa waziri wa mambo ya kigeni wa ufaransa katika kitabu chake "Rehani za Ufaransa katika zama za utendawazi": *"Hakika nguvu hii ya kipekee (Amerika) ambayo yatawala nyanja zote za kiuchumi, kiteknolojia, kijeshi, kifedha, kilugha na kithaqafa ni hali ambayo haijawahi kutokea katika*

*historia”* kulingania na maelezo yake. Kisha Vidrin anaweka mpangilio maalumu wa nchi kulingana na nguvu na ushawishi kwa kusema: *“Amerika inashikilia nafasi ya kwanza ulimwenguni pasina mpinzani, na baada yake katika nafasi ya pili zinafuatia nchi saba zenye ushawishi wa kiulimwengu, nazo ni: Ufaransa, Uingereza, Ujerumani, Urusi, Uchina, Japan na India kwa sharti ikiwa itapanua mtazamo wao ambao bado ni wa kikanda”.* Na anasema: *“Vipimo vya mpangilio huu ni vingi ikiwemo: pato la nchi, kiwango cha teknolojia, na silaha za nuclear, kisha kiasi cha idadi ya silaha na viwango vyake, na mafungamano na vyama na miundo ya kimataifa, kama vile: baraza la usalama na mjumuiko wa 8, au muungano wa kiuropa, kisha kukuza lugha na taathira ya kithaqafa iliyorithi kutoka kale”.*

Lakini rai ya kina zaidi kuliko rai hii ya Vidrin ni kuwa, baada ya nchi kubwa ya Amerika ambayo haijakaribiwa na nchi yoyote katika mwanzo wa karne ya ishirini na moja, baada yake zinakuja nchi tatu kubwa kihakika, nazo ni: Urusi, Uingereza, na Ufaransa, kisha baada ya hizi tatu inafuatia Ujerumani, na nchi hizi nne zina malengo yake kimataifa katika sehemu nyingi za dunia. Kisha Uchina, nayo ni nchi kubwa katika mipaka ya mizunguko yake ya kimaeneo/kikanda, na lau kama sio ufinyu wa malengo yake ya kimataifa basi ingeshindana na zote au baadhi ya nchi nne zilizotangulia. Ama Japan: nayo ni dola kubwa zaidi baada ya Amerika kiuchumi. Hivyo basi mpangilio wa nguvu za nchi utakuwa ni kama ifuatavyo: Amerika, Urusi, Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Uchina, Japan mtawalia, kwani hizi nchi saba ndizo zinazoweza kuitwa nchi kubwa. Ama India, Canada, na Itali: hizi hazistahiki kuitwa nchi kuu, pamoja na kuwa ndizo zinazofuata hizi saba, na pamoja nazo zinaunda nchi kumi za mwanzo ulimwenguni.

Na kwa kumalizika karne ya ishirini na kuanza elfu ya tatu ya miladi, idara ya George Bush mwana ilijaribu kugeuza misingi ya mchezo, ikawacha sera za ushirikiano zilizoanzishwa na Clinton, na ikaanza kulazimisha nchi kubwa sera zake kwa njia ya nguvu, na

ikajiondoa katika mikataba kadhaa ya kimataifa mfano makubaliano ya Kyoto, na mahakama ya jinai ya kimataifa (ICC), na makubaliano ya Salt ya kupunguza uenezaji wa silaha za kibalistiki, na mikataba mengineo. Na ikachafua zaidi na zaidi mahusiano kati yake na nchi kuu kwa kutokea tukio la 11/Septemba/2001 milai, yalipolipuliwa makao makuu ya biashara za kiulimwengu huko New York na jengo la Pentagon huko Washington, na hilo likapatia msukumo mpya wa kuelekea kwenye upweke, na kutokana na hiyo milipuko ikapata kisingizio cha kupigana kile kilichoiitwa "Ugaidi" basi ikakoloni Afghanistan na Iraq chini ya kisingizio hiki. Na kiburi ya kisiasa ikatawala idara ya kiamerika, na ikabeba sera hii: "***ima uwe pamoja na sisi au dhidi yetu",*** na hizi sera mpya zikaibua radiamali (reactions) za hasira kutoka kwa wauropa na wengineo, na wakawataka waamerika kurudi katika mashauriano na ushirikiano, na wakaituhumu kuwa hiyo (kiburi) ni jinga, lakini waamerika wakakataa kurudia misingi ya ushirikiano na mashauriano iliyofuatwa na Clinton. Na wanaoitwa "wahafadhina wapya" chini ya uongozi wa Dick Chenny aliyekuwa makamu wa raisi, na Ramsfield aliyekuwa waziri wa ulinzi na Wolfwetz naibu wake, na Richard Bearl aliyekuwa raisi wa baraza la sera za ulinzi, na Douglas Faith, na John Bolton, na Condoleza Rice, na wengineo, hawa wakaweza kuathiri maamuzi wa Bush, kwani walitumia uwezo wao wote na ushawishi wao na mashirika yanayowasaidia, ili kutumikia hizo sera.

Na katika yaliyodhihirika zaidi miongoni mwa sera hizi ni kutourudia umoja wa mataifa na sheria zake katika kufanya maamuzi, bali masilahi ya kiamerika ndio yakapewa kipaumbele, na iwapo masilahi yao yatagongana na sheria za kimataifa basi sheria za kimataifa zitapuuzwa, na iwapo hazitagongana basi zitatekelezwa, na ikaamiliana hivyo na baraza la usalama, iwapo itafaulu katika kuitoza maazimio kutoka kwa baraza la usalama basi ni sawa, la sivyo basi itaipuuza na kuachana nayo.

Na Uropa ikiwakilishwa na Uingereza ilijaribu kuizuia idara ya Amerika kuzizunguka sheria za kimataifa, na majaribio haya yakamvutia waziri wa mambo ya kigeni Collin Poul, na raisi Bush pia akavutiwa nayo, lakini kile kikundi cha wahafidhina wapya waliyaangusha majaribio hayo, na Amerika ikaendelea kupuuza sera za ushirikiano, kadhalika ikapuuza kuupatia dori ya kivitendo umoja wa kimataifa.

Lakini pamoja na hayo, idara ya Bush mwana haikuweza kuangusha nchi kubwa, kama vile: Uingereza, Urusi, Ufaransa, na Ujerumani katika kucheza dori zao kwenye siasa za kimataifa, bali siasa zilizofuatwa na idara ya Bush mtoto zilitilia nguvu misimamo ya nchi hizi na wala hazikudhoofika, kwa sababu zilikimbilia kuungana ili kujihami dhidi ya mashambulizi makali ya Amerika kwayo, kwa hivyo Ufaransa, Ujerumani, na Urusi kundi hili kwa kusaidiana na Uingereza kwa siri, nchi hizi kwa mapambano na ulaini zikaweza kuhifadhi nafasi zao kama nchi kuu zenye athari kiasi fulani katika siasa za kimataifa.

****

## [4] DESTURI NA KANUNI ZA KIMATAIFA

Zamani katika kushindania nafasi ya kwanza ilikuwa hakudhihiriki matendo ya kisiasa yaliyofungamana na kanuni ya kimataifa, kwa sababu ya kutokuwepo kwake, bali kulikuwa hudhihirika matendo ya kijeshi kupitia vita, mapigano na kupunguza vipande vya nchi tangu mwanzo wa historia. Na hali ikaendelea hivyo hadi katikati mwa karne ya kumi na nane, ambapo ilipopanuka kanuni ya kimataifa, au kwa usahihi zaidi tuseme: kukapatikana muundo wa kanuni na sheria. Tangu wakati huo vitendo vya kisiasa vikaanza kuchukuwa sehemu muhimu katika mahusiano ya kimataifa, katika kutatua matatizo ya kimataifa. Vikawa vitendo vya kisiasa vyachukuwa mahali pa vitendo vya kijeshi katika kutatuwa matatizo, kusitisha udhibiti wa nchi ya kwanza, na katika kushindania nafasi yake. Tangu hapo ikazidi kuhukumu kwa kanuni za kimataifa katika mahusiano ya kimataifa,

na vitendo vya kisiasa vikazidi kufanywa kuwa ndio chombo cha kutatua mizozo, ima peke yake au pamoja na vita na mapigano. Na hili likamakinika kwa uwazi zaidi baada ya 1919 M, ilipobuniwa umoja wa mataifa, kuhukumiana kwa kanuni na desturi za kimataifa kukazidi. Vitendo vya kisiasa vinavyotekelezwa nchi zote kwa sura jumla, na nchi zinazoshindana na nchi ya kwanza, na pia nchi ya kwanza yenyewe kwa sura makhsusi, zote katika vitendo vyao hutegezea kile kinachoitwa desturi za kimataifa na kanuni za kimataifa. Hivyo basi hapana budi kutupia jicho la haraka desturi za kimataifa na kanuni za kimataifa, ili kufahamu uhakika wa vitendo vya kisiasa na namna ya kufanya vitendo vya kisiasa upande wa kimataifa.

Ama desturi za kimataifa: hizi zipo tangu kuwepo kwa serikali, tawala na miundo mbali mbali, nazo ni mkusanyiko wa misingi iliyojitokeza kutokana na mahusiano baina ya makundi wa wanadamu katika hali ya vita na hali ya amani. Na kwa sababu ya kufuatwa na mikusanyiko ya wanaadamu kwa muda mrefu, basi zikawa ndizo desturi za kimataifa, kisha mkusanyiko huu wa misingi ikamakinika kwa nchi mbali mbali, zikawa nchi zajifunga na kushikamana na desturi hizi kwa hiyari, basi hizi desturi zikawa zimefanana na kanuni. Na kushikamana huku ni kushikamana kwa kimaana wala si kushikamana kwa kimada, ikawa makundi ya wanadamu yanazifuata kwa hiyari na kwa kuogopa rai jumla, na asiyezifuata amejiingiza katika hatari ya kuchukiwa na rai jumla na kuaibishwa kwa hilo. Na kule waarabu kabla ya Uislamu kukubaliana kuzuia mapigano ndani ya miezi mitukufu yazingatiwa ni katika desturi ya kimataifa. Ni kwa sababu hiyo ndipo maqureshi walimkosoa Mtume (s.a.w) pindi kikosi cha Abdillah bin Jahshi kilipomuua Amru bin al-Hadhramy, kikawateka watu wawili wa kiqureshi, na kuchukua msafara wa biashara, hapo wakasimama maqureshi kukosoa hilo, na kueneza kila mahali kwamba Muhammad na maswahaba zake wamevunja heshima ya mwezi mtukufu kwa kumwaga damu ndani yake, kuchukua mali, na kuteka

watu wawili. Basi wakachochea uwadui wa rai jumla dhidi yake kwa kuwa amekhalifu desturi za kimataifa.

Hivi ndiyo ilivyokuwa, baina ya mikusanyiko ya wanaadamu wote kulikuwa na misingi iliyozoeleka wakiifuata katika vita na amani, ikiwemo misingi inayohusiana na wajumbe au wanaoitwa mabalozi, na zikiwemo desturi za ngawira za vita, na nyenginezo. Isipokuwa desturi hizi kuna zile ambazo ni jumla zinazofuatwa na makundi yote ya wanaadamu, kwa mfano desturi kuhusu mabalozi, na kuna desturi zengine ni makhsusi kwa makundi maalumu. Basi desturi hizi zikawa zaendelea kulingana na haja za nchi, tawala, na miundo mbali mbali, yaani kulingana na haja ya mikusanyiko ya binadamu katika mahusiano yao na wengine kama mikusanyiko. Ikawa desturi hizi za kimataifa watu wakihukumiana nazo kwa rai jumla na kuaibishwa anaye zikhalifu, na zikawa zafuatwa kwa kujitolea na kwa hiyari kwa kuathirika kimaana tu na si kwa jengine, kwani hakukuwepo nguvu ya kimada inayozitabikisha. Basi vitendo vya kisiasa vikawa vyatekelezwa na makundi ya wanaadamu kwa kutegemea desturi hizi.

Ama kile kinachoitwa “kanuni za kimataifa” hakika hii ilitokea na kupatikana dhidi ya serikali ya kiislamu iliyokuwa ikiwakilishwa na serikali ya Kiuthmani. Hilo ni kwamba serikali ya Kiuthmani kwa sifa yake kuwa ni serikali ya kiislamu, ilisimama kuipiga vita Ulaya na kuwatangazia Jihad Wakristo wa Ulaya, na kuanza kufungua miji yao mji baada ya mji, ikashika ile inayoitwa Yunani, Romania, Albania, Yugoslavia, Hangari na Austria, mpaka ikakomea kwenye kuta za Vienna. Ikawatia khofu Wakristo wote huko Ulaya, na ikapatikana desturi jumla kwa Wakristo kwamba “jeshi la kiislamu halishindwi” na kwamba Waislamu wanapopigana hawajali mauti, kwa itikadi yao kwamba wako na pepo wakiuwawa, na kuitakidi kwao Qadar na ajal. Wanasara waliona ushujaa wa Waislamu na ukali wa hamasa zao, hali iliyowafanya wao kuwatoroka, hali iliyowarahisishia Waislamu kukomboa miji na kuifanya inyenyekee kwa utawala wa kiislamu.

Na Wanasara wa Ulaya zama hizo walikuwa ni tawala na falume, zikiwa ni serikali zilizotawanyika, kila serikali imegawanyika katika vijimbo, na kila moja wapo ikitawaliwa na bwana wa utawala akigawanyiana na ufalme katika uongozi, hali iliyomfanya mfalme asiweze kulazimisha tawala hizi kupigana, wala asiweze kuzungumza kwa niyaba yao mbele ya wapiganaji kuhusu chochote kinachoitwa mambo ya kigeni. Hilo likawasahilishia Waislamu kupigana na kukomboa. Hali ya serikali za Ulaya ikaendelea kuwa hivyo hadi zama za kati, yaani hadi mwishoni mwa karne ya kumi na sita. Hapo nchi za Ulaya zikaanza kuungana na kuunda jamii moja inayoweza kusimama mbele ya serikali ya kiislamu, likawa kanisa ndilo lenye kuwadhibiti na dini ya kikristo ndio yenye kuwaunganisha. Kwa hiyo zikawa zajaribu kuunda jamii ya kikristo kutoka kwa nchi tofauti tofauti, wakaanza kuweka mahusiano baina yao, basi kutokana na hayo ndipo kukapatikana misingi waliyokubaliana ili kupangilia mahusiano kati yao. Huo ukawa ndio mwanzo wa kupatikana kwa kilichoitwa baadaye kuwa ni “kanuni za kimataifa”. Kwa hivyo, msingi wa kupatikana kwa kanuni za kimataifa ni nchi za wakristo wa Ulaya kukusanyika kwa msingi wa fungamano la ukristo kwa ajili ya kusimama mbele ya serikali ya kiislamu. Hilo likapelekea kupatikana kwa kinachoitwa familia ya kikristo ya kimataifa, na wakakubaliana juu ya misingi maalumu baina yao, miongoni mwazo: ni usawa baina ya watu wa nchi hizi katika haki, na kwamba hizi nchi ziko na mifumo na maadili ile ile ya pamoja, na nyengine ni kwamba serikali hizi jumla zasalimu amri kwa Papa wa kikatholiki na utawala wa juu wa kiroho licha ya tofauti za madhehebu yao. Basi ikawa misingi hii ndio chanzo cha kanuni za kimataifa. Isipokuwa muungano wa serikali za kikristo mwanzoni haukuathiri, kwa sababu misingi waliyokubaliana haikuweza kuwaunganisha, kwa kuwa nidhamu ya kimajimbo iliendelea kuwa kizuizi cha nguvu ya nchi na kuwazuia kujenga mahusiano ya kinje, na kule kanisa kudhibiti serikali kukazifanya kuwa ni wafuasi katika wafuasi wa kanisa na kuzinyima ubwana na uhuru wake. Kwa hivyo kukapatikana mvutano ndani ya serikali ili iwashinde watawala wa majimbo, mwishowe serikali ikashinda na

nidhamu ya kifalme na majibo ikaondoka. Wakati huo huo pia kukaibuka mvutano baina ya serikali na kanisa, uliopelekea hatimae mamlaka ya kanisa katika mambo ya kindani na ya kigeni ukaondoshwa yakawa ni mamlaka ya serikali, baada ya kuwa mwanzo ilikuwa kanisa ndio yenye kutawala, lakini serikali iliendelea kuwa ni ya kikristo bali kikubwa kilichobadilika ni kwamba tu ilipanga mahusiano kati ya serikali na kanisa kwa namna itakayohakikisha kwamba serikali itakuwa huru. Hili lilipelekea kupatikana kwa serikali yenye nguvu ndani ya Ulaya, lakini pamoja na hayo haikuweza kusimama kidete mbele ya serikali ya kiislamu. Basi hali ikaendelea hivyo hadi katikati ya karne ya kumi na saba, yaani mwaka wa 1648 M, ambapo katika mwaka huo serikali za kikristo za Ulaya ziliweka kongamano la **Westphalia**, katika kongamano hili kukawekwa misingi thabiti ya kupangilia mahusiano baina ya nchi za kinasara za Ulaya, na kupangwa familia ya nchi za kinasara itakayopambana na serikali ya kiislamu. Basi hili kongamano likaweka misingi inayofuatwa ya kile kinachoitwa "kanuni za kimataifa", lakini hazikuwa kanuni za kamataifa za kuenea, bali zilikuwa ni kanuni za kimataifa za nchi za kinasara za Ulaya na si nyenginezo. Serikali ya kiislamu ikakatazwa kuingia katika familia ya kimataifa au kuambatanishwa na kanuni za kimataifa. Basi tangu wakati huo kukapatikana kile kinachoitwa jamii/familia ya kimataifa, na ilikuwa imeundwa na nchi za kikristo za Ulaya, zote bila ya kutafautisha, hakuna tofauti baina serikali za kifalme na serikali za kijamhuri, au baina ya serikali za kikatoliki na serikali za kiprotestanti. Na mwanzoni ilikuwa imefungika tu kwa serikali za magharibi mwa Ulaya, lakini kisha serikali nyengine za kinasara za Ulaya zikajiunga, kisha zikaenea serikali za kinasara zisizo kuwa za Ulaya, lakini ikabakia ni haramu kwa serikali ya kiislamu hadi kufikia nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa, ilipokuwa serikali ya kiislamu ipo katika hali ya udhaifu, ikaitwa mtu mgonjwa, hapo serikali ya kiuthmani ikaomba kuingia katika jamii ya kimataifa, na ombi lake likakataliwa, kisha ikakazania sana, basi ikawekewa masharti makali, miongoni mwazo ni kutohukumu na Uislamu katika mahusiano yake ya kimataifa, kuingiza baadhi ya

kanuni za kimagharibi, na serikali ya kiuthmani nayo ikakubali hayo masharti na kuyanyenyekea. Baada ya kukubali kwake kujiondoa kuwa ni serikali ya kiislamu katika mahusiano ya kimataifa basi ombi lake likakubaliwa na ikaingizwa katika jamii ya kimataifa mnamo mwaka wa 1856M, kisha baada ya hapo nchi zengine zisizokuwa za kikristo kama vile Japan nazo zikajiunga na jamii ya kimataifa. Kwa hivyo, kongamano la Westphalia lililofanywa mwaka wa 1648M huzingatiwa kuwa ndilo lililopanga misingi ya inayofuatwa ya kanuni za kimataifa. Na juu ya misingi yake hii vikapatikana vitendo vya kisiasa kwa sura tofauti na kupatikana pia vitendo vya kimataifa vya kipamoja.

Na iliyodhihirika zaidi katika hiyo misingi ni fikra mbili hatari: Kwanza: **Fikra ya uwiyano wa kimataifa.** Pili: **Fikra ya makongamano ya kimataifa.** Ama kuhusu fikra ya uwiyano wa kimataifa: hupitisha kwamba mojawapo ya nchi ikijaribu kujitanua dhidi ya nchi nyengine, basi nchi zengine zitaungana kuizuia isijitanuwe, ili kuhifadhi usawa wa kimataifa ambao utadhamini kuzuiwa kwa vita na amani kuenea. Ama kuhusu fikra ya makongamano ya kimataifa: ni kwamba kongamano hubuniwa na nchi kadhaa za Ulaya, ili kutatua matatizo yao na mambo yao kulingana na maslahi ya Ulaya, kisha fikra hii ikaendelea hadi kukawa na makongamano ya kimataifa makubwa yanayowekwa ili kuangalia mambo ya ulinwengu kulingana na maslahi ya hizi nchi kubwa. Na hizi fikra mbili ndizo msingi wa yale magumu yanayokumba ulimwengu, ambapo imekuwa ni vigumu kuondoa udhibiti wa nchi za kikoloni na wa nchi kubwa.

Mara ya mwanzo zilipotumika fikra hizi mbili ilikuwa ni zama za Napoleon, mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, kwani pindi yalipotokea mapinduzi ya kifaransa, na kuenea kwa fikra zilizo simama juu ya uhuru na usawa na kutambuliwa kwa haki za watu binafsi na haki za mataifa, hapo yaliweza kubadilisha ramani za kisiasa za Ulaya na kukabuniwa nchi mpya na nchi za zamani zikatoweka. Ndipo zilipokusanyika nchi za Ulaya kwa hoja ya uwiyano zikashirikiana dhidi ya Ufaransa. Na baada ya kushindwa

kwa Napoleon hizo nchi zikakusanyika katika kongamano la **Viena** mwaka wa 1815M na kujadili kuhusu kurudisha upya uwiyano na kupanga mambo ya jamii ya kimataifa ya nchi za kikristo: basi ufalme wa Prussia na Austria ukarudishwa, na kukaundwa muungano wa majimbo baina ya Sweden na Norway, na Ubelgiji na Uholanzi zikaunganishwa na kuwa nchi moja itakayozuia kujitanua kwa Ufaransa, na Swizerland ikawekwa katikati daima. Na ili kutekeleza maazimio ya kongamano hili basi serikali zilizoshiriki katika kongamano ziliunda muungano baina yao, nao ni muungano kati ya wafalme wa Prussia, Urusi, na Austria kwa makubaliano ya mfalme wa Uingereza, kisha Ufaransa nayo ikajiunga, yaani ni muungano baina ya nchi kubwa ili kudhibiti nchi zengine. Kisha mwaka wa 1818M uliwekwa mkataba wa Aix-la-Chapelle baina ya Urusi, Uingereza, Prussia, Austria na Ufaransa, ambapo nchi hizi zilikubaliana kuingilia kisilaha ili kuzuia harakati yoyote ya kimapenduzi inayotishia matokeo yaliyokubaliwa katika kongamano la Viena. Hivi ndivyo nchi tano kubwa zilivyojiamulia zenyewe kuwa ndio muundo utakaohifadhi usalama na nidhamu katika jamii ya kimataifa, yaani katika familia ya kimataifa ya kikristo. Kisha zikapanua mamlaka yake hadi zikakusanya baadhi ya miji ya kiislamu baada ya kudhoofika kwa serikali ya kiuthmani. Kisha hizi nchi ziliingilia nchi zengine mara kadhaa kwa hoja ya kuhifadhi amani, zikaingilia Napoli mwaka wa 1821M, zikaingilia Spain mwaka wa 1827, Ureno mwaka wa 1826, na Misri mwaka wa 1840. Pia hizi nchi kubwa zilijaribu hata kuiingilia Marekani, zikajaribu kuisaidia Spain kurudisha koloni zake kutoka Marekani, lakini Marekani kwa kuwa tiyari ilikuwa ni nchi yenye nguvu inayopigiwa hesabu ikazuia hilo, raisi wa Marekani James Monroe akatoa taarifa yake mashuhuri inayojulikana kama taarifa ya Monroe mwaka wa 1823 M kwa kusema: **“Hakika Marekani hatoruhusu nchi yoyote ya Ulaya kuingilia mambo ya bara la Marekani na kunyakuwa sehemu yake”** ndipo zile nchi kubwa zikakoma kuingilia.

Hii ndio asili ya kanuni za kimataifa, na ndizo zilizoleta visingizio vya kuingilia, zikaruhusu nchi kubwa kuzidhibiti nchi ndogo, na ndizo hutegemezewa matendo ya kisiasa yanayofanywa na nchi mbali mbali ili kukidhi maslahi yao au kushindana na nchi ya kwanza (super power). Isipokuwa kanuni hizi za kimataifa zimefanyiwa mabadiliko kidogo, lakini yote ni mabadiliko kwa ajili ya maslahi ya nchi kubwa na kwa ajili ya kupangilia tama zao, au kwa matamshi mengine: ili waweze kugawanyiana manufaa ya ulimwengu baina yao kwa namna ambayo haitopelekea vita na mvutano wa kisilaha. Kwa sababu karne ya kumi na tisa Miladi ilikuwa ni zama za ukoloni, nchi zilimimika ulimwenguni zikikoloni nchi dhaifu, ikawa hutokea mizozo kwa ajili ya ukoloni huu, ambao haukufikia kiwango cha vita vikubwa, lakini Uingereza, Ufaransa, na Urusi zilipogundua kwamba Ujerumani kwa nguvu zake kubwa yazitishia, na zilipoona kwamba itachukua petroli ya miji ya kiislamu Iraq, na kwamba Ujerumani yaitishia Uingereza kuchukua petroli ya Iran na Bara Arabu, basi hapo hizi nchi tatu zikaungana dhidi ya Ujerumani na zikaitangazia vita, na serikali ya kiuthmani nayo ikaingia vitani ikiwa upande wa Ujerumani dhidi ya ule muungano, na hatimae ushindi ukawa ni wa ule muungano, isipokuwa Urusi ilijitoa katika muungano zikabakia Ufaransa, Uingereza, na Marekani. Na Marekani nayo ilirudi kwenye kujitenga kwake, hivyo uwanja ukabakia baina ya Uingereza na Ufaransa. Basi hizi nchi mbili zikabuni umoja wa mataifa ili kupangilia ukoloni baina yao na kuzuia kupatikana kwa mivutano ya kisilaha, hilo ni kwa ajili ya kupanga mambo ya nchi mbali mbali na kuzuia vita baina yao. Na umoja wa mataifa mbali na kuundwa kwake katika hali tata na mgongano, ilikuwa inayumbayumba, kwa kuwa sera za nchi kubwa hazikubadilika, hivyo ikawa hamu ya kila moja wapo katika kongamano la suluhu ni kuhakikisha uwiyano wa nguvu tofauti, kuhami maslahi yao, na kugawana milki za Ujerumani na serikali ya kiuthmani, nchi za kikoloni hazikukubali kuguswa ubwana wake kivyovyote na zikahifadhi koloni zake, na zikazidisha namna nyengine ya ukoloni ulioitwa kwa jina la kuhadaa: “nchi zilizo chini ya uwangalizi”. Ikawa katika athari ya

haya ni umoja wa mataifa kushindwa katika jaribio lake la kuunganisha serikali na kumakinisha amani, ikajaribu kuweka mikataba ya kimataifa ili kudhamini amani, yaani kudhamini mataifa kutozozana juu ya koloni, basi Protokal (rasimu) za Geneva 1924 M zikawekwa chini ya usimamizi wa umoja wa mataifa, malengo yake yakiwa ni kusuluhisha mizozano kwa njia ya amani, na kulazimisha kurudia hukumu kinguvu. Halafu ikawekwa mikataba ya **Locarno** 1925M iliyopitisha ubadilishanaji wa dhamana na kusaidiana, na ukawekwa mkataba wa **Briand-Kellogg** 1928 M ukakataza kukimbilia vita, na mkataba wa **Geneva** 1928 M ambao ulikuwa makhsusi kwa kuhukumu kwa nguvu. Lakini mikataba yote hii haikuweza kuzuia kufeli kwa umoja wa mataifa katika jukumu lake, na mbele ya masikio yake na macho yake vikatokea vita kadhaa, miongoni mwazo ni: vita vya Uchina na Japan mwaka wa 1933 M, vita vya Utaliano na Uhabeshi mwaka wa 1936 M, vita vya Ujerumani na Austria mwaka wa 1939 M, na vita vyake dhidi ya Czechoslovakia mwaka wa 1938 M, kisha dhidi ya Poland mwaka wa 1939 M, mpaka vilipotokea vita vya pili vya dunia mwaka wa 1939 M.

Haya ndio mabadiliko yaliyotokea katika mahusiano ya kimataifa, yakabadilika kutoka kwenye makongamano na kuwa ni taasisi ya kimataifa iliyosimamia kuhifadhi amani ya kimataifa, lakini haya maendeleo hayakubadilisha kitu, kwani nchi kubwa ziliendelea kuzozania ngawira mpaka vilipotokea vita vya pili vya dunia. Baada ya vita vya pili vya dunia zile nchi kubwa zikaona kwamba kuanzisha taasisi ya kimataifa ndio mbinu bora zaidi ya kupanga mahusiano baina yao. Na mwanzoni walifanya kuwa taasisi ya nchi zilizoingia vitani, kisha wakaipanua na kuifanya ni ya kiulimwengu inayorusu nchi zote kuingia, na ikapanga mahusiano ya kimataifa kwa mikataba ya hii taasisi. Kwa hiyo mahusiano ya kimataifa yatakuwa yamebadilika kutoka hatua ya kongamano la nchi kubwa ili kuudhibiti ulimwengu, kugawana ngawira baina yao, na kuzuia isizuke nchi nyengine kubwa, yakabadilika na kuwa taasisi ya kimataifa inayopanga mahusiano

baina yao, na kudhamini udhibiti wa nchi kubwa, na kisha ikawa ni chama cha kimataifa kitakachokuwa kama serikali ya kilimwengu itakayopanga mambo ya serikali za kilimwengu na kuzidhibiti.

Hakika msimamo wa kimataifa baada ya kongamano la Viena 1815M ulikuwa ukionekana katika nchi nne kubwa: Prussia, Urusi, Austria, na Uingereza. Na Ufaransa ilipojaribu kuzitingisha hizi nchi ili kuzitoa kwenye nafasi zao, na kubadilisha ramani ya ulimwengu, basi na msimamo wa kimataifa ukabadilika, na ikawa ndio nchi ya kwanza, hapo zile nchi kubwa na nyenginezo zikaungana dhidi yake na kumaliza tamaa yake, kisha zikashirikiana naye ili kuudhibiti ulimwengu, basi ukawa msimamo wa kimataifa waonekana katika hizi nchi tano. Halafu Uingereza nayo ikaanza kudhihiri kidogo kidogo mpaka ikawa ndio nchi ya kwanza, na Ujerumani ilipojaribu kuzozana na nchi ya kwanza na kunyakuwa mafuta ya miji ya kiislamu, Uingereza, Ufaransa, na Urusi zikaungana dhidi yake na wakapambana nayo na zikamaliza tamaa ya Ujerumani, na zikawa ndizo nchi zenye koloni pekee katika sehemu nyingi za ulimwengu, na fungu la Uingereza katika hizo koloni ni fungu la simba, na ikairidhisha Ufaransa kwa mabaki ya chakula na kuipa baadhi ya koloni. Basi msimamo wa kimataifa ukawa waonekana kwa Uingereza na Ufaransa wakiwa na Italiano, lakini Uingereza ilibakia kuwa ndio nchi ya kwanza, kisha ukapatikana “umoja wa kimataifa”, na umoja huu japo ulibuniwa kwa hoja ya kuhifadhi amani ya dunia, lakini lengo la kihakika la kuundwa kwake ilikuwa ni kuhifadhi nafasi ya nchi ya kwanza, na kuzuia nchi zengine zisishindane nayo, na kuzuia nchi yoyote isiwe kuwa nchi kubwa. Na Ujerumani kwa mara nyengine tena ilipojaribu kushindana na nchi ya kwanza na kuwa nchi kubwa, basi Uingereza na Ufaransa mwanzo ziliungana kisha Uingereza, Ufaransa, Urusi, na Marekani wakaungana na wakaanzisha vita vya pili vya dunia mpaka wakaimaliza Ujerumani.

Isipokuwa matokeo ya vita hivi mara hii vilikuwa dhidi ya Uingereza, kwani ilitoka vitani ikiwa imevunjwa mbavu, nchi iliyotoka mshindi ni Marekani. Kwa hiyo nguvu ya kimataifa

ikabadilika kutoka mkononi mwa Muingereza hadi kwa Marekani, ikawa Marekani ndio nchi ya kwanza, na msimomo wa kimataifa ukawa waonyesha kwamba Marekani ndio nguvu kuu, na muungano wa kisovieti ndio unaozozana nayo, na kwamba Uingereza na Ufaransa ni nchi mbili zilizo daraja ya pili, yaani nchi mbili za upili katika msimamo wa kimataifa.

Lakini baada ya vita vya pili vya dunia kulitokea kitu kipya katika msimamo wa kimataifa, nacho ni ulimwengu wa kimataifa kugawanyika kwenye kambi mbili, na hiki ndicho kilichozidisha ukali wa mivutano wa kimataifa na kusababisha mchanganyiko, kwani msimamo wa kimataifa haukuwa kama ulivyokuwa kabla yake. Ndio, msimamo wa kimataifa kabla ya vita vya kwanza vya dunia ulikuwa umeundwa kimakundi, lakini hakukuwa na kambi. Na pia kabla ya vita vya pili vya dunia ulikuwa umegawanyika mirengo ya kidemokrasia na mirengo ya kidikteta ya Unazi na ufashisti, lakini haukuwa mgawanyiko kwa sura ya kikambi za kimfumo, kwa kuwa unazi na ufashisti si mifumo wala haikufikia kuitwa mfumo, kwa hiyo kabla ya vita vya pili vya kilimwengu hapakuwa na kambi kwa maana ya kimfumo. Lakini baada ya vita vya pili ulimwengu ukawa umegawanyika kimataifa kwenye kambi mbili: kambi ya magharibi, na kambi ya kimashariki, Marekani ikizingatiwa ni nchi ya kwanza katika kambi ya kimagharibi na Urusi (muungano wa kisovieti) ikichukuliwa ndio nchi ya kwanza katika kambi ya mashariki. Na hata kama kambi mbili hizi zilikuwa zavutana kwa msingi wa kimfumo na kuzozania maslahi yanayogongana baina yao, lakini pia zilikuwa zimesimama juu ya msingi wa kimataifa, kwani mfumo peke yake haukuwa ndio sababu ya mgawanyiko wa kambi mbili, bali kuna na maslahi ya kimataifa pia. Ila maslahi haya ya kimataifa yalikuwa katika kambi ya mashariki yaenda kulingana na mfumo wa kikoministi, na kulingana hali zinazolazimu kuenea kwake, na kambi ya magharibi nayo ilikuwa ikienda kulingana na sera za kueneza mfumo kulingana na maslahi ya kitaifa na kizalendo kwa msingi wa kirasilimali unaofanya manufaa ndio kipimo cha vitendo vyote maishani. Ndio

maana twapata katika kambi ya magharibi kuna nchi zisizokuwa na mfumo wake lakini tu maslahi yake yamefungika na maslahi ya mfumo, na haya hayakupatikana katika kambi ya mashariki, kwani nchi zote za kambi ya mashariki zilikuwa ni za kikoministi na katika kambi hiyo hiyo, wala hapakuwa na nchi isiyokuwa ya kikoministi huko, kwa kuwa kiini chake ilikuwa ni mfumo, wakati kambi ya magharibi ilikuwa haina mshikamano, hivyo basi ilikuwa yawezekana kusababisha mwanya katika kambi ya kimagharibi, na yawezekana kutolewa nchi humo hadi kambi ya mashariki, na pia kulikuwa na uwezekano katika kambi ya kimagharibi kuzuka kambi nyengine isiyokuwa hizi kambi mbili ikasimama peke yake na ikawa na athari zake katika misimamo ya kimataifa katika hali ya amani na hali ya vita.

Anayeangalia kwa makini kambi ya kimagharibi atapata kulikuwa na mgawanyiko wa kindani uliotokamana na Marekani kuwa katika nafasi ya nchi ya kwanza, baada ya kuwa hiyo nafasi ilikuwa ni ya Uingereza, wakati Marekani ilipokuwa nyuma imejitenga katika msimamo wa kimataifa. Mgawanyiko huu ulikuwa wazi haukufichika, nao ndio uliokuwa ukicheleweshа kuibuka kwa vita vya kilimwengu. Na nchi ya kwanza katika sera ya kimataifa haikufuata kama kiongozi wa kambi kama ilivyokuwa hali ya Uingereza ilipokuwa ndio nchi ya kwanza, bali ilikuwa ikienda kama kiongozi wa kambi lakini kwa kulazimisha uongozi huu kwa wanajeshi tu kikamilifu, ndio maana katika hii kambi nchi zilizokuwa karibu na nchi ya kwanza kinguvu kama vile Uingereza ilikuwa na chuki zaidi na kuasi sana kuliko hata zile nchi ndogo. Na siri ya hayo yarudia sera ya Marekani yenyewe, kwani baada ya kushinda kwake katika vita vya pili vya ulimwengu iling’ang’ania kuuvua ubwana kutoka kwa nchi zote, kama ilivyoazimia pia kulazimisha ubwana wake ulimwenguni, na ikaghurika na ilipofikia na nguvu zake na wingi wa utajiri wake, mpaka ikajiona kwamba ni lazima itawale ulimwengu mzima, na kwamba mataifa na nchi zote zahitaji msaada wake na kutaka ridhaa yake. Kwa hiyo ikapambana na Ulaya kwa vitendo vya kisiasa, miradi ya kimali, na kisha

baadaye kwa mapinduzi ya kijeshi katika koloni zake haswa Uingereza ambayo ilikuwa nchi ya kwanza na ni nchi yenye koloni nyingi zaidi, kisha Ufaransa, kisha Uholanzi. Nayo Amerika badala ya kuvamia koloni, ilivamia nchi kikoloni zenyewe kwa mradi wa Marshal, na kwa kutoa misaada na madeni, mpaka ilipojimakinisha ikaelekea katika makoloni, ikaanza kuyashika na kuyakalia kidogo kidogo mpaka ikachukuwa koloni zake zote, lakini kwa mbinu tofauti na mbinu iliyoshambulia nayo nchi zengine za Ulaya.

Kwa hivyo tofauti ikaenea baina ya nchi za kambi ya kimagharibi, na tofauti hii si mpya bali ni tofauti ya zamani, kwani ilianza hata kabla ya vita vya pili vya dunia, isipokuwa tu haikuwa tofauti katika kambi moja bali ni tofauti ya kiuchumi baina ya nchi mbili, kisha ikabadilika na kuwa ni tofauti ya kisiasa ndani ya kambi moja. Na chanzo cha tofauti hizi ni matatizo ya kiuchumi na haswa tatizo la petrol, kwa sababu makubaliano yanayoambatana nayo ni baina ya Uingereza na Marekani, na Uingereza kuhitaji kusaidiwa na Marekani ndio kilichopelekea tofauti baina ya hizi nchi mbili na mwishowe baina ya nchi za kambi ya kimagharibi. Hiyo ni kwamba Uingereza baada ya kujimakinisha msimamo baada ya vita vya kwanza vya ulimwengu, na Ufaransa ikawa ndio inayozozana nayo, na mzozano huu ilikuwa wazi, basi Uingereza ikawa yafanya kazi kuidhoofisha Ufaransa kwa kuipa nguvu Ujerumani upande mmoja, na kwa upande mwengine kuzihamasisha harakati za kizalendo na kitaifa katika makoloni, hivyo ikamsababishia shida Ufaransa na kuishughulisha na kujikinga na hatari ya Ujerumani.

Isipokuwa katika msimamo wa kimataifa wakati huo kulijitokeza suala la Italiano, na likadhihirika pia suala la nguvu za Ujerumani zinazotishia msimamo wa Uingereza pamoja na Ufaransa, na ikadhihirika mzunguko wa Roma - Berlin. Basi ikawa hakuna budi lazima Uingereza kuitoa Marekani kutoka katika kujitenga kwake na kumtia tamaa na petroli ya mashariki ndipo kukawa na makubaliano ya petroli. Lakini Marekani nayo baada ya kuanza kuchimba petroli mashirika ya kimarekani yakajua thamani ya petroli ya mashariki, sio tu kulingana na faida ya kiuchumi peke

yake bali pia kwa muundo wa Marekani yenyewe. Kwa hivyo ikaanza kunyakuwa visima vya mafuta na faida za petroli kutoka kwa mashirika ya Uingereza na ikaanza kuizidi, basi kukawa na mashindano baina ya mashirika ya Uingereza na Marekani, na kwa mashirika ya Marekani kuelekea huko mashariki Marekani ikatoka kutoka kujitenga kwake, kisha vilipotokea vita vya pili vya ulimwengu basi Marekani ikasongea mpaka daraja ya nchi ya kwanza, na Uingereza na Uholanzi zikashuka. Ama kuhusu Uholanzi: hakika kwa sababu ya udhaifu wake mambo yake yalimalizika. Ama kuhusu Uingereza: kwa hakika ilipata hasara kwa kupoteza baadhi ya ushawishi wake huko mashariki, na ikapata hasara kwa kupoteza baadhi ya ushawishi wake kwa kuingia bahari ya kati, na ikapoteza baadhi ya ushawishi wake ndani ya baadhi ya nchi ndogo, hali iliyosababisha msimamo wake wa kimataifa kushuka hadi kiwango cha chini, na Marekani ikawa yaendelea kuifuata ili kutokomeza ushawishi wake ulimwenguni kote. Ama kuhusu Ufaransa: hakika baada ya kupoteza koloni zake huko mashariki ya mbali na Afrika mambo yake yalidhoofika, licha ya majaribio ya De Gaulle ya kuinyanyua na kurudisha tena ushawishi wake wa kimataifa, lakini hakuweza kuirudisha kwenye ulingo wa kimataifa kama ilivyokuwa mwanzo, ingawa bado yahesabiwa kuwa ni miongoni mwa nchi kubwa.

Basi kutokana na yote hayo, yabainika kwamba kugawanyika kwa kambi ya kimagharibi na kuvunjika kwake baada ya vita vya pili vya dunia na wakati wa vita baridi kulidhoofisha nchi zake zote isipokuwa Marekani, kwani kwa sababu ya kuzisambaratisha kwake hizi nchi kwa kuchukuwa koloni zake, na kwa sababu ya nguvu ilizokuwa nazo ilibakia kuwa ni nchi ya kwanza na nafasi yake ikazidi kuwa na nguvu. Lakini Uingereza ilibakia kwa kipindi fulani ikitekeleza mivutano ya kisiasa na matendo mengineo ya kijeshi ili kuathiri nafasi ya mshirika wake “Marekani” na kuitikisa ili kuitoa katika nafasi ya nchi ya kwanza, ila kisha baada ya kumbainikia kiasi cha udhaifu wake na jinsi nguvu zake zilivyodorora, hasa katika kupambana na nchi kubwa kama Marekani yenye uwezo

wake wa kijeshi na kiuchumi, basi Uingereza ikatosheka na kujaribu kuhifadhi tu maslahi yake pasi na kuathiri nafasi ya mshirika wake. Kwa hiyo, kambi ya kimagharibi kwa kuizingatia kama kundi ikawa imevunjika, nchi zake zote zimekumbwa na mizozo na mipasuko, na zashindania manufaa, na zafanyiana vitimbi zenyewe.

Ama kambi ya kimashariki: hakika ilisimama juu ya msingi wa kimfumo peke yake hadi mwanzo mwa miaka ya sitini ya karne iliyopita, na ilikuwa ikiongozwa na Urusi (muungano wa kisovieti) kwa muongozo wa kifikra na kijeshi, basi ikawa kwa upande mmoja ina nafasi ya kama mwalimu aliyehusiwa, na kwa upande wa mwengine ina nafasi ya mlinzi na kiongozi. Kwa hivyo basi katika nchi zake hapakuwa na yoyote anayeshindana na Urusi (muungano wa kisovieti) juu ya uongozo wa kifikra na kisiasa, bali hapakuwepo na hata anayethubutu kukosoa sera za kisovieti, na ikitokezea basi ilikuwa ikimalizwa kwa nguvu za kijeshi ikilazimu. Sera ya kambi ya kimasharika tangu zama za Stalin kindani ilikuwa imesimama juu ya msingi wa kutia nguvu nguzo za serikali, na kuandaa nguvu za kijeshi za kivita ili kujilinda na kuvamia kwa wakati mmoja. Na sera yake ya kigeni ilisimama juu msingi kwamba haiwezekani kuishi pamoja kwa amani kati ya urasilimali na ukoministi, kwa hiyo ikawa yaona kwamba ni lazima kuufanya urasilimali kuwa ni mtesi wa kisiasa daima, kwa sababu ni mtesi wa kifikra. Pindi vilipotokea vita vya pili vya dunia, basi Urusi (muungano wa kisovieti) na Uingereza, Ufaransa, pamoja na Marekani walishirikiana vitani, na wakaishi kiujirani kwa mda, lakini hii ilikuwa ni hali tu ya kidharura iliyovuliwa haikuendelea, kwani mara tu baada ya vita kumalizika, vita baridi baina ya Urusi (muungano wa kisovieti) na serikali za kimagharibi vilirudi, japo mshikamano wa kisiasa ulibakia. Lakini mshikamano huu wa kisiasa ulikuwa katika baraza la umoja wa mataifa, katika makongamano ya kimataifa, kuonyeshana uzuri wa kidiplomasia, kuongezea na uwakilishi, ila hayo hayakumaanisha kubadilika kwa sera ya kimsingi ya kikoministi, bali ilikuwa ni mojawapo ya *uslubu* kati ya *uslubu* za kisiasa. Ama sera ya kikoministi kwa kambi ya kimagharibi: msingi wake ni kuwa

yatokana na fikra ambayo muungano wa kisovieti umesimama juu yake, nayo ni kwamba mfumo wa koministi waonyesha kuwa urasilimali na ukoministi haiwezekani kuishi pamoja kwa amani, lazima mwishowe mmoja ushinde mwengine. Na vitabu vyote vya kikoministi vyasema kuwa ni muhali kuepukana na mizozo baina ya hii mifumo miwili, na rai hii ni katika rai wanazoafikiana Lenin na Stalin wala hakuna kati yao aliyetafautiana na mwengine kirai, na wakoministi wote walikubaliana juu ya hii fikra, na hakuna mwanasiasa yoyote wa koministi, awe ni mtawala au la aliyeruhusiwa kufuata sera ya kuishi pamoja kwa amani baina ya urasilimali na ukoministi, kwa sababu ilizingatiwa kwamba atakuwa ametoka nje ya fikra ya kikoministi katika sera za kigeni.

Hiyo ndio hali halisi ya jinsi kambi mbili zilivyokuwa katika upande wa kimfumo, kisiasa, na upande wa kimataifa. Lakini tangu mwaka wa 1961 M kulitokezea mabadiliko ndani ya kambi mbili kwa upande wa kimataifa, mabadiliko yaliyopelekea hali yao ya kihakika kubadilika na kusababisha kupatikana kwa mabadiliko ya misimamo ya kimataifa. Hilo ni kwamba, hizo kambi mbili tangu nusu ya pili ya mwaka wa 1956 M kila moja ilianza harakati na kugaagaa na ikazidi mpaka ikapelekea kupasuka kwa kambi mbili mpasuko kamili, kambi mbili zikawa ni nchi mbili: Marekani na muungano wa kisovieti, pasi na hizi nchi mbili kupigia hisabu yoyote nchi yoyote katika kambi zao.

Ama kwa upande wa kambi ya kikoministi: hakika dola ya kikominista haikusimama juu ya msingi wa utaifa, bali ulisimama juu ya msingi wa kimfumo, yaani ilisimama juu ya msingi wa kuwa serikali ya kikoministi ulimwengu mzima na kwa walimwengu wote. Msingi huu uliilazimu mambo mawili: **kwanza**: daima kuendelea kuwa katika hali ya utayari kindani, na kuandaa nguvu za kiuchumi na za kijeshi kisawasawa kwa ajili ya kueneza ukoministi. Haya yalilazimu mikazo mikali kwa raia kwa sura ya kudumu katika upande wa kisiasa na upande wa kiuchumi. Ndio maana dola ya kikoministi ikaendelea kuwa Jinamizi zito kwa raia wa Urusi, kwa upande wa kiuchumi Mrusi akaendelea kunyimwa mahitaji ya

kistarehe, bali na hata baadhi ya mahitaji ya kimsingi, yote hayo ni kwa ajili ya kueneza ukoministi ulimwenguni. Ama jambo la **pili** lililolazimu dola ya kikoministi: ni kuwa katika hali ya utesi na nchi zote za kimagharibi kwa sifa ya kuwa ni nchi za kirasilimali za kibepari, na kuwasha vita baridi dhidi yao kwa sura ya kudumu, na kujiandaa kuingia vitani vikali kila wakati, na hili ndilo lililofanya ulimwengu kuwa kambi mbili zilizo na uadui wa wazi na namna itakayowapelekea katika vita kila wakati. Isipokuwa ubovu wa kikoministi uliozidi haukuwawezesha watu wake kuendeleza hatua za nadharia yake hadi mwisho, kwani mwishoni mwa miaka ya hamsini ya karne iliyopita, chuo kipya kilifika kwenye utawala, kikaanza kufasiri ukoministi kwa tafsiri mpya inayoendana na maslahi ya Urusi, na ilikuwa ni tafsiri iliyo karibu zaidi na utaifa kuliko kuwa ya ukoministi. Kulingana na sera ya kindani hiki chuo kikaleta faraja kwa watu kwa upande wa kisiasa na wa kiuchumi: wakawakhafifishia watu mikazo, na wakaanza kidogo kidogo kuruhusu bidhaa za matumizi. Na kwa upande wa sera za kigeni: wakaanza kujaribu kujiweka karibu na Marekani, na kuleta mahusiano yenye nguvu nayo, basi mawasiliano ya haraka na ya kisiri yakawa yanaendelea baina ya Urusi (muungano wa kisovieti) na Marekani ili wakubaliane kuzuia vita baina yao, kisha nyanja za hayo mawasiliano zikaendelea kupanuka mpaka zikajumuisha maswala yote ya kimataifa wanayoweza kuwa na tofauti baina yao. Na mawasiliano haya yalipoiva, kukawa na mkutano hatari baina ya Khrushechev na Kennedy mwezi wa sita, mwaka wa 1961 M, yakapatikana makubaliano jumla juu ya maswala yote ya kimataifa. Hapo Urusi (muungano wa kisovieti) ikaachana na fikra muhimu upande wa kimataifa nayo ni fikra ya uadui wa kudumu baina ya ukoministi na urasilimali, na ikakumbatia sera ya kuishi pamoja kwa amani kwa maana yake ya kirasilimali.

Ama kuhusiana na kambi ya kirasilimali: hakika Marekani ilitambua kwamba Uingereza yamuendea kinyume na kwamba yajaribu kushindana nayo juu ya ngawira, na ikaona kwamba hali ya vita baridi vinavyoendelea baina ya kambi ya kimashariki na kambi

ya kimagharibi ni hali inayoangamiza nguvu zake, kwani ni hali isiyokuwa ya kivita ili ishughulike na maandalizi ya kijeshi na iachane na kujikuza kiuchumi, wala sio hali ya amani ili ijishugulishe na kukuza uchumi na iachane na maandalizi ya kijeshi, bali vita baridi ni hali baina ya amani na vita, nayo hutumia kiwango kikubwa katika mali za serikali katika kujiandaa kijeshi kwa vita visivyojulikana kwamba vitatokezea au la. Mbali na hayo pia Marekani ikaona kwamba Uingereza yenyewe kumbe ndio yenye kuwasha moto wa hivi vita baridi na kuviendeleza kwa kuwa lengo lake katika hayo ni kubakisha Marekani katika hali itakayoimaliza nguvu na mali yake, ili uweza wake udhoofike polepole, ili kusiwe na usawa wa kimataifa wakati huo. Basi Marekani ikaona kwamba maslahi yake ni kujikurubisha na Urusi (ukoministi) dhidi ya Uingereza (urasilimali). Na kwa kuwa ufisadi wa kirasilimali umezidi pia, kwa sababu kwa warasilimali maslahi ndio kilele cha cha juu zaidi katika ngazi ya thamani, ambapo hakuna thamani thabiti kwao bali ni kuyapapia tu maslahi ya kimada, hivyo basi Marekani pia ikawa yajaribu kubana sehemu ya mgawanyiko baina yake na Urusi (muungano wa kisovieti), ikaanza kujaribu kuingia naye katika mazungumzo, na hayo ni tangu nusu ya pili ya mwongo wa sita katika karne iliyopita, yaani tangu zama za Eisenhower na kabla kuja kwa Kennedy, na Kennedy alipokuja alikimbilia kutimiza hatua za kukaribiana baina ya Marekani na Urusi, kwani haukupita mwaka na baadhi miezi tangu alipochukuwa utawala mpaka kukawa na mkutano wa Viena mwezi wa sita 1961 M baina yake na Khrushchov, yakapita makubaliano jumla juu ya maswala jumla ya kimataifa inayowezekana kuwa na tofauti baina yao. Na kwa kupatikana hayo, Marekani nayo mwishowe ikaachana na fikra muhimu iliyokuwa nayo kwa muda unaokaribia nusu karne, nayo ni fikra ya kuumaliza ukoministi na kuundoa kutoka ramani ya ulimwengu. Ikaanza kujikurubisha na muungano wa kisovieti katika kile kilichoitwa mkataba wa kuishi kwa amani, na ikaendelea hivyo kwa muda unaozidi miongo miwili hadi alipokuja Reagan kutawala Marekani miaka ya themanini, ambapo alirudia kuhuisha upya kazi ya kuumaliza muungano wa kisovieti.

Hivi ndivo maslahi ya viongozi wa kambi mbili yalivypkubaliana, ili waendelee kuwa wenye usemi wa kimataifa na kuzuia kutokezea wasiokuwa wao. Na pia yaonyesha kwamba waliafikiana juu ya siasa ya kumzingira Mchina, na kumtoa Muingereza kwenye koloni zake na kung’oa ushawishi wake huko mashariki ya kati na ya mbali, na kuzuia Ujerumani kurudi kuwa nchi ya kinuklia. Kisha wakakubaliana juu ya kuishi kwa amani baina yao au kile kilichoitwa mkataba wa amani, na kadhalika kutokimbilia kutumia nguvu za kijeshi katika kutatua mizozo baina yao. Wakakubaliana pia juu ya kugawana ulimwengu baina yao na kupanga maeneo ya ushawishi wa kila mmoja wao, pamoja na kiasi cha ulazima wa kusaidiana kati yao katika maeneo yao, na kwa maana nyengine hizi nchi mbili zilikuwa washirika wawili walioungana na kuwa nguvu moja ya kilimwengu, na kutokana na hayo makubaliano yote hali ya ulimwengu na msimamo wa kimataifa zote zilibadilika.

Ama kuhusu msimamo wa kimataifa: hakika ulimwengu haukuwa tena kambi mbili zenye kuzozana kisiasa na kiuchumi, na mahusiano baina yao kuzungukwa na matatizo mengi kama hali ilivyokuwa kabla ya 1961 M, ndio ulimwengu ulikuwa kambi mbili kifikra kwani fikra ya kikoministi ilibakia kwa kipindi hicho, ikibebwa na serikali za kikoministi, na fikra ya kirasilimali ikionekana katika serikali za kirasilimali. Kwa hivyo fikra mbili haziwezi kupatanishwa, basi kwa upande huu kweli ulimwengu ulikuwa kambi mbili bila shaka, lakini kwa upande wa kimataifa kambi mbili ziliondoka, ulimwengu wote ukawa ni nguvu moja inayowakilishwa na Marekani na Urusi, wakawa mababe wawili hawa peke yao ndio wenye kudhibiti ulimwengu na Marekani akiongoza kwa kuwa katika nafasi ya nchi ya kwanza.

Kwa hivyo basi kambi mbili ya kimashariki na ya kimagharibi ziliondoka na hazikubakia kambi za kimataifa ulimwenguni. Na kwa hakika msimamo wa kimataifa ulibadilika kimsingi, ukarudi kama ulivyokuwa kabla vita vya kwanza vya dunia, yaani kila nchi

imekuwa kivyake na kila serikali yenda mbio kuchukua ngawira na kudhoofisha serikali nyengine, na mikwaruzano ikawa ni baina ya serikali na serikali wala sio baina ya kambi na kambi. Na tofauti baina ya hali katika kipindi cha mapatano baada mkutano wa Viena na hali kabla vita vya kwanza vya dunia: ni kwamba msimamo wa kimataifa ulitawaliwa na nchi mbili kubwa na nchi zilizobakia zajaribu kujikinga na shari za hizo nchi mbili, na kuungana baina yao ili kuwa nguvu moja itakayosimama mbele ya hizo nchi mbili kuu, tofauti na hali ilivyokuwa kabla vita vya kwanza vya dunia, ambapo nchi kubwa zilikuwa takriban zakaribiana kinguvu, ingawa nchi ya kwanza ilikuwa na nguvu zaidi ya zote, na kukaribiana huku kulipeleka kuharibika kwa mizani ya nguvu na kusababisha mivutano juu ya ngawira, hali iliyopelekea kuwasha moto wa vita vya kwanza dunia.

Lakini katika kipindi cha mapatano, nguvu za nchi mbili zilizoungana zilikuwa zimezidi sana nguvu za nchi yoyote ile katika serikali za kilimwengu, au hata zaidi ya nguvu za nchi zote zikijumlishwa pamoja. Ndio maana havikuibuka vita vikubwa vya kilimwengu kwa maana inayojulikana zamani, bali hapakuwepo na hata uwezekano wa nchi zengine kuungana na kusababisha mizozano itakayopelekea katika vita vya kilimwengu. Vilevile pia hali ya msimamo wa kimataifa katika kipindi cha mapatano ni tofauti na ilivyokuwa kabla ya vita vya pili vya dunia. Kwa sababu kabla ya vita vya dunia vya pili nchi zilikuwa zimetengana, japo zilikuwa kama muundo wa miungano lakini kwa hali yoyote ile mwanzoni nguvu zilikuwa zakurubiana, kisha kukakosekana usawa: Ujerumani, Italiano, na Japan zikawa na nguvu, wakati Uingereza na Ufaransa hazikuwa na nguvu, na Marekani ilikuwa imejitenga kando. Ukosefu huu wa usawa katika nguvu kukaisukuma Italiano, Ujerumani na Japan kila moja kivyake katika kuchukua nchi kwa njia ya kivita. Na kuendelea kwa hali hii kukapelekea mikwaruzano mikali iliyosababisha vita vya pili vya dunia. Kinyume na hali ilivyokuwa katika kipindi cha mapatano, kwani msimamo wa kimataifa ulikuwa ukionekana kwa wababe wawili wakubwa na

makubaliano baina yao, na hiyo ni hali isiyoruhusu kutokezea mivutano ya kimataifa itakayopelekea katika vita vya kilimwenu, bali iliruhusiwa tu mvutano baina ya baadhi ya nchi na nchi au baina ya baadhi ya serikali kwa nyengine, lakini mivutano kama hii hata ikisababisha vita basi ni vya kimaeneo tu, na nguvu za zile nchi mbili kuu zilikuwa zatosha kuzima hivyo vita wapendapo.

Lakini sera ya mapatano iliyoanza na makubaliano ya 1961 baina ya Marekani na muungano wa kisovieti, hii sera haikumaanisha kumalizika kwa mvutano baina ya urasilimali na ukoministi, isipokuwa tu kulikuwa na visingizio na sababu zake, kwani pande zote mbili zilikuwa zimechoshwa na vita baridi kwa kujiandaa dhidi kitu kisichojulikana kuwa kitatokezea au la, basi zikaelekea katika mapatano na kugawana ulimwengu, ili kila mmoja wao aweze kupata na kupanga mambo yake ya kindani. Na kwa kumalizika vita vya Vietnam mkataba ukaanza kukosa umuhimu wake. Kwani Ufaransa ilitolewa katika koloni zake ikabidi kurudia Ulaya ili kupata nguvu. Ama kuhusu Uingereza: hakika ilihisi udhaifu wake basi nayo ikaanza kujaribu kujijenga nguvu na Ulaya ili kuokoa kinachowezekana kuokolewa. Na muungano wa kisovieti ikawa ni nguvu kubwa ya kijeshi na kimkakati, na ikawa na mafanikio ya juu katika upande wa anga, na ikaweza kupanua uwepo wake katika maeneo ya mbali na maeneo yake muhimu, hivyo ikawa ni nguvu ya kilimwengu yenye kuathiri.

Makundi mengi ya kisiasa -hasa ya mrengo wa kulia na walibrali - yakaanza kushambulia sera za mapatano, na Marekani ikaanza kujiondoa kwenye maafikiano. Na sababu ya hilo ni kwamba muungano wa kisovieti ulijenga katika kivuli chake nguvu kubwa yenye maangamizi jumla, hadi ikawa ndio tishio hatari kwa Marekani, hivyo zama za Marekani kuwa na amani ya kiujumla zikamalizika, bali ikawa amani yake yasimama juu ya ukomeshaji wa kubadilishana, yaani kufungamanisha hatima na hatima nyengine. Ikawa katika athari zake za kando ni nchi za Ulaya kuanza kujitenga na Marekani, na zikawa zafuata sera zake tofauti na za Marekani katika kuamaliana kwao na muungano wa kisovieti, hali

iliyomfanya Kissinger kuuita mwaka wa 1973 M kuwa ni mwaka wa Ulaya. Na sababu ni kuwa, kwa kuingia mwaka 1973 na kutiwaa saini mkataba wa Paris kuhusu hali ya Vietnam, Marekani na Urusi (muungano wa kisovieti) walikuwa washaitoa Ufaransa kwenye koloni zake nyingi, na wakailazimisha Uingereza kuziondoa kambi zake nyingi ulimwenguni na kuitowa kutoka kuloni zake nyingi, na Uchina ikawa ishazingirwa, kwa hiyo basi yale makubaliano yakawa yamekosa visingizio. Wala hapana shaka kwamba Marekani ilitoka kwenye makubaliano kama nguvu kubwa ya kijeshi zaidi ya ilivyokuwa awali, kama ambavyo pia ilikuwa na ushawishi mkubwa wa kisiasa kwa sababu ya kuitoa Uingereza, Ufaransa, na Uholanzi kutoka katika koloni zake na kuchukua mahali pao. Kwa hiyo mapatano yakawa yameshaleta matunda yake kulingana na Marekani, hapo hilo halimaanishi kukosekana mabaya, lakini mabaya yake hayakuwa ya kulinganishwa na mazuri yake kwa upande wa Marekani. Lakini katika mwaka wa 1973 mapatani yalikosa visingizio vyake, basi Marekani ikageukia kumaliza athari zake mbaya zilizotokana na sera ya mapatano, na ikawa katika vipaumbele vyake ni: kuwekea mkomo muungano wa kisovieti katika kutanua kwake maeneo ya ushawishi wake mbali na maeneo yake muhimu, kuugandamiza muungano wa kisovieti kiuchumi, na kurudisha Ulaya kuwa chini Mwavuli wa Marekani.

Ama kuhusu muungano wa kisovieti kukunjua ushawishi wake nje ya maeneo yake muhimu, kwa hakika ilikuwa dhaifu, na sababu ni udhaifu wa uchumi wa kisovieti kwani ilikuwa rahisi sana kuung’oa wakati wowote, lakini ulikuwa waupatia muungano wa kisovieti haki ya kushiriki katika kadhia za kimataifa, na hili ni kinyume na inavyotaka Marekani, kwani ilikuwa yaona kwamba sera ya makubaliano ni njia ya kuudhibiti muungano wa kisovieti, sio kuufanya kuwa mwenza wa Marekani. Kwa hiyo Marekani ikaona ulazima wa kuutoa huo muungano kutoka kwenye maeneo anayoyatawala nje ya maeneo yake muhimu.

Ama kuhusu kuugandamiza muungano wa kisovieti kiuchumi: Marekani iliona kuingia katika kushindana na muungano wa kisovieti katika kuwa na silaha kutaugandamiza kiuchumi na kuupelekea kuporomoka. Basi hayo yakaanza katika miaka ya sabini zama za Carter, lakini likazidi na kuwa tukio lililojitokeza wazi zaidi katika sera a idara ya Reagan, kwani yeye ndie aliyechochea mashindano ya kisilaha, akafuata mpangilio uliowekwa na mtangulizi wake ambaye ni Carter, muhimu zaidi ni makombora ya M-X yanayosonga, naye (Reagan) akazidisha kwa kutabanni mpango wa kujihami wa kistratejia au vita vya nyota. Na mkakati huu wahitaji kuundwa kwa teknolojia ya kinga dhidi ya makombora ya maadui. Hali iliyoufanya muungano wa kisovieti kudhani kwamba ghala lake la silaha za kinuclear hazitakuwa na umuhimu vitakapotibuka vita vya kinuclear, na kwamba hii itamaanisha kukosekana kwa usawa wa nguvu na kuishajiisha Marekani kutekeleza vita vya kinuclear. Basi muungano wa kisovieti ukijisukuma kujaribu kuboresha mfumo wake wa kujihami. Hilo ni kwamba kulingana na data zilizopo haiwezekani tena wa kushindana katika upande wa silaha za kushambulia, hivyo mashindano yakatoka katika hatua ya kuendeleza mbinu za silaha za uvamizi hadi kuendeleza mbinu za silaha za kujihami. Pamoja na kuwa mikakati ya Reagan ya kujihami au vita vya nyota japo mwanzoni ilikuwa na maendeleo, lakini haikufikia kiwango cha kusemwa kwamba wamefikia teknolojia inayoweza kujenga kinga hii ya makombora, kwani imethubutu kisayansi kwamba ni kama haiwezekani kufikia kuwa na makombora ya Laser inayoweza kuelekeza sawa miale ya Laser kwa kiwango kinachotakikana, ili kuweza kuharibu makombora yanayopita mabara yakiwa angani kabla ya kurudi kwake kwenye maeneo ya anga, lakini Reagan alitangaza haraka kutabanni kwake mbinu hii ya kujikinga, pamoja na kuwa ilikuwa haijafikia hatua za nzuri za kuiboresha. Basi kwa hatua hii akaweza kuubabaisha muungano wa kisovieti, na kuuvuta katika mashindano ya kuboresha silaha mpya, hali ya kuwa uchumi wake hauhimili, uchumi ambao tiyari ulikuwa wayumbayumba. Haya ni licha ya kuwa hii mikakati ya vita vya nyota yakhalifu

mkataba uliotiwa saini na Marekani na muungano wa kisovieti mwaka wa 1972 M, unaohusiana na makombora yanayokinga dhidi ya makombora. Lakini Reagan alikazania kuwa hii mikakati yake haigongani na huo mkataba, akachochea msimamo dhidi ya muungano wa kisovieti. Na yaweza kusemwa kuwa kwa kitendo chake hiki atakuwa amemaliza mwisho wa ishara za sera ya mapatano.

Vitendo hivi vya Reagan viliuvuta muungano wa kisovieti kwenye mashindano mapya ya kisilaha, japo mara hii ni kwa kuendeleza mfumo wa silaha za kujihami na si ya kushambulia. Reagan alifanya hayo ili kuugandamiza muungano wa kisovieti kiuchumi na kuulazimisha kurudi katika maeneo yake muhimu waliyokubaliana katika mkataba wa 1961 huko Viena, au kuuporomosha kabisa uchumi wake.

Ama Ulaya ambayo ilipatiliza kipindi cha mapatano ili kujikomboa kutokana na udhibiti wa Marekani, wanasiasa wa kimarekani walifanya vitendo vyao ili kuirudisha chini ya mwavuli wa Marekani baada ya kukaribia kuuwacha huu mwavuli tangu 1973 mwaka ambao Kissinger aliuita kuwa ni mwaka wa Ulaya, pale nchi za Ulaya zilipoanza kukariri kwamba maslahi yao sio maslahi ya Marekani, na zikaanza kujitenga kuingia vita zikiwa upande wa Marekani kwa ajili ya kutetea maslahi ya Marekani peke yake. Basi mwaka wa 1982 Marekani ikaeneza ndani ya Ulaya makombora yake aina ya Perishing-2 na Cruz yenye upeo wa kati kwa kisingizio kwamba muungano wa kisovieti waeneza makombora ya masafa ya kati ndani ya Ulaya na baada ya kukataa kuyaondoa. Kwa hiyo Marekani ikafungamanisha usalama wa nchi za Ulaya na usalama wake, kwa hoja ya kuzitetea, na ikafungamanisha hatima ya Ulaya na hatima ya Marekani, kwa namna ambayo Ulaya haitoweza kujiondoa.

Wakati Reagan aliposhinda kipindi cha pili cha uraisi, Gorbachev akawa ndie kiongozi wa muungano wa kisovieti mwaka

wa 1985, na Gorbachev alipofika uongozini tu basi na muungano wa kisovieti ukaanza ku kujiuzulu maslahi yake kwa ajili ya maslahi ya Marekani, basi kwa hilo muungano wa kisovieti ukawa wayumbayumba ukielekea kuporoka. Ndio maana Reagan alikuwa mkweli alipokuwa anaondoka Nyumba nyeupe alipoulizwa kuwa ni jambo gani analoamini kuwa ndio mafanikio yake muhimu zaidi kama raisi? Reagan akajibu: *''Wanasema kwamba Mimi nimeshinda vita baridi''.*

Hivi ndivyo yalivyotokea mabadiliko ya kimsingi katika misimamo ya kimataifa wakati Reagan akiondoka Nyumba nyeupe, kwani sera ya mapatano ilikuwa ishamalizika kabisa, na muungano wa kisovieti ukawa wayumbayumba kwa sababu ya kuingizwa katika mashindano ya kisilaha, kugandamizwa kiuchumi, kuongezea na Marekani kuwanga mkono waliojitenga na Soviet na kuunga mkono safu za wapinzani, na ikaanzisha kampeni za vyombo vya habari vya kimataifa kupigana na aidiolojia ya kisovieti, ikiwa na maana kwamba Marekani haitambui tena kitu kinachoitwa mapatano. Bali zaidi, Marekani ilimimina mashambulizi ya siasa, kiuchumi, na kiaidiolojia dhidi ya muungano wa kisovieti, yaliyosababisha kudhoofika kwa ushawishi wake au majaribio yake ya kuwa ushawishi ulimwenguni nje ya maeneo yake muhimu, na kupelekea kuporomoka kiuchumi kindani, mbali na kudhihiri upinzani dhidi ya sera za kisovieti ndani ya muungano wenyewe wa kisovieti na ndani ya kambi ya kimashariki kwa sifa jumla, na kote ulimwenguni, kisha ikaendelea hivyo hadi muungano wa kisovieti ukaporomoka mwanzoni mwa miaka ya tisaini katika karne iliyopita, ikawa Marekani ndio dola ya kwanza bila ya kuwa mpinzani anayekaribiana naye, kama hali ilivyokuwa mwanzo.

Kwa ufupi: hali za nchi ulimwenguni ziligeuka, kwa sababu zamani nchi zilizokuwa zikidhibiti ulimwengu ni dola ya kiuthmani, Urusi, Austria, Uingereza na Ufaransa, serikali hizi ndizo zilizokuwa zikiendesha mambo ulimwenguni, kutishia amani na

kuamua vita. Kisha ikapatina Marekani, ikaziwekea mipaka nchi hizi na kuzifungia ndani ya ulimwengu wa kale na kuziweka mbali na Marekani. Kisha Austria ikaanguka ikawa haizingatiwi tena kuwa ni nchi kubwa, zikabaki nchi tano: Urusi, Ujerumani, Uingereza, Ufaransa na dola ya kiuthmani. Halafu serikali ya kiuthman nayo ikaanguka zikabakia nchi kubwa zenye kutawala ulimwenguni ni nne: Urusi, Ujerumani, Ufaransa na Uingereza. Na baada ya vita vya kwanza vya dunia, Urusi ikawa imejitenga kwa kusimamiwa na ukoministi na kutawaliwa na vyama vya kikoministi. Kisha Ujerumani nayo ikaanguka kwa kushindwa katika vita vya kwanza vya dunia, nchi kubwa zikawa ni mbili: Uingereza na Ufaransa. Uingereza ikawa ndio yenye kuendesha mambo ulimwengu mzima isipokuwa Marekani, na Ufaransa ikawa iko nyuma ya Uingereza. Na mwanzoni mwa mwongo wa nne, yaani mwaka wa 1933, chama cha Nazi kikashika uongozi, kikafanya kazi kuinua Ujerumani mpaka ikarudi tena kuwa nchi kubwa, na kabla ya hapo kidogo Mussolini alinyakua uongozi Itali na akafanfa kazi kuinua Itali mpaka ikawa yazingatiwa ni katika nchi kubwa. Na nyota ya Japan ikadhihiri na ushawishi wake ukapanuka baada ya kuwa nchi ya kiviwanda, basi ikawa nayo yachukuliwa ni katika nchi kubwa. Kisha nguvu za muungano wa kisovieti zikarudi na kuonekana tena katika ulingo wa kimataifai, ikarudi tena kuwa ni nchi kubwa, hivyo nchi kubwa zikawa ni sita: muungano wa kisovieti, Ujerumani, Uingereza, Ufaransa, Italiano na Japan, wakati Marekani ikiwa bado ipo katika kujitenga. Baada ya vita vya pili vya dunia, Ujerumani, Utaliano na Japan zikashindwa na hizi nchi tatu zikadhoofika, Marekani nayo ikatoka katika kujitenga kwake ikaanza kushiriki katika mambo ya kilimwengu, na ikahifadhi Uingereza na Ufaransa kuendelea kuwa ni nchi kubwa, kwa hiyo nchi kubwa zikawa ni nne: muungamo wa kisovieti, Uingereza, Ufaransa na Marekani. Kisha baada ya muungano wa kisovieti na Marekani kufunga mkataba mwaka wa 1961 Uingereza na Ufaransa zikatoka katika kuzingatiwa kwake kuwa ni nchi kubwa, hivyo nchi kuu zikawa ni mbili tu: muungano wa kisovieti na Marekani, kwa kupatana kwao zikawa nguvu moja, ukawa ulimwengu una nguvu

moja kuu iliyoundwa na serikali mbili, hivyo ulimwenguni hakukuwa na nchi zengine kuu zinazodhibiti dunia mbali na hizi mbili hadi kabla kidogo ya kuporomoka kwa muungano wa kisovieti.

Kisha muungano wa kisovieti ukavunjika, na Urusi ikarithi uwezo wake na nguvu zake za kijeshi, isipokuwa nayo ilikuwa yasumbuka kutokana na kufilisika kisiasa, kukosa utambulisho wa kimfumo, mbali na matatizo ya kindani ya kiuchumi na kisiasa, kwa sababu ya hali iliyoachwa nyuma na ukoministi, na kupelekea athari yake katika siasa ya kilimwengu kurudi nyuma.

Kwa hiyo Marekani ikawa ndio nguvu kuu ya kipeke yake ulimwenguni, yenye uweza wa kushika usukani wa sera za kilimwengu pasina kuwa na mpinzani wa kushindana naye katika hiyo nafasi, hata kama nchi tatu za Ulaya (Ufaransa, Uingereza na Ujerumani) zilijaribu na wanajaribu kuingia katika mduara wa mashindano, kama ilivyotokea wakati wa uvamizi wa Iraq mwaka wa 2003, na kama ilivyotokea katika mikutano yao kuhusu kuunda nguvu ya Ulaya mbali na muungano wa NATO mwaka huohuo, na kujadili kwao mradi wa Marekani kwa mashariki ya kati uliotolewa katika nchi kuu nane za viwanda mwezi wa sita mwaka wa 2004 M, (pamoja na yote hayo) lakini hakuna ila ni majaribio tu yasiyofika katika kuitwa kuwa ni kushindana kunakojulikana katika kwenye nafasi ya nchi ya kwanza, bali ni kujaribu tu kushirikiana na Marekani kwa kiwango fulani katika kuathiri sera za kimataifa.

Na yatakikana ieleweke kwamba inayodhibiti ulimwengu katika zama zote ni nchi zilizo kubwa na haswa nchi ya kwanza. Na ifahamike kwamba nchi kubwa hudhoofika na nchi zengine huchukua mahali pake na zikabadilisha msimamo wa kimataifa. Pia ijulikane kwamba mabadiliko haya katika hali ya kimataifa ndio yanayobadilisha hali ya mahusiano baina ya nchi kubwa na kutofautisha kati ya nguvu na udhaifu za nchi ya kwanza na nchi nyengine zinazoshindana nayo. Hivyo msimamo wa nchi ya kwanza

hudhoofika kama ilivyotokea kwa Uingereza wakati Ujerumani iliposhindana nayo, au hupata nguvu kama ilivyotokea kwa Marekani ilipomaliza ushawishi wa Uingereza na Ufaransa na kubakisha uwezo wa kuathiri kimataifa kwake na kwa Urusi tu baada ya mkutano wa Viena, au wakati mwengine nchi ya kwanza hubaki bila ya mpinzani katika hiyo nafasi kama ilivyotokea baada ya kuporomoka kwa muungano wa kisovieti. Kwa hivyo basi hapana budi kufahamu yote hayo tena kwa ufahamu wa kina na wa kuendelea ili mtu aweze kufahamu siasa za kimataifa.

****

## [5] SABABU ZA MVUTANO BAINA YA NCHI:

Tangu mwanzo wa historia hadi Qiyama kusimama, hakuna mvutano wa kimataifa unaotokea isipokuwa ni kutokana na moja wapo ya sababu mbili kuu: Ima ni kupenda ubwana na ufahari, au kufuata maslahi ya kimada. Na kupenda ubwana: ima ni kutaka ubwana wa umma na raia, kama ilivyokuwa hali ya Ujerumani chini ya chama cha Nazi na Utaliano chini ya chama cha ufashisti, au ni kupenda ubwana wa mfumo na kuueneza, kama ilivyokuwa hali ya serikali ya kiislamu kwa muda wote unaokaribia miaka 1,300, na kama ilivyokuwa hali ya serikali ya kikoministi kwa muda wa miaka thalathini katika umri wake kabla ya kuporomoka mwanzoni mwa miaka ya tisini katika karne iliyopita, baada ya miaka sabini tangu kuanzishwa kwake.

Ama msukumo wa kuwekea mpaka ukuwaji wa nguvu za serikali/nchi nyengine, kama zilipoungana nchi kadhaa dhidi ya Napoleon, na kama zilivyoungana pia dhidi ya serikali ya kiislamu, na kama ilivyotokea kwa Ujerumani ya chama cha Nazi: hakika msukumo huu waingia katika kupenda ubwana, kwa kuwa vitendo hivi ni kusimama mbele ya ubwana wa mwengine.

Kwa kuondoka serikali ya kiislamu, na kuondoka serikali ya kisovieti, imekuwa sababu ya mivutano inayotawala ulimwengu

mzima ni kukimbilia maslahi ya kimada tu, nayo itaendelea hivyo hivyo mpaka itakaporudi serikali ya kiislamu kama serikali kuu inayoathiri mivutano ya kimataifa, na kwa kurudi kwake irudi tena ile sababu ya kupenda ubwana wa mfumo na kuueneza.

Msukumo hatari zaidi unaopelekea mvutano baina ya nchi ni msukumo wa ukoloni kwa aina zake zote, kwa sababu ndio uliosababisha vita vidogo vidogo, na ndio msukumo uliosababisha pia vita viwili vya kilimwengu, ndio uliosababisha vita vya Ghuba, vita vya Afrika, vita vya Afghanistan, Iraq, na ndio bado wenye kusababisha majanga na matatizo ulimwenguni. Bali hata mashindano, chuki, na mivutano ya wazi na iliyofichika iliyopo leo baina ya Marekani, Uingereza, Ufaransa, na Urusi, kuhusu kadhia za Iraq, Afghanistani, Mashariki ya kati, kadhia nyenginezo za kimataifa, hakika yote hayo ni kwa ajili ya ukoloni, na kwa ajili ya kudhibiti maslahi na mapato. Kwa hivyo, sasa hivi ukoloni ndio unaotawala katika mivutano ya kimataifa, inayojumlisha kuzozania malighafi, mivutano wa ushawishi, na kushindania kudhibiti kwa sura na sampuli zake zote.

Hakika kukimbilia manufaa ya kimada, na haswa ulafi wa kikoloni, ndio ulioleta mivutano ya kisiasa baina ya nchi kuu, mivutano hii ikasababisha vita vya kimaeneo na vita vya kilimwengu. Na kwa ajili ya kuepuka vita hivi kukabuniwa kile kilichoitwa “amani na usalama wa kilimwengu” na ikapatikana hoja ya kuhifadhi usalama na amani.

Na hiyo hoja ya kuhifadhi usalama sio mpya ulimwenguni, bali ni hoja ya zamani ilipatikana tangu mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa miladi, kwani mkataba ulioitwa mkataba wa **Ex-lachaple** mwaka wa 1818 baina ya nchi tano kuu wakati huo, mkataba huu ulipatikana kwa hoja ya kuhifadhi usalama, na kupitia mkataba huu -au muungano huu - hizo nchi tano kuu zikajifanya ndio walinzi wa amani na nidhamu katika jamii ya kimataifa, na kuingilia mambo ya nchi zengine kila watakapohisi (kulingana na

madai yao) kwamba kuna tishio la amani au nidhamu. Hoja hii ya kuhifadhi amani na nidhamu katika jamii ya kimataifa, ndio baadaye ilifanywa kisingizio cha nchi kuu kuingilia mambo, na kuwa sababu ya vita, na ikawa ni nembo ya kimataifa inayotumiwa kama chombo cha kuhifadhi ukoloni na ushawishi wake.

Na huo usalama umekuwa ukihifadhiwa -kwa madai yao - kwa njia ya muungano wa nchi kuu, au kwa njia ya makongamano ya kimataifa. Na baada ya vita vya kwanza vya dunia ikawa yahifadhiwa kwa njia ya taasisi za kimataifa, kukawekwa kifungu katika mikataba ya sulhu ya mwaka wa 1919 kifungu cha kuanzisha taasisi ya kimataifa itakayohifadhi amani, nayo ni umoja wa mataifa (UN). Na ilipaswa taasisi hii iwe ndio ya kuhifadhi amani, lakini nchi zilizoibuni zikakiuka mikataba yao na zikakhalifu malengo ya kuasisiwa kwake, kwani ilipaswa nchi hizi kujiondoa kwenye makoloni yake, na taasisi hii yenyewe ndio ihifadhi amani na kuzuia vita. Lakini nchi kuu hazikujiondoa katika koloni zake, wala hali zao hazikubadilika, bali ikawa hamu ya taasisi ni kuhakikisha usawa baina ya nguvu tofauti, na kuhami maslahi yao, na zaidi ya hayo nchi kuu ziligawanyiana milki za Ujerumani na serikali ya kiuthmani baina yao, huku Uingereza ikichukua fungu la simba. Hayo yakapelekea kuharibika kwa amani ambayo taasisi ilibuniwa kwa ajili yake na kuingia katika vita kadhaa ambavyo mwishowe ni vita vya pili vya ulimwengu. Baada ya vita vya pili vya ulimwengu majaribio ya kuunda taasisi ya kilimwengu itakayohifadhi amani ya kimataifa yaliendelea, nchi kuu ambazo ni: Uingereza, Marekani, na muungano wa kisovieti, na baadaye wakamshirikisha Ufaransa, wakajadiliana kuhusu kuanzisha ulimwengu wa baada ya vita, kwa namna mpya itakayodhamini kumakinika kwa amani na kuzuia vita, wakaongezea pia urahisishaji kusaidiana kiuchumi baina ya serikali tofauti, na kuhami haki za binadamu. Kutoka hapo umoja wa mataifa ukawa ndio unaohami amani, na neno “amani” na amani ya kilimwengu ikawa ni nembo ya kimataifa inayoimbwa na wote, na nchi kuu kwa hoja ya kuhifadhi amani zikawa zazuia nchi zengine kujikomboa na kujitoa kutoka kwenye kitanzi cha ukoloni. Hivi

ndivyo fikra ya kuhifadhi amani ilivyoendelea mpaka ikamakinika kama ilivyo sasa.

Suala la kuhifadhi amani kupitia taasisi ya kimataifa lilizua uongo wa kuondoa silaha. Ambapo Umoja wa mataifa ikajaribu kufuata maudhui ya kuondoa silaha, na Uingereza ikaifanya ndio njia ya kuidhoofisha Ufaransa na kuhimiza Ujerumani kujihami kisilaha ili kupatikane usawa Ulaya baina ya Ujerumani na Ufaransa, maudhui ya kuondoa silaha ikafeli na vikaibuka vita vya pili vya dunia.

Ilipokuja Umoja wa mataifa ikaenda hivyo hivyo katika maudhui ya kuondoa silaha, isipokuwa mpaka sasa hakuna nchi yoyote kuu iliyoweza kuihadaa nchi nyengine kama Uingereza ilivyoifanyia Ufaransa kupitia Umoja wa mataifa, vilevile umoja wa mataifa haukuweza kuiletea athari yake na ndio maana hata watu ni kama hawahisi uwepo wake, na bado umebaki kuwa ni jina lisilo na maana.

Mivutano baina ya nchi kuu pia ilileta kile kinachoitwa makongamano ya kimataifa, na vilevile pia kile kinachoitwa miungano. Ama kuhusu makongamano: la mwanzo ni kongomano lililofanyika kuhusiana na jambo hili ni kongomano la Viena, lililofanyika mwaka wa 1815, kisha kabla vita vya kwanza vya dunia yalifanywa makongamano kadhaa, miongoni mwake ni kongamano la Berlin lililowekwa kwa makubaliano ya kumaliza uwepo wa serikali ya kiislamu na kugawanya milki zake. Na baada ya vita vya pili vya ulimwengu yakawekwa makongomano mengine likiwemo kongamano la Berlin, na kongamano la Geneva na la Paris. Lakini baada ya Marekani na Urusi (muungano wa kisovieti) kukubaliana kuunda nguvu moja ya kilimwengu, hayakuwekwa makongamano yoyote isipokuwa mwaka wa 1969 pale wawakilishi wa nchi kuu: Ufaransa, Uingereza, Urusi (muungano kisovieti) na Marekani walipoweka kongamano katika vitendo baraza la umoja wa mataifa, ili kuangalia kile kinachoitwa tatizo la mashariki ya kati.

Lakini kongamano hili kufanywa na viongozi wa serikali haliitwi kongamano kwa kuwa limefungika ndani ya baraza la umoja wa mataifa.

Makongamano yalikuwa yakifanywa baada ya vita vya pili vya ulimwengu, kwa ajili ya kuyafanyia utafiti matatizo yaliyopo baina ya kambi mbili: ya mashariki na magharibi, kwa kuwa kambi ya mashariki ni dhaifu ndani ya baraza la umoja wa mataifa, na ndio maana Urusi (muungano wa kisovieti) ikajaribu kuchukua usukani wa uongozi kutoka kwa kambi ya kimagharibi, ikafanya kazi kuiondosha Marekani kutoka nafasi ya kuwa nchi ya kwanza, ikawa yajaribu kuhamisha matatizo kutoka katika baraza la Umoja wa mataifa, na ikafaulu katika kongamano la Berlin kwa kupanua mpasuko wa tofauti baina ya Uingereza na Ufaransa na baina ya Marekani, na katika kuchukuwa uwamuzi wa kueka kongamano la Geneva na kufaulu katika kongamano la Geneva. Basi ikawa kuwekwa makongamano ni kudhoofisha Marekani na kutia nguvu Urusi (muungano wa Kisovieti). Na Uingereza ilijaribu kuweka makongamano baina yake na Marekani ili kutatua matatizo yake nje ya baraza la Umoja wa mataifa, likawekwa kongamano la Bermuda lakini haikufaulu hapo. Kisha hakukuwekwa kongamano lolote baina ya serikali za kambi ya kimagharibi, wakatosheka na mikusanyiko ya kawaida baina ya Marekani na Uingereza. Marekani ikatambua kwamba kuwekwa makongamano nje ya baraza la Umoja wa mataifa kunadhoofisha msimamo wake na kwapelekea kudhoofika kwa nafasi ya kimataifa. Kwa hiyo ikawa haikubali kuwekwa makongamano nje ya baraza la Umoja wa mataifa, haswa baada ya mapatano - bali muungano - baina yake na Urusi (muungano wa kisovieti) baada ya mkutano wa Veina mwaka wa 1961.

Ama kuhusu suala la miungano baina ya nchi: hakika hili pia ni la zamani sana, na hufanywa na nchi kwa lengo la kujijengea nguvu dhidi ya nguvu nyengine, au kwa lengo la kuzuiana kuharibu usawa baina yao. Kwa hiyo mkataba wa Ex-lachaple uliofungwa

mwaka wa 1815 ni aina ya muungano. Na miungano iliyokuwa baina ya Uingereza na Ufaransa na baina ya Austria na Ujerumani nao ni muungano wa kutiliana nguvu na kuhifadhi usawa. Kisha muungano uliofanyika baina ya Ufaransa na Uingereza dhidi ya Ujerumani katika vita vya kwanza vya ulimwengu, na muungano baina ya Marekani, Uingereza, Ufaransa, na Muungano wa kisovieti dhidi ya Ujerumani katika vita vya pili vya ulimwengu: hii ni miungano dhidi ya nchi kubwa. Na NATO iliyobuniwa baada ya vita vya pili vya ulimwengu dhidi ya Urusi (Muungano wa kisovieti) na Warsaw iliyobuniwa baada ya vita vya pili vya ulimwengu dhidi ya kambi ya kimagharibi: yote hiyo ni miungano iliyobuniwa dhidi ya nguvu nyengine. Kwa hivyo, itakuwa miungano ni mfano wa makongamano ya kimataifa, ni mbinu ya kutiliana nguvu dhidi ya nguvu nyengine, au ni kwa ajili ya kuhifadhi usawa, hii ndio miungano inayozingatiwa kama chombo katika vyombo vya mivutano ya kimataifa.

Na pia kuna miungano au mikataba inayofungwa na nchi kubwa baina ya nchi ndogo au baina yake na nchi ndogo, basi miungano hii haizingatiwi kuwa ni chombo miongoni mwa vyombo vya mivutano ya kimataifa moja kwa moja, bali huzingatiwa kama mbinu za ukoloni, au ni mbinu za kutilia nguvu nchi kubwa zinazo simamia kufungwa kwake. Kwa hiyo muungano uliobuniwa baina ya Iraq na Uturuki na mkataba kabla ya vita vya pili vya ulimwengu unaojulikana kama mkataba wa Saad-Abad, uliosimamiwa na Uingereza ili kumakinisha ushawishi wake ndani ya hizo nchi na kwa ajili ya kuzidisha mizani yake ya kimataifa mbele ya nchi zengine kama vile Ufaransa na Muunguno wa kisovieti. Na mikataba iliyofungwa baina Uingereza na Iraq na baina yake na Misri kabla ya vita vya pili vya dunia: hii ni katika mbinu za kumakinisha ukoloni wake na si kwa ajili ya vita. Kadhalika miungano iliyowekwa na Uingereza baada ya vita vya pili vya dunia kama muungano wa Baghdadi, au iliyowekwa na Marekani kama muungano wa kusini mashariki mwa Eshia, au ilivyofanya Marekani kwamba Kuwait, Pakistan, Misri, Morocco, Agentina,

Korea kusini, Bahrain, Australia, Newzealand, Ufilipino, Thailand, kuongezea na (Israel): nchi hizi kuunda kile kinachoitwa muungano wa washirika wa kimkakati kando na NATO, hii pia ilikuwa ni mbinu ya ukoloni ili kuthibitisha ushawishi wake wala haikuwa miungano ya kivita. Pia mfano wa miungano kama hii haizingatiwi kuwa ni vyombo vya mivutano ya kimataifa moja kwa moja, bali tu vyombo hivi ni miungano inayowekwa baina ya nchi kubwa baadhi yake kwa baadhi nyengine.

Na ilikuwa yatakiwa kazi ya NATO imalizike kwa kuporomoka Muungano wa kisovieti na kambi ya kimashariki, lakini Marekani iliubakisha huu muungano, bali na ikaenda mbio kuupanua na kulitekeleza hilo kivitendo, ikaunganisha nao nchi nyingi za Ulaya mashariki, na yaenda mbio kuziunga nchi nyenginezo pia. Na sababu ya hayo ni kubadilika kwa lengo la muungano huu, kwani sasa haikuwa ikielekezwa dhidi ya kambi ya kimashariki, bali ikielekezwa dhidi ya kambi ya kimagharibi ambao ni wanachama wake. Na sababu ni kwamba Marekani ilihisi kwamba wayuropa wanajaribu kujikomboa kutoka mkononi mwake, hivyo ikaubakisha muungano huu ili kuwabakisha chini ya wasia wake, haswa kwa kuwa yeye ndiye anayedhibiti muungano wa NATO, ili amani yao na utetezi wao ubakie ukiwa umefungamanishwa na Marekani.

Katika zama hizi zile nchi zilizoshirikiana na Marekani katika vita vya Ghuba vya pili, na katika kuivamia Iraq, na ambazo zaitwa nchi washirika, hizi huzingatiwa kuwa ni mfano wa miungano ambayo lengo lake ni kutilia nguvu ushawishi wa Marekani ndani ya maeneo hayo, na kutilia nguvu upande wa idara ya Marekani, nayo ni mbinu katika mbinu mpya za kikoloni za Marekani.

Hii ndio misingi ambayo siasa za kimataifa zimesimama juu yake kwa sura jumla, na ambayo pia husimama juu yake sera za kila nchi katika nchi zinazoathiri katika siasa za kimataifa. Na kulingana na misingi hii ndio itawezekana kufahamu matendo ya kisiasa

yanayofanyika ulimwenguni, na yawezekana kufasiri vitendo hivi tafsiri inayokubaliana na ukweli na kuambatana na hali halisi au kukaribiana nayo. Kwa hivyo vitendo vya kisiasa vinavyotekeleza nchi sawa iwe nchi kubwa au ndogo, haiwezekani kuvifahamu isipokuwa kwa misingi hii au yanayotokana nayo au yanayofungamana nayo, ndipo itajulikana ni kitendo gani, chafanyika wapi, na mazingira yake, kisha kuunganishwa na msingi katika misingi iliyotangulia, na hapo ndio hujulikana ni nini kilichofanyika, na hujulikana sababu zake pia, ili iwezekane kutambua matokeo yake.

***

## [6] MASWALA MAKUBWA YA ULIMWENGU

Hakika vitendo vya kisiasa vinavyofanyika ulimwenguni ni vingi, vikoihusiana na ya kadhia nyingi, lakini maswala muhimu zaidi kati ya hayo yawezekana kuyakusanya kuwa kadhia sita kubwa, nazo ni: kadhia ya Ulaya, kadhia ya Mashariki ya kati, kadhia ya Eshia ya kati, kadhia ya mfano wa Bara Hindi, kadhia ya Mashariki ya mbali, na kadhia ya Afrika.

Katika utafiti tumetosheka na hizi kadhia sita kwa sababu zifuatazo:

1. Mivutano iliyopo baina ya nchi kubwa au mashindano baina yao hakika hufanyika katika maeneo haya. Kwa hiyo ni jambo la kimaumbile kadhia zake kuwa ndio kadhia muhimu zaidi ulimwenguni.
2. Watu katika maeneo haya wanaishi katika hali ya kuchemka sana na kutaka kujikomboa. Kwa hiyo ikawa ni lazima (nchi kubwa) kujaribu kudhibiti hali ya raia hawa, haswa na ikizingatiwa kwamba maeneo hayo raia wake wengi ni Waislamu, wenye kiu ya kutaka kuwang’oa viongozi wao ili kusimamisha serikali ya kiislamu.

3. Matukio mengi ya kisiasa yanayotokea ulimwenguni kiuhalisia yazunguka katika haya maeneo, kwa hiyo yana mfano mzuri wa kufahamu kadhia nyenginezo za kisiasa.
4. Haya maeneo yana mapato na utajiri mwingi wa malighafi chungu nzima. Ndio sababu nchi nyingi za kikoloni na mashirika ya ukiritimba yazozana juu yake, na wakienda mbio kwa nguvu zote walizo nazo ili kuzidhibiti na kushika utajiri wake wa malighafi.
5. Kwa kuwa maeneo ya bara la Marekani yalitenganishwa na mivutano tangu mwanzo wa Monroe mwaka wa 1823, ambapo kwa mujibu wake Marekani ilizuia nchi kubwa za Ulaya kuingilia bara la Marekani na kutishia maslahi nyeti ya Marekani katika bara hil, kwa hivyo hakuna mvutano wa kimataifa katika bara hili kwa maana inayojulikana, kwani maslahi ya Marekani humo yako mbali na kutishiwa kihakika. Ama kuhusu mahusiano yaliyokuwa kati ya Muungano wa kisovieti na Cuba mwishoni mwa miaka ya hamsini katika karne iliyopita na mwanzoni mwa miaka ya sitini katika karne iliyopita: Marekani iliyanyamazia kwa sababu ilikuwa yataka kuuvuta Muungano wa kisovieti polepole ili upanue majukumu yake nje ya maeneo ya Muungano wa kisovieti na Ulaya mashariki, kwa lengo la kuuchosha kiuchumi na kijeshi kwa namna ambayo itabidi Muungano wa kisovieti kuihami Cuba dhidi ya hatari ya Marekani. Kwa hiyo kuzidisha uzito kwa Muungano wa kisovieti katika kuihami Cuba ndiyo sababu iliyofanya Marekani kunyamazia mahusiano yake na Cuba. Ndio maana mambo yalipozidi na kufikia hadi kambi ya nuklia, Marekani ikafanya bidii kutoa kambi hizo kutoka Cuba.

Kwa ufupi: bara la Marekani liko nje ya mvutano wa kimataifa kwa maana inayojulikana, bali kila kinachowezekana kutokea humo ni fujo za kindani ambayo Marekani huwa haiko mbali nazo.

Kwa hivyo hayo maswala sita ndio maswala makubwa ya ulimwengu. Na kabla ya kuyazungumzia twastahiki kuzijua nchi kubwa zenye athari katika siasa za kimataifa, kwa sababu kadhia yoyote ili izingatiwe kwamba ni kadhia kubwa ya kilimwengu, kwanza hiyo kadhia yahitakia iwe ni uwanja wa matendo ya kisiasa yanayo athiri. Na kwa kuwa matendo ya kisiasa yenye kuzingatiwa ni matendo yanayofanywa na zile nchi kubwa, basi hapana budi kuzijua nchi kubwa katika kila zama.

Nchi kubwa ni zile zinazoathiri katika sera na siasa za kimataifa, na zinazo tekeleza matendo yanayoathiri nchi nyenginezo, nchi kubwa sio zilizo na idadi kubwa ya wakaazi, wala sio zilizo tajiri, au yanayo fanana na hayo, bali nchi kubwa zilizokusudiwa ni zile nchi zilizo na athari katika siasa za kimataifa na katika nchi zengine. Kwa msingi huo basi nchi kubwa kwa sasa - yaani karne ya kumi na tano Hijria (1425 H) na karne ya ishirini na moja Miladi (2004 M) - ni Marekani. Kwa sababu iko na athari kubwa katika siasa za kimataifa, bali yakaribia kutawala msimamo ya kimataifa peke yake, na nchi zengine hazifikii kiwango cha kushindana na Marekani katika nafasi yake au kutawala msimamo wa kimataifa. Lakini kwa sababu Urusi ambayo ni mrithi wa Muungano wa kisovieti uliokuwa  ukizingatiwa kama nchi kubwa hadi kuporomoka kwake, na kwa sababu Uingereza na Ufaransa pia zilikuwa nchi kubwa kabla ya vita vya pili vya ulimwengu, na wote wanang’ang’ania kubakia katika siasa za kimataifa, kila mmoja wao kivyake au kupitia Ulaya hufanya matendo yanayoathiri siasa za kimataifa na kuiathiri Marekani, hata kama athari hii itakua dhaifu haifikii kuitwa kuwa ni kushindania nafasi ya Marekani katika siasa za kimataifa kwa maana inayojulikana, kwa sababu hizo basi hizi nchi tatu pia zaweza kusifiwa kuwa ni nchi kubwa, na  hiyo ni kwa kufumbia jicho sifa hiyo, kwa kuangalia matendo ya kisiasa yanayofanywa na Uingereza na kuhisika uwepo wake au baadhi ya kuwepo katika siasa za kimataifa, na kwa kuangalia pia matendo ya Ufaransa na Urusi zikijaribu ya kuthibisha uwepo wao katika ulingo wa siasa za kimataifa kama ilivyokuwa katika matatizo ya vita Iraq.

Ama kuhusu Ujerumani: kwa upande wa raia wake na serikali yake katika historia ilikuwa ikizingatiwa kuwa ni nchi kubwa, lakini baada ya kushindwa kwake katika vita vya pili vya ulimwengu haizingatiwi tena kuwa ni nchi kubwa kabisa, mfano wa kuanguka kwake baada ya kushindwa katika vita vya kwanza vya ulimwengu. Lakini kama ilivyorudi kuwa nchi kubwa baada kidogo ya vita vya kwanza, basi yawezekana kurudi kuwa nchi kubwa mara ya pili namna muda utakavyokuwa mrefu, na harakati zake pamoja na Ufaransa katika baadhi ya maswala ya kimataifa zaonyesha hivyo.

Ama kuhusu China: hakika ni vigumu kuizingatia kuwa ni katika nchi kubwa inayoathiri katika siasa za kilimwengu kwa maana inayojulikana, yaani kuathiri ulimwenguni au katika maeneo yake mengi, licha ya kuwa wakaazi wake ni watu bilioni 1.2, licha ya kuwa Urusi yaipigia hisabu, na licha ya kuwa hata Marekani nayo pia yatalia maanani katika hesabu za kimataifa, lakini pamoja na yote hayo China haizingatiwi kuwa ni nchi kubwa kwa sababu mbili: Moja ni kwamba haijawahi kuwa nchi kubwa katika zama zozote zile, na haijawahi kuathiri katika siasa za kimataifa katika wakati wowote uliopita. Juu ya hayo, China tangu ilipokuwa ni nchi ya kikoministi mpaka sasa wala haikutilia umuhimu suala la kueneza ukoministi ulimwenguni na kuathiri maeneo tofauti ulimenguni, bali imejifunga shughuli zake katika ukanda wake, na haswa baada ya majaribio yake ya kisiasa ndani Afrika kuanguka na pia ndani ya baadhi ya nchi za Asia, uchangamfu huu haukuathiri kwa lolote, kisha haikuweza kufuatilizia badala yake ikarudi katika mipaka yake ya kiasili.

Ama kuhusu India: ingawa watu wake wamezidi milioni 935, na iko na silaha za kinuklia, lakini athari yake katika siasa za kimataifa yakaribia kukosekana. Kwa hiyo haisihi hata kupita akilini kwamba ni nchi kubwa, kwa sababu hakuna uwezekano wa India kuathiri katika siasa za kimataifa.

Ama kuhusu Japan: hakika kabla ya vita vya pili vya ulimwengu katika zama za mzunguko ilikuwa ina athari katika siasa za kimataifa, lakini athari yake ilikuwa ni ya muda tu kama vile Italia. Kwa hiyo Japan wala Italia hazizingatiwi kuwa ni nchi kubwa.

Ama kuhusiana na Ummah wa kiislamu: kwa hakika ulikuwa na serikali kubwa hadi vita vya kimsalaba, kisha ikarudia tena kuwa serikali kubwa tangu ilipofaulu kumaliza vita vya kimsalaba, na ikaendelea hivyo kuathiri katika siasa za kimataifa hadi karne ya kumi na tisa miladi. Kisha baada ya hapo athari yake kimataifa ikadhoofika hadi ilipomalizika serikali ya huu Ummah mwanzoni nwa karne ya ishirini baada ya vita vya kwanza vya ulimwengu. Lakini vigezo vya serikali kuu bado vinapatikana ndani ya huu Ummah, na ishara za nguvu zake zilianza kuonekana tangu mwishoni mwa karne iliyopita, na kwa sasa alfajiri yake imeanza kuchomoza, itarudi upya kuwa serikali kubwa, bali itakuwa nchi ya kwanza kwa idhini ya Allah.

Kwa hivyo basi hapana budi kujua haya mataifa na nchi hizi, kwa sababu ndizo huathiri kadhia kubwa za ulimwengu:

**Kwanza**: Nchi nne kubwa za mwanzo: Marekani, Uingereza Ufaransa, na Urusi.

**Pili**: Watu wa serikali zilizowahi kuwa kubwa na zinazojiandaa kurudi kuwa nchi kubwa tena, nao ni: Umma wa kiislamu na Ujerumani.

**Tatu**: Taifa la Japan huzidishwa katika mataifa na serikali hizi: kwa kuwa na nguvu za kiuchumi zenye kuathiri pakubwa uchumi wa kimataifa katika kadhia kubwa za ulimwengu, hata kama Japan si nchi kubwa kwa maana inayojulikana.

Ama China ingawaje ni nchi kubwa lakini katika maeneo yake ya kimajimbo, yaani yawezekana kuitwa kuwa ni nchi kubwa katika kanda/majimbo yake. Ndio maana kuathiri kwake katika kadhia za

kimataifa katika maeneo tofauti ulimwenguni ni kuathiri kuliko dhaifu, isipokuwa maeneo yake tu. Kwa hiyo hatutoizungumzia hapa katika utafiti wa nchi na mataifa yenye kuathiri kiulimwengu, bali tutaizungumzia tutakapoingilia kadhia za maeneo ya China.

Basi tuanze kuzungumzia nchi na mataifa haya kwa namna ifuatayo:

1. **UMMAH WA KIISLAMU:**
   Huu Ummah ulidhihiri baada Allah (Swt) kumtuma Mtume wake Muhamad (saw) na Uislamu ili kuwaokowa watu kutokana na giza la kijahiliya hadi kwenye nuru ya Uislamu. Kisha serikali ya kiislamu, serikali ya huu Ummah ikadhihiri baada ya Mtume (saw) kuhamia Al-Madinatul-Munawarah.

Na baada ya Mtume (saw) kuondoka, serikali ya kiislamu ikaendelea katika zama za makhalifa waongofu na makhalifa baada yao, ikikomboa na kueneza kheri ulimwenguni, mpaka ilipovunjwa mwazoni mwa karne iliyopita, na yatarajiwa kurudi tena baada muda mfupi kwa idhini ya Allah.

Mwanzo waarabu ndio waliobeba serikali, kisha ikaenea ulimwenguni, na watu wengi wenye asili mbali-mbali waarabu na wasiokuwa waarabu wakaingi katika Uislamu, na wote wakayeshwa na Uislamu, ikawa hakuna tofauti baina ya asiyekuwa Muarabu na waarabu isipokuwa kwa Uchajimungu tu.

Kwa kuwa waarabu ndio watu wa mwanzo kuubeba Uislamu, basi hapana budi kujua jamii ya waarabu haswa, kisha Ummah wa kiislamu kiujumla.

**Ama jamii ya waarabu:** walikuwa wakiishi katika vita, walizowea kupigana, kwa sababu hiyo ikapatina kwao kinachoitwa "tabia ya kijeshi" na kinachoitwa: "kuhisi majukumu kwa wengine". Kwa hiyo wakawa wanastahiki kubeba ujumbe wa kiislamu kwa njia yake aliyoteremsha Allah, nayo ni ulinganizi na Jihad, yaani

kupigana vita vya kimada kwa ajili ya kueneza kheri wala sio kwa lengo la Utumwa. Hivyo basi wakawa wanaingia vitani na watu baada ya kuwafikishia Uislamu kwa namna inayozindusha macho, kwa ajili ya kueneza fikra ya kiislamu waliyoibeba, na sio kwa ajili ya kukoloni mataifa mengine na kuwafanya watumwa. Kukapatikana kwa waarabu fikra ya kuwa Mshumaa unaochomeka ili kuangazia wengine, na ikawa katika sifa zao mashuhuri zaidi ni kuhisi na kubeba majukumu juu ya wengine, na kuhisi usawa nao.

Ummah wa kiislamu baada ya kishikana na Uislamu basi Waislamu wote wakawa kama taifa/jamii moja, ikapatikana kwao kile kinachoitwa tabia ya kijeshi ya kijihadi, kwa kuwa Jihadi ni kilele cha dini yao, ikapatikana kwao fikra ya kueneza uongofu kwa watu, na nusra ya kibinadamu ikawa ndio asili yao. Kwa hivyo Waislamu namna watakavyodorora, namna zama zitakavyo waeka mbali na mababu zao walioshikana na Uislamu na wakaubeba kwa njia yake ambayo ni da'wa na Jihad, basi kwa ujumla wao bado wako na ile tabia ya kijeshi ya kijihadi, na kile kinachoitwa kuhisi majukumu juu ya wengine, na kueneza uongofu kwa watu, hali yao ni kama ya waarabu ambao ndio wa mwanzo kubeba Uislamu, wakati jamii zilizosilimu zilipoyeyushwa na Uislamu bila kujali asili zao.

2. **TAIFA LA UJERUMANI:**

Hii ni jamii ya kale na yenye asili, ni yenye uzowefu sana, shupavu, waliokazana, na mashujaa, lakini wamezidi katika kujiamini, wakavuka mipaka katika kudai haki ya ubwana juu ya wengine. Uwanajeshi na vita yazingatiwa kuwa ni katika tabia zao, yaani ni kama kwamba ni jambo la kimaumbile kwao au ni kama sifa za kimaumbile wanazozaliwa nazo. Na huu uwanajeshi wa kijerumani ndio unaowaogopesha majirani zake, haswa nchi kubwa kama Uingereza, Ufaransa, na Urusi. Wajerumani walimaliza miaka mingi katika vita vya nje na vya kindani, vikapita vizazi kadhaa katika vita na majirani zake kwa mfano Ufaransa. Maisha yao yalikuwa ni uundaji/viwanda na haswa viwanda vya kivita vilivyoboreshwa. Ndio maana hata kama wamekatazwa kumiliki

silaha za kinuklia bado wanawaogopesha majirani zao na huwatia uoga washindani wake na maadui zake. Ndio sababu mara nyingi nchi zenye nguvu zimekuwa zikipanga njama ya kuzuia Ujerumani kusonga mbele na kuwa katika safu za nchi kubwa. Lakini pamoja na hayo, hili ni taifa hai, kuna uwezekano wa kuja kuwa nchi kubwa, kwa sababu ukuwaji wa vitu vilivyohai kikawaida huvishinda vizuizi.

Ujerumani ni kama mataifa mengine ya kimagharibi, waliposhikana na Urasilimali basi “Maslahi” yamekuwa ni sehemu katika maisha yake, kwa hiyo Ujerumani nayo yazingatiwa kuwa ni nchi ya kikoloni, ilishawahi kuwa na koloni zake kabla ya vita vya kwanza vya dunia, na ikaingia vita vya pili vya dunia ikiwa nia yake ni kurudisha koloni zake ilizopoteza, kunyakuwa makoloni zaidi kutoka kwa nchi nyenginezo, na kupata koloni mpya. Kwa hivyo basi ukoloni ni sera ya kijerumani na sio kama inavyodhaniwa kuwa ilikuwa sera ya *Hitler* peke yake. Na Ujerumani ya leo haiko mbali sana na ukoloni, kwani hata kama imenyimwa ukoloni mpana wa moja kwa moja, lakini leo bado ni katika nchi zinazoongoza katika ukoloni wa kiuchumi, ikijitanuka kiuchumi haswa katika maeneo ya nchi za Ulaya mashariki katika udhibiti wa kivyake kiuchumu.

Ama kuhusu nidhamu yake ya utawala: pamoja na kudai kwake kuwa ni nchi ya kidemokrasia lakini bado udikteta ndio unaodhihirika kwa sura ya wazi, nao hudhihirika katika tabia za viongozi wote wa Kijerumani wa zamani na hata wa sasa.

Ujerumani baada vita vya kwanza vya ulimwengu, licha ya kulazimishwa vikwazo vigumu, lakini iliweza kuvishinda na ikarudi kuwa nchi kubwa. Na mambo mawili ndio yaliyoisadia kufikia hilo: **Kwanza**: kuhisi kifikra iliyodhihiri kwa watu wake, ikawasukuma kufanya kazi ili kurudi kuwa nchi kubwa. Na sababu ya **pili**: ni kwamba Uingereza ilitaka kuharibu mizani ya kimataifa baina yake na Ufaransa, hivyo ikaishajiisha Ujerumani kisiri ili irudi katika kushindana na Ufaransa na kusimama dhidi yake, hilo likapelekea Ujerumani kuweza kurudi kuwa nchi kubwa. Ama baada ya vita vya

pili vya ulimwengu, hakuna sababu yoyote iliyomsaidia kurudi kuwa nchi kubwa, kwani washirika wake wote waliweka vikwazo vyote vinavyozuia Ujerumani kurudi kuwa nchi kubwa. Na mambo muhimu zaidi yanayozuia Ujerumani hadi sasa kurudi kuwa nchi kubwa: **Sababu ya kwanza**: ni watu wake kushughulika na uchumi na kuacha viwanda vya silaha, na hatimaye hilo likaathiri katika siasa za kimataifa na kuelekeza hamu yao kwa upande tu wa kiuchumi, hali iliyobadilisha hisia zao na kugeuza uchangamfu wao wakaachana na upande wa viwanda vya kivita ambavyo ndio kinachofanya nchi kuwa nchi kubwa inayoathiri, na kuimakinisha upande wa kisiasa yenye natija. **Sababu ya pili:** ni Urusi (muungano wa kisovieti) daima kuwa macho kuhusiana hatari ya Ujerumani dhidi yake, na haifumbii macho hatari ya Ujerumani hata kidogo, wala haichelewi kuweka sera kali isiyokuwa na huruma yoyote mbele ya Ujerumani, sera isiyokuwa na maadili yoyote ndani yake, na wala hakuna kinachosukuma sera hizi dhidi ya Ujerumani isipokuwa kitu kimoja: kuiangamiza Ujerumani kabisa milele, ndio maana Urusi kusambaratisha kila jaribio la harakati za Ujerumani. Hii ndio sababu Marekani ilipotabanni kuhuisha upya uwanajeshi wa kijerumani baada ya mwaka wa 1955 haikufaulu katika hilo, wala haikufaulu Uingereza pia katika kurudisha umoja wa Ujerumani, wala haikufaulu Ufaransa pale De Gaulle alipojaribu kuleta umoja wa Ulaya, ili umoja huu uwe msaada kwa Ujerumani na kuiwezesha kisilaha na kurudisha umoja wake, halikufaulu jaribio lolote kati ya hayo kwa sababu ya Urusi (muungano wa kisivieti) kusimama kwa ukakamavu usoni mwake.

Ama umoja wa Ujerumani uliotokea sio kutokana na sera, au matendo ya kisiasa, au mikakati na mipango ya kisiasa iliyofanywa na wanasiasa wa Ujerumani, bali ulikuja kutokana na Urusi kukubali kulegeza msimamo kwa Marekani wakati muungano wa kisovieti ulipoporomoka, na hilo ni kwa kuwa Marekani ilionelea kupiga umoja wa Ulaya kwa umoja wa Ujerumani, kwa kuuwekea vizingiti au kwa kuchelewesha kupatikana kwake, kwa kusababisha matatizo ya kiuchumi kwa Ujerumani yenye umoja, ambayo ndio mfadhili

mkubwa wa umoja wa Ulaya, kwa kushikana na Ujerumani mashariki ambayo ni dhaifu kiuchumi. Lakini Ujerumani iliweza kuvuka hiki kizingiti, na ikaanza kujipanga jinsi atakavyojikomboa na ugandamizaji wa Marekani, ikaelekea Ulaya na haswa kwa Ufaransa ili iwe katika sura ya matukio na kujaribu kuathiri humo. Na ilikuwa na mchangio wa kihakika katika soko la pamoja la Ulaya ambalo baadaye liligeuka na kuwa ndio umoja wa Ulaya. Lakini Ujerumani bado yaliendea mbio hilo kwa mbinu za kiuchumi, ikiwa na maana kwamba itakuwa na ushawishi katika nchi za Ulaya, haswa za kimashariki kupitia njia ya misaada ya kiuchumi. Ila hilo halina maana kuwa Ujerumani itakuwa na nafasi katika siasa za kimataifa, kwa sababu kuathiri katika siasa za kimataifa kimsingi hutegemea nguvu za kijeshi na matendo ya kisiasa yanayopelekea katika utekelezaji na kufikia mipango ya kisiasa, na hayo ni mambo ambayo Ujerumani bado yayahitajia, ingawa imeanza kulijaribu hilo kwa kushikamana na Ufaransa, lakini hayo ni majaribio au vitendo ambavyo havichukuliwi kuwa ni vitendo vya maana, bali zaidi ni radiamali tu (Reactions). Lakini hata radiamali hizi zilipanda kwa kiwango cha kuweza kuwa athari mbele ya Marekani kama katika matukio ya kiadui ya Marekani dhidi ya Iraq, kadhalika jaribio la Ujerumani na Ufaransa kisha kwa kushirikiana Uingereza kuhusu maudhui ya kuwa na nguvu ya pamoja za kujilinda nchi za Ulaya mbali na muungano wa NATO, hii maudhui iliisumbua Marekani, japo ilikuwa bado ndio inaanza kubuniwa.

Haya yote yajulisha kwamba Ujerumani imeanza kuwa na matarajio ya kuwa na mchangio katika siasa za kimataifa. Hivyo basi hata wakati ukiwa mrefu vipi hakika Ujerumani kurudi kuwa nchi kubwa mara nyengine ni jambo linalotarajiwa, kwa sababu nguvu bandia namna zitakavyofaulu kuzuia kuinuka kwa mataifa yaliyo hai, hakika kufaulu huku kutakuwa ni kwa muda tu, lakini mwisho kiumbe hai lazima kitashinda vikwazo vyote vinavyozuia ukuwaji wake.

Kwa hivyo twaweza kufupisha siasa za Ujerumani leo kama ifuatavyo:

Hakika siasa ya Ujerumani ya Ulaya imejengwa juu ya misingi ya vitendo vya Ulaya, kwa hivyo kwa upande mmoja yasaidiana na Ufaransa ili kuunda ngome ya Ufaransa-Ujerumani kwa kuzingatia kuwa hili mbeleni litakuwa jambo la kimsingi katika siasa za umoja wa Ulaya, na kwa upande mwengine Ujerumani yachunga maslahi ya Marekani ndani ya Ulaya, na pia huchunga ulinzi wa kimikakati ya Marekani kwa usalama wa Ujerumani baada ya vita vya pili vya dunia, na kamwe haiwezi kuhatarisha maslahi ya Marekani bali daima huyaweka katika ngazi ya juu ya vipaumbele vyake. Na kwa upande wa tatu: hakika sera za Kijerumani hutia maanani ubinafsi wa kiuchumi, na sera hii huonekana katika kujaribu kwake kujipwekesha na uchumi wa nchi za Ulaya mashariki na kumeza peke yake bila kuwashirikisha washirika wake wa Ulaya.

Na hivi mwishoni yaonekana katika siasa za Ujerumani kwamba imeanza kudhihirisha kujali sana upande wa kijeshi na wa kisiasa yenye upeo wa kiulimwengu. Mfano wa hayo ni mchangio wake uliozidi katika harakati za muungano wa NATO huko Afghanistan, Bosnia, na Kosovo, na waziri wake wa mambo ya nje kushiriki katika harakati za kisiasa pamoja na wenzake wawili wa Ufaransa na wa Uingereza, ambapo hao mawaziri watatu walizuru Iran na kuishinikiza ili ikubali kutia saini itifaki ya ziada itakayoruhusu mitambo yake ya kinuklia kufanyiwa upekuzi wa ghafla. Na katika mifano pia ni mchangio wa harakati zilizofanikiwa ziliofanywa na Ujerumani, pale ilipokuwa kati baina ya umbile la kiyahudi na Hizbullah kubadilisha mateka.

Hivi ndivyo tunavyoona mabadiliko katika siasa ya Ujerumani, ambapo zamani ilikuwa imejitenga, hali iliyoifanya Ujerumani kulemea upande wa kiuchumi peke yake, lakini mtu akichunguza ataona kwa sasa dori ya Ujerumani ya kisiasa inayozidi kukuwa yadhihirika kama kwamba iko sawa na dori ya Ufaransa na Uingereza.

Ujerumani ikitaka kuharakisha kurudi kwake kuwa nchi kubwa, basi ni lazima kukimbilia viwanda vya silaha na kuvifanya kuwa ndio suala nyeti kwake. Pia iwe muelewa kisiasa katika mikutano yake na Ufaransa na Uingereza, kwa sababu inavyojulikana ni kwamba Ufaransa na Uingereza wanakwenda mbio kuutumia muungano wa Ulaya kwa ajili ya kutilia nguvu ushawishi wao wa kimataifa. Na pia yajulikana kwamba Ufaransa yajipatia nguvu kupitia Ujerumani ili (Ufaransa) ipate kujitokeza ndani ya Ulaya. Na kwamba Uingereza hutumia ujanja wake wa kisiasa katika kukutana na Ufaransa na Ujerumani ili kufikia maslahi yake. Kwa hivyo basi ni wajibu kwa Ujerumani - hata kama itaendelea kuungana na Ufaransa haswa na kuungana na nchi nyenginezo za Ulaya kiujumla - ijiangalia yenyewe ili iwe na nguvu za kijeshi zenye uzito wa kisiasa wa kijerumani ndani ya muungano, ili isitumiwe tu kwa ajili ya maslahi ya wengine, na ichunguze msimamo wa kimataifa kwa mtazamo wa kiujerumani na sio kiulaya, na ipate funzo katika historia ya Ulaya.

3. **Ama kuhusu watu ya Japan:** Hakika waliinukia na biashara na ubaharia, wakaishi katika miji midogo, na utapata katika sifa zao iliyo wazi zaidi ni ushujaa, na miongoni mwa sifa zao muhimu zaidi ni umakini katika kufanya mambo. Ndio maana wakakimbilia kwa haraka viwanda pale tu yalipopatina mapinduzi ya kiviwanda, ikawa yahesabiwa ni katika nchi kubwa licha ya udogo wa miji yake. Wala haikujali kuingia vitani na Uchina na kumega sehemu yake, wala haikusitasita katika kuishambulia Marekani, kwa kuwa iliiona kuwa ni hatari kwake. Ndio maana katika mikakati muhimu ya kimarekani ili kuhakikisha kuidhibiti Japan ikiawa ni kufanya viwanda vyake visijengwe juu ya msingi wa kivita, bali vijengwa juu ya msingi wa kibiashara na kukuza uchumi, hayo yote ni kwa ajili ya kuizuia kusonga mbele kufikia nyanja za kimataifa. Na Japan kwa sasa ni nguvu kubwa ya kiuchumi yenye kupigiwa hesabu zote.

4. **Ama kuhusu watu wa Marekani:** hakika hili ni taifa tajiri linalopatikana katika miji ambayo utajiri wake ni mkubwa, kisha likaingia katika mivutano mikali na nchi za Ulaya zilizokuwa zikiikoloni na haswa Uingereza, ikapata uhuru wake kwa nguvu ya silaha kupitia ufahamu na kujua. Na hili lilileta kwa wamarekani tabia kadhaa, tabia muhimu zaidi miongoni mwazo ni ni ile inayojulikana kama *(pragmatism)* yaani falsafa ya hoja. Na baada ya kupambana kwao na ukoloni wa Ulaya ikapatikana kwao tabia ya kuegemea maadili ya juu na kuziheshimu. Lakini raia wa Marekani waliamini mfumo wa Urasilimali kama ulivyo ulimwengu wote wa kinaswara, basi wakawa wanadhibitiwa na misukumo miwili: msukumo wa kukinai na kujichunga, na msukumo wa manufaa/maslahi na ukoloni. Kwa hivyo Uingereza ikawa yapatiliza msukumo ya kwanza ikiwatumia ili wawe nguvu yake katika vita na uchumi wakati ambao inapokuwa msukumo wa kwanza ndio unaowatawala. Na mara tu vilipokuja vita vya pili vya dunia na raia wa Marekani kuonja utamu wa ukoloni ndani ya mafuta ya Ghuba, basi ule msukumo wa pili (maslahi na ukoloni) ukamtawala na wakaendeshwa na mfumo wa kirasilimali, Marekani ikatoka katika ile hali ya kujitenga na ikawa yakoloni mataifa, na kuuweka ulimwengu chini ya udhibiti na nguvu zake. Na kamwe Marekani haitorudi kwenye hali ya kujitenga kwa mara ya pili ila kwa nguvu, kwa sababu mfumo wa kirasilimali umemtawala na ndio inayoendesha maisha yake, na maslahi peke yake ndio kinachotawala nyendo zake, ukiuongezea na ubabe na kujiona vilivyojaa katika maisha yake.

Marekani ilikuwa imekoloniwa na nchi za Ulaya haswa Uingereza, ikawa imegawanywa katika nchi kadhaa, basi kwanza ikajaribu kapunguza mbano wa ukoloni wa Uingereza, kisha ikaingia vita vikali vya kujikomboa vilivyopelekea kuifukuza Uingereza kutoka katika miji yake. Halafu hizo nchi zikakubaliana

kuungana na kuunda nchi moja, na hilo likatimia. Kisha ikawa yaunganisha na nchi zengine nayo, mara kwa hiyari na mara nyengine kwa nguvu za kijeshi na kuyafanya ni majimbo ndani ya nchi, mpaka muundo wake ukakamilika kwa sura ilivyo leo, ikawa sasa na majimbo hamsini na moja. Na ilianza ikiwa nchi yenye nguvu, na ikaendelea katika mapambano ya kimataifa ikiwa nchi yenye nguvu, ikaweza kuhami mabara mawili ya Marekani dhidi ya kudhibitiwa na nchi za Ulaya, ikawa ni ulimwengu mwengine, nao ndio unaojulikana kama ulimwengu mpya. Marekani imejengwa juu raia wachangamfu, waliopatikana katika miji yenye utajiri mkubwa.

Na Marekani hata kama nidhamu yake ya utawala ni katika nidhamu za kidemokrasia, lakini ilijiwekea nidhamu iliyowekwa kupitia fikra ya kina na kwa kutambua maana utawala, na kuwa ni utawala wa kibinadamu, unaotawaliwa na watu miongoni mwa binadamu, wala haikufikiria utawala kwa fikra ya kimantiki, bali iliutambua utawala kiuhalisia wake na kivitendo, na hilo laonekana wazi katika namna ya kumtawaza kiongozi wa jamhuri, katika uwezo mpana aliopewa, katika jukumu lake ndani ya serikali, katika kupanga uwezo wa kila nguzo katika nguzo zengine za serikali, katika nguvu ya umoja inayoonekana katika serikali na kusimama juu yake pamoja na kuwa utawala wa muungano, na pia yaonekana katika nafasi kubwa waliyopewa raia katika kumchaguwa raisi wa serikali na katika kuchaguwa nguzo zake. Na yote hayo yakawa na athari kubwa katika nchi kuwa na nguvu, na kukuza nguvu hizi kwa haraka sana.

Marekani kabla vita vya pili vya ulimwengu ilikuwa imetoka katika upweke wake na kushiriki katika kuendesha ulimwengu, bali ikajaribu kuwa peke yake katika uendeshaji huu. Kisha adui wake ambaye ni Urusi ya kisovieti akashirikiana naye tangu mwaka wa 1961 hadi 1979 katika kuendesha ulimwengu, na kuwekea mpaka tamaa za nchi zengine kubwa. Kisha Marekani ilipoona kwamba ishatimiza malengo kutokana na mapatano na ushirikiano na Urusi (muungano wa kisovieti), na kwamba ushirikiano huu umemletea

baadhi ya hasara: zikawa nchi za Ulaya zajaribu kumuepuka na kuanzisha mahusiano na Urusi, na kwamba muungano wa kisovieti umeanza kufanya majaribio ya kishujaa hata kama hayakufaulu kwa kuingia katika uwanja wa siasa za kimaifa, ili kwa hilo ujichukulie kuwa ni mbabe wa kimataifa kando na siasa za kimarekani - Marekani ilipoona yote hayo - iliamua kurudia kupandisha joto na Urusi (muungano wa kisovieti), kwa kuingia katika mashindano mapya ya silaha, maamuzi yaliyopelekea vita baridi vipya. Marekani ikaingia katika vita vya kihadhara, kifikra, na kiuchumi dhidi ya Urusi (muungano wa kisovieti) na kambi ya kimashariki, ikawafunga na mikataba iliyopelekea mwisho wa siku kuporomoka kwa muungano wa kisovieti. Marekani ikabaki kuwa ndio nchi ya kwanza na mbabe mwenye athari sana katika siasa za kimataifa.

Ndani ya Marekani kuna vyama viwili vikuu: Chama cha demokrasia (Democrats), na chama cha kijamhuri (Republicans). Wala mtu hawezi kuona tofauti kubwa baina ya sera zilizoandikwa za hivi vyama viwili, mpaka kwenye sera zinazofatwa. Vyama hivi viwili takriban hufata njia moja, wala takriban hakuna mabadiliko katika kubadilishana utawala baina vyama viwili, sawa iwe ni katika sera za kindani au sera za kigeni, na yakitokea mabadiliko basi itakuwa mabadiliko yaliyolazimishwa na mabadiliko ya dhurufu fulani, lakini sio tofauti ya sera za vyama viwili.

Chama cha demokrasia ndio chama kikongwe zaidi na ndio chama cha wengi kikiwa na kiwango kikubwa cha wafuasi. Ndio maana mara nyingi Congress huwa ni kutoka upande wake. Ama chama cha jamhuri ni chama kilichobuniwa baadaye kutokana na chama cha demokrasia, nacho ni chama cha matajiri, wengi katika wanachama wake ni watu wenye mali nyingi, watu wenye mashirika na viwanda vya ukiritimba, na pia kina idadi kubwa ya wasomi. Wala haijishughulishi kuvuna watu wengi wala hawana haja watu jumla kuwa upande wake, na lau sio nidhamu ya uchaguzi wa uraisi kuisaidia basi haingefaulu kamwe kuchukua uraisi, kwani hiki ni chama cha watu wachache sio chama cha wengi.

Marekani kama nchi nyenginezo za kirasilimali hudhibitiwa na watu wa mashirika ya ukiritimba na wafanyibiashara, nao ndio wenye kuathiri katika sera zake. Lakini kwa kuangalia kwamba kila mmoja kivitendo anufaika na haki ya uraia na aweza kuathiri katika utawala, sawa iwe ni upande wa uchaguzi, au kwa upande wa kuwajibisha, hivyo basi Marekani hudhihirika katika utawala wake kwamba ni utawala wa raia wote zaidi ya nchi nyenginezo za kirasilimali. Na kwa kuangalia utajiri wake ambao ni chemichemi isiyokauka, na kwa kuangalia pia wingi wa wasomi wenye thakafa na mufakirina ndani yake, na kadhalika tukiangalia hali ya (uhuru) na hali ya uchangamfu iliyotanda humo: basi hakika nguvu zake ni nguvu za kihakika wala sio nguvu za dhahiri tu. Na wamarekani japo sio watu wa kale katika uwepo wao, kwani ni watu binafsi na makundi yaliyotoka maeneo tofauti, lakini uraia na uzalendo unawaunganisha kwa kweli katika fungamano lenye nguvu, bali hata mgeni anayeishi miaka michache na kisha achukuwe uraia na awe na haki ya uraia, basi huwa na pupa juu ya nchi, raia, na maslahi zao zaidi ya pupa yake kwa nchi yake ya asili. Hili limetokana na nguvu ya nchi katika watu wake, na katika mahusiano baina ya watu.


Ama kuhusu sera zake za nje: ni sera za matajiri na watu wenye mashirika ya ukiritimba, yaani ni sera za kikoloni tu, hazina nafasi ya kuchunga thamani/maadili ya juu. Na pamoja na ujinga wanaodhihirisha wanasiasa wake ambao wakati mwengine wakaribia kuwa mpumbavu, lakini hakika huwa wana undani wa kufikiria huwashinda wanasiasa wengi ulimwenguni, pia ni wepesi sana wa kubadilisha, kubuni mbinu tofauti, na kutatua matatizo. Huenda msukumo wa kikoloni na thakafa yao ya juu ndio zenye athari katika uchangamfu wao wa kisiasa, kwani wao huuangalia ulimwengu wote kama shamba lao, na huangalia nchi zengine zilizowahi kuwa kubwa kwamba hazistahiki kuwa na ushawishi wowote na kwamba sasa ni lazima zistaafu zipumzike, na ziridhike na vile ulimwengu wote ulivyo: kunyenyekea udhibiti wa wenye nguvu.


Marekani leo yamiliki kiwanda kikubwa cha silaha za kinuklia yashinda mara nyingi zaidi ya zinazomiliki nchi zengine za nuklia zikikusanywa kwa pamoja. Bajeti ya jeshi la Marekani ukilinganisha na nchi zengine kubwa hudhihirisha jinsi Marekani inavyozishinda nchi hizo, katika mwaka wa 2002 M bajeti za kijeshi za nchi kubwa za kimagharibi zilikuwa kama ifuatavyo:

1. **Uingereza: Dolari bilioni 35.**
2. **Ufaransa: Dolari bilioni 32.**
3. **Ujerumani: Dolari bilioni 23.**

**Jumla: Dolari bilioni 90**

Wakati Marekani peke yake ilitumia dolari bilioni **350**.




Mbali na hayo, kuna tofauti ya aina za silaha zenyewe. Na baadhi ya wasomi wanasema: kwamba Marekani imeizidi Ulaya kwa makumi ya miaka katika maendeleo ya teknolojia. Pia Marekani yadhibiti umoja wa mataifa na mashirika yanayotokana nayo, yamiliki fungu kubwa katika benki kuu ya kimataifa (WB) na shirika la kifedha duniani (IMF) hivyo basi imedhibiti nguvu pana za kisiasa inayofanywa na benki ya dunia na shirika la fedha juu ya serikali za dunia. Marekani pia imeenda mbio kuzitilia nguvu bishara zake kwa njia ya sera za utandawazi, ikaandalaa shirika la biashara za kimataifa na kuitumia kama moja ya mbinu zake za kuingilia masoko ya maeneo kwa hoja ya ushuru mmoja wa forodha, ikatekeleza hilo kwa kuziacha huru biashara. Na kwa sababu kwamba yamiliki uwezo mkubwa wa kiuchumi, na ina idadi kubwa ya mashirika yenye uraia tofauti au yanayovuka bahari, basi imefaidika na pazia ya kikanuni inayopewa na shirika la biashara za

kimataifa ili kufungua masoka yaliyokuwa ni kama yamefungwa au yaliyokuwa na ugumu wa kujiingiza katika uchumi huru wa kiulimwengu unaosimamiwa na Marekani.

Uwezo huu mkubwa wa kijeshi, kisiasa, na kiuchumi umeifanya Marekani kuingilia nchi zote ulimwenguni na kufanya hilo ndio sehemu ya sera za serikali zote ulimwenguni leo, ikijaribu kutekeleza sera za ubabe juu ya nchi zote bila ya kubagua, hakuna tofauti baina ya nchi zilizoendelea na zilizo nyuma, pamoja na kushindwa kwake wakati mwengine katika huo ubabe, lakini haiwachi kujaribu kudhibiti.

Kwa hivyo, Marekani ina mchangio mkubwa katika matatizo yote yaliyopo ulimwenguni, ndio inayowasha moto wa mivutano katika maeneo yanayowaka, imeleta mpangilio mpya wa nchi kwa kutumia mfano wa istilahi ya "nchi za mkondo wa shari" na istilahi ya "nchi zinazochunga/fadhili ugaidi" au yanayofanana na hayo katika usanifu ambao hata nchi ambazo ni washirika au ni wafuasi wake zote hazikusalimika na madhara yake, bali iliwajibisha ulimwengu ima uwe pamoja naye au uwe na ugaidi, ama kutokuwa na wao au kutokuwa na ugaidi hilo halikubaliki.

Marekani huzua matatizo na kusababisha mivutano, kisha baadaye huendesha mivutano hii, na kuzitafutia suluhisho. Na hufanya yote hayo kwa kuzingatia kuwa ni sehemu katika mikakati yake ya kuutawala ulimwengu na kuudhibiti.

Marekani imezitumia vibaya sana nguvu zake za kijeshi na kiuchumi katika vitendo vyake vya kisiasa, kwani ushawishi wake haukufungika kwa upande wa kiuchumi na kibiashara kama ilivyo hali ya nchi zengine za kikoloni, bali ikaieneza ushawishi wake katika Nyanja zote za maisha ya kiraia: kielimu, vyombo vya habari, jamii, fikra na thakafa, na usalama.

Ama katika masomo: dori yake imekuwa wazi katika kubadilisha mitaala ili iende sambamba na mitazamo yake ya kiaidiyolojia. Ndio maana tukapata dole za kiarabu kama vile

Saudia, Kuwait, Jordan, Misri na nyenginezo, zasumbuka katika kuangalia upya mitaala yake kwa hoja ya kuiboresha ili iende sawa na wakati. Saudia ikabadilisha mojawapo ya masomo muhimu ya kidini katika madrasa, kifungu kigawanyo cha ((al walaa-u wal baraa-u)). Na Jordan, Misri, Kuwait na nchi zengine zikabadilisha masomo yanayohusiana na kupambana makafiri wenye uwadui miongoni mwa Mayahudi na Manasara na kupigana nao, na yanayofanana na hayo katika fikra za kiislamu ambazo Marekani anazichukia.

Ama katika vyombo vya habari: Marekani hutenga mamia ya mamilioni ya dolari kwa ajili ya kuwaathiri waarabu na Waislamu kihabari, ikaanzisha ((Radio sawa)) na stasheni ya Runinga ya ((Al-hurra)) ili kueneza sumu zake ndani ya kila nyumba katika miji ya kiarabu.

Na katika upande wa kijamii: Marekani ikasisitiza juu ya mwanamke, ili kumuweka mbali na maadili ya kiislamu, na ikatenga mali, na kuzishinikiza serikali ziweke makongamano kwa ajili ya mwanamke, ikashinikiza kumtia mwanamke serikalini na bungeni, na ikaenea upya fikra ya uhuru wa mwanamke kwa mbinu mpya na mitindo mipya.

Ama katika upande wa fikra na thaqafa: Marekani imekusanya vituo vya fikra, demokrasia, vyama vingi, na ikabuni mashirika ya haki za kibinadamu, vikawa vituo na mashirika haya yaeneza fikra za uhuru kwa ufahamu wa kimagharibi, na kwa njia ya kimarekani, na ikayasaidia mashirika haya na vituo hivi kwa filamu za *Hollywood* na uzalishaji wa kisanaa za kiteknolojia za kisasa zinazotawala katika vipindi vingi vya Runinga za kiarabu na zisizokuwa za kiarabu.

Ama kwa upande wa usalama: ilichofanya Marekani ni kufungamanisha vitengo vya kijasusi katika nchi za kiarabu na serikali zilizopo katika ulimwengu wa kiislamu na vitengo vyake vya kijasusi na haswa vitengo vya CIA na FBI, mpaka tumekuwa twawaona majasusi wa Marekani wakizurura ndani ya miji ya

kiislamu wakiwa na uhuru kamili, chini ya ulinzi wa kanuni kama hali ilivyo Sudan, Yemen, Kenya, Tanzania, Libya, Pakistan na nchi nyenginezo. Huku kufungamanisha kwa ujasusi ni pamoja na kuwasalimisha wanaotakikana na Marekani, na kuruhusu uwepo vikosi vya Marekani haswa kwa kazi maalum dhidhi ya wale ambao Marekani yawaita kuwa ni “magaidi”.

Hivi ndivyo mikono ya Marekani ilivyoingilia maisha ya kila siku katika mujtama za miji ya kiislamu na katika mujtama za miji isiyokuwa ya kiislamu, ikaeneza uharibifu humo kama apendavyo, kama afanyavyo Mashariki ya kati, Afrika, Kusini mwa Eshiya, mpaka Latin Marekani. Ikamuangusha Aristide kiongozi wa Haiti aliyechaguliwa na kumhamisha nje, na yenda mbio sasa kumuangusha Chavez raisi wa Venezuela kwenye utawala. Kwa hiyo ikawa Marekani imezidhibiti nchi dhaifu kwa sababu ya watawala wake kunyenyekea na kujidhalilisha kwake.

Lakini kudhibiti huku kwa Marekani hakutodumu mda mrefu, kwani yaelekea kuondoka, licha ya Marekani kuonekana kila pembe ya dunia, licha ya watawala na serikali zao kusaidia kuwepo huku, lakini kuzidi kwa chuki za watu haswa ya Waislamu dhidi ya Marekani, na wengi kuwachukia wamarekani kwa sababu ya kujiona kwao na kibri chao na wao kupendelea Mayahudi, na kwa sababu ya ukoloni wao na utumwa wao kwa wengine, twasema: Hakika hizi chuki zinazozidi kukuwa zitasababisha mapambano na mvutano dhidi ya uwepo wa Marekani kila mahali, sawa iwe ndani ya bara lake au nje yake. Ukiongezea juu ya hayo nchi kubwa zengine kupatwa na dhiki na maslahi yao kuharibiwa kwa sababu ya ubabe wa Marekani na kunyakua manufaa peke yake na kujaribu kwake kudhibiti koloni, na pia kujaribu kwake kukiritimba katika kusimamia mambo ya kimataifa.

Hakika kuwepo kwa nchi inayotabani mfumo wa kirasilimali uliosimama juu ya ukoloni na kunyonya damu za wengine, nchi hii kuongoza ulimwengu pasi na kupatikana nguvu nyengine sawa inayoshindana nayo katika kuupeleka ulimwengu, hufanya

ulimwengu kuwa katika mateso ya kuendelea, matatizo na majanga ya kufuatana na kufuatana, kama inavyoonekana Marekani ilivyoharibu ulimwengu na kuzusha matatizo.

Mateso ya ulimwengu yanayotokana na nchi za kirasilimali na haswa Marekani hayataondoka ila kwa kusimamisha serikali ya Khilafahh itakayotabikisha mfumo wa haki: Uislamu mtukufu ulioteremshwa na Allah kwa Mtume wake (s.a.w) ili uwe rahma kwa walimwengu, hapo ndipo uadilifu wa Uislamu utakapofichua uovu wa urasilimali na fikra yake ya kimada na njia yake ya kikoloni. Vile vile nguvu bora ya Uislamu itakomesha dhulma za Marekani na kiburi chake, na kuilazima irudi kwenye kutenga kwake na ibakie katika ulimwengu wake mpya, kama basi itakuwa na ulimwengu mpya wakati huo, kisha kheri ienee kote ulimwenguni, ulimwengu upumuwe baada ya kuteseka na shida na mateso mda mrefu.

5. **Ama kuhusu taifa la Uingereza:** Hakika uvuvi wa samaki na uundaji majahazi ndio zaidi tangu kuinukia kwake, kisha kukapatikana ubaharia na biashara kwake, hili likawajengea tabia ya uvuvi wa maslahi, kuwatumia watu, na tabia ya mfanyibiashara. Na kwa kuangalia udogo wa nchi yake ikawa ni lazima kutafuta msaada kutoka kwa wengine, kama ilivyo kawaida ya wavuvi kusaidiana baharini, ni mara chache mvuvi kutoka peke yake. Kisha ulipokuja mfumo wa kirasilimali wakauingia na kipimo cha maslahi kikakita kwao, ndio maana utapata maisha ya kisiasa ya Uingereza tangu ilipopatikana hadi sasa imesimama juu ya kutegemea wengine, na kuweka chambo kila inapotaka kushika kitu, sawa iwe ni kukoloni nchi au inapotaka msada wa nchi. Kwa hivyo siasa zake zote zimesimama juu ya miungano, makundi, na kushirikiana katika ukoloni, ni kwa sababu hiyo ndio katika karne ya kumi na tisa ikashirikiana na nchi zengine katika kukoloni na ikawaachia wenzake ili wakoloni baadhi ya nchi ili wawe upande wake katika kutetea maslahi yake. Ndio maana ikaitia Ufaransa Mashariki ya kati baada ya vita vya mwanzo vya dunia, ili isimame upande wake inapopatikana hatari katika

> maeneo hayo, na kuiweka mbele yake mpaka ikasemwa: Hakika Uingereza hupigana mpaka mwanajeshi wa mwisho wa kifaransa.

Hivi ndivyo zile tabia za Uvuvi wa samaki zilivyozalisha kwake tabia za kutaka msaada ili kufikia maslahi yake. Kisha kuna tabia nyengine aliyojulika nayo Uingereza, bali ndio katika tabia zake muhimu zaidi, nayo ni kushikamana na ya kale na kutoyabadilisha au kuyaendeleza isipokuwa polepole na itakapokua hakuna budi ila na mabadiliko, basi watu wa Uingereza ni wahafidhina kikweli. Nayo tangu zamani hadi sasa yadhibitiwa na familia kongwe, matajiri na wenye rasilimali kubwa, licha ya madai kuwa yaenda kidemokrasia na kwamba ni taifa la kidemokrasia, lakini kwa kuangalia kwa makini yabainika kwamba sio hivyo, kwani raia hawana athari yoyote katika kuleta viongozi, bali wanaomchagua kiongozi ni zile familia kongwe na wenye ukiritimba na si raia, wala hakuna tofauti katika hilo baina ya zama zilizopita na sasa, kwani bado mpaka sasa kama ilivyokuwa zamani wenye maamuzi ya hatima yake ni familia kongwe na warasilimali. Ilikuwa tangu zamani kila harakati yoyote ya kiraia inapojitokeza ndani yake basi Uingereza hupambana nayo kikatili na kuimaliza kwa mbinu chafu kama iliyvyo yenyewe. Na mapinduzi ya Cromwell inayojifakhiri nayo Uengereza hayakuwa mapenduzi ya raia bali ni mapenduzi ya familia kongwe dhidi ya mapenduzi ya kiraia. Kwa sababu wakati huo mapenduzi ya kiraia yalitaka kuuondoa uongozi wa familia kongwe ya kirasimali, na yalikaribia kufaulu, lakini hizo familia kongwe zikafanya njama zikamtuma Cromwell ili kuleta mapinduzi akidai baadhi ya haki na watu wengi wakamuunga mkono, wakapewa baadhi ya madai yao, akayamaliza mapenduzi ya kiraia na kuyaua tangu mwanzo.

Chama kinachotawala Uingereza tangu makumi ya miaka ni chama kihafidhina *(Conservative)*, ama chama cha wafanyikazi hakikuwa isipokuwa ni chombo kinacholetwa Uingereza inapokihitajia, au pindi kutakapokuwa na mambo yatakayoshinda

chama cha kihifadhina kuyatatua, ndipo huitwa chama cha wafanyikazi na kutumika katika kuyatatua. Na yaonyesha kwamba viongozi wa chama cha wafanyikazi mwishowe walijua uhakika huu wakajaribu kuenda nao, ikawa vyama viwili hivi kupokezana utawala ni kama tu kubadilishana zamu baina ya wahafidhina na wafanyakazi, kuliko chama cha wafanyikazi kuwa ni chombo mkononi mwa wahafidhina. Ndio maana twapata kwamba Tony Blair kiongozi wa chama cha wafanyakazi sasa (2009) na ambaye ni waziri mkuu wa Uingereza amebadilisha tabia ya chama na kukaribia sana sera za chama cha kihafidhina. Na katika sura ya siasa kikadhihirika kwa njia isiyotafautina na sura ya vigogo wa chama cha kihifadhini, mpaka akamfanya Margaret Thatcher aliyekuwa kiongozi wa chama cha kihafidhina kuwa ndio kielelezo chake katika sera za ndani za nje. Hivyo chama cha wafanyikazi kikawa hakitafautiani sana na chama cha kihafidhina, vyama hivi viwili Uingereza vikawa ni mifano wa vyama vya jamhuri na demokrasia ndani ya Marekani.

Chama chenyewe cha wafanyikazi ndani yake kukipatikana watu wanaojua kuwa Uingereza yadhibitiwa na familia kongwe na warasilimali, basi watu hao huwekwa katika dhurufu zitakazowaeka mbali na kuathiri katika chama na kuathiri katika siasa. Mwanachama wa wafanyakazi Bevan miaka ya thalathini hadi miaka ya sitini, na George Brown katika miaka ya sitini: hawa ni mfano bora katika kuonyesha kwamba chama cha kihafidhina kinadhibiti mpaka chama cha wafanyakazi, na kwamba wale wanaotaka kuweka mpaka kwa udhibiti wa nguvu ya utawala katika utawala hao hutengwa mbali. Na chama cha kihifadhina chenyewe pia hakichagui viongozi wake, bali huteuliwa na kiongozi aliyetangulia, kama Macmillan alipomteuwa Lord Hume na Margaret Thatcher alipomteuwa John Major. Hata kama Thatcher na Major walichaguliwa lakini ni uchagusi wa kisura tu kwa sababu kwanza huteuliwa kisha uchaguzi hufanyika kisura. Kwa hivyo, nidhamu ya kiutawala Uingereza, hata ikiitwa ya kidemocrasia

lakini uhakika wake ni kuteuliwa, na huteuliwa na tabaka maalumu, nalo ni familia kongwe, mabepari, na wenye ukiritimba.

Kwa kuzingatia kuwa Uingereza ni kisiwa katikati mwa bahari, kisiwa chake hakitoshelezi wakazi wake kwa maisha yao, hivyo basi kutoka kwao kisiwani ili kutafuta maisha ni jambo lisilokuwa na budi. Lakini hata wakitoka kwa ajili ya biashara, hakika huwa wametoka kwa ajili ya kukoloni na sio kwa ajili ya biashara, wametoka ili kunyonya damu za mataifa mengine na kupora mali zao sio kutaka kubadilishana mali, kwa sababu mwanzoni hata hawakuwa na mali ya kubadilishana, basi wakatoka ili kutafuta mali. Hii ndio iliyokuwa hali yao tangu walipotoka kisiwani, na waliposhikana na mfumo wa kirasilimali na maslahi kuwa ni sehemu yake isiyoweza kuepukana nayo, mfumo huu ukakubaliana na tabia yao, basi ukoloni ukakita mizizi ndani yake ikawa ni nchi ya kikoloni daraja ya kwanza. Kisha walipokuwa kiidadi ni wachache wala hawawezi kusimama mbele ya nguvu iliyowazidi, basi walijiokoa kwa kuwatumia watu wengine na serikali mbalimbali kuwasaidia, na hii misaada wakaiweka kwa miundo ya washirika, miungano, makongaman, na mikataba. Ndio sababu miungano ni sehemu isiyoweza kujitenga nayo katika siasa yake.

Na waingereza japo katika werevu ni kama watu wengine lakini tofauti ni kuwa wanatumia werevu wao hadi kiwango cha mwisho kabisa, ndio maana wakabobea katika kufahamu matendo, kufahamu siasa, na katika kutatua matatizo, aqliya ya kutatua matatizo ikawa wazi kabisa kwao. Kwa kuangalia ya kupanuka wakaweka viwanda vyao kwa msingi wa viwanda vya kivita, hali iliyopelekea wao kujenga nchi ya kihakika: wakiwa na nguvu za kivita, ala za kivita, nguvu ya kiviwanda, mbali na ujuzi wao wa kindani katika siasa na utawala, pamoja na ujanja mchafu wanaosifika nao mara nyingi.

Ama kuhusu sera yao ya nje: hakika hii yasimama juu msingi wa kikoloni, lakini ndani yake hudhihirika mambo mawili: **Kwanza**: kuhifadhika uwiyano wa kimataifa. **Pili:** kuhifadhi uwepo

wao katika siasa za kimataifa bila kujali thamani itakayowagharimu. Ndio maana walishiriki katika vita vya kimsalaba kwa sura ya wazi, na katika “muungano mtukufu” wakawa katika nchi kubwa zilizo mbele-mbele, na alipotokea Napoleon na ukombozi waliongoza vikosi vilivyomvunja na kumrudisha mfaransa alikotoka, na wakati Ujerumani ilipotaharaki katika zama za Bismarck basi Uingereza ilishiriki katika kongamano la Berlin, ikiwa katika malengo yake ni kuziwekea mpaka nguvu za Ujerumani, na ilipohisi kwamba nguvu za Ujerumani zakuwa kwa namna isiyo ya kawaida basi ikamtangazia vita na akampiga katika vita vya kilimwengu mara mbili, na akajaribu kuuvuta ulimwengu wote kwenye vita vya kilimwengu ili kubadilisha ramani ya ulimwengu na kwa ajili ya kudhoofisha wababe wawili wakubwa wa wakati ule (Marekani na Muunano wa sovieti) waliokuwa wakitawala ulimwengu katika kipindi cha mapatano. Na Uingereza ilipotengwa na siasa za kimataifa baada ya mkataba wa wababe wawili ikawa kama iliyokosa muundo wake, basi ikawa yenda kiubaguzi huku ikijaribu kwa bidii sana kurudisha uwepo wake kimataifa na kushiriki katika siasa ya kimataifa.

Na Uingereza hutegemea mbinu ya kufunga mikataba na nchi, kutafuta watu na kuathiri kupitia kwao, wala haijali kumlisha mtesi wake chakula kikubwa katika njia ya maelewano, na katika siasa haimtambui rafiki wala adui, bali inachotambua ni maslahi tu wala haijui jengine, na hata kile kinachoitwa “maadili ya kiamatifa” hukichulia kuwa ni chombo cha kuhadaa lakini haiamini kuwepo kwake. Na hutumia uongo kama silaha yake ya maana sana yenye kuathiri katika siasa zake, ingawa yajaribu usidhihirike kwake ili watu wamuamini. Churchill aliyekuwa waziri mkuu wa Uingereza katika mkutano wake na Roosevelt na Stalin katika mazungumzo yao kuhusu vita na hali ya baadaye ya Ujerumani, ikawa katika yale aliyowaambia kwa uwazi kabisa ni: “Ukweli katika vita ni wenye thamani kiasi kwamba ni lazima kuufadhi kwa urongo kamili” maneno haya yakionyesha kwa kiwango gani urongo ni jambo msingi katika siasa za Uingereza.

Huu ndio uhalisia wa Uingereza na uhalisia wa siasa zake. Kwa hivyo kuamiliana nayo ni lazima kuwe juu ya msingi kwamba ni nchi ya kikoloni, na kwa msingi kuwa yaishi kwa kuwatumia raia wake. Wala miaka na matukio hayakuweza kubadilisha njia yake hii, na kwamba ilipangia njama mapenduzi ya kiraia waliyoyatekeleza ili yasifaulu. Kadhalika kupambana na ukoloni wake haitowezekana ila kwa kujua mbinu zake, na kwa makabiliano ya wazi yaliyoambatana na uhodari unaoonekana kama ujinga, lakini yaliyo na mbinu zilizofichika. Uingereza ikiwa ndani ya miji yake nguvu zake ni kama mshairi alivyosema: "Na nitibu kwa yaliyokuwa maradhi". Na nguvu zake nje ni kuwatumia wengine kwa ajili ya maslahi yake, huwatumia hata wale wanaopambana naye. Kwa hivyo, hakuna njia ya kumshinda isipokuwa kwa kumpokonya silaha zake za jadi za kisiasa, na kupambana nayo ikiwa peke yake bila ya kuwa na wa kumnusuru au mshirika.

6. **Ama watu wa Ufaransa:** Ni watu waliojenga nchi yao kongwe kati kati ya Ulaya, na wanajifakhiri juu ya nchi zengine za Ulaya kwamba taifa la Ufaransa ndilo lililokuja na fikra za juu kama vile: *uhuru*, *uadilifu*, na *usawa*, na kwamba yajulikana kwa kutoa watu wa kipekee katika siasa na fikra. Na Ufaransa kwa namna yoyote ile pia ni nchi ya kikoloni, yatafautiana na nyenginezo kwa kuathirika na fikra za uhuru, kwa sifa yake kua ni sifa ya juu zaidi ya mtu binafsi, sifa iliyobadilika na kuwa umbile miongoni mwa maumbile, bali tabia katika tabia zao.

Taifa la Ufaransa tangu lilipofanya "uhuru" kuwa ndio fikra yake basi mgawanyiko umekuwa ndio asili yake, ikawa yafanana zaidi kuwa ni mkusanyiko wa watu binafsi kuliko kuwa ummah au taifa au kundi. Ndio maana ni nadra kwao kuwa na serikali zenye nguvu, na ni mara chache kutawaliwa na serikali yenye nguvu, kwa ajili hiyo ikawa rahisi kwa Uingereza kuitumia Ufaransa mara kwa mara. Kwa hiyo Ufaransa baada ya kuondoka Napoleon hadi zama za de Gaulle, yafuata mkumbo wa Uingereza, kwa sababu ya fikra

ya uhuru kumakinika kwake, hata wakati Ufaransa ilipotoka ili kuikoloni Marekani, Urusi, na Afrika hakika Uingereza ndio iliyoitoa ili ipate nguvu, hata kama katika historia ya ukoloni yadhihirika kama kwamba hizi nchi mbili zilikuwa katika mashindano.

Kwa hivyo, hakika mtu hawezi kuhukumu taifa la Ufaransa kwa sifa moja maalumu zaidi sifa ya uhuru. Sifa ya *uhuru wa kifikra* ikazalisha: wanafalsafa, washairi, mufakirina na wengineo. Na *uhuru wa kisiasa* ukazalisha: hadhi, heshima, na kujiamini, na ukaleta kundi kubwa la watu wa kipeke yao. Na *uhuru wa kibinafsi* ukafanya Paris kuwa ndio kituo cha umalaya, machafu, na kukimbilia matamanio na ladha. Uhuru hizi ndizo zilizoleta mwanya wa wageni kuingia humo haswa Uingereza. Kwa hiyo, uhuru kwa maana yake kamili huchukuliwa kuwa ndio msingi wa balaa ndani ya Ufaransa.

Wala mtu hawezi kusema kwamba Ufaransa kuna vyama kadhaa, na kwamba chama fulani ni kadhaa na chama fulani ni kadhaa, kwani ni vigumu bali haiwezekani kwa watu ambao hii ndio hali yao kuwa na vyama kwa maana ya chama, bali hupatikana tu mikusanyiko ya watu binafsi wakajiita “chama”. Ndio maana ni vigumu kupatikana utawala wenye nguvu au utawala uliomakinika, kwa sababu kila mfaransa ajitawala mwenyewe, na kila mfaransa atamani kuwa mtawala! hivyo basi mtu hawezi kusema kwamba sera ya kindani ya Ufaransa ni kadhaa na sera ya kifaransa nje ni kadhaa, kwani sera ya kindani huwa kulingana na hisia za watawala na kulingana na ufahamu wake kuhusu uhuru. Na sera ya nje yaenda kulingana na uwezo wa Ufaransa wa kushinda wengine ili kuwakoloni na kueneza ushawishi wake kwao. Ufaransa yazingatiwa kuwa ni nchi ya kikoloni, kwa kuwa inaamini mfumo wa kirasilimali, hivyo manufaa/maslahi ni kiungo msingi katika maisha ya kifaransa, ndio maana ikawa na pupa ya ukoloni na kuwa na pupa ya kubakia koloni hizo.

Ikiwa hakuna budi kupeana fikra jumla kuhusu sera ya nje ya Ufaransa, basi yaonekana kuwa siasa/sera yake imejengwa juu ya

msingi wa kujipatia ushawishi wa nje, sawa iwe ni kwa makoloni, au kwa ushawishi wa kithakafa, au wa kiuchumi. Na matendo yake ya kisiasa dhidi ya nchi kubwa hakika yalenga kudhihirisha utambulisho/shakhsia yake, na kushiriki katika utukufu na udhibiti. Na Ufaransa haijui vizuri mitego na mbinu za kisiasa, bali zaidi mara nyingi hutumia makabiliano ya moja kwa moja, ndio maana ni rahisi kugundua kuwepo kwa mvutano baina yake na Marekani katika zama hizi, lakini ni vigumu kugundua hilo kati ya Marekani na wengine haswa Uingereza. Kwa hiyo, njia ya kufuatwa katika kupambana na matendo yake ni kutokujeruhi kiburi chake, na kutoimakinisha kuanzisha jambo mwanzo, na kutoizingatia kuwa ni nchi kubwa isipokua kwa kiwango kinachokubaliwa na nchi kubwa zengine katika siasa ya kimataifa.

7. **Ama taifa la Urusi:** Ni watu wenye uchangamfu na nguvu, lakini wana ujinga na ukawaida. Nao japo mwanzo walijiunga na mfumo wa kirasilimali, kisha ukoministi, kisha wakarudia tena mfumo wa kirasilimali, lakini bado walibakia kuwa nyuma ya Ulaya, wala hawakufika daraja ya mataifa ya Ulaya. Kwa hivyo Urusi ikawa na kifundo cha upungufu kwa watu wa Ulaya, na kifundo hiki kikawa na athari hasi katika nyendo zake dhidi yao.

Taifa la Urusi ni taifa la kupigana, lina ushujaa ndani ya miji yake, lakini linapotoka nje yake hukosa sifa zake, ndio maana ilitarajiwa kukosa udhibiti wake juu ya nchi za mashariki ya Ulaya tangu kipindi kirefu, na ndio hivi sasa ishazikosa kihakika baada ya kukosa kwake muungano wa kisovieti. Na hakika za kihistoria zathibitisha kwamba Urusi haijawahi kushinda ikiwa nje ya miji yake katika matukio yote ya kihistoria, na tatizo la Chechniya ambayo ni nchi ndogo lathibitisha hilo. Lakini hapo-hapo ilikuwa ikiwashinda maadui zake wanapomvamia ndani ya miji yake, na miongoni mwa ushindi wake mashuhuri ni wakati ilipovamiwa na Napoleon na Hitler ndani ya miji yake.

Nidhamu ya kiutawala ya Urusi wakati wa makaisari ni tofauti na ile ya wakati wa ukoministi, na pia ni tofauti na ya wakati wa sasa, lakini katika hali zote ni ya udikteta na ukandamizaji. Kwani Kaisari alikuwa akitewagemea haswa wabepari wa ardhi, na mabwanyenye wenye kumiliki ardhi wakiungana na matajiri wakubwa wakawa ndio wanaodhibiti nchi kama mabwana, wakawa wanaunga mkono kikamilifu sera za kindani na nje za kikaisari, wakawa hawa wote wakiwanyanyasa vibaya raia, hali iliyopelekea nchi kuporomoka na raia kurudi nyuma.

Na Urusi kabla ya vita vya kwanza vya dunia ilikuwa nyuma kuliko Ulaya, ikitumiwa na baadhi ya nchi za Ulaya, kwani viwanda vya kimsingi ndani ya Urusi vilikuwa mikononi mwa Ufaransa, Uingereza na Ubelgiji. Na mitambo muhimu ya kuchimba madini ikawa mikononi mwa wafaransa, na kiwanda cha makaa huko Donitess kikawa katika mikono ya wageni, na karibu nusu ya visima vya Petroli vikiwa viko mikononi mwa Uingereza na Ufaransa, na kiwango kikubwa katika faida za viwanda vya Urusi huenda kwenye benki za kigeni, haswa benki za Uingereza na Ufaransa. Kwa hiyo nchi hii mpaka mwaka wa 1914 ilikuwa imerudi nyuma katika nidhamu ya kiutawala, kiuchumi, kithakafa na kielimu pamoja na hayo Urusi ilikuwa ni nchi kubwa, na kimataifa ilizingatiwa kuwa ni katika nchi kubwa, na ilikuwa ikiathiri katika siasa ya kimataifa. Na chama cha kikoministi kiliposhika uongozi hali ya uongozi haikubadilika isipoluwa katika mbinu tu, kwani wakoministi waliongoza nchi kwa chuma na moto, kuua na umwagaji wa damu, mateso na ugaidi, wakamakinisha utawala wao juu ya fuvu za raia. Wakaweza kuilazimisha nchi ya kwanza kuachana na fikra ya kuipiga vita, wakaingia katika mikataba nayo hadi ikawa mshirika wake au kama mshirika, hadi ikawa Urusi (muungano wa kisovieti) na nchi ya kwanza wanashirikiana kuendesha ulimwengu, bali kiuhakika ulimwengu wote ukawa watawaliwa na wababe wawili tu: Urusi na Marekani.

Ama siasa ya Urusi ya kikoministi ilikuwa imesimama juu ya fikra, kwani fikra yake ilikuwa ni kueneza ukoministi, na njia yake

ilikuwa ni: uharibifu, kuvunja, na kubomoa, kusababisha migongano, nayo kila mara ikipata nafasi basi hujaribu kuingiza Ukoministi katika baadhi ya nchi, kama inavyojaribu kuzidhibiti nchi ambazo nidhamu yake ya kiutawa ni nidhamu ya kikoministi.

Ama baada ya kuporomoka ukoministi watu wa Urusi na viongozi wake walijikuta wakiwa na haja ya utambulisho mpya unaotafautiana na Urusi ya kikaisari, na unaotafautiana na kipindi cha ukoministi, wakarudia urasilimali, basi hali yake ikazidi kuwa mbaya, sura ya Urusi na nafasi yake ulimwenguni ikatingishika.

Kwa hivyo, nidhamu ya kiutawala ya Urusi imekuwa ni ya kirasilimali, ikawa yafanana na zama za makaisari, pamoja na kuhifadhi baadhi ya alama za kipindi cha ukoministi. Tabaka la mabepari na wenye utajiri makubwa wakarudi na wakaathiri katika utawala kikamilifu kama hali ilivyokuwa katika zama za kaisari, lakini mara hii badala ya makaisari Urusi ikawa yatawaliwa na majasusi wa kisovieti waliotangulia (KGB) na wanasiasa wa zamani, waliobadilisha ngozi zao wakawa warasilimali kulingana na mtindo mpya.

Ama kuhusu sera yake ya nje: imekuwa ni kuelekeza juhudi zake katika kuwa na dori tu, pasina kuwepo mtizamo wa kilimwengu katika sera ya nje. ndio maana uwepo wake katika ulingo wa kilimwengu ukadhoofika, ikawa yatafuta tu iwe na japo na nafasi yoyote ile na asitolewe kabisa katika siasa za kimataifa. Hali hii ya watu wa Urusi kukosa utambulisho wa fikra ya kiitikadi na hali ya kufilisika kisiasa kwa ngazi ya watawala na raia wa kirusi, yatoa fursa ya kuweza kusimama mbele ya siasa za kirusi kwa kutengeneza mahusiano ya kibiashara na Urusi ili kuwawezesha Waislamu kuingia Urusi na ili Urusi iweze kuuona Uislamu ukiwa hai katika mahusiano ya watu. Na kupambana na majaribio ya Urusi ya kuathiri katika siasa za kimataifa ni kwa kutoipatia fursa ya kufanya hivyo, na kufunga nayo mahusiano upande wa kibiashara tu na kupambana nayo katika nyanja zengine kama inavyotakiwa kufanyiwa nchi zengine za kirasilimali, kwa sababu sera yake ya

kigeni imejengwa juu ya kupora na kukoloni, hata kama haya hayadhihiri isipokuwa katika nchi zilizo jirani jirani nayo.

Hakika mataifa manne ya mwisho: Marekani, Uingereza, Ufaransa, na Urusi ndizo nchi ambazo kwa sasa zatambulika kuwa ni nchi kubwa zenye tamaa ya kutawala katika siasa za kimataifa maeneo tofauti-tofauti ulimwenguni na kuyazozania, pamoja na kutofautiana baina yao kwa nguvu na udhaifu. Na kwa kufuatilia athari zake katika siasa za kimataifa katika karne hii ya ishirini na moja miladi, twaweza kueleza kiufupi misingi jumla ya kisiasa za hizi nchi nne kama ifuatavyo:

**Ama Marekani:** Nguvu zake zimekuwa kwa njia ya haraka haraka tangu kuanguka kwa muungano wa kisovieti kighafla, hivyo ikawa ndio nchi kuu yenye nguvu za kuathiri ulimwengu, haswa na kwamba pengo lililowachwa na muungano wa kisovieti hakuna nchi yoyote kubwa iliyoweza kulijaza, mpaka Marekani ikawa ndio nchi kubwa pasina mvutano, na mpaka sasa hakuna nchi yoyote miongoni mwa nchi kubwa iliyopanda hadi daraja ya pili iliyokuwa ikiwakilishwa na muungano wa kisovieti. Hali hii mpya katika hali za kimataifa iliyofanya Marekani kuwazidi wengine, ndio iliyowapelekea wanasiasa wa kimarekani kujawa na kiburi na kujinaki katika kuamiliana na wengine, huenda ikawa maneno ya waziri wa mambo ya nje wa Marekani wakati wa Clinton Bi Madeleine Albright yaelezea kuhusu hali hii, pale aliposema: *“Hakika Marekani ni (ummah-dharura) nayo ndio yenye majukumu ya ulimwengu, iko tayari kufanya chochote, wakati wowote ikitaka. Na wote wajue kwamba sisi twafanya tutakavyo na twabadilisha tutakacho, wala hakuna vizuizi vyovyote vitakavyosimama njiani mwetu. Kwa sababu ulimwengu wote ni wetu, ulimwengu ni wa wamerikani”.*

Huku kujinaki na kujigamba katika siasa ya kimarekani kulisababisha mpaka watu wa Ulaya waliokuwa washirika wake kuwa hawatoweza kuvumilia kujikuza kwake ulimwenguni, wala kuvumilia matamko hayo kwa sauti ya juu ya kujitukuza. Ndio

maana wakamrudi kupitia magazeti yao iliyokuwa ikieleza kuudhika kwao, gazeti la kifaransa (Le Monde diplomatique) likasema kurudi tamko la Albright: *"Hakika udhibiti wa Marekani hakufai kuwa ndio majaaliwa yasiyokuwa na budi, Marekani ifahamu kwanzia sasa na kuendelea, kwamba haina uwezo wa kulazimisha kanuni zake kwa mabara matano kulingana na maslahi yake peke yake, kama ambavyo pia haitokuwa (askari wa ulimwengu) katika maeneo ya mivutano na matatizo milele"*.

Kwa hiyo basi, Marekani katika sera zake huenda kwa mtizamo kwamba yeye ndiye mmliki wa ulimwengu huu na mwenye haki nao zaidi na ndiye mwenyewe! Yatangaza mchana wazi peupe kwamba yeye ndiye kiongozi wa ulimwengu, kama alivyosema Bush wakati wa kampeni zake za uchaguzi wa Marekani katika mwezi wa nane mwaka wa 2004, ilipokuwa ikitangaza miradi ya ulimwengu (ulimwengu mpya), (mashariki ya kati mpya), (mashariki ya kati kubwa) … hadi mwisho. Lakini hiki kiburi na kujinaki huku kwa Marekani matokeo yake yatakuwa mabaya kwao, bali ishara zimeshaanza kudhihiri. Kwani Marekani imeshazama ndani ya matope ya Afghanistan na Iraq, ikadhalilishwa na kuvunjwa haiba yake, licha ya vitendo vyake vya kihalifu vya kuwapiga raia mabomu bila mpango, na licha ya vitendo vya fedheha na kinyama anavyofanya ndani ya majela. Lakini hata hivyo imekuwa ikirudisha Marekani mizonga ya majeshi yake baada ya kuuliwa ndani ya Afghanistan na Iraqi. Na watu wa maeneo tofauti wamejawa na chuki kwa uhalifu wao muovu uliowafika watu, miti, mawe, bali hata mitaala ya kielimu, vyombo ya habari, na fikra…

Vilevile Ulaya, bara Eshia, na Afrika wameumizwa na waliyofanyiwa na Marekani: kuporwa utajiri wao, na uwadui wa kuendelea dhidi ya nchi na watu, na Marekani pekee kujaribu kudhibiti kiubabe maeneo yote ya kilimwengu.

Kwa hivyo, kinachotofautisha siasa ya Marekani ni: Kiburi, kujiona, kubobea katika fani za uhalifu, na kuuona ulimwengu wote kuwa ni shamba lake. Na kwa upande mwengine: Ni chuki kubwa na hasira nyingi dhidi yao kutoka kwa mataifa yote ya ulimwengu,

katika maadui zao na hata wale waliokuwa ni marafiki zao pia. Haya yote yakiashiria mwisho mchungu kwa Marekani na kuporomoka vibaya kama wababe wengine wote ulimwenguni waliotangulia.

**Ama Uingereza:** Hakika hii huweka mguu mmoja Ulaya na mguu mwengine Marekani, kwa upande mmoja huvutwa na Ulaya na kwa upande wa pili ni *Anglo-Saxon*, nayo huchunga uwiyano baina ya pande mbili.

Huo uwiyano ndio umekuwa msingi wa mahusiano yake na Marekani na Ulaya, kwa hivyo yacheza na kamba mbili na kufaidika kutoka pande zote, hupata nguvu kwa Ulaya na Marekani wakati mmoja, basi haiwezi kuiwacha Marekani wala kujitenga na Ulaya, lakini maslahi yake zaidi yalemea upande wa Ulaya. Ndio maana twaipata yajikurubisha nayo zaidi kadri masiku yanavyosonga, na kuingia kwake katika muungano wa Ulaya ni dalili juu ya hayo.

Uingereza mwishowe imechangia kuweka msingi wa jeshi la Ulaya mbali na muungano wa NATO, ikafanya hivyo kwa kusaidiana na Ufaransa na Ujerumani licha ya Marekani kupinga vikali. Kwa hivyo hii ndio siasa ya Uingereza huko Ulaya, na huo ndio msingi inayotoka matendo yake ya kisiasa huko Ulaya.

**Ama Ufaransa:** Hii ni kinyume na Uingereza, kwani siasa yake husimamisha juu msingi wa kiulaya mia kwa mia, wala haitilii umuhimu wowote kwa Marekani. Nayo yajaribu kutilia nguvu muungano wa Ulaya na yajaribu kuidhibiti ili iwe nguvu ya kisiasa ya Ulaya iliyoungana, iliyojitenga kabisa na Marekani, ili muungano huu uwe nguvu pinzani inayolingana na nguvu za Marekani katika nyanja zote za kisiasa, kiuchumi, kijeshi, na kithakafa, wala isijifunge tu na uchumi peke yake au kusaidiana kisiasa juu-juu.

Na Ufaransa kujikurubisha na Ujerumani hufanya kuwa ndio jambo la kimsingi katika kuifikia hii siasa, ndio sababu imekuwa yachukulia muungano wa Ufaransa na Ujerumani kuwa ndio msingi wa siasa hii ya umoja wa kiulaya.

Hii ndio siasa ya Ufaransa ya kiulaya, nayo ni siasa ya kujitegemea kivyake, na ni yenye kutoa changemoto za wazi, iliyofanya Ufaransa na Ujerumani ndio moyo wa nguvu za Ulaya na dainamo inayoiharakisha.

**Ama Urusi:** Siasa yake kwa sasa upande wa Ulaya yabainika katika mambo mawili:

**Kwanza:** Kuingia katika jukwaa la nchi za Ulaya, na kushirikiana nazo katika kutatua mambo ya Ulaya kwa usawa. Na ilifaulu kwa hili kwa kiasi fulani, kwani ilifanikiwa kuingia katika kikao cha Ulaya, kwenye muungano wa nchi saba zenye uwezo mkubwa wa kiviwanda duniani, lakini haikufaulu kuingia katika muungano wa Ulaya au hata kugombea ili kuingia humo.

**Pili:** Kujaribu kuhifadhi mahusiano mema na nchi zilizokuwa zamani ni sehemu ya muungano wa kisovieti, na nchi zilizokuwa zikizunguka katika mzunguko wake, ili mahusiano yawe ni ya usimamizi wa kudumu, lakini ilifeli vibaya sana katika hili, kwani ilikosa udhibiti wake kabisa juu ya nchi zote za Ulaya Mashariki nazo ni: Bulgaria, Romania, Czech, Slovakia, Poland, Hangary na nchi za Yugoslavia zilizotawanyika, na ikaanza kukosa sehemu ya udhibiti wake juu ya  Georgia, Azerbaijan, Armania, Ukrania, Belarus, Moldovo, na jamhuri za kiislamu za Eshia ya Kati, na haikubakiwa na ubwana kamili isipokuwa juu ya Kazakhastan, kama ilivyokosa mapema kabisa udhibiti wake wote katika nchi tatu za Baltic nazo ni: Lithuania, Estonia na Latvia.

Kwa ufupi: siasa ya Urusi kwa Ulaya ni kwamba haikuweza kustahiki Ulaya kwa kiwango ilichopanga na kuendea mbio, na labda huenda ikawa kilichomfanya kushindwa hilo ni kwa kuwa ni nchi ya Euro-Asian yaani Ulaya ya Asia, haiwezi kudai kuwa ni ya Ulaya kamili wala haiwezi kupuuzia upeo wake mpana wa Asia, au kuachana na mahusiano yake na maslahi yake makubwa na wawasiokuwa wa Ulaya. Kwa hivyo yashuhulika kupanga upeo wake muhimu na mpana, nayo kwa hilo yababaika haiwezi kumakinika katika jambo la Ulaya peke yake.

Hadi hapo tutakuwa tumeshajua sifa za watu ya nchi kuu (Marekani, Uingereza, Ufaransa na Urusi) na pia (Ummah wa kiislamu) ambao karibuni serikali yake kubwa Khilafah rashida itarudi, pamoja na taifa la Ujerumani linalotarajiwa kurudi kwake tena kuwa nchi kubwa hata ikikawiya. Kisha pia tumetaja Japan kwa sababu ya athari yake kubwa ya kiuchumi.

Itadhihirika kuathirika na athari ya mataifa haya katika siasa za kimataifa wakati wa kuweka wazi maswala makubwa ya ulimwengu.

****

## [1] KADHIA YA ULAYA:

Kadhia ya Ulaya ndio kadhia ya mwanzo ulimwenguni tangu karne nyingi zilizopita, nayo ni kadhia inayohusiana na nchi kubwa na uwiyano baina yao. Pia yahusiana na kudhibiti ulimwengu kikoloni na upeo wake kijeshi, kiuchumi, kisiasa, na kithakafa. Nayo ni katika kadhia za kitambo sana na ya hatari sana kwa kile kinachoitwa “amani ya dunia”.

Ama sababu ya kuwa hii ndio kadhia ya kitambo: ni kwa kuwa ndio iliyoleta kile kinachoitwa “jamii ya kimataifa” au “muungano wa kimataifa ulimwenguni”, ambayo kwa ajili yake kulipatikana kile kinachoitwa “kanuni za kimataifa”. Kwa ajili ya Ulaya kusimama mbele ya Uislamu ndio ikapatikana “jamii ya kimataifa” iliyoundwa na nchi za kikristo za Ulaya, na kwa ajili ya kumpiga Napolean na kuzuia kupanuka kwa Ufaransa ndio kikapatikana kile kinachoitwa “Muungano Mtukufu”. Kisha kwa lengo la kuzuia Ujerumani kuchukua mafuta ya mashariki ya kati, na kuziwekea mpaka nguvu zake ndio kukawa na vita vya kwanza vya dunia. Kisha kwa lengo la kupambana na Ujerumani na kuizuia isiharibu mizani ya nguvu huko Ulaya ndio sababu nchi nne kubwa: Uingereza, Ufaransa, Marekani na mungano wa kisovieti zikakubaliana kuisambaratisha Ujerumani na kuizuia isirudi tena kuwa nchi kubwa. Na kwa lengo la kuzuia Ulaya kuungana, na ili kuzuia Ujerumani kutiliwa nguvu, ndio maana kukawa na mivutano ya kisiasa ilizozuia miaka kadhaa kubuniwa kwa muungano wa

Ulaya, vilevile ikazuia makumi ya miaka Ujerumani kuungana, na wale wababe wawili wakafanya matendo kadhaa kwa malengo hayo kabla ya mapatano yao na baada yake. Na Ufaransa mwanzoni ilikuwa na dori fulani katika hayo, lakini baadaye ikaachana nayo, ikawa yenda mbio kutilia nguvu Ulaya kupitia Ujerumani. Na Uingereza pia ilikuwa na mchangio katika hayo japo ilijionyesha kuwa eti yaenda mbio kuunganisha Ulaya. Kwa hivyo, kadhia ya Ulaya na yanayohusiana nayo ndio miongoni mwa kadhia za kitambo zaidi.

Ama sababu ya kusema kuwa hii kadhia ndio kadhia hatari zaidi kwa kile kinachoitwa "amani ya ulimwengu": hakika hilo lilijitokeza wazi katika nyendo na tabia za kila mmoja katika Ufaransa, Uingereza, Ujerumani, na katika matendo ya Muungano wa kisovieti na Marekani kabla ya kupatana kwao, na katika tabia za wababe wawili: Marekani na Muungano wa kisovieti baada ya mapatano yao, na hata baada ya kumalizika kipindi cha mapatano yao, bali hata mpaka baada ya kuporomoka kwa muungano wa kisovieti na kambi ya kimashariki na kuvunjwa mkataba wa Warsaw.

Ama Ufaransa, Uingereza, na Marekani kabla ya wababe wawili kukubaliana ndio waliokuwa wakiwakilisha kambi ya kimagharibi. Na kadhia ya Ulaya ilikuwa ikiwakilisha kuondoa vita vya pili vya dunia, ikawa yaonekana baina ya kambi mbili katika kutafuta mustakabli ya magharibi mwa Ulaya na mustakbali ya Ujerumani. Kambi ya magharibi ilikuwa ikiona kuunganisha Ulaya ili kusimama mbele ya muungano wa kisovieti, Marekani ikawa yakusudia kwa namna fulani kufufua uwanajeshi wa kijerumani, ili kupata jeshi la Ujerumani lenye nguvu ili liweze kusimama mbele ya muungano wa kisovieti, na kupatikane uwiyano mpya baina ya Ujerumani, Ufaransa, na Uingereza. Ama muungano wa kisovieti ambao ulikuwa ukiwakilisha kambi ya kimashariki, ulikuwa waona kwamba hatari ya hakika dhidi yake yatoka Ulaya na haswa Ujerumani. Ndio maana ukawa kikwazo mbele ya kuunganishwa kwa Ujerumani, mbele ya kuunganisha kwa Ulaya, dhidi ya jeshi la

Ulaya, na dhidi ya Ujerumani kurudisha kujihami. Na kwa kupitia vita baridi, matendo ya kisiasa, na shughuli za kidiplomasia huu muungano ukaweza kufaulu. Ukaweza kuzuia Ulaya makumi ya miaka isiweze kupiga japo hatua moja katika kadhia yake.

Ama baada ya kupatikana wababe wawili na kwa mapatano yaliyofanyika baina ya Khrushchov na Kennedy, hakika hali ilibadilika, kwani rai ya Marekani na muungano wa kisovieti ziliungana kuhusu kadhia ya Ujerumani, na wakawa na rai moja kuhusu kadhia ya Ulaya. Haya yalimedhihiri mara tu baada ya kukutana kwao, ambapo John Kennedy ambaye ni raisi wa Marekani wakati huo alisema wazi: ***"Hakika muungano wa kisovieti una sababu tosha za kuhofia kuvamiwa kijeshi na Ulaya. Kwa sababu katika historia Urusi ilishapigwa na Ulaya mara mbili: mara ya kwanza ilipigwa na Ufaransa wakati wa Napoleon, na mara ya pili ikaipiga na Ujerumani wakati wa Hitler. Kwa hivyo ni lazima kupatikane kitakachodhamini kutokuweko hatari dhidi ya muungano wa kisovieti kutoka Ulaya, kwa mfano: kuondoa silaha za Ulaya ya kati".***

Tamko hili laonyesha dalili ya wazi kabisa kwamba muungano wa kisovieti na Marekani rai zimeungana kuhusu ya kadhia ya Ulaya na haswa kuhusu kadhia ya Ujerumani. Na hata baada ya mapatano kumalizika rai ya Marekani kuhudu Ulaya haikubadilika hasa kuhusu ulazima wa kudhibiti na kupiga malengo yake ya kujikomboa na kushiriki katika kuchora siasa za kimataifa. Pia Marekani haikubadilisha rai yake kuhusu kuizuia Ulaya isirudi katika maeneo yake ya zamani aliyokuwa na ushawishi ndani yake, na kumaliza ushawishi wake ndani ya kusini mashariki mwa Asia na maeneo ya ghuba, na kufanya Ulaya inyenyekee na kubakia chini ya mwavuli wa Marekani ndani ya NATO, na kuwa kikwazo mbele ya jaribio la Ulaya kuanzisha nguvu ya kijeshi makhsusi kwake.

Hilo ni kwa sababu Ulaya ilipojua kwamba baada ya mkataba hofu ya vita imeondoka, na baada ya kurudisha afya na kumakinisha uchumi wake, ilianza mipango ya kushirikiana na wale wababe wawili katika kuchora siasa za kimataifa, na kujenga sera zake kwa

Marekani juu ya msingi wa ushirikiano na usawa wala sio msingi wa kufuata. Kama ambavyo pia Ulaya - haswa Uingereza na Ufaransa - ilianza kufanya kazi ili kurudi katika maeneo yake ya ukoloni ya zamani, hali iliyofanya Marekani kuchunguza shughuli za Ulaya kwa makini sana. Kama ambavyo Marekani nayo baada ya kuporomoka kambi ya mashariki na kuvunjika muungano wa Warsaw, ilikimbilia kuziba pengo lililotokana na hayo ndani nchi za Ulaya Mashariki kwa kuanzisha mahusiano nao, ili kukata njia kwa muungano wa Ulaya - haswa Ujerumani - isiweze kujitanua mashariki. Pia Marekani ikabakisha NATO, na ikapinga - na bado yapinga – kubuniwa kwa muungano wa kijeshi la Ulaya mbali na NATO.

Ama kuhusiana na Urusi iliyorithi muungano wa kisovieti: hii haifichi hofu yake kuhusu muungano wa Ulaya kujitanua Mashariki, hivyo ikafanya bidii ili kupata dhamana, lakini kwa sababu ya msimamo wa kimataifa uliotokana na kuporomoka kwa muungano wa kisovieti na kambi ya kimashariki, na kwa sababu ya kuhisi kwake udhaifu mbele ya Marekani, basi haikuwa na budi kujipanga na nchi za Ulaya ili kupata muwafaka kuhusiana na faili ya mambo ya Ulaya Mashariki. Kama ambavyo pia ilifanya bidii kwa kupanga na baadhi ya nchi za muungano wa Ulaya, ili iweze kuathiri katika siasa ya kiulimwengu, kilichompelekea kupunguza misimamo mikali dhidi ya muungano wa Ulaya na nchi zake, kinyume na hali ilivyokuwa mara tu baada ya vita vya pili vya dunia, katika kipindi cha mapatano, na baada ya hapo kidogo.

Ama kuhusu Ufaransa: baada ya de Gaulle kushika utawala na mpaka de Gaulle alipozuru Marekani na kukutana na Nickson mwezi wa tatu 1969 M, Ufaransa ilikuwa yafanya kazi kuunganisha Ulaya na kuifanya kuwa ni nguvu ya tatu itakayosimama baina ya kambi mbili. Kwa hiyo ikawa yaitilia nguvu Ujerumani kwa kiwango ambacho haitakuwa hatari kwa Ufaransa, na yafanya bidii kuunda muungano wa *confederal* baina ya nchi za Ulaya, pamoja na kudhamini ubwana wa Ufaransa. Na ilikuwa na bidii sana ya kuitenga Uingereza kutoka Ulaya, kwa kuitakidi kwamba siasa yake

ni ya tangu jadi ni kuzuia muungano wa Ulaya kwa mbinu zote. Lakini baada ya de Gaulle kujiuzulu mwaka wa 1969 na kisha kufa baada mwaka mmoja, Pompidou ambaye ni raisi wa Ufaransa alikutana na waziri mkuu wa Uingereza Edward Heath mwaka wa 1971 katika mazungumzo marefu, ambapo mwishowe Pompidou alikubali uwanachama wa Uingereza.

Bado Ufaransa na Ujerumani haswa wanaendelea kuboresha sera za nje za Ulaya kwa ushirikiano, haswa kwa kuwa Ujerumani yajua kiwango cha upinzani dhidi ya nguvu ya Ujerumani, hivyo basi hujaribu kushikana na Ufaransa ili kudhihiri kama nguvu ndani ya umoja wa Ulaya, kupitia hilo ikaweza kufikia mengi katika malengo yake binafsi kama vile kujitanua upande wa mashariki. Na wakati wa vita vya Iraq mwaka wa 2003 hizi nchi mbili zilifaulu kudhihiri na msimamo mmoja wa kupinga vita hivi, hali inayoweza kuandalia Ufaransa na Ujerumani mazingira ya kuzifanya kuwa kituo cha kuvutia kuhusiana na sera za kigeni za Ulaya zenye ushirikiano. Na hazikuwa mbio za hizi nchi mbili kwa ajili ya kutunga kielelezo cha katiba mpya ya Ulaya, na kuunda ushirika wa majenerali wa kijeshi wa Ulaya mbali na NATO, -hazikuwa mbio hizo - isipokuwa ni kwa ajili ya kuifanya Ulaya kuwa nguvu ya kiulimwengu inayoathiri katika siasa za kilimwengu.

Ama kuhusu Uingereza: katika kile kipindi cha mapatano ilikuwa yajaribu kuimarisha mahusiano yake na Ujerumani na kuifahamisha njama za Marekani na Urusi (muungano wa kisovieti) dhidi ya manendeleo ya Ujerumani na dhidi ya kupata kwake nguvu. Kisha baada ya hapo ikaamua kujiunga na soko la ushirika la Ulaya, baada ya ule mkao mrefu baina ya Pompidou na Edward Heath mwaka wa 1971, ilifanya hivyo licha ya upinzani mkali wa kindani. Uingereza ikajaribu kupata nguvu kwa Ulaya katika kukabiliana na wale wababe wawili (Marekani na Muungano wa kisovieti) kabla ya kuporomoka muungano wa kisoveiti na baada yake, lakini haikuwa na msimamo wa kiuadui wa wazi dhidi ya Marekani, hilo ni kwa sababu ya dharura ya kipindi hicho, kwa sababu Ulaya ilikuwa – na hadi sasa - iko katika mwanzo wa njia ya kuelekea kuwa nguvu ya

kiulimwengu, na njia yake hii imezungukwa na hatari na yawezekana isifikie malengo yake, haswa kwa kuwa Marekani nayo iko macho yajua malengo ya Ufaransa na Ujerumani, na yaenda mbio daima - nayo ndio yenye nguvu zaidi katika uwanja wa kimataifa - ili kufelisha mipango ya Ufaransa na Ujerumani na ina uwezo wa kufanya hivyo kila inapopata nafasi. Na sera ya Uingereza leo imesimama juu ya kuweka mguu mmoja Ulaya na mwengine Marekani ikiwinda maslahi popote itakapoyapata.

Uhalisia huu wa watu unaotafautiana baina ya nchi za Ulaya, haswa zile kubwa kati yake, ndio unaonekana kuwa kikwazo mbele ya kujenga Ulaya iliyounganishwa na yenye nguvu inayoathiri katika siasa ya kimataifa kwa pamoja. Na kinachothibisha hayo ni kile tulichokijua wakati wa kuandaa kitabu hiki, kwamba muungano wa Ulaya unaoundwa na nchi ishirini na tano, mkutano wao uliofanyika Dablin tarehe 18/6/2004 ulivunjika na hawakuweza kukubaliana kumchagua kiongozi wa muungano, wakauahirisha hadi wakati mwengine.

Pamoja na hayo, na licha ya ukabila na maslahi ya kirasilimali yanayobebwa na nchi za muungano, ambapo hizi mbili ndio kikwazo cha umoja wa kihakika wa Ulaya, lakini pamoja na hayo muungano wa Ulaya umekuwa ni nguvu kubwa ya kiuchumi inayoshindana na nguvu ya kiuchumi ya Marekani, ambapo yuro yashindana na dola katika kiwango cha miama ya kimataifa. Kama ambavyo kuathiri kisiasa kimataifa - pamoja na maslahi kutafautiana, na licha Marekani kupenya katika nchi za muungano kupitia njia ya mahusiano yake mazito na baadhi ya nchi, haswa nchi za Ulaya Mashariki zilizoungana karibuni 1/5/2004 – pamoja na yote hayo muungano umekuwa ukileta dhiki nzito kwa kiwango fulani dhidi ya mipango ya kiuchumi ya Marekani.

Kwa ufupi twaweza kusema kwamba, lau muungano wa Ulaya ungekuwa umeshikamana kisawasawa basi ungeweza kushindana na Marekani katika ushawishi wa kimataifa kichumi, kisiasa na labda hata kijeshi kwa kiwango fulani. Lakini ni muungano unaoyumbayumba, na hili huudhoofisha zaidi kuliko kuutia nguvu.

Na hii ndio tabia ya <u>muungano</u> wowote, huwa hauna zile nguvu zinazopatikana katika <u>umoja</u>.

Muungano wa Ulaya ni mbabe wa kiuchumi ambao Marekani anauogopa, na hufanya bidii zake zote kuushusha, kwa kuwa ni mshindani wake wa kihakika katika upande wa kiuchumi. AFP tarehe 19/4/2003 ilinukuu kwamba: *"Hakika Marekani yategemea uwekezaji wa umoja wa Ulaya kwa kiwango cha juu ili kuziba upungufu wake mkubwa katika bajeti inayoendelea unaozidi dolari bilioni (500) mwaka wa 2000 M kulingana na Fred Bergsten msimamizi wa taasisi ya uchumi ya kimataifa, nayo ni kituo cha utafiti makhsusi huko Woshington".*

Nchi kumi huko zilitia saini huko Athens tarehe 16/4/2003 M ili kujiunga na nchi kumi na tano zilizotangulia katika muungano wa Ulaya. Na baada ya takriban mwaka mmoja (mwanzo wa mwezi wa tano 2004 M) Ulaya imekuwa eneo kubwa la kibiashara duniani linalokusanya watu milioni 450.

Ama katika upande wa kisiasa na upande wa kijeshi: hakika muungano wa Ulaya ni dhaifu ukilinganisha na Marekani. Na Marekani imefaulu katika kuudhoofisha kwa sababu kadhaa, miongoni mwazo ni:

A. Kubakisha muungano wa NATO ambao ulipaswa kumalizika tangu kumalizika kwa mkataba wa Warsaw chini ya uongozi wa muungano wa kisovieti uliovunjika. Lakini Marekani ikang'ang'ania kuwa muungano wa NATO uendelee kwa hoja ya kuzihami nchi za Ulaya dhidi y Urusi na nchi nyenginezo ikilazimu. Kwa hiyo mamlaka ya kijeshi ya Marekani juu ya Ulaya yakabakia. Mkuu wa tume ya Ulaya tarehe19/4/2003 aliseme*: "Hakika ni lazima muungano wa Ulaya ifanye sauti yake isikike ndani ya muungano wa NATO. Hapo ndipo muungano utakapokuwa umesimama juu ya misingi miwili: Ulaya na Marekani"* akaendelea kusema*: "Wakati huo ndio kutakuwa na muungano wa NATO wa kihakika badala ya muungano tuliouzoea ambao huitikia Marekani peke yake"* na

akasema tena: *“Hatuwezi kupatia Ulaya majukumu ya hazina na kumuachia Marekani mkoba wa amani”.*

B. Kutokana na sera za Uingeeza isiyotaka kuyayuka ndani ya muungano wa Ulaya ikawa kama Luxembourg kwa mfano, hivyo ikawa yaweka mguu wake mmoja ndani ya umoja wa Ulaya na mwengine Marekani, ili maslahi yake yakutane na maslahi ya Marekani katika nukta ya kudhoofisha muungano wa Ulaya: ili Uingereza ibakie kuwa ndio yenye usemi ndani ya Ulaya, na ili Ulaya isishindane na Marekani lau kama itakuwa nguvu yenye umoja.

C. Zile nchi kumi zilizotia saini tarehe 16/4/2004 ili kujiunga na muungano wa Ulaya mwanzoni mwa mwaka wa 2004, nyingi kati yao ni maeneo ambayo Marekani ana ushawishi ndani yake, au kama alivyosema Prodi tarehe 19/4/2004: *“Baadhi ya nchi mpya katika muungano wa Ulaya ziko na mahusiano ya nguvu na Marekani katika mambo yanayohusiana na usalama”.*

D. Kuzidi kwa mamlaka ya Marekani juu ya visima vya mafuta pia huzidi kuipa Marekani mamlaka ya ziada juu ya nchi za muungano wa Ulaya zinazohitaji mafuta. Vilevile kuzidi kwa mamlaka ya Marekani juu ya viongozi wa ulimwengu wa tatu humfanya ajipendelee zaidi katika mikataba ya kibiashara zenye faida na kupora utajiri wa ulimwengu huu, hali inayozinyima nchi za Ulaya hizi faida.

Kwa hiyo twasema kwamba, hakika mizani ya nguvu za Ulaya hazikushikana, na yakaribia kukosekana nguvu moja ya Ulaya, bali ni nchi zenye nguvu ndani ya Ulaya, zikiongozwa na Ufaransa ambayo yafanya kazi kupatikane muundo wa nchi zengine za Ulaya pamoja nayo, ili ipatikane nguvu ya Ulaya. Na Uingereza kwa upande mwengine haina haja kupatikana muundo wa Ulaya wenye nguvu, bali Uingereza yataka ibaki kuwa ndio yenye usemi mkubwa ndani ya Ulaya.

Hivi ndivo ilivyo, maingiliano ya kadhia ya Ulaya na mahusiano yake ya kimataifa yaliyoko baina yao au baina yake na Marekani, au baina yake na kadhia moto moto zengine, bado maingiliano haya ndio hufanya Ulaya yote iwe na umuhimu wa kimataifa. Na tofauti ya uwiyano humo, na maslahi na mahusiano kugongana ndio hufanya kadhia ya Ulaya kuwa kadhia ya hatari kwa kile kinachoitwa "amani ya ulimwengu, sawa iwe ni kumakinika kwake au kutikisika kwake.

Kwa hivyo haiwezekani kupuuzia namna kadhia ya Ulaya inavyoathiri katika zile kadhia tano zengine na kuingiliana nazo. Hicvyo basi hapana budi kuangalia kadhia ya Ulaya kwa mtizamo unaokubaliana na hali yake halisi na hatari yake, tangu Ulaya ilipokuwa ni nchi zinazozozana hadi ilipokuwa ni soko la kiuchumi la ushirika, kisha kuungana kwa Ulaya kunakoleta uzito maalumu ulimwenguni, na hilo litabainika kwa uwazi tutakapoeleza kadhia zengine na mahusiano yake na Ulaya.

****

## [2] KADHIA YA MASHARIKI YA KATI:

Hakika hii ni kadhia inayohusiana na Uislamu, hatari yake kwa Magharibi, kuwepo kwake katika maeneo ya "kistrateji" (kimkakati), na kudhibiti kwake njia za mawasiliano kati ya Ulaya, Afrika, na Asia. Pia ni kadhia inayohusiana na muundo wa kiyahudi ambao ndio msitari wa mbele katika kutetea maslahi ya kimagharibi, yahusiana pia na ukoloni na maslahi yake ya kimada haswa mafuta. Kwa hivyo basi kadhia inayohusiana na Uislamu, maeneoya kimikakati, nchi ya kiyahudi, ukoloni na mafuta: hapana shaka kwamba kadhia kama hii ina umuhimu wa hali juu sana, sio tu kwa watu wa maeneo hayo na Waislamu peke yao bali kwa ulimwengu mzima.

Ama kuhusu Uislamu: hakika ulikuwa na bado ni hatari kubwa Marekani na Magharibi. Eneo la Mashariki ya kati huzingatiwa kuwa ndio sehemu ya kimaumbile ya ulinganizi wa kiislamu kuanzia na kwenda ulimwenguni. Kwa hivyo halikuwa ni jambo

geni kwamba Marekani imeufanya Uislamu kuwa ndio adui mkubwa na wa kipeke yake baada ya ukoministi kuanguka, na ikatumia nembo za "*ugaidi*", *"kuvuka mipaka kidini*" na "*siasa kali"* kama kizibo cha mapambano yake dhidi ya Uislamu na Waislamu katika maeneo haya, nayo yafanya bidii kwa nguvu zake zote kuziweka mbali harakati za kiislamu za kisiasa na utawala, kupitia mbinu za kutishia, kushika, kuadhibu, na kuzidhibiti, kama inavyofanywa serikali vibaraka zinazomfuata katika maeneo haya.

Bush alitangaza wazi kabisa vita vipya vya kimsalaba dhidi ya Waislamu, na John Ashcroft ambaye ni waziri wa "uadilifu" wa Marekani akasema: *"Kwa uwazi, hakika ugaidi uko ndani ya Uislamu wenyewe, na wala sio tu ndani ya baadhi ya wafuasi wake"*, na kulingana na madai yake akasema kwamba Allah ahimiza ugaidi ndani ya Qur'an.

Ama kuhusu umuhimu wa kistratejia wa Mashariki ya kati na kudhibiti kwake mawasiliano: umuhimu wake ni kwa sababu ni eneo la makutano ya mabara matatu ya zamani: Afrika, Ulaya na Eshia, na kudhibiti kwake mapito membamba ya mlima Twariq, Basphorous, Adan, Hormoz, Swez Canal, bahari Nyeupe ya kati, bahari Nyeusi, bahari Nyekundu, na Ghuba, na kuongezea kuwa ndio makutano ya njia za malighafi na bidhaa baina ya mabara matatu. Na umuhimu wake wa kistratejia (kimkakatu) ulileta ugumu baina ya kambi mbili za Magharibi na Usovieti kabla ya mapatano yao, kwa sababu Mashariki ya Kati ni kama ukanda wa Magharibi katika maeneo ya kambi iliyopigwa dhidi ya muungano wa kisovieti uliyotangulia, ukanda huu ukawa ndio safu ya kwanza ya Magharibi kutetea Mashariki ya Kati na Afrika dhidi ya muungano wa kisovieti, ndio maana zikabuniwa kambi za kijeshi ndani ya Mashariki ya kati, zikiwemo kambi za kinuklia, na yakafanywa majaribio kadhaa ya kuunganisha nchi zake katika miungano ya kijeshi, na vikabuniwa viwanja vingi vya Ndege, na njia pana zinazoitwa *autostrada*, na zikawa na umuhimu wa kimikakati.

Ama baada ya wale wababe wawili kupatana mwaka wa 1961, maeneo haya hayakuwa na umuhimu huu wa kijeshi, ndipo suala la miungano ya kijeshi likapuuzwa na kambi za kinuklia zikaondolewa, na wababe wawili wakaendelea kuziondoa kambi za Uingereza, wakafaulu kuondoa kambi ya Adan, Libya, na Suez Mashariki, na wakafanya bidii kuondoa kambi zake Cyprus, hivyo basi wakati huo Mashariki ya kati haikuchukuliwa kuwa na umuhimu kimikakati. Lakini baada ya vita baridi kumalizika na muungano wa kisovieti kuondoka, umuhimu wa Mashariki ya Kati wa kimikakati ukarudi, haswa kwa Marekani mbele ya Urusi na Ulaya, ndio maana Marekani ikarudia kuweka kambi za kijeshi Ghuba, ikakoloni Afghanistani na Iraq, ikatangaza kuwa Pakistani na Kuwait ni washirika wa kimikakati baada ya Bahrain.

Kisha Marekani ikachukulia Mashariki ya Kati kuwa msitari wa mbele katika kutetea usalama Marekani (U.S.A) na ikaandaa mradi iliyouita "Mradi wa Mashariki ya kati kubwa" kisha ikaubadilisha na kuuita: "Mradi wa Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini" na ikauwasilisha katika mkutano wa nchi nane zenye uwezo mkubwa wa kiviwanda uliofanyika mwezi wa sita 2004 katika maeneo ya Sea Island.

Kwa hivyo, twaweza kusema kwamba maeneo muhimu ya Mashariki ya Kati yanayojumlisha kutoka magharibi ya bahari ya Atlantic kwa upande wa Mashariki, na upande wa Magharibi ni Iran na Iraq kupitia Ghuba, na kutoka Kaskazini mwa Uturuki hadi jangwa kubwa la Afrika kwa upande wa Kusini. Yaani yajumuisha nchi zote za kiarabu kuongezeka na Uturuki na Iran. Umuhimu wa maeneo haya yamefanya kuwa ndio kibla cha wakoloni na panapokusudiwa na wenye tamaa, kwa ule umuhimu wake mkubwa katika usafirishaji na mawasiliano, sio tu katika kipindi hiki peke yake bali tangu wakati wa vita vya kimsalaba mpaka leo hii.

Ama kuhusu suala la umbile la kiyahudi lililochomekwa ndani ya Palestina: hakika hili limekuwa ndio kiini cha kadhia ya Mashariki ya Kati, na limekuwa ndio sababu ya kukosekana utulivu sio kwa

Mashariki ya Kati peke yake, bali ulimwengu mzima. Hilo ni kwa wamagharibi wenyewe kukubali kwamba asilimia 90% ya matatizo ya ulimwengu wa kiislamu yanayomlaza macho mmagharibi chanzo ni tatizo la kuwepo nchi ya kiyahudi ndani ya Palestina, yaani kati kati ya ulimwengu wa kiislamu.

Ama umuhimu wa Mashariki ya Kati kikoloni: hakika hili ndilo lililoisababishia balaa, ikaiondolewa sifa yake kuwa ni nchi kubwa na nguvu ya kiulimwengu, ikabadilishwa kuwa koloni ya kimagharibi ambapo nchi za kimagharibi huzozana kuikoloni na kutanua nguvu zao. Kwani mafuta yaliyopo huko yanazidi nusu ya mafuta ya ulimwengu, na malighafi zilizopo Jordan, Iraq, Sirya, Uturuki, Iran na nyenginezo ni utajiri mkubwa ambao ni zaidi ya mara kumi ya utajiri wa Ulaya zikichanganywa na Marekani zote mbili. Ndio maana nchi mbali mbali zashindania kukoloni maeneo haya na kuvutana kwa ajili yake, na vita vya Marekani ili kudhibiti maeneo haya ni mfano wazi.

Kwa hivyo basi, hayo mambo matatu: Uislamu, petrol, umuhimu wa maeneo kimikakati, na (Israel) kuchanganyika kwa pamoja ndani ya kadhia moja yatosha kufanya kadhia hii kuwa ni miongoni mwa kadhia hatari zaidi na yenye misokotano sana kwa kiwango ambacho imekuwa ni katikati ya fundo na tatizo la matatizo mengine, fundo ambalo imeshindikana kufunguliwa na nchi kubwa na zimeshindwa kulifahamu, kwani ni kadhia sugu iliyozidi ugumu, na haitotatuka isipokuwa kwa kusimama serikali ya kiislamu (Khilafahh).

Mashariki ya Kati ilikuwa chini ya utawala na mamlaka ya Uislamu na serikali ya kiislamu hadi katikati ya karne ya kumi na nane. Na tangu kongamano la Berlin, yaani tangu mwishoni mwa karne ya kumi na nane nchi kuu za Ulaya zilianza kujaribu kuipiga vita Mashariki ya Kati, Ufaransa, Uingereza na Italiano zikavamia, halafu vita vikaendelea hadi walipoiangusha serikali ya kiislamu kwa kuiangusha serikali ya kiuthmani kwa kuindosha Khilafah, hapo Mashariki ya Kati ikawa chini ya ukoloni Uingereza na

udhibiti wake, na mamlaka yake yakaenea nchi zote mpaka nchi zisizokuwa za kikoloni kama Uturuki na Afghanistan. Na Ufaransa haikuwa na sehemu isipokuwa ndogo iliyofungika katika sehemu ya Kaskazini mwa miji ya Shamu zinazoitwa Sirya na mwambao wake ulioko kusini magharibi unaoitwa Lebanon. Na hali ikaendelea hivyo hivyo mpaka mwisho wa vita vya pili vya dunia, wakamfukuza mfaransa na hapo ukoloni wa Uingereza ukabadilika kwa mbinu nyengine mpya: kwa kumakinisha kugawanya miji vipande na kila kipande kikapewa jina na kuitwa nchi. Kwa hiyo vita vya pili vya dunia vikamalizika ikawa Mashariki ya Kati yote yachukuliwa kuwa ni koloni ya Magharibi au kwa usahihi zaidi tuseme ni koloni ya Uingereza. Ndio maana ikawa yachukuliwa kuwa ni ulimwengu huru na sehemu katika kambi ya kimagharibi wala humo hapakuwepo na kambi ya kimashariki.

Kuna sababu mbili zilizosaidia Uingereza kukoloni Mashariki ya Kati peke yake:

1. Kudhoofika kwa Ufaransa kisiasa, kiuchumi na kimataifa, hivyo haikuweza kushindana na Uingereza na kuzozana nayo katika kukoloni Mashariki ya Kati.
2. Marekani baada ya vita vya kwanza vya dunia kuendelea kufuata sera ya kujitenga. Kwa hiyo Uingereza ikawa peke yake katika kukoloni Mashari ya Kati mda wote ndani ya karne ya kumi na tisa hadi katikati ya karne ya ishirini.

Lakini baada ya 1950 hali ikawa tofauti na kubadilika kimsingi, mivutano ya kikoloni baina ya Uingereza na Marekani ikadhihirika, na kupelekea kupatikana vita na mapinduzi, uchokozi na njama, mivutano ikawa yazidi kwa kipindi fulani na kupungua wakati mwengine, mpaka Marekani ikaweza kuchukuwa uongozi Mashariki ya kati, na Uingereza ikadhoofika hadi ikawa haiwezi kupambana na Marekani kiwazi, lakini ikabakia na kushikamana na kuhifadhi koloni zake kiasi cha uweza wake, na ikafanya hima ya kuwepo katika maeneo hata kama ni sehemu, na hilo ni kwa kushirikiana na Marekani katika miradi yake kama ilivyofanyika katika kuinyakuwa Iraq.

Kutokana na hayo, twaweza kusema kwamba hakika mvutano wa Mashariki ya Kati baada ya vita vya pili vya dunia ulikuwa zaidi kiathari ni baina ya Marekani na Uingereza kama ifuatavyo:

- Sera za Marekani na Uingereza kuhusu kadhia ya mashariki ya Kati baada ya vita vya pili vya dunia ziliendelea kufuata njia ya kushirikiana, hizi nchi mbili zikawa zakutana na kujadiliana kuhusu sera zao, kuunganisha mipango na mbinu baina yao, Uingereza ikaendelea kuiruhusu Marekani kubugia baadhi ya maslahi haswa mafuta ya Bara Arabu, ikaendelea kushirikiana naye mara nyengine, lakini husimama mbele yake mara nyengine katika yale aliyokuwa akiyaona yana madhara kwa maslahi yake.
- Kadhia ya Mayahudi ndani ya Palestina ilipozuka, ikawa rai ya Marekani ni kubuniwa nchi ya kiyahudi ndani ya Palestina, ili kuifanya kuwa chombo cha kukolonia maeneo hayo. Lakini Uingereza ilikuwa bado haijakata shauri kuhusu kubuniwa nchi ya kiyahudi, ikawa ina shaka baina ya Palestina kuwa ni nchi inayodhibitiwa na Mayahudi, au iwe nchi ya kiyahudi. Ikawa yataka kupangilia pamoja na koloni zake nyengine za miji ya kiarabu, hivyo basi haikukata uwamuzi, ikarudisha hii kadhia kwa baraza Umoja wa Mataifa, na baraza la Umoja wa Mataifa kwa shinikizo la Marekani ilipopitisha kubuniwa nchi ya kiyahudi, Uingereza ikanyamaza na kuwacha wakati uwamuwe: Je, hili eneo litaweza kuwacha nchi ya kiyahudi baina ya Waislamu? ama mwili huu wa Waislamu utaitema? Ikawa siasa yake kuhusu nchi ya kiyahudi ni kungojea masiku yatakavyoamua.

Amma Marekani hakika ilianza kukaza mwendo katika mipango ya kumakinisha (Israel) na kumaliza kila kinachozuia kuimakinishwa kwake, Uingereza ikawa yaenda kinyume na hilo lakini kwa njia za kisiri, basi kukapatikana mvutano mkali baina ya Uingereza na Marekani kuhusu kuwepo kwa nchi ya kiyahudi.

Kando na hayo, Marekani ikajaribu kupitisha bomba za Petroli kupitia Jordan, Syria na Lebanon katika bahari Nyekundu ya kati,

Uingereza ikawa kikwazo njiani kwake, na kwakuwa ndio iliyokuwa zamani katika maeneo haya, inayoweza kuathiri viongozi wote eneo, kwa sababu ni vibaraka wake, hapo basi Marekani ikaona kuwa mbinu pekee ya kugeuza hali ya eneo ni kutekeleza siasa aliyoitumia huko Marekani Kusini nayo ni kuweka viongozi wa kijeshi kupitia mapenduzi. Marekani ikafanya mapinduzi ya kwanza ya kijeshi yaliyotekalezwa na Husni Al-Za'im wa Syria. Akaipa Marekani fadhila kwa kuweka bomba za Petroli, akarefusha bomba na kumaliza tatizo hili. Lakini Uingereza ilipohisi kwamba Marekani yataka kukoloni eneo hili na kulichukuwa kutoka kwake, ikaanza kupambana na Marekani vikali, lakini kwa mbinu za kisiasa, hila na kwa kuwatumia wenye eneo.

Baada ya mapenduzi ya Husni Al-Za'im, na baada ya kuzidi mapambano ya Uingereza kwa miradi yote ya Marekani, hapo mivutano ya kisiri baina ya hizi nchi mbili ilibadilika na kuwa mivutano inayokaribia kuwa wazi. Wawakilishi wa kidiplomasia wa Marekani huko Mashariki ya Kati wakaona yanayotishia maslahi ya Marekani kijeshi na kiuchumi katika eneo, na wakaona kuwa sera za Marekani kubakia sambamba na za Uingereza maana yake ni Marekana kubakia kuwa kama ilivyokuwa kabla ya vita vya pili vya dunia, ambapo ilikuwa ni chombo kinachotumiwa na Uingereza, inayotosheka kwa kuipa Marekani tonge dogo tu ili kumbakisha katika eneo na kuitetea, huku ikiinyima kheri zote za hili eneo, ili eneo lote liendelee kuwa chini ya mamlaka ya Uingereza peke yake.

Wanadiplomasia hawa wa kimarekani wanaotegemewa na mkusanyiko wa waarabu waliyaona hayo, wakawa na yakini kuwa ni lazima kuingiza baadhi ya mabadiliko ya kimsingi katika kuelekeza sera za Washington na kuzirekebisha upya kwa namna ambayo zitafanya msingi wa uboreshaji wa sera hizi na kuzikamilisha ni kusaidiana na wakaazi wa biladi. Lakini wenyewe wakati huohuo wakajikuta mbele ya matatizo makubwa, ikiwa (Israel) itasimama wakati Waislamu wakiwa na chuki nayo.

Kwa hiyo, wakaona kwamba ni lazima kutatua matatizo haya kabla ya kufikiria kisawasawa, na kabla ya kuanza kubadilisha eneo

badala ya kuwa ni kambi ya Uingereza liwe ni kambi ya Marekani, basi wakaitisha kongamano miongoni mwao kujadili maudhui hii. Mwezi wa kumi na moja 1950 wakaweka kongamano lao la kwanza Istanbul, na kongamano likisimamiwa na bwana George Maggie ambaye ni muwakilishi katika wizara ya nje ya Marekani katika mambo ya Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini. Kongamano hili la kisiri likaendelea kwa muda wa siku tano mfululizo, wakajadiliana kuhusu hali za eneo hili kisiasa, kimikakati, na kiuchumi. Wakakubaliana rai kwamba hakuna njia sera za Marekani kubakia kufungamana na sera za Uingereza ikiwa kihakika yataka kubadilisha Mashariki ya Kati kuwa kambi ya Marekani, na ikiwa yataka kufanya kusaidiana na watu wa biladi kuwa ndio mbinu katika mbinu za kubadilisha eneo hili. Na wakafanya yale yaliyotokea Syria ambapo Shukri al-Quwatli ambaye ni raisi wa jamhuri kukataa kupitisha mabomba ya Petrol, na Marekani ikafanya hivyo kinguvu kupitia njia ya mapenduzi yaliyotekelezwa na Husni al-Za’im, - wakafanya hayo yaliyotokea - kuwa ni dalili ya wazi juu ya usahihi wa rai yao, hasa kwa kuwa Uingereza nayo mwaka uleule wa 1949 ilifanya mapenduzi yaliyofanywa na Al-Hanawy na kumuondoa Husni Al-Za’im, hapo Syria ikarudi tena kwa Uingereza. Hii pia likawa lawasaidia katika rai yao kwamba ni lazima kutenganisha sera za Marekani na sera za Uingereza ikiwa kweli Marekani yataka kufanya kazi katika eneo.

Hili kongamano lazingatiwa kuwa ni miongoni mwa vyombo muhimu vya kuelekeza diplomasia ya Marekani katika ardhi ya waarabu. Na hili kongamano lilitoa mapendekezo kwa ikulu ya nyumba nyeupe, wizara ya nje, wizara ya ulinzi, na jeshi la wanamaji. Na mapendekezo haya muhimu ufupisho wake ni kama ifuatavyo:

Uzowefu wa vita vya pili vya mwisho umethibitisha kwamba eneo la Mashariki ya Kati ni kambi ya kimsingi inayokusanya vipengee vyote muhimu vya kuingia kwenye vita dhidi ya muungano wa kisovieti, na kwamba kufikiria kuvamia visima vya mafuta vya Urusi huko Caucasus, na kuzuia chombo cha vita cha

kisovieti katika mapato yake ya juu ya mafuta, kwamba fikra hii haina uwezekano mkubwa wa kufaulu kupitia njia ya kusaidiana kijeshi na Uturuki peke yake, bali hakika hayo yalazimu kupatikana kambi za anga zilizopangwa Syria, Lebanon na Palestina kwa sharti Iraq na Misri ziwe ni hazina kubwa inayodhamini kutuma watu, silaha, na gharama katika mpango wowote wa uvamizi unaolenga kuzingira na kuharibu visima vya mafuta vya kiSoviet huko Baku na Caucasus kiujumla.

Kama ambavyo mashambulizi ya kijeshi dhidi ya Ugiriki, Sicily, na Italiano kwa muda wote tangu mwaka wa 1941 hadi 1944 ikawa wazi kwa namna isioyohitaji mjadala wala utafiti, kwamba Mashariki ya Kati eneo muhimu katika usambazaji na kufanikisha mfano wa vitendo vya kivita vikali aina hii, vilivyodhamini ushindi kwa vikosi vya muungano na kuzingira majeshi ya maadui ndani ngome ya Ulaya.

Kisha ikamalizika kwa makubaliano ya wote waliokuwa katika kongamano kwa sura ya maazimio manne yafuatayo:

1. Kujitenga na siasa za Uingereza katika mambo yote yanayokusanya kadhia zinazohusiana baina yake na baina ya ulimwengu wa kiarabu.
2. Kufanya uungaji mkono wa matakwa ya kikabila ya waarabu kuwa ndio msingi wa sera za Marekani kwa Mashariki ya Kati.
3. Kusaidia Misri katika matakwa yake kutoka kwa Uingereza, na kushajiisha kukuwa kwa mfano wa harakati hizi huko Iraq.
4. Kuacha kuendelea kuisaidia Israel kidiplomasia na kiuchumi, badali yake kuhimiza Umoja wa Mataifa kutekeleza mradi wa kugawanya Palestina kuwa nchi mbili: ya kiarabu na kiyahudi, na kutekeleza maamuzi ya baraza la usalama la kimataifa kuhusiana na kusawazisha suala la wakimbizi wa kiarabu, kwa msingi wa kuwarudisha katika miji yao na kuwafidia wale wasiokuwa na haja ya kurudi.

Yasemekana kwamba walitoa mapendekezo maalumu kuhusu Misri, kwani walihusia ulazima wa Marekani kuchukuwa Misri kutoka kwa Uingereza na kuitimua humo, na kusimamisha humo uongozi wenye nguvu utakaosimamia kuongoza eneo lote, kwa sababu imethubutu katika historia kwamba Misri ndio mlango wa eneo la Mashariki ya Kati.

Haya mapendekezo yakapelekwa kwa kitengo cha uongozi wa Marekani, na wakati huo chama cha demokrasia ndicho kilichokuwa madarakani, na hiki chama kawaida huegemea kuipaka mafuta Uingereza, na ikawa Truman ndie raisi wa Marekani. Na huyu Truman aliingia kwenye utawala kwa misukumo miwili: **Kwanza:** ushawishi wa kiyahudi, na **pili**: ushawishi wa Uingereza katika baadhi ya vitengo vya Marekani. Truman akajifunga na majukumu kadhaa mbele ya Uingereza pia mbele ya Mayahudi. Ndio maana yale mapendekezo hayakuchukuliwa kwa umuhimu waliotarajia wale wanadiplomasia, ingawa katika zama za Eisenhower yalipewa umuhimu wake.

Kivyovyote vile, hakika siasa za Marekani zilichangamka Mashariki ya Kati baada ya lile kongamano la wanadiplomasia waliotajwa, Marekani ikajaribu kiujasiri kupatikana suluhu baina ya nchi za kiarabu na (Israel), na kuitoa Uingereza huko Jordan na Iraq, ambapo diplomasia ya Marekani iliwasiliana na mfalme Abdulaziz na kujadiliana naye kuhusu kufunga mkataba naye, ufupisho wake ni kwamba mfalme Abdulaziz aachane na Uingereza na awe na Marekani, na kwamba Marekani itamuacha ajiunganishie Iraq na Hijaz aunde nchi kutokana na Jordan, Iraq, na Hijazi, na pia aiunganishe na Syria na Lebanon, kwa mkabala wa kufanya sulhu na (Israel), na kwamba Marekani itampa mikopo na misaada inayolazimu ili kuzikuza kiuchumi hizi nchi mpya, mfalme Abdallah akakubali hayo. Kisha akaanza kazi kufanikisha huu mradi, akenda Iraq akakutana na Abdul-Ilah na Nuri al-Said na kuwafahamisha kuhusu hii maudhui, akawataka waende pamoja naye. Basi hakuna walichofanya isipokuwa kuwasiliana na balozi wa Uingereza huko Baghdad na kumjulisha kuhusu mpango wa

mfalme Abdallah, Uingereza ikawakataza kwenda naye, kwa hiyo hawakukubali aliyoyasema wala kuyakataa wakaacha mambo hivyo hivyo.

Mfalme Abdallah akarudi Jordan akatumtumia barua Riadh Al Sulh amuunge mkono ili amsaidie ule mradi, na Riadh Al Sulh akakubali hilo. Ni wazi ni kwamba alikuwa amegeuka na wamerekani, basi muingereza akakimbilia kumuua Riadh Al Sulh huko Amman, akiwa njiani kuelekea uwanja wa Ndege akirudi Beirut, kisha baada ya wiki moja akauwawa mfalme Abdallah huko Al-Qudsi katika msikiti wa Al-Aqswa, ikiwa ni matokeo ya njama iliyogunduliwa iliyopangwa na Cloob kumuua, na balozi wa Marekani alikuwa ashamtahadharisha wazi siku moja kabla ya kuuwawa kwake kuhusu njama na safari, kwa hivyo mradi huu ukafa.

Mwaka uleule wa 1952 ukafanyika uchaguzi wa uraisi Marekani, chama cha jumhuri kikaibuka na ushindi na Eisenhower akawa rais, akashika uongozi mwanzo wa mwaka wa 1953, na kwa kushika utawala basi mvutano baina ya Uingereza na Marekani ukazidi, kwa kuwa Eienhower ajulikana kwa kutanguliza maslahi ya Marekani ya juu katika pande zake mbili: kijeshi na kimataifa licha ya kubinywa na mayahudi na Uingereza. Basi mvutano baina ya Marekani na Uingereza ukawa mkali, katika alama zake za wazi ikawa ni Marekani kuichukua Misri kutoka kwa Uingereza, kisha mwishowe kumtimua kabisa. Na kabla ya hayo Marekani ilifanya mapinduzi Syria na kibaraka wake ambaye ni Adib Shishakly akachukua utawala. Kwa hiyo Misri na Syria zikawa ziko na Marekani. Tangu zama hizo biladi za kiarabu zote zimekuwa ni uwanja mpana wa mvutano wa Uingereza na Marekani, kukatukia matendo mengi yanayofanya hii miji kama mpira unaotoka katika mikono ya Marekani hadi mikono ya Uingereza, na kutoka mkononi mwa Uingereza hadi mkono wa Marekani n.k. hayo yakadhihirika katika matendo kadhaa yaliyojumlisha Misri, Syria, Jordan, Iraq, Saudia na Yemen, na zaidi yakiwa ni ndani ya Syria kwa kuwa ndio ilikuwa kama mtu wa kati kwenye mikataba, ikawa yaathiri miji yote ya kiarabu kiujumla, basi yakatokea matendo mengi ya kisiasa

ndani ya Syria, ya muhimu zaidi kati yake ni mapinduzi kuzidi, kwani punde tu baada ya kuuwawa Husni al-Za'im ikadhihirika chuki ya Uingereza kwake na utawala wake kumalizika, Uingereza ikawa yafanya kazi kumakinisha utawala Syria kwa msingi wa demokrasia, na kufanya kazi ili kuiunganisha na Iraq kama hatua ya kuunda *hilali ya rutuba*, na kivitendo uchaguzi ukafanyika Syria, kukawekwa katiba ya nchi, na chama cha raia (hizb aljumhur) na chama cha kizalendo (alhizb al-wataniy) vikashika madaraka, na hivi vyama vikatangaza katika sera zao za kampeni kuungana na Iraq. Marekani ikajaribu kuzuia juhudi za Uingereza lakini haikuweza kupata fursa hadi Adib Shishakly alipokuja madarakani, kwanza akayanyakua kwa nyuma ya pazia, kisha akayadhibiti kiwazi akajiweka mwenyewe kuwa raisi wa jamhuri, hapo Syria ikaingia mikononi mwa Marekani na ikaendelea kuwa katika mikono yake hadi Mei 1954 ambapo vibaraka wa Uingereza kwa usaidizi wa Iraq wakampendua Shishakly ndipo Syria ikarudi katika mkono wa Uingereza na utawala wa bunge ukarudi, na wakati huu Uingereza ikaanza kudhihirisha muungano wa Baghdad kuwa wazi.

Na mara tu ulipoingia mwaka wa 1955 eneo hili nalo likaingia katika hatua mbaya zaidi katika mvutano wa Uingereza na Marekani. Ambapo Marekani kupitia Misri ikaanza kucheza mchezo wa "ukombozi", "umoja", na "ujamaa". Na Abdinasir akaanza kuingia katika mvutano mkali kwa niyaba ya Marekani dhidi ya Uingereza, akatekeleza amri ya Marekani kwa kufunga mkataba mkubwa wa bishara kwa kununua silaha kutoka kwa kambi ya kikoministi, na kuwadanganya wananchi kwamba amekuja kuipiga (Israeli) na kuivunja. Hayo yakawa na athari kubwa kwa raia wote wa kiarabu, akatabani ukabila wa kiarabu na kutangaza kwamba Misri ni nchi ya kiarabu, na hilo akalisajili katika katiba ya nchi ya Misri, akawa ananadi kuhusu uadilifu wa kijamii na umoja. Matendo yake hayo yakapelekea waarabu kumuunga mkono akawa ni kigogo miongoni mwa vigogo wa biladi za kiarabu. Na yaliyosaidia kufanikisha hayo ni mbinu walizotumia Marekani katika kuipiga Uingereza, ili kuleta vurugu baina ya watu wa biladi,

kwani licha ya uadui mkali uliokuwepo wakati huo baina ya Marekani na Urusi (muungano wa kisovieti) Marekani ilitumia mbinu za kuvutia Urusi katika maeneo haya, na kuifanya ni mchezaji wa kimataifa ndani ya eneo, na kumfanya kuwa ni mchezaji wa kimataifa dhidi ya Uingereza.

Pamoja na Marekani kuipiga vita ukoministi lakini ilimkinaisha Jamal Abdinasir kiongozi wa Misri kuukubali ukoministi na kuulingania, basi kule Misri kununua silaha kutoka kambi ya kikoministi ikawa ni sababu iliyoingiza Urusi (muungano wa kisovieti) katika eneo, na kule Abdinasir kulingania uzalendo ikawa ni sababu msingi iliyofufua uzalendo wa kiarabu baada ya kuwa umekufa au kukaribia kufa, na kutabanni kwake ukominsti ulioendelea kutokana na fikra ya "uadilfu wa kijamii" ikawa sababu iliyochangia kuenea kwa mrengo wa kushoto, na kutawala rai jumla ndani ya hili eneo. Kisha kule Misri kutabanni kushambulia miungano ya kigeni haswa muungano wa Baghdad hili likawa na athari kubwa katika kumuondolea shaka Abdinasir kuwa kibaraka wa Marekani, haswa kwa vile alivyokuwa akihujumu ukoloni wa Marekani. Kwa hiyo haikubakia shaka hata kidogo kwa waarabu wote kwamba Jamal Abdinasir ndie mkombozi mkubwa aliyemtumwa na Allah kuja kuukomboa huu Ummah kutokana na ukoloni, basi watu wote wakajifunga naye isipokuwa kundi moja lililokuwa likijaribu kumfichua na kumhujumu, lakini hilo halikuathiri chochote, akaendelea kudhibiti rai jumla kikamilifu. Na kutokana na udhibiti huu basi vibaraka wa Uingereza huko Jordan na Iraq kwa sifa ya kuwa viongozi nafasi yao ikawa yayumbayumba, na vibaraka wa Uingereza huko Syria na Lebanon pia wakawa katika hali mbaya kiraia. Kwa hiyo yakapatikana mazingira mazuri kwa Marekani kufanya kazi kuimaliza Uingereza bila eneo hili kuzinduka kwamba matendo yanayofanyika ni kuingiza mamlaka ya Marekani katika eneo kuchukua mahala pa Uingereza, na walipaswa kufahamu kwamba wajibu ilikuwa ni kumaliza ukoloni wa hizi nchi mbili: Marekani na Uingereza, na sio kubadilisha moja kwa nyengine.

Wakati huu yakatokea mabadiliko ya kindani huko Syria, lakini uungwaji mkono wa raia alioupata Abdinasir ulikuwa na athari katika kuzuia mabadiliko haya, kwani chama cha ba'thi kiliungana na chama cha kiarabu cha kikomisti (Al-hizb al-rabiy al-ishtiraakiy) kuungana huku kukaipatia chama cha ba'ath kuwepo katika jeshi. Kisha hivi vyama viwili vikanyanyua miito ya (Umoja, Uhuru na Ukoministi), vikawa na athari serikalini, na kikweli vikashirikiana vikapata kutoka kwa Abdinasir na anacho kinacholingania kuwa ni fursa kwao ya kuwafanya raia kuwakubali, na kuendesha "Umoja na Ukoministi" wanaotaka kufuata kwa hatua za wazi. Kwa hiyo Syria ikawa yatawaliwa na tawala zilizodhibitiwa na chama cha ba'ath ili kuepukana na shari yake, kuogopea yaliyokuwa yakidhaniwa kuwa wanauungwaji mkono wa raia watu. Kwa hiyo Syria ikawa na Uingereza kihakika, lakini ikitawaliwa na fikra mbili ya umoja na ukoministi kutokana fikra hizi kuathiri rai jumla. Kisha Abdinasir akabinafsisha Suez Canal, ukatokea uadui wa nchi tatu dhidi ya Misri, hapo uungwaji mkono wa Abdinasir kutoka kwa raia ukawa mkubwa sana. Ndio maana vibaraka wa Uingereza hawakuwa na ujasiri wa kudhihirika ulingoni, sauti zao zikafifia mpaka ikawa hakuna yoyote anayewahisi.

Katika mwezi wa nane 1957 wakakusanyika maofisaa kadhaa wakuu wa kijeshi na kushauriana kuhusu utawala wa Syria unavyofuata Magharibi, na ushawishi wa Magharibi unavyozidi kumakinika humo, basi wakaamua kunyakua madaraka lakini utawala uendelee, yaani raisi wa jamhuri na mawaziri wabakie na vyeo vyao, na hao maofisa wa kijeshi waendeshe mambo na kusimamia mambo ya utawala. Basi wakatekeleza kivitendo na kutenganisha Syria na ukoloni wa Magharibi, kwani Syria ilikuwa na Uingereza kihakika kabla ya huku kutenganishwa na ukoloni wa Magharibi, lakini kwa dhahiri yazingatiwa kuwa imefungwa na Marekani, kwakuwa fikra zilizo tawala ni fikra anazolingania Abdinasir: "*Uhuru*, *Ukoministi* na *Umoja*" na chamacha ba'ath chenye neno la kwanza katika rai jumla chadhihirisha kama kwamba

ni rafiki wa Abdinasir au mshirika wake. Ndio maana kikachukulia kuitenganishwa kwake na Magharibi ni hujuma dhidi ya Marekani, ingawa kihakika iliekezwa kwa Uingereza zaidi kuliko wamarekani.

Licha ya hayo, Uingereza walinyamazia kimya kutenganishwa huku wala haikufanya chochote. Lakini Marekani ilishikwa na wazimu ikaanza kutumia ubaguzi wazi kwa kuwapiga wale maofisaa na kuirudisha Syria katika zizi la Magharibi. Kukapatikana majaribio kadhaa kwa ajili ya hilo, lakini yote yakashindwa. Baada ya Marekani kushindwa kutatua matatizo, Abdinasir akajitokeza kuyatatua: akamtuma Mahmud Riadh, huyu akawa afanya kazi kupatikane muungano kati ya Misri na Syria, hapo Misri iwe itashika usukani wa utawala huko Syria. Basi Marekani ikachukua uongozi na ikawa yafanya kazi kuifukuza Uingereza kutoka Iraq na Lebanon.

Ilipofika tu mwaka wa 1958, kukawa na mapenduzi Lebanon kisha mapenduzi ya Iraq, hapo ikawa Syria, Iraq, Lebanon na Misri zote ziko mkononi mwa Marekani, wala haikubakia kwa UIngereza isipokuwa Jordan, na Abdinasir akawa huiandama hata huko Jordan, basi Uingereza ikawa iko karibu kumalizwa katika eneo lote, isipokuwa Uingereza haikuvunjika moyo, ikaanza kufanya kazi katika kambi yake Jordan. Na ilipofika tu mwaka wa 1961 ikawa ina nguvu zinazofanya kazi Syria, zikakusanyika nguvu jumla za kisiasa, chama cha wananchi, chama cha kizalendo, na chama cha Ba’ath au (vyama viwili vya ba’ath na al-hizb al-arabiy wal-ishtirakiy) vikakusanyika vyote hivi dhidi ya Abdinasir na dhidi ya umoja, Syria ikatengana na Misri, vibaraka wa Uingereza wakarudi kudhibiti utawala. Isipokuwa Marekani nayo ikamtoa Abdulkarim Qasim katika utawala huko Iraq baada ya kuwacha kuwa kibaraka wake na kuwa na wakoministi, hivyo huko Iraq ukapatikana utawala wa kimarekani unaosimamiwa na chama cha ba’ath, kikawa chafanya kazi kubadilisha hali ya Syria na Jordan ili kuziunganisha na Iraq. Uingereza ikawa na hofu juu hilo, basi vibaraka wake wa huko Damaskas wafanya mapinduzi ya kimaksudi na wakafanya chama cha ba’ath ni pazia ya utawala.

Isipokuwa mwaka wa 1971 baada ya Hafidh Al-asad kwenda Misri na kuingia katika umoja wa wanne, alirudi Syria kutoka Misri kwa uso tofauti na alioenda nao, kwani ilikinaishwa huko kwamba aweza kuwa raisi wa jamhuri ya kiarabu ya Syria licha ya kuwa yeye ni Alawiyya Nasiriyya. Na ikadhihirika wazi wakati huo kwamba Marekani ilikuwa nyuma ya hilo, kwamba itamtilia nguvu madamu ataifuata, kama ambavyo Misri itafanya kundi lake huko kumuunga mkono, na kwamba Misri na nyuma yake Marekani watafanya kazi kuondoa kizuizi kinachomzuia yeye kuwa raisi wa jumhuri kwakuwa ni Alawiyyu na watu wa Syria hawakubali kutawaliwa na Alawiyya bali MUislamu. Na hivyo ndivyo Marekani ilivyomuandalia mambo na kumuondolea vikwazo baada ya yeye kukubali kuifuata. Basi mchakato wa kutekeleza hayo ukaanza, polepole akaanza hatua za kuelekea uraisi wa jamhuri, akaanza kuzuru Kaskazini, kisha akakutana na wananchi. Na alipoona kuwa wananchi wanamfuata mtawala na kwamba hakuna upinzani wa wazi kwake, basi akakimbilia kufanya hilo kivitendo, Hafidh Al-asad akapendekezwa kuwa rais wa jamhuri ya kiarabu ya Syria, na tarehe 12/3/1971 ikafanywa ndio siku ya kura, kisha Hafidh Al-asad akawa raisi wa jamhuri ya Syria, hapo Syria ikarudi tena kwenye makucha ya Marekani, na bado hadi leo.

Hiyo ndio mifano ya mivutano ya Uingereza na Marekani huko Syria, nalo ndio dhihirisho la wazi zaidi la mivutano yao. Ama katika nchi za kiarabu zilizobakia, hakika Jordan iliendelea kuwa kivuli chini ya udhibiti wa Uingereza, kwakuwa thuluthi mbili za wananchi wake ni wapalestina, na wengi wao wanaishi kwa vitambulisho vya Umoja wa Mataifa, na maisha ya watoto wake ni wanaofanya kazi nje ya Jordan, na thuluthi yake ni mabedui wa mashariki mwa Jordan na wengi wao wakiishi kwa kazi ya watu wao ndani ya jeshi. Kwahiyo Marekani haikupata katika wananchi wa Jordan hali nzuri kama ilivyoipata huko Syria, hivyo basi hakukutokea ndani ya Jordan kitendo chochote cha kisiasa kinachodhihirisha mvutano wa kimataifa, isipokuwa tu maandamano yaliyotokea dhidi ya muungano wa Baghdad, jaribio

la mapenduzi yaliyofanywa na mfalme Hussein mwaka wa 1957 aliyofanya ili kuwafukuza baadhi ya vibaraka wa Abdinasir katika miji. Kwa hiyo haizingatiwi kwamba ndani ya Jordan kulifanyika matendo muhimu ya kisiasa yanayohusiana na mivutano, ingawa ni miongoni mwa sehemu kubwa inazofanyika mivutano baina ya Marekani na Uingereza kwa sababu ya utajiri wa ajabu ulio chini ya ardhi yake na chini ya maji yake.

Ama kuhusu Iraq: licha ya kuwa Abdul Salam Arif alichukua utawala baada ya watu wa chama cha ba'ath, alikuwa akifuata nyayo za Abdinasir, lakini vibaraka wa Uingereza miongoni mwa wanasiasa na maofisaa wakuu wa jeshi walipata fursa muhimu ya kuchangamka, kwa juhudi ndogo wakadhibiti jeshi, na kutokana na matukio ya kiuchumi Iraq ikarudi kwa Uingereza. Pamoja na kuwa Marekani ilirudia Iraq katika zama za Abdurrahman Arif, lakini waingereza katika watu wa ba'ath na wengineo walidhibiti utawala mwaka wa 1968, ushawishi wa Uingereza huko Iraq ukaendelea mpaka 9/4/2003 Baghdad ilipoanguka, kwa kuanguka nidhamu ya Saddam Hussein na ba'ath kutawala Iraq, wakati Iraq ilipoingia chini ya ukoloni wa Marekani.

Ama kuhusu Misri: hakika tangu Abdinasir alipochukua utawala ikawa ni kambi kubwa ya kimarekani na bado mpaka sasa ni kambi muhimu ya kimarekani, wala haikutokezea amali zozote muhimu za kisiasa zinazoingia katika mvutano isipokua yaliyotokea baada ya kufariki Abdinasir kwa mda mchache, kwani kulipatikana mambo matatu ambayo ingewezekana kurudisha Misri kwa Uingereza:

**Kwanza:** kulisimama utawala dhaifu usioweza kujihifadhi wenyewe, achilia mbali kuziba nafasi aliyoiwacha Abdinasir.

**Pili:** Ndani ya Misri kulipatikana harakati katika jeshi na wananchi wakitangaza kutaka vita na zikitangaza kumfukuza mrusi (muungano wa kisovieti) na kutangaza kujikomboa kikamilifu.

**Tatu:** Mawasiliano baina ya Uingereza na Misri yaliyoanza kwa ziara ya Douglas Home waziri wa nje wa Uingereza kwa Misri, kwa

hoja ya kuhudhuria jeneza la Abdinasir, halafu zikafuatia ziara kadhaa kutoka Uingereza kupitia Libya, kisha ikawa rasmi si kwa ziara ya Muhammad Hassanein Heikal peke yake bali kwa barua rasmi, Misri kutaka kiwazi kujenga mahusiano baina yake na Uingereza, ikawa suala la Misri kurudi kwa Uingereza ni suala la wakati tu na wala sio suala la kufanywa juhudi kulingana na Saadat kuwa msimamo wa wasiwasi mwanzoni mwa utawala wake, lakini licha ya hayo Marekani ikaweza kummakinisha Saadat katika utawala, ikabuni vita mwaka wa 1973 ili kuandaa mazingira ya kufanya amani na (Israel) ikamfanya Saadat kuwa shujaa ikammakinisha akaweza kuyadhibiti mambo, kwa hiyo mvutano wa kimataifa ndani ya Misri ukafichika na kuendelea kuwa kambi kubwa na muhimu ya Marekani mpaka sasa.

Ama kuhusu nchi za Kaskazini mwa Afrika: hakika Moroko iliingia chini ya udhibiti wa Marekani wakati ilipopapata uhuru wakati wa Muhammad wa tano, na Aljeria ikawa ya Marekani kwa sababu ya Ahmed bin Bella, lakini hayo hayakudumu mda mrefu, kwani Muhammad V (wa tano) alifariki na mwanawe Hassan akashika utawala na kuifuata Uingereza, ama bin Bella Uingereza ilimuandalia mapinduzi dhidi yake kipitia njia ya mfalme Hassan na Muhammad Khidar, wakawavutia Twahir Zubeiri na Abu Madin wakafanya mapinduzi yaliyomuangusha Muhammad bin Bella, hivyo Marekani ikatolewa Aljeria na Uingereza ikawa ndio yenye mamlaka humo. Ama Libya na Tunisia: hakika Marekani haikuweza kuingia kwa yoyote wala kutekeleza amali yoyote ya kisiasa kwa yoyote, bali ushawishi wa Uingereza yaliendelea katika hizi nchi mbili, kwa hiyo Marekani na Uingereza hawakushiriana katika mvutano.

Ama Yemen na nchi za ghuba isipokuwa Saudia: zote zanyenyekea mamlaka ya Uingereza wala hakuna mvutano kwa maana inayojulikana isipokuwa huko Yemen ambapo ushawishi wa Uingereza humo hukumbana na usumbufu na hali ya vuta-nikuvute kutoka kwa Marekani. Ama Saudia Marekani iliweza kuvuta baadhi ya watu wa familia ya ufalme, na wengine kati yao wakabaki kwa

Uingereza, hivyo basi mvutano wa Uinereza na Marekani humo hutokea kupitia wanafamilia wa ufalme, kwa mfano kutokea Fahdi bin Abdulaziz kufika madarakani Saudia ikawa katika mzunguko wa siasa za Marekani, na lau hali itabadilika kwa mmoja kati ya vibaraka wa Muingereza kushika utawala kama Abdallah aliyekua mfalme mtarajiwa, basi Hijaz na Najdi mwishowe zitarudi tu kwa Uingereza, hivi ndivyo ilivyo, japokuwa Marekani baada ya ulipuaji wa 11/9/2001 yajaribu kudhibiti mamlaka yake ndani ya Saudia kwa kufanya mabadiliko katika mtindo unaofuatwa bila kuogopa kubadilikabadilika kwa familia ya ufalme. Na yaonekana hayo mabadiliko bado yanafanyiwa utafiti na waundaji sera wa Washington, kama zinavyonukuu vyombo vya habari.

Mvutano wa Marekani na Uingereza uliendelea kuzidi sana katika miji ya kiarabu miaka ya hamsini na sitini ya karne iliyopita, na kadhia ya Palestina ikaendelea kuwa ndio msingi wa mvutano huu, kwani Uingereza mwaka wa 1964 ilifikia kukinai kuhusu hili eneo kwamba hakuna uwezekano wa kukubali nchi ya kigeni kindani, na kwamba jaribio la kubuni nchi ya kiyahudi ndani ya Palestina ni jaribio la kufeli. Kwa hiyo ni bora kuunda serikali ya kielmani (kisekyula) kwa mtindo wa serikali ya Lebanon, na hilo ni kwa kurudia kuhuisha ule mradi wa karatasi nyeupe ambao Ungereza iliweka mwaka wa 1939 na kuufanya kuwa ndio msingi wa utatuzi wa hii kadhia. Ikaongea na wakubwa wa kiyahudi nao wakakinai na hii fikra, na Habib Bourguiba kiongozi wa Tunisia akafanya ziara ya Misri, Jordan, Lebanon, Kuwaeit, na Saudia na kuufikisha huo mradi wa Uingereza uliotajwa kwa viongozi wa kiarabu na baadhi ya Wapalestina, akachukuwa makubaliano jumla juu ya mradi ule, na Uingereza ikaanza kujaribu kuutekeleza, lakini Marekani kupitia kibaraka wake Abdinasir ikaweza kuuangusha mradi huu kwa kuupinga vikali.

Kutokana na yote hayo yabainika kwamba kadhia ya Mashariki ya Kati kwa upande wa kimataifa, ilipaswa iwe ni kadhia ya mvutano baina ya watu wa eneo na nchi za kikoloni, kama

ilivyotokea kwa Marekani yenyewe ilipowatimua wakoloni kwake, na kuunda nchi ya muungano wa majimbo (U.S.A) na kama China ilivyofanya baada ya vita vya pili vya dunia ilipofukuza ukoloni wa Japan na ushawishi wa kigeni na kuunda nchi ya kikoministi yenye daraja yake ulimwenguni, kama ilivyo kawaida katika kila nchi iliyokoloniwa, iliyowezeshwa kimataifa na kimaeneo kujikomboa kutokana na mamlaka ya kigeni na kujiundia nchi yenye hadhi ya kimataifa. Lakini - kwa masikitiko makubwa- kadhia ya Mashriki ya Kati haikuwa hivyo, bali kadhia yake ya kimataifa imekuwa ni mvutano mkali baina ya Marekani na Uingereza wa kukoloni hili eneo na kulipora, na kuliwekea vikwazo vipya vikali vinavyowazuia watu wa eneo wasifikirie - japo kufikiria tu- kujikombo na kuwa huru. Hivyo basi katika miaka ya sabini na ya thamanini ya karne iliyopita mvutano baina ya Marekani na Uingereza ukaendelea lakini haukua mkali sana.

Na kwa kuanguka muungano wa kisovieti mwanzoni mwa miaka ya tisini karne iliyopita, na kwa Marekani kufaulu katika vita vya Iraq na kudhibiti Kuweit na eneo la Ghuba, uwiyano wa nguvu ulimwenguni ulibadilika, Marekani ikaanza kuchora ramani mpya ya eneo hili, kwa mujibu wake waingereza wakageuka kuwa mchezaji wa pili, wakawa hawana nguvu tena ya kupambana na Marekani, kiwango chao kikashuka na kupungua uzito wao, basi wakalazimika kutumia uchimvi na hila dhaifu, na wakalazimika kutegemea muungano wa Ulaya ili kupitisha mipango yao iliyokuwa kiasli ni mipango ya kirongo, mfano mikataba ya Oslo waliyojaribu wakati huo kuizingira Marekani nayo, lakini Marekani ikaweza kuibadilishia njia nyengine ili itumikie malengo yake. Kisha Uingereza ikalazimishwa kukubali kuanguka kwa mradi wake wa nchi ya kielmani na kutangaza kumalizika kwake na kukubabali mradi wa Marekani uliopitisha kuundwa nchi ya kiarabu ya kipalestina upande mmoja, na nchi ya kiyahudi kwa upande mwengine. Arafat aliyekuwa raisi wa taasisi ya ukombozi wa Palestina rasmi akaachana na fikra ya nchi ya kielmani katika kongamano la kitaifa la Palestina lililofanywa Aljeria mwaka wa

1988 M, na akatangaza rasmi kukubali fikra ya nchi mbili katika vikao vyote vya kimataifa tangu tahere hiyo. Na mfalme Hussein pia kishingo upande akalazimika kutangaza kutenganishwa kikanuni na idara baina upande wa kimagharibi na wa kimashariki wa mto wa Jordan na kutambua udharura wa kuundwa nchi ya Palestina.

Hivi ndivyo ulivyoanguka mradi wa nchi ya kielmani kivitendo na kirasmi, na haikubakia isipokua mradi wa Marekani, nao ni kuundwa nchi ya Palestina pambizoni mwa (Israel), ukawa mradi huu ndio hitajio la kimataifa ambalo umoja wa mataifa, muungano wa Ulaya, Urusi, pamoja na Marekani wote wamelitabanni. Hizi nchi na pande nne zikashikana kutilia nguvu fikra ya kuundwa nchi ya Palestina kando ya (Israel) kupitia mpango wa Bush ulioitwa "ramani ya njia", na Marekani kwa sasa haitekelezi hiyo *ramani ya njia* kikweli. Kwa kuwa mwaka huu 2oo4 M ni mwaka wa uchaguzi kwake, inataka tu kulishuhulisha eneo kama ilivyozowea kushuhulisha eneo kwa mradi baada ya mradi, hadi utakapofika wakati muwafaka wa kutimiza maslahi yake, na hapo Mayahudi watanyenyekea amri za Marekani pindi ikitaka kwao kikweli kutekeleza miradi yake, nao hawawezi kukataa watakapoelekezwa vikali na haswa kwakuwa wanajuwa kuwa Marekani inapotimiza maslahi yake kupitia miradi yake kwa eneo pia wakati huohuo yachunga maslahi ya nchi ya kiyahudi pia.

Kama Uingereza ilivyolazimika kufuatana na Marekani katika fikra ya nchi ya kipalestina pia ililazimika kufuatana nayo katika vita vya Iraq na kibaraka wake Saddam Hussein kumalizwa ili kuhifadhi baadhi ya mapato yatakayobakishwa na nchi kubwa lakini kwa pumzi ya Marekani yenyewe.

Pia Marekani iliweza kuingiza ushawishi wake kwa uzito pambizoni mwa ushawishi wa Uingereza ndani ya nchi zote za Ghuba, Yemen na Jordan. Kama ilivyoweza kuvutana na ushawishi wa nchi mbili ya Uingereza na Ufaransa ndani ya nchi za Kaskazini mwa Afrika na Uturuki. Kwa hiyo Marekani itakuwa ndio

iliyodhibiti kihakika nchi za eneo la Mashariki ya Kati ambazo zaidi ya nchi ishirini na nne, na Uingereza yalazimika kuifuata nyuma Marekani ili kupata baadhi ya mabaki, na kumsumbua nyuma ya pazia bila ya kuwa na ujasiri wa kupinga kiwazi mradi wake haswa kama ilivyokuwa nyuma ikivutana na miradi wa Marekani katika eneo. Kwahiyo twaweza kusema kwamba mvutano wa wazi baina ya hizi nchi mbili ulimalizika mwishoni mwa karne iliyopita mpaka leo, ukabadilika na kuwa kwa mbinu ya ushirikiano na mikataba pamoja na kuivisha Marekani taji kama kiongozi wa kwanza katika eneo hili na mwenye mkataba mkubwa, wakati Uingereza hubakia tu kama mtumishi ili kubakia katika mwangaza, kwani uwezo wa Uingereza leo - bali uwezo wa muungano wa Ulaya kwa ujumla wake – ni dhaifu katika kulazimisha miradi ya utatuzi ndani ya hili eneo, ndio maana twaona Uingereza na nchi za muungano wa Ulaya hushikana na miradi ya Marekani na kushughulika nayo, Uingereza wala muungano wa Ulaya hawawezi kutekeleza chochote pasi na mchangio wa Marekani. Lakini pamoja na hayo hatuwezi kusema kuwa dori ya Uingereza katika hili eneo imemalizika, bali hakika hisia zake za ukubwa na kwamba ni nchi kubwa bado ipo, na uhodari wake wa kisiasa haujazima, kadhalika bado vibaraka wake wanapumbua, yaani hakika nguvu ya Uingereza bado imejificha na yaweza kushughulika wakati wowote.

Ama Ufaransa: bado yapambana ili iwe na kitu katika ushawishi ndani ya Aljeria, Tunisia na Libya kwa kuwa kuna idadi kubwa ya wenye thakafa ya kifaransa ndani hizi nchi, baada ya kupoteza nguvu zake kikamilifu huko Moroko na Mauritania.

Ama (Israel): imepanga sera zake pamoja na maslahi ya marekani na kuchanganyika kikamilifu ndani ya maslahi hayo, haswa katika zama za wahafidhina wapya katika idara ya Bush mwana, na ikadandia kwa joto na haraka mawimbi ya kutetewa, na Marekani nayo ikaihifadhia cheo chake kama nchi kubwa ya kieneo ndani ya eneo hili, na ikachukulia kwamba kutetea kuwepo kwa

Israel ni kuitetea Marekani yenyewe, hivyo (Israel) ikababakia kuwa ni mtoto aliyetendekezwa ambaye mzazi wake hataki akasirike.

Ama watawala wa biladi za kiarabu: wameendelea kuitumikia Marekani hadi kufikia kiwango cha utumwa, na kwa hilo wakapoteza kilichobakia katika uaminifu wa wananchi wao, wakafanywa wajinga na mabwana zao, na wakazidi kudhalilishwa. na kuwataka kuzidi kulegeza misimamo, kwa hivyo wakawa ni vyombo ambavyo ni rahisi kubadilishwa kupitia mikono ya maadui kama ilivyofanyika kwa Saddam na huenda yakatokea kwa wengine, Nao kwa hilo wakapoteza uungwaji mkono wa wananchi wao, na wakaendelea kuwa katika utawala kwa uungwaji mkono wa mabwana zao na chini ya huruma na fadhila za hawa mabwana. Kwa hivyo hali yao ikawa ni ngumu zaidi kuliko nyuma kwakuwa wamekuwa baina ya moto mara mbili: moto wa wananchi wao na moto wa mabwana zao, wakawa baina ya nyundo ya wananchi wao na chuma cha mabwana zao. Kwa hiyo eneo la Mashariki ya Kati limekuwa ni eneo lenye hatari ya kulipuka wakati wowote, na lina uwezekano mkubwa wa kuzaliwa serikali ya kiislamu ya kihakika, na uchungu wa mazazi yake yameshaanza kuonekana wazi.

***

## [3] KADHIA YA MASHARIKI YA MBALI

Hakika mambo ya Mashariki ya mbali ni tofauti na kadhia ya Mashariki ya Kati, hata kama ni kadhia ya kimkakati na kadhia ya kikoloni, lakini hali yake yatafautina sana, na ikiwa tutazingatia kwamba Bara Hindi yaweza kuwa kadhia peke yake katika zama hizi, basi Mashariki ya mbali itabakia na mataifa matano nayo ni: taifa la Uchina, taifa la Japan, taifa la Korea, taifa la Indo-china na taifa la Indonesia, na kila taifa lina kadhia yake. Kabla ya kuzungumzia kadhia za Mashariki ya mbali kiufafanuzi kwanza twajumlisha kadhia yake kwa sura ya ujumla: katika upande wa kimikakati huchukuliwa kuwa ni muhimu kwa Marekani na kwa Urusi pia. Kwani kwa upande wa bahari ya Hindi huchukuliwa kuwa ipo katika mipaka ya Marekani, na kuna nguvu mbili kubwa

zinazoweza kuwa hatari kwa Marekani, nguvu hizi mbili ni China na Japan, yawezekana pia kuwa hatari kwa Urusi. Kiupande huu huchukuliwa kadhia yake kuwa ni kadhia ya kimikakati. Ndio maana Marekani ikawa na pupa kuwa na nguvu Mashariki ya mbali na kuendelea kubakia humo mpaka kabla ya kupigwa na Japan katika bandari ya Pearl kwenye vita vya pili vya dunia, na baada ya kupigwa humo Mashariki ya mbali ikawa ni eneo muhimu kwa Marekani kiupande wa kimikakati. Ndio sababu manuwari zake za kivita na Ndege zake zikaendelea kuwa katika eneo lile kwa sura ya kudumu kwenda na kurudi.

Ufilipino huchukuliwa kuwa ni kambi ya Marekani tangu kabla ya vita vya pili vya dunia mpaka leo, kwani yatilia sana umuhimu eneo hili kwa kujihami dhidi ya hatari iliyojificha ndani yake. Ama kuhusu Urusi: kwa kuwa yapakana na eneo hili na wala haikutenganishwa na bahari kama hali ilivyo kwa Marekani, ndio ikawa haiweki tahadhari za kijeshi dhidi yake, japo huhifadhi mipaka yake na China na kujaribu daima hufanya mahusiano ya mapenzi na urafiki baina yake na Japan.

Ama kuhusu upande wa ukoloni: takriban daima ukoloni ulikuwa ukifanywa tu na Uingereza, Ufaransa, Uholandi na Ureno, kwa kuwa Marekani ingawa iliidhibiti Ufilipino na kuwa ni koloni yake au inayofanana na koloni yake, isipokuwa haikushiriki katika ukoloni nje ya ulimwengu mpya pindi yalipofurika mawimbi ya ukoloni katka karne ya kumi na tisa. Kwa hiyo yaweza kusemwa kwamba Uingereza, Ufaransa na Uholandi, ndio daraja ya kwanza katika nchi zilizoanza kukoloni Mashariki ya mbali, na Ureno ikashirikiana nao katika sehemu ndogo.

Ama Uingereza: hii ilikoloni kisiwa cha Hong Kong katika mwamao wa China kusini mashariki, ikakoloni Malay na Singapore na sehemu ya Kaskazini katika kisiwa cha Borneo, na ikakoloni Burma na Silan kando na ukoloni wa India. Na sera zake zote zimesimama juu ya kuhifadhi hizi koloni. Na wakati ilipokuwa kambi ya Magharibi ni moja kabla ya wale wababe wawili kuafikiana, sera ya Uingereza ilitafautiana na sera ya Marekani kwa Mashariki ya mbali, licha ya kumhitahijia sana Marekali ili kuisaidia

kuhifadhi koloni zake. Uingereza ilikuwa ikiangalia China kwamba ni soko la biashara zake, ndio maana haikuchukulia China kuwa pamoja na kambi ya kimashariki kuwa italeta hatari kwake ndani ya Mashariki ya mbali, ndio sababu haikupata sababu ya kuishambulia China na kusuguana nayo katika eneo lile, na hujaribu eneo hili libakie na utulivu na umakinifu, kwakuwa harakati yoyote itakayopatikana katika eneo hili italeta shida kwa makoloni.

Ndio maana ikapambana na harakati za Indonesia za kuifukuza Uholandi, na ikajipendekeza kwa China ya kiujamaa na kuitambua na ikafungua mlango wa biashara nayo, ikawa yasimama dhidi ya Marekani katika sera za Mashariki ya mbali. Hayo yote yakawa ni ajili ya kuhifadhi koloni hizi, sio tu kwa kuwa hizi koloni zilikuwa masoko ya bidhaa zake, bali pia kwa sababu ni zina utajiri wa malighafi ambazo Uingereza huzipora peke yake na kujimakinisha humo tangu zamani. Kwa sababu hiyo msimamo wake kwa Mashariki ya mbali huzunguka juu ya kwamba ukoloni wake ubakie ndani ya biladi hizi, iwe ni kwa namna yoyote ya ukoloni, na ushawishi wake katika eneo kubakia.

Ama kuhusu Ufaransa: hakika baada ya vita vya pili vya dunia ilirudisha Indo-chine nayo ni: Vietnam, Loas, na Cambodia, na hizi huzingatiwa kuwa ni miongoni mwa koloni za thamani na kubwa zaidi kwa Ufaransa, kwa kuwa ni vyanzo katika vyanzo vya utajiri mkubwa wa Ufaransa, kwa sababu ya hii miji kuwa na utajiri wa malighafi. Lakini Ufaransa haikuweza kuhifadhi koloni hizi, kwani China ilivamia na kudhibiti upande mmoja na Marekani upande mwengine, mpaka ikalazimika kuwacha koloni zote na kutoka.

Ama China: iliunda na kuiunga mkono harakati ya ukombozi iliyotangulia huko Vietnam, nayo ni harakati ya (Viet-menh), haya mapenduzi yakaweza kuishinda Ufaransa mpaka ikalazimika kujiondoa kutoka miji mingi huko Vietnam, ikavunjika kijeshi na kisiasa hadi mwishowe ilipojiondoa kutoka koloni hizi.

Ama Marekani: ilikuwa ikitaka kuchukua koloni za Indo-chine kutoka kwa Ufaransa, ikawa yajifanya kuisadia Ufaransa na wakati

huo huo ikishajiisha mapinduzi dhidi yake kwa mbinu za kisiri, ikaifanya Ufaransa kuwa baina ya matarajio ya kubakia kwa fadhila ya msaada wa kijeshi kutoka kwa wamagharibi haswa Marekani, na baina ya kukata tamaa ya kuyashinda mapenduzi. Mwishowe likawekwa kongamano la Jeneva, ili kuangaliwa suala la Indo-chine, matokeo yake ikawa ni Ufaransa kutoka na marekani kuchukua mahali pake huko Lois, Vietnam kusini, na Kambodia, na China kuchukua mahali pake huko Vietnam Kaskazini, yaani nyuma ya nchi ya Vietnam Kaskazini iliyojitenga na nchi (kisha baadaye ikajiunga na Vietnam). Kwa hiyo mwishowe Ufaransa ikasafishwa kutoka hili eneo.

Ama Uholanzi: hakika Marekani iliwashajiisha waindonesia kufanya mapenduzi dhidi ya Uholanzi, wakatekeza mapenduzi makali ambayo Urusi (muungano wa kisovieti) na Marekani licha ya kugongana kwao waliyasaidia, na Uingereza ikasimama upande wa Uholanzi dhidi ya waindonesia, mwishowe waindoneshia wakaishinda Uholanzi kijeshi, wakapeleka kadhia hii kwa Umoja wa Mataifa, na Marekani kuwasaidia. Umoja wa Mataifa ikaamua kujikomboa kwa Indonesia, kwa hivyo Uholandi ikatoka Indonesia na haikubakiwa na isipokuwa Irian Magharibi. Lakini Indonesia ikaifuata huko pia kwa kuwezeshwa na Marekani, ikaendelea kuiandaman nyuma mpaka ilipoitoa huko pia, kwa hiyo Uholanzi ikatoka kabisa katika eneo lote wala haikubakiwa uwepo wowote wa kikoloni.

Ama kuhusu Ureno: ilikuwa ikikoloni Goa huko India, na India ilipoona kwamba Uholandi imetolewa kutoka eneo ikahamasika kuitimua Ureno, na kwa kuungwa mkono na Uingereza na Marekani ikaikoloni Goa na kuifukuza Ureno, ikawa ni sehemu ya India. Kwa hiyo hakuna nchi yoyote ya kikoloni iliyobakia katika eneo hili isipokuwa Uingereza na Marekani. Na kabla ya kambi mbili (Marekani na mungano wa kisovieti) kupatana Uingereza ilikuwa na matumaini ya kubakia, lakini baada ya makubaliano yao na msimamo wa kiamataifa kubadilika Uingereza ilianza kuwa

wasiwasi juu ya koloni zake na hatari ikaanza kumtishia. Hilo ni kwa sababu Marekani ilianza kujaribu kuitoa Uingereza kwenye eneo ili kuchukua mahali pake kwa kutumia mbinu mpya ya kikoni chini ya fikra ya kumaliza ukoloni na kuyapa mataifa uhuru wake, fikra ambayo Umoja wa mataifa iliitabanni na ikawa yaifinya Uingereza na kuikazia ili kuyapa mataifa uhuru wake, Uingereza nayo ikatumia hila katika hayo na kuweka muungano baina ya kisiwa cha Borneo Kusini, Sarawak, na Sabah na baina ya Malay na Singapore, kwa mujibu wake ikaunda nchi ya muungano iliyoiita Malaysia, kwa hiyo ikabadilisha sura ya kikoloni na kuendelea kuwa mkoloni wa biladi.

Basi haikuwa kwa Marekani isipokua kuchochea Indonesia kuomba Kaskazini mwa bara la Borneo, ikawa Indonesia yatekeleza uvamizi wa Borneo Malay na Singapore kwa uvamizi kutoka kwa wanamgambo, ikawa yahimiza watu kufanya mapenduzi dhidi ya Uingereza, kwahiyo baina ya Indonesia na Malaysia kukawa na hali inayofanana na vita iliyoitwa kwa jina la siasa ya makabiliano. Hali ikaendelea hivyo miaka kadhaa, na walipoafikiana wale wababe wawili, ikawa katika jumla ya waliyoafikiana ni kuondoa kambi za kijeshi ulimwenguni na kuisafisha Uingereza kutoka Mashariki ya mbali, basi mikazo ikazidi kwa uingereza huko Mashariki ya mbali, Uingereza ikaamua kuwacha kambi ya Singapore na kuondoa kambi zake za kijeshi kutoka Seuz Mashariki na Mashariki ya mbali, na ikachangamka kupitia vibaraka wake wa Indonesia kupambana na Sukarno aliyekua akiongoza siasa ya makabiliano. Hapo Marekani ikaridhia kuondolewa kwa Sukarno Indonesia na kuleta vibaraka vyake wengine katika jeshi wakiongozwa na Suharto. Baada ya Uingereza kutoka kambi ya Singapore ilitenganisha Singapore na Malaysia, hivyo Malaysia ikawa imeundwa kutokana na Borneo Mashariki, Sarawak, Sabah, na Malay.

Baada ya hivi vitendo, hili eneo likatulia kiasi, vitendo vikafungwa na kujiandaa kuipiga China. Na yadhihirika kwamba katika jumla ya mipango ya wababe wawili ndani ya Mashariki ya mbali ilikuwa ni kuisafisha kabisa Uingereza kutoka hili eneo na

kutoibakisha. Ikawa yatarajiwa hao wababe wawili kufanya kazi kumaliza uwepo wa Uingereza huko baada ya kufunga faili ya China, lakini kutokana na matukio kufatana kwa kasi, na Marekani kurudi katika kupandisha mgogoro na muungano wa kisovieti punde baada ya kumalizika vita vya Vietnam, na China kunyenyekea matakwa ya wababe wawili, na Marekani kudhania kwamba kuingia kwake Malaysia kupitia miradi ya kiuchumi na mashirika ya kimaeneo kutamuwezesha kuchukua nafasi ya Uingereza hapo Malaysia, haya yote yalizuia kufikia malengo (ya kuitokomeza Uingereza) mpaka sasa, ndio maana Uingereza bado ina ushawishi huko Mashariki ya mbali.

Ama Marekani na Ufilipino wamefunga mikataba ya kikoloni inayofanana sana na mikataba ya kikoloni iliyokuwa Uingereza ikifunga nayo Misri, Jordan, Iraq na nchi nyenginezo. Kwa hiyo Ufilipino hata kama kinadharia si koloni ya Marekani, lakini ni koloni yake kivitendo. Baada ya Marekani kufaulu kuitoa Uholanzi kutoka Indonesia ilijaribu kuingia mahali pake, lakini waindonesia wakapambana naye kwa miaka mingi, wakakataa kutoa ukoloni na kuingiza ukoloni mwengine. Marekani ikaanza kuweka vikwazo mbele ya Indonesia, kutekeleza mapenduzi ya kiraia dhidi yake na kunyamazia majaribio ya Uingereza kuingia Indonesia kupitia vibaraka, na kuwashajiisha wachina kuhamia Indonesia kama ilivyo shajiisha Ujamaa kuingizwa. Na kutokana na hivi vikwazo watawala wa Indonesia wakanyenyekea ukandamizaji huu, wakakubali mikopo ya Marekani na misaada ya kijeshi, Indonesia ikaingia chini ya ushawishi wa Marekani, hivyo ikawa yahesabiwa ni katika wafuasi wa Marekani tangu zama za Suharto. Na baada ya mapatano ya wale wababe wawili nafasi ya Marekani huko Indonesia ikawa na nguvu, ikawa ndio yenye kuidhibiti, haswa kudhibiti jeshi na uchumi wa nchi, na kuendelea hivyo mpaka leo.

Mbali na Indonesia, Marekani ilitawala sehemu nyingi za Indo-chine baada ya kuifukuza Ufaransa, na Korea Kusini baada ya vita vya Korea, na bado yajaribu kuchukua nafasi ya Uingereza

katika koloni zake huko Mashariki ya mbali baada kumfukuza humo. Na ikifaulu kwa hilo basi kadhia ya Mashariki ya mbali itabadilika kutoka kuwa kadhia ya kimataifa na kuwa shamba la Marekani.

Hiyo ndio hali ya Mashariki ya mbali kiujumla, ama kuhusu watu wa Mashariki ya mbali: hakika watu hawa kwa upande wa kifikra ni chini ya kiwango cha watu wa Mashariki ya kati, lakini fikra ya kujikomboa na ukoloni iliyoenea ulimwenguni kabla ya vita vya pili vya dunia na wakati vikiendelea, na kuzidi kuendelea baada yake, iliwaathiri watu wa eneo hili zaidi kuliko ilivyowaathiri watu wa Mashariki ya mbali. Hilo ni kwa sababu hiyo fikra walioileta ni watu wa ujamaa, nayo ni sehemu ya mapambano ya ujamaa dhidi ya urasilimali. Ndio maana hiyo fikra hii ikapenya kutoka Urusi (muungano wa kisovieti) kupitia njia ya China hadi kwa watu wa Mashariki ya mbali kwa nguvu na kuwasha moto ndani ya hawa watu. Ndio sababu twapata kwamba watu wa Indo-chine wakaigeuka Ufaransa kabla ya vita vya pili vya dunia na baada yake, na watu wa Indonesia nao wakaigeuka Uholanzi kabla ya vita vya pili vya dunia na baada yake. Watu wa Korea wakaamini fikra ya kiujamaa na ikawaathiri, mpaka watu wa Malay, Borneo Kaskazini, Singapore, nao wakageuka Uingereza. Ikawa natija ya mapenduzi haya ni Indonesia kupata uhuru wake, na kumfukuza mholanzi, na Vietnam Kaskazini kufikia kuzingatiwa kuwa ni nchi yenye nguvu, na Uingereza ikalazimika kuunda muungano wa Malaysia. Haya yote ni kwa sababu ya fikra ya kujikomboa kutokana na ukoloni (fikra) iliyokuwa imesambaa katika hili eneo.

Na kwa hakika Marekani na Uingereza walijua jambo hili, kwa hiyo hufanya bidii ili mwenendo wa kikoloni wa zamani usidhihiri katika ushawishi wao ndani ya eneo, bali ni mahusiano ya kibiashara, kisiasa, kithakafa na mikataba mfano wa hayo, kwa namna ambayo itadhihirika kiwazi kwamba ni mahusiano ya kimataifa na sio amri za kikoloni.

Kuna maangalizo mawili yaliyobakia kuhusu kadhia ya Mashariki ya mbali:

1. Yale Anayochochea Marekani kuhusu Korea Kaskazini na kuiondolea silaha zake za kinuklia.
2. Kuzidi kuenea kwa Uislamu katika hili eneo, haswa Indonesia na Malaysia.

Ama kuhusu maudhui ya Korea Kaskazini: hakika Marekani huyachochea ili kubuni tatizo motomoto katika mipaka ya China. Kwani sera ya Marekani ya kudumu katika eneo hili ni kuizingira China kwa nchi zenye nguvu au kuizulia matatizo makali yatakayo ishughulisha yenyewe ili isiangalie nje yake, kwa kuogopea isije kushindana nayo katika ushawishi na kuathiri maslahi ya Marekani. Na lau Marekani ingeweza kurudi kuunganisha Korea kama ilivyotokea kwa Vietnam, ili kuwe na nchi zenye nguvu kuizunguka China, basi isingechelewa kufanya hivyo kama inavyofanya kwa India mbele ya China.

Kwa hiyo basi, kinachotarajiwa ni kwamba Marekani itaendelea kulitingisha suala hili ili liendelee kuwaka pasi na kutulia, lakini kwa sharti ya kuishughulisha China na matatizo, sio kuwa matatizo yawe ni ya Marekani peke yake. Na ni kwa sababu hii ndio maana ikawa na pupa kushirikisha nchi za eneo lile katika tatizo la Korea, ikawa yaweka mikutano ya nchi sita: Marekani, Korea Kaskazini, China, Urusi, Japan, na Korea Kusini.

Na kusababisha matatizo makali ndani ya China au katika mipaka yake ni msitari thabiti kulingana na sera ya Marekani, huuchagulia wakati mzuri, wakati mwengine huyatingisha kupitia India, au huyatingisha kindani chini ya mwito wa haki za kibinadamu, au kwa kupasha anga joto na Korea katika mipaka ya China, au yasiyokuwa hayo, na hupatiliza kila fursa nzuri katika mwelekeo huu, ikaja fursa mnasaba kwa Marekani upande wa kuweka wakati, kwa kuwa ilikuwa ikipanga uwadui dhidi ya Iraq, na kutaka kuutekeleza baada ya kumalizana na Afghanistan. Ikawa kisingizio dhidi ya Iraq ni silaha za kuangamiza, na wenye kutuhumiwa ni Iraq na Iran na hizi nchi mbili ni za Waislamu. Ili isidhihirike kwamba Marekani wako

dhidi ya silaha hatari zenye kuangamiza zinapokuwa tu mikononi mwa Waislamu, lakini zikiwa kwa wengine basi haifanyi chochote, basi Bush akapata fursa muhimu ya kuitingisha maudhui ya silaha za Korea Kaskazini, na kuziweka na Iran na Iraq katika mhimili wa uovu, kama ilivyokuja katika taarifa yake mwezi wa Januari 2002 M, akafanya hivyo ili kuepusha tuhuma dhidi yake kwamba anaifanyia uwadui Iraq kwa sababu ni biladi ya kiisilamu inayomiliki silaha zenye kuangamiza kwa madai yake, bali Marekani pia (eti) huweka nchi nyengine za kiujamaa katika mhimili wa uovu pamoja na Iran na Iraq. Wakati mkusudiwa hasa ni Iraq kwa uwadui, kama ilivyokuja katika ushahidi wa Colim Powell kwa Kongresi baada ya wiki mbili tangu Bush kuzungumza kuhusu mhimili wa uovu, akasema kuhusu Iran na Korea Kaskazini: *"Hakuna mpango wa kuanzisha vita dhidi ya nchi hizi…wala hatuna mpango wa kuipiga Korea Kaskazini au kuingia katika mvutano na Iran".* Kwa hiyo haitarajiwi Marekani kukusudia kuzidisha misimamo na kufikia matendo ya kisilaha katika kutatua maudhui ya silaha hatari zenye kuangamiza huko Korea Kaskazini.

Ama kuhusu kuendelea kukuwa kwa Uislamu: hili ndio wasiwasi ya nchi kubwa zote haswa Marekani, na Magharibi kwa sifa jumla. Wasiwasi wao huu ndio huwaacha wakipeleleza hatari iliyo ndani ya Uislamu na muamko wa kiislamu, hasa tukijua kwamba zaidi ya Waislamu milioni mia mbili na hamsini wanaishi katika eneo lile, Indonesia ikiwa ndio biladi kubwa zaidi ya kiislamu, nayo ndio nchi ya nne kwa ukubwa ulimwenguni kwa upande wa wakaazi, yaani yaja moja kwa moja baada ya China, India na Marekani.

Kwa hivyo, Indonesia na Malaysia zaweza kuleta nguvu ya kutosha katika eneo, isiyopungua nguvu kubwa zenye kuathiri katika eneo lile, hapo ni pale Indonesia na Malaysia watakapofanya Uislamu kuwa ni mfumo na nidhamu ya maisha, kama ambavyo Indonesia na Malaysia zina uwezo wa kuwasiliana na ulimwengu wa kiislamu, pamoja na kuwepo kwa haya maendeleo ya kielimu katika teknolojia ya usafiri na mawasiliano.

Haya yanatilia nguvu sababu zinazofanya Mashariki ya Mbali kuwa ni kadhia ya kimataifa.

****

## [4] KADHIA YA ASIA YA KATI:

Kadhia ya Asia ya kati mambo yake yatafautina na Mashariki ya Mbali na Mashariki ya Kati, hilo ni kwa sababu hata kama yazingatiwa kuwa kijografia imeshikana na Mashariki ya Kati na wala haiwezekani kuitenganisha na Mashariki ya Mbali, lakini yatafautiana kwa aina ya ukoloni na ushawishi humo, hivyo basi hata aina ya mivutano na malengo yake pia yatafautiana. Kama ambavyo pia eneo la Asia ya Kati hadi kuporomoka kwa muungano wa kisovieti lilikuwa sehemu yake, na mvutano wa Asia ya Kati na Caucasus haukuanza ila baada ya kuanguka muungano wa kisovieti. Ndio maana pande za mivutano humo ni tofauti na za Mashariki ya Kati na ya mbali.

Ama kuhusu malengo ya mivutano: ni kuwa malengo ya Marekani katika mvutano ni kumtoa Mrusi katika maeneo ya ushawishi wake, kuipunguza upana wake kwa kuiondoa kutoka maeneo yake muhimu na hilo ni kwa kuitoa katika nchi za Caucasus na Asia ya Kati.

Kwa hivyo, hii kadhia ilizuka baada ya mwaka wa 1991 M wakati mkataba wa muungano wa kisovieti kuporomoka na kubuniwa jamhuri kumi na tano mpya juu ya vifusi vyake, kati yake kuna jamhuri tano zilizoko ndani ya Asia ya Kati na wengi wa wakaazi wake ni Waislamu, na jamhuri hizi ni: Uzibekstani nayo ndio kubwa yake iliyo muhimu zaidi, Kazakhastani, Turkimenstani na Kargizia, hizi jamhuri nne zazungumza lugha zinazpkaribiana na Uturuki. Na jamhuri ya tano ni Tajikistani, nayo yazungumza lugha ya kifursi.

Hizi jamhuri tano zina muungano wa kijografia na watu, na zote pamoja na sehemu ya magharibi (ya kiislamu) kutoka China iliyoshikana nayo huitwa: Turkistani (Turkistani Mashariki sehemu ya China na Turkistani Magharibi sehemu ya Asia ya Kati). Jamhuri hizi ni tano ziko Mashariki na Kaskazini mwa bahari ya *Caspian* na

zashikana na China inayokalia sehemu ya Turkistani Mashariki, na kwa upande wa Kaskazini zapakana na Urusi, na kwa upande wa Magharibi zapakana na bahari *Caspain* na Urusi, na kwa upande wa Kusini zapakana na Afghanistani na Irani.

Kabla ya kuingia katika ufafanuzi wa mvutano, ni wajibu kuangazia umuhimu wa Asia ya Kati na *Caucasus* kimikakati. Ama kwa upande wa kimikakati: eneo hiili huzingatiwa kuwa ni utanuzi wa Urusi ndani ya Asia hadi Mashariki ya Kati, wala hakuna mipaka yoyote ya kimaumbile inayotenganisha na Urusi kama vile bahari, na hivyo hivyo pia kwa China, kwa hivyo eneo hili huchukuliwa kuwa ni mlango wa nyuma wa China. Na kwa kuangalia kuwa wengi wa wakaazi wake ni Waislamu, basi China yaogopa wasije kuwaathiri Waislamu ndani ya China katika jimbo la Turkistani Mashariki. Kutokana na umuhimu huu wa kimikakati ndio Marekani ikaweka mipango yake ya kuingilia hili eneo tangu muungano wa kisovieti uliporomoka, kwa lengo la kuidhoofisha Urusi kwa upende mmoja, na upande mwengine kuizingira China na kuizuia isiwe na ushawishi kwa majirani zake.

Hakika Marekani ilifaulu katika kufikia baadhi ya malengo yake, ikaweka kambi za kijeshi huko Uzbekistan baada ya kiongozi wake Karimov kunyenyekea kwake kinyonge. Na kwa kisingizio cha kupambana na ugaidi ikaweza kushirikiana na Tajikistan kijeshi, na kusaidina na Kirgiztan kiuchumi na kithakafa, na hujaribu kuendeleza hilo hadi Kazakastani, na bado yajaribu kupenya ndani ya nchi zilizobakia za eneo lile na kuzichukua kutoka kwa Urusi. Na huko *Caucasus* Marekani iliweza kumuangusha Shevardnadze na kuweka serikali inayomfuata huko Tiblisi, hilo likawa pigo kubwa la kuitishia Urusi kwa ndani. Hilo ni kwa sababu kuondoka kinachotenganisha baina ya kambi za muungano wa NATO huko Uturuki na mipaka ya Urusi kwa kuwepo serikali inayoifuata huko Georgia.

Ama kwa upande wa ukoloni: hakika Asia ya Kati na haswa eneo la bahari ya *Caspain* ina utajiri wa mafuta, pia hili eneo lina utajiri mkubwa wa madini yenye thamani kama vile dhahabu. Na hili eneo kama ilivyo Mashariki ya Kati huzingatiwa kuwa ni katika maeneo tajiri zaidi ulimwenguni kwa kuwa na mali asili na utajiri, ndio ikawa mabepari wa kimarekani wakatokwa na nyute na kuwasukuma kutumia juhudi zote kuingiza mashirika makubwa katika hili eneo kwa kisingizio cha uwekezaji. Kama ilivyo hali ya Mashari ya Kati, upande wa kikoloni huzingatiwa kuwa ndio sababu kubwa ya balaa katika eneo hili, na ndio sababu msingi ya mvutano humo.

Ama ukoloni ndani ya Asia ya Kati na *Caucasus* ulianza tangu karne ya kumi na nane katika zama mbaya zaidi za ubepari wa Ulaya, wakati Urusi ilipojikatia yale mapande makubwa ndani ya Asia ya Kati na *Caucasus* kutoka kwa serikali ya kiuthmani na serikali ya Safavid na kuziunganisha kinguvu na Urusi ya kikaisar. Na baada ya mapenduzi ya Bolshevik, Urusi iliendelea kushikana na Asia ya Kati na Caucasus kwa mkono wa chuma, wala haikuachia nchi zengine fursa yoyote ya kuingilia. Lakini muungano wa kisovieti ulipoporomoka na Urusi kupatwa na udhaifu, hapo Marekani ikapata hamasa ya kuingia katika eneo hili, bali ikawa yafanya majaribio ya kufatana ili kuondoa ushawishi wa Urusi. Hilo ni kwa sababu Marekani ilijiona kwamba ndie mrithi pekee wa ulimwengu baada ya kuanguka kwa muungano wa kisovieti na kambi ya kimashariki kuondoka, kama ilivyojichukulia kuwa mrithi wa ukoloni wa Magharibi baada ya vita vya pili vya dunia, ulipokuwa muungano wa kisovieti bado upo, hivyo na wakati ulipoanguka muungano wa kisovieti ikajichukulia kuwa ni mrithi. Hakika Marekani imetawaliwa na kiburi na kughurika ndio maana yajiona kwamba ndio yenye haki zaidi na huu ulimwengu. Ndio sababu yaenda mbio nchi zote ulimwenguni zinyenyekee mamlaka yake, na hiyo ni kwa kuzitoa nchi kubwa kwenye koloni zake na sehemu walizo na ushawishi nazo, bila kumsaza Urusi.

Urusi hakika ilijaribu kuwa ndie mrithi wa muungano wa kisovieti huko Asia ya Kati na *Caucasus*, ndio maana ikakimbilia haraka kurudisha muundo wa jamhuri za muungano wa kisovieti baada ya kuanguka kwake kwa kubuni Jumuia ya madola ya nchi huru (Comon wealth) au "Nchi za fungamano huru" ikaziunganisha nayo nchi zilizokuwa katika muungano wa kisovieti, pia ikabakisha muundo wa muungano wa Urusi, ili sehemu pana ya *Caucasus* iendelee kubaki chini ya mamlaka yake kama Chechniya, Anghoshia, Dagestan, na nyenginezo.

Pamoja na kuwa majaribio ya Marekani yalifaulu huko Uzibekstani na Georgia, na ikafaulu na kuikalia kimabavu Afghanistani ambayo na ujirani wa moja kwa moja na Asia ya Kati, na kutangaza mikakati ya washirika wa mikakati huko Asia, ikatangaza kuwa Pakistani ni mshirika wa kimikakati huku ikijiandaa kutilia nguvu msimamo wake huko Asia ya Kati baada ya kuikoloni Iraq, na pamoja na kuwa mashirika ya Marekani yamekuwa ndio yenye mkono mrefu katika kuchimba mafuta na madini huko Asia ya Kati na *Cascasus*, (pamoja na yote hayo) lakini mvutano wa kisiasa juu ya ushawishi yazingatiwa kuwa bado ni mwanzo, na kwamba mvutano kumaliza kwa maslahi ma Marekani bado bado hilo lahitajia wakati zaidi. Kwa sababu hili eneo hata kama ni muhimu kwa Marekani, lakini ndio mapafu inayopumulia Urusi, na ndio mlango wake wa kuingilia maeneo mengine ulimwenguni, kwa hiyo si rahisi Urusi kujiondoa. Hivyo basi haitarajiwi kuwa Urusi kutoka kwenye eneo lote, angalau kwa mustakbali wa karibuni.

Na ili kufahamu mikakati ya kimarekani huko Asia ya Kati yalazimu kutizama taarifa za wasimamizi wa kimarekani na vibaraka wake ndani ya eneo hili na majirani zake:

Mwanzoni mwa huu mwaka 2004, Pervez Musharraf alipendekeza fikra ya kuwa nchi yake iwe ni mapitio ya biashara na mabomba ya kawi baina ya majimbo matatu: Asia ya Kati, Asia Kusini (India), na Asia Magharibi (Mashariki ya Kati) ikifaidika na

nchi yake kuwa kati ya hayo majimbo … Islamabad ikaweka ya msururu mkubwa wa fuo katika bahari ya Arabu, iliyoshikana kwa mtandao wa kisasa wa barabara za haraka kwa mtindo wa Marekani, inayoenda hadi mipaka ya Afghanistani.

Na Powell alieleza mukhtasar wa miradi huu katika taarifa yake mbele ya kamati inayohusika na matumizi ya kijeshi inayofata baraza la wazee la Marekani 27 Machi 2004 M aliposema: *"Hakika eneo la Caucasus, Asia ya Kati, Asia Magharibi na Kusini mwake zitakuwa na fursa kubwa litakapounganishwa kwa mtandao wa biashara na Mawasiliano. Lakini hili lawekana tu ikiwa tutaweza kuweka usalama na amani"*. Akaongezea: "*Hakika Pakistani yafikiria hili jambo, na imerudi kutengeneza upya muundo wake na fuo/bandari zake (...) na tutaendelea kujenga mtandao wa barabara ndani ya Afghanistani kwa msaada wa washirika wetu wasaudi na wajapani".*

Na harakati za kidiplomasia za Marekani zaonyesha kulikinaisha eneo kuunda miungano (ya kijeshi, kiuchumi, na kisiasa) inayoanza kutoka mipaka ya Pakistan na Afghanistan, inayopitia Tehran na Kabul, ikiandaa mazingira ya kurudisha ramani ya washirika wa kimikakati katika nafasi yao. Na chanzo (source) cha kisiasa huko Islamabad chaonyesha kutarajiwa uwezekano wa taasisi mbili za kijeshi za Woshington na Islamabad kuunda ushirikiano mpya utakaokua zaidi ya vita dhidi ya ugaidi. Na kuna fununu yazunguka kwamba Marekani yatazamia kuunda muungano wa Nato ya Asia itakayoongozwa na Marekani inayofanana na NATO ya Ulaya, itakayokusanya washirika wa Woshington wa kale katika eneo pamoja na washirika wapya wa Woshington huko Uzibekstan, Turkmestan, Kazakhastan, na Azerbaijan, unaolenga kuweka nidhamu ya kimajimbo itakayohakikisha usalama wa kijeshi kwa mtandao wa mabomba ya ya kawi, na hivyo kuzuia kijitokeza kwa udhibiti wowote wa Uchina au wa Urusi.

Kama ambavyo kulipatikana migongano ya misimamo baina ya Woshington na Moscow kuhusu matatizo yanayohusiana na jamhuri zilikuwa za kisovieti nyuma, hayo yalidhihiri wakati wa ziara ya waziri wa mambo ya nje wa Marekani Colin Powell huko Moscow mnamo 26/01/2004, ambapo balozi wa Marekani huko Moscow alitamka wazi kabla kidogo ya ziara kwamba Powell ana nia ya kujadiliana na upande wa Urusi kuhusu maswala yanayohusiana na jamhuri zilizokuwa za kisovieti, akiashiria kuwa moja wapo ya malengo muhimu ya ziara yake ni kutafiti juu ya "nukta za kukutana" baina ya upande wa Urusi na Marekani kuhusu anga ya Usovieti ya zamani. Na balozi wa Marekani alikubali kuwepo "matatizo maalumu" yanayokwaza usawazishaji wa mahusiano baina ya pande mbili katika hili eneo. Wakati Moscow ikikanusha kuwepo kile kilichosifiwa kuwa ni mkataba baina ya pande mbili kuhusu kugawana mamlaka katika eneo hili, vyanzo vya Marekani viliashiria kuwepo "matatizo" yanayokumba mahusiano ya nchi mbili kuhusu kuamiliana na hi failii. Ikadhihirika kwamba kuchacha kwa mjadala katika hili jambo kulikuja wakati mmoja na vyombo vya habari vya kimagharibi kuvujisha taarifa kuhusu kilichotajwa kama mipangilio ya "mkataba" wa Urusi-Marekani inayolenga kugawana mamlaka katika maeneo yaliyokuwa ya kisovieti nyuma, na wadadisi wa Urusi wakazingatia kuwa maneno ya balozi wa Marekani huko Moscow yaliashiria makubaliano baina ya pande mbili.

Kinachojulikana ni kwamba Moscow ilikuwa imedhihirisha kubabaika kutokana kuzidi kwa ushawishi wa Marekani ndani ya nchi kadhaa zenye fungamano huru, haswa kuhusu kuwepo kwa kambi za kijeshi za Marekani katika jamhuri za Asia ya Kati na Georgia, kuongezea na yale yaliyotajwa kuwa Marekani inaingilia moja kwa moja katika kupangilia mambo ya kindani za nchi kama Georgia.

Chini ya kivuli cha ziara ya Powell, wanasiasa wa kirusi walikuwa wametaka kujadili hili faili pamoja na waziri wa Marekani, na mwenyekiti wa kamati inayohusu mambo ya kigeni

katika bunge la Urusi Konstantin Kosachev akataka faili la kuwepo kambi za kijeshi za Marekani kwenye eneo liwekwe katika orodha ya kazi za ziara.

Yaliyotangulia yanaonyesha kwamba Marekani bado iko mwanzo wa njia huko Asia ya Kati na Caucasus, na kwamba mipango ya kimarekani bado haijavuka hatua ya kwanza. Hilo ni kwa kuwa mvutano bado ni mbichi katika hili eneo kwa sababu hadi zama za hivi karibuni ilikuwa ikichukuliwa kuwa hili ni makhsusi kwa muungano wa kisovieti tu. Lakini kwa kuwa mvutano katika eneo hili ndani yake muna tishio kwa maslahi muhimu ya Urusi, na kutishia majimbo ya China, na pia kwa sababu kuna maslahi ya kimikakati ya Marekani ili kufikia mipango yake ya kubakia kuwa nguvu kubwa ya kipekee ulimwenguni, na hilo lahitaji kuiondoa Urusi kwenye maeneo yake ya ushawishi na kuidhoofisha China, hayo yote hufanya kadhii hii kuwa miongoni mwa kadhia muhimu za kimataifa ambayo mvutano wake huvuka mipaka ya kikanda.

Kisha kuna sababu nyengine inayofanya eneo hili kuwa ni kituo muhimu kwa nchi zenye athari kikanda na kimataifa, na kufanya kadhia yake kuwa ya kimataifa, sababu yenyewe ni kwamba hili eneo limeruka kwa Uislamu wake baada ya kuzuiwa kinguvu katika zama za Ujamaa inaokaribia miaka sabini. Watu wakakimbilia kwenye Uislamu wao kwa kasi ya kuzindua, sio katika ibada peke yake bali wamekuwa wakiomba kuhukumiwa na Uislamu na nidhamu ya Khilafah kwa kiwango cha kushangaza, hadi **Hizb ut tahrir** kwa ulinganizi wake wa **Khilafah** ikawavutia maelfu ya watu wake kwa waume ndani ya miaka michahe tu. Na imani yao ikawa ni ya ajabu, wakipambana na mambo magumu wala hawaogopi kwa ajili ya Allah lawama za wenye kulaumu.

Lakini watawala wao wanaojinasibisha na enzi zilizotangulia hawakufurahishwa na kurudi huku kwenye mizizi kwa kasi ya nguvu, wakawa wanawashika na kuwatesa wananchi wao, wakasaidiana na Urusi, Marekani, Uingereza na hata Mayahudi

kuzuia Uislamu wa kisiasa kurudi katika utawala, na vitengo vya kijasusi katika maeneo hayo vikisaidiana na vitengo vya kijasusi vya Urusi, Marekani na Uingereza vikashirikiana ili kukomesha huu ukuwaji wa Uislamu kwa nguvu katika nchi hizi. Wakatumia mbinu za kutisha, kushika, na kutesa, pia wakatumia mbinu za kutia shaka dhidi ya fikra ya kiislamu na kuifanya kuwa regerege, na mbinu za kupamba fikra ya kielmani. Lakini Uislamu katika nafsi zao ulikuwa umemakinika nao wazidi nguvu siku baada ya siku, wala mbinu hizi za kishetani hazikuyumbisha Uislamu wao na imani yao. Hata wamagharibi walijua uhakika wa Uislamu kumakinika katika nyoyo za wananchi hawa na kuwabadilisha kuwa kinga cha moto uliowashwa. Asema Robert D. Kaplan amabye ni mtaalamu wa Marekani kuhusu mambo ya ulimwengu wa tatu: *"Katikati mwa Asia… katika sehemu hii ya ulimwengu, ndipo kutakuwa na Uislamu, kwa sababu ya kuungwa mkono kijumla na wenye kutenzwa nguvu na waliodhulumiwa na kuwavutia zaidi, kwani dini hii inayoendelea kuenea katika ngazi ya kiulimwengu ndio dini pekee iliyojiandaa kwa mapambano na mvutano".*

Eneo hili limekuwa ngome muhimu miongoni mwa ngome za Uislamu, nayo ndio upeo wa uta wa kiislamu ulioenea kutoka Indonesia, na Malaysia huko Kusini Mashariki mwa Asia, ulioungana na eneo la Mashariki ya Kati. Kama ambavyo uwezekano wa hili eneo kuungana na Pakistani na Iran kijografia, hili latuma onyo la hatari kwa Urusi na Marekani kwamba serikali kubwa ya kiislamu na ya kinuklia yawezekana kusimama katika eneo hili pana zaidi. Ndio maana moja ya sababu za Marekani kuikalia kimabavu Afghanistani ni kufuatilia kwa ukaribu eneo hili, haswa kwa kuwa watawala humo sio katika jinsi ya Ummah na wanaelekea kuondoka.

Hatari ya msimamo unaotokana na kukuwa kwa harakati za kiislamu ndani ya hizi nchi imekuwa ni sababu ya Urusi na China kuwekwa makongamano na semina kuhusu nchi hizi, ili kuzuia hatari inayotoka eneo hili, ikawa miongoni mwa kongamano muhimu zaidi ni la Shanghai ambalo iliweka moja ya vipaumbele

vyake ni kupambana na hatari iliyoitwa Uislamu wa siasa kali na harakati za kiislamu.

Hivi ndivyo utajiri mkubwa wa eneo hili, umuhimu wake wa kimikakati kwa na Urusi na China, na tamaa ya Marekani, kuongezea na muamko wa kiislamu unaokuwa humo, mambo yote haya kwa pamoja yamechangia kuifanya Asia ya Kati kuwa ni kadhia muhimu ya kimataifa.

****

## [5] KADHIA YA BARA HINDI

Hakika kadhia ya bara Hindi ni kadhia ya kale, lakini zamani haikuwa wazi kama ilivyo leo, wala haikuwa ni kadhia kubwa katika kadhia nyeti za kiulimwengu. Na mambo mapya katika kadhia hii na kiubadilisha kuwa kadhia kubwa ni mambo matatu:

1. Kutanuka kwa Uislamu ulioliipuliwa na kadhia ya Kashmir.
2. Ukubwa wa nguvu ya China katika eneo hili.
3. India na Pakistani kujiunga katika nchi zenye nuklia.

Ama kuhusu kutanuka kwa Uislamu: imekuwa sio jambo rahisi tena kuudhibiti. Ndipo ikawa moja katika sababu za Marekani kuivamia Afghanistan ni kutekeleza mashambulizi mapya ya kimsalaba kwa kupiga harakati za kiislamu zinazowaunga mkono Waislamu wa Kashmir, na haswa kwamba nguvu ya Waislamu ilidhihiri wazi mwaka wa 1999, ambapo wanamgambo wa kiislamu kwa msaada wa Pakistani waliweza kupiga milima ya Argyle iliyoko mipakani mwa Pakistani na India kutoka milima ya Kashmir, wakakaribia kulishinda jeshi la India na kuikomboa Kashmir lau si khiana ya Nawaz Sharif aliyekuwa waziri mkuu wa Pakistani, na komanda wake wakati ule Pervez Musharraf ambao waliondoa vikosi vya mashambulizi kwa kufuata amri ya Marekani.

Basi tukio hili kihakika liligonga kengele ya hatari kwa wamarekani, jambo lililowafanya wakipiga hesabu alfu ukuwaji wa nguvu za Waislamu katika eneo lile. Ndipo wakamkazia kibaraka wao raisi wa Pakistani Pervez Musharraf ili apige na kutawanya kambi za kiislamu ndani ya Pakistani, kwa kisingizio kwamba

wapiganaji dhidi ya India huko Kashamir wanatoka humo, na kwa kisingizio cha kuwa ni magaidi.

Kisha Marekani kwa mara ya pili ilimkazia Pervez Musharraf kwa kumlazimisha kutupa msimamo wa kisiasa na kutosaidia kadhia ya kiislamu ya Kashmir, naye akaitikia maombi haya pia ya kimarekani na kutangaza kujiondoa katika haki ya watu wa Kashmir kuamua kuhusu hatima yao, na kivitendo yakaanza mazungumzo huko Islamabad baina ya India na Pakistani ili kutokomeza kadhia ya Kashmir kwa msingi wa makubaliano baina ya pande mbili. Majadiliano yakaanza kwa utawala Pakistani kukubali kuwepo haki ya wahindi huko Kashmir wakijadiliana ili ipewe uhalali badala ya kuwafukuza wakoloni wa wakihindi kutoka Kashmir.

Lengo la Marekani kumbana kibaraka wake Pervez Musharraf kuhusu suala la Kashmir haswa, sio tu kupiga nguvu za kiislamu zinazokuwa huko Pakistani, bali pia kusawazisha eneo hili, ili India isishughulike na kuzozana na Pakistani, ili hatimaye China iwe ndio nguvu ya kipekee katika eneo hili, bali Marekani ilitaka kutuliza mambo baina ya India na Pakistani ili India ipambane na China ikiwa na amani katika mipaka yake ya magharibi na Pakistani. Ndio maana India na Pakistani zikaunganishwa katika muungano wa (SAARC) ya nchi za kusini mwa Asia, ili ipatikane nguvu kubwa yenye uwezo wa kusimama mbele ya China kwa ujasiri wote. Ama lau kama mvutano wa India na Pakistani ungeendelea, basi hakika India isingeweza kupambana na China au kulingana nayo, haswa kwa kuwa ina nguvu ya kiuchumi inayokuwa, ina nguvu ya demografia ya kwanza ulimwenguni, na ina kiti cha kudumu katika baraza la usalama, isitoshe ni nchi ya kale ya kinuklia, yaani kwa vipimo vyote huzingatiwa kuwa ni nguvu inayopanda, kama imbavyo haikuingia katika makosa kama ilivyoingia Urusi, kwani ilihifadhi mshikamano wake wa kindani, asema kiongozi mwenye nguvu aliyefanya upya China baada ya Mao Zedong: *“Hakika makosa makubwa aliyoyafanya Gorbachev ni kwamba aliruhusu uhuru wa kisiasa kabla ya kutengeneza upya uchumi”*.

Hivyo basi Marekani imekuwa ikiipigia hisabu kuinuka kwa China, na yataka kuishughulisha katika eneo kwa kuiundia nguvu itakayosimama mbele yake, ndio maana ikachukulia umuhimu kumaliza mvutano baina ya India na Pakistani ili zipate nafasi ya kuishughulikia China. Hii ndio inayofasiri sababu ya Marekani kunyamazia na kuridhia India na Pakistani zote kumiliki silaha za kinuklia, bali na kuiwezesha India kwa sura maalumu kumiliki silaha zilizo endelea na kuirahisisishia kufikia yaliyopungukia katika teknolojia ya silaha. Dalili ya hayo ni kwamba Marekani iliikataza (Israel) kuuza Ndege za rada za falcon za kisasa kwa Chini wakati ambapo iliiruhusu India kuuza Ndege hizi, bali zaidi ni kuwa Marekani yenyewe ilifanya makubaliano ya kushirikiana kimikakati na India, yaani imekuwa ikiamiliana nayo kama inavyoamiliana na (Israel) licha ya kuwa si nchi ya kimagharibi wala sio nchi ya Anglo-Saxon.

Haya ndio mambo wazi zaidi yaliyo katika hii kadhia, nayo ni: ukuwaji wa Uislamu, ukuwaji wa China, na ukuwaji wa nuklia. Ndipo Marekani ikaweka mikakati yake ndani ya hili eneo juu ya msingi wa kuwekea mkomo ukuwaji wa Uislamu na China, na kusawazisha nguvu za China kwa kulituliza eneo na kuliondolea sababu za mvutano, ili liendelee kuwa na nguvu kubwa zinazolingana na nguvu ya China.

****

## [6] KADHIA YA AFRIKA

Hakika kadhia ya Afrika ni kadhia mpya, kwani haikupatikana katika ulingo wa kilimwengu isipokuwa baada ya mwaka wa 1960. Na kadhia yake ni kadhia ya ukoloni tu si nyengine. Kwa sababu Afrika ni bara iliyoko nyuma kifikra, ina utajiri mkubwa wa malighafi, ina utajiri wa mashamba na wanyama kwa sura ya ajabu. Ndipo nchi za kikoloni mwishoni mwa karne ya kumi na tisa zilipotoka kwa kasi kukoloni, ikawa jumla ya sehemu zilizovamia ikawa ni bara hili la Afrika. Kila nchi ikaanza kukoloni humo kiasi inachoweza, wala haukutokea mkwaruzano mkubwa baina ya nchi

mbali mbali katika kukoloni kwake. Ndio maana nchi nyingi za kikoloni zilipata utulivu humo, bara lote likawa ni koloni ya Ulaya: kukawa na koloni za Uingereza, Ufaransa, Uhispania, Uholanzi, Ujerumani, Italiano, Ubelgiji, na Ureno, huku Uingereza ikiwa na fungu la Simba humo, ikifuatiwa na Ufaransa, kisha Ubelgiji, kisha Ureno.

Hizi nchi nane za kikoloni ziliendelea kudhibiti koloni zake hadi vilipomalizika vita vya pili vya dunia. Na ulipowekwa mkataba wa umoja wa mataifa, kukawekwa vifungu ndani yake vinavyohusiana na kukomesha ukoloni ndani ya Afrika, lakini hivi vifungu viliwekwa kwa namna ambayo itafanya ukoloni kuondoka polepole, ndio maana mataifa makubwa hayakufanikiwa kujadili kuhusu kumaliza ukoloni humo ila baada ya mwaka 1960, lakini kabla ya hapo baadhi ya nchi zilizokaliwa ziliwekwa chini uwangalizi, kama vile koloni za Italiano, kama utangulizi wa kumaliza ukoloni humo, na pia kukafanyika matendo ya kisiasa kama hatua za kuandaa mazingira ya kumaliza ukoloni. Na miongoni mwa matendo muhimu ya kisiasa ilikuwa ni fikra ya kutoegemea upande fulani kwa njia chanya, na kufanywa makongamano ya kutoegemea upande fulani kwa njia chanya.

Ama kuhusu fikra ya kutoegemea upande fulani kwa njia chanya: kiasili ilikuwa ni fikra ya Uingereza iliyotolewa na waziri mkuu wa Uingereza Churchil na kumpa kibaraka wake Nehro, na akamtaka atangaze kuwa ndio sera ya India na aifanyie kazi ndani ya nchi za Asia. Na siri ya Uingereza kumpa kibaraka wake hii fikra ni kwamba Uingereza iliona koloni zake huko Mashariki ya mbali na Asia zinatishiwa na Marekani na Muungano wa kisovieti, ambapo hatari ya huu muungano ni kuwachochea wenye hizi nchi kujikomboa kutokana na ukoloni, hasa baada ya kuona yaliyotokea huko Indonesia. Na hatari ya Marekani ni kuwa yaibana Uingereza ili utowe uhuru kwa koloni zake, kisha kuzivuta kwake (kwa Marekani) kupitia mikopo na wataalamu.

Ama kuhusu fikra ya kupeana uhuru, kwa hakika hii ni fikra ya kale kwa Uingereza, ambayo imekua ikiitumia kama mbinu ya kubadilisha aina ya ukoloni, kwani iliwapa uhuru baadhi ya koloni zake na kuzifanya kuwa nchi huru na kuziunda kwenye kile walichokiita “Common Wealth za Uingereza”, ndio maana haikujali sana kuhusu fikra ya kutoa uhuru, bali iliipenda na kwenda sambamba nayo. Kwa sababu ilijua jinsi ya kuitumia ili kumakinisha ukoloni wake, lakini ilikuwa ikihofia isije Marekani ikadhibiti zile nchi huru kupitia mikopo, misaada, na wataalamu, ndio maana ikabuni fikra ya kutoegemea upande wowote na ikampa Nehro ili aifuate na awe kikwazo mbele ya Marekani na Urusi (Sovieti). Naye Nehro akachamka kikweli kulingania hii fikra, na Urusi ikatambua lengo lake hivyo ikamvutia, akaipatiliza, kwa sababu nchi huru yoyote kuwa na msimamo wa kutoegemea upande wowote ina maana kuwa kuna matumaini ya kuitenganisha na Ulaya.

Ama kuhusu wanasiasa wa Marekani: wao walitofautiana kuhusu hii fikra, baadhi yao waliipenda kwa sababu itaiwezesha Marekani kuzivuta kwake hizo nchi zisizoegemea kokote kwa kukubali mikopo na zawadi, na wengine kati yao waliipiga vita kwa sababu ni fikra itakayoiwezesha ujamaa kuingia kwenye hizo nchi. Kivyovyote vile, Nehro aliendelea kulingania fikra, na akawa ataka kufanya matendo ya kimada yatakayowakilisha hiyo fikra, hivyo akawasiliana na China na kuitaka iweke kongamano na zile nchi zisizoegemea kokote, nayo ikakubali haraka, ikaunda kamati ya kutayarisha kongamano. Hii kamati ikawa yawasiliana na baadhi ya zile nchi zilizokuwa zimekoloniwa na kuzitaka kuhudhuria kongamano la kutoegemea kwa njia chanya upande wowote, na Indonesia ilikuwa ni moja ya wanakamati, na wakati huo ilikuwa bado haijavutwa na Marekani, lakini ilihofia isije hilo likawa ni kufuatana na ujamaa. Na inavyodhirika ni kwamba ilijaribu kutaka ushauri wa Marekani, nayo ikamshajiisha, kwani Izahor ndie aliyekua madarakani na alikua akiamini fikra ya kutoegemea kokote, ndio maana Indonesia ikajisukuma kwa hiyo fikra na

kupendekeza kwamba hilo kongamano lifanyike Bandong Indonesia, na kamati yote ikaafiki hilo, hivyo kongamano likafanyika mwaka wa 1955 huko Bandong, na kila mmoja kati ya Urusi, China, Uingereza, na Marekani akawa anajaribu kulipatiliza.

Lakini kongamano lilimalizika na natija iliyoiridhisha Urusi, China, na Marekani, kwani lilitoka na maamuzi ya kutolewa uhuru, hivyo Uingereza haikuridhika, kwa sababu ilikuwa yataka kujadiliwe tu kuhusu kutoegemea kokote. Kisha Marekani ikapatiliza sana hili kongamano, kwani iliwafanya Titto, Sorkano, na Abdunasir kutabanni hili kongamano na hiyo fikra kwa sura ya nguvu sana, wakashikamana na Nehro kibaraka wa Uingereza ambayo ndio asili ya ile fikra, wakafanya hii ni mbinu ya kulingania kujikomboa kutokana na ukoloni, na kuzishambulia nchi za kikoloni, na walikuwa wakielekeza zaidi juhudi zao kwa daraja ya kwanza huko Afrika.

Na ulipoingia tu mwaka wa 1960 ikawa fikra ya uhuru imeshachukua dori yake ndani ya Afrika, na Marekani ikawa ishapata vibaraka humo, basi kwanzia wakati huo mvutano ukahamia Afrika, na Marekani ikawa yajaribu sana kuzitoa nchi zengine za kikoloni ndani ya Afrika na kuchukua mahala pao, ndio maana ikawa yazibana hizi nchi ziwape uhuru wao. Lakini kabla ya hapo na haswa mwaka 1954 ilikuwa Marekani imetabanni kuwasha moto wa mapinduzi ya kiraia huko Aljeria na kujitengenezea vibaraka, na ikalazimisha Misri na nchi nyenginezo za kiarabu kuunga mkono hayo mapinduzi. Na haya mapinduzi yalikuwa na athari kubwa kwa nchi za kikoloni katika kuyaacha makoloni yao.

Ama Uingereza: hii yajua vizuri sana maana ya kupeana uhuru, ndio maana kwa mda mfupi ikapeana uhuru kwa koloni zake kadhaa, kukapatikana nchi kama: Zanzibari, Tanganyika, Naijeria, Uganda, Muungano wa Rudisya Kusini na Rudisya Kaskazini, na Nyasland, na nyenginezo. Ama Ufaransa, ilijivutavuta kwanza, lakini Degol alipoona jinsi msimamo wa ulimwengu ulivyobadilika kwa kasi, basi alifuata mwendo wa Uingereza, akazipa uhuru nchi

kadhaa: kukapatikana nchi kama vile Aljeria, Tunisia, Senegal, na Gabon na nyenginezo. Ama Ubelgeji: ilikuwa ikikoloni Congo, nayo ndio hazina ya Afrika, kwani yamiliki kiwango kikubwa cha Ureniam, ambayo ndio kitu muhimu zaidi cha kutengenezea mabomu ya kinukliya, kwa hivyo haikuwa rahisi kuipa Congo uhuru wake, haswa kwa kuwa Uingereza ndio iliyokuwa ikidhibiti mashirika yanayopatiliza migodi huko Katanga ambayo ni moja ya mikoa ya Congo. Kwa hiyo kuipa Congo uhuru wake ilikuwa ni tatizo kubwa, lakini Marekani ilizidi kuikazia sana Ubelgeji hadi ikabidi iipe Congo uhuru wake, hatimaye ikawa nchi huru. Hapo Uingereza ikapandwa na wazimu wake, kibaraka wake ambaye ni Mois Chombi akatangaza kuwa Katanga imejitenga, Marekani ikapeleka hii kadhia kwa Umoja wa mataifa, ikatuma vikosi vya kimataifa ili kuirudisha Katanga. Katibu mkuu wa wakati huo Mr. Hamirshord naye akaenda, Uingereza ikampangia njama ikamuua, hapo mvutano kati ya Marekani na Uingereza ukachacha, na ukaendelea kwa miaka kadhaa hadi Marekani ilipofanikiwa kuiteka miji na kuweka serikali kibaraka na kumfukuza Chombi huko. Ndipo kadhia ya Congo ikatulia japo kwa mda.

Wakati huo Uingereza ikawa na hofu kuhusu muungano wa Rudisya Kusini na Kaskazini na Nyasland, ikavunja huu muungano na kuipa uhuru Nyasland ikaitwa: Malawi, na ikaipa Rudisya Kaskazini uhuru wake ikaitwa: Zambia, na ikaanza kujaribu kuiweka Rudisya Kusini katika hali ambayo itamdhaminia kuendelea kuikoloni. Lakini kwa sababu ya Marekani kuendelea kuifuatilia, mwishowe ikaipa uhuru na ikajulikana kama Zimbabwe.

Na Marekani ilifaulu katika kuinyang'anya Ufaransa nchi za pembe ya Afrika, nchi za Maziwa makuu, Uganda, Rwanda, na Burundi, lakini haikufaulu kuipokonya Chad mwishoni mwa miaka ya tisaini. Na Idris Debby kibaraka wa Ufaransa akafanikisha ushindi wake kwa kuwashinda wanajeshi wa Hussein Jabri ambaye hakuwa na ufuasi wa kudumu wa upande mmoja, kwani mwanzoni alikuwa akiifuata Ufaransa kisha Marekani ikamvuta kwake, jambo

lililoifanya Ufaransa kuunga mkono wanajeshi wa kibaraka wake dhidi yake Idris Debby na kumuwezesha kushika utawala.

Kanali Idris Debby alikuwa katika wanajeshi wa Hussein Jabri na mshirika wake wa nguvu, na alikuwa na cheo cha kiongozi mkuu wa wanajeshi wa Chad, hadi mwaka wa 1989, na ndie aliyeongoza vikosi vya Hessein Jabri kwenye mapambano ya (Viyalarjo) mwaka wa 1983, na akafaulu kufukuza jeshi la Libya ndani ya Chad. Lakini tofauti za kikabila zilipelekea Debby na mshirika wake Hassan Jamos kushirikiana kujaribu kufanya mapinduzi yaliyofeli, baada ya kuuzuliwa cheo chake katika mwezi wa Aprili mwaka wa 1989, kisha baada ya hapo akatorokea Sudan na kuunda harakati ya kitaifa ya ukombozi, makabila mawili ya Raghawa na Hijara yakaungana kupinga serikali ya Rais Jabri, na hayo makabila yalikuwa mipakani mwa Chad na Sudan. Na kanali Debby alikuwa na mafungamano ya nguvu na Ufaransa, na alitokana na taasisi ya kijeshi ya Ufaransa, na akanyenyekea semina ya kivita huko Paris mwaka wa 1958. Kwa hivyo ushindi wa Debby dhidi ya Jabri ulikuwa ni pigo kubwa kwa ushawishi wa Marekani na kutilia nguvu ushawishi wa Ufaransa, kwani Ufaransa iliweza kufanya haraka kwa kukatiza njia ya ushawishi wa Marekani unaoendelea kukuwa.

Na kutokana na wahafidhina wapya kufika madarakani huko Marekani, Marekani ilianza kutumia mbinu mpya za kuvamia bara Afrika, ikawa haitosheki tu na kuchochea vita vya kikabila na kusababisha majanga, na kuunga mkono harakati za waasi, ili kuweza kuwamaliza vibaraka wa nchi za Ulaya, na kuwaeka vibaraka wake madarakani huko Afrika, mbali na mbinu hizi - kama ilivyo katika sera ya idara ya ulinzi na mambo ya kigeni ya Marekani – bali pia ikaongezea na mbinu ya kuingilia kijeshi moja kwa moja. Hivyo ikafanya haraka kutengeneza mahusiano na kufunga mikataba ya kijeshi na nchi kadhaa za Kaskazini, Magharibi, na katikati mwa Afrika, kwa kisingizio cha kupambana na Ugaidi, jambo linaloashiria kwamba Marekani kuingilia kijeshi moja kwa moja kutacheza dori msingi katika mvutano juu Afrika katika zama zijazo, mbali na mbinu nyenginezo.

Hivi ndivyo mivutano ya mataifa makubwa juu Afrika yalivyozidi tangu miaka ya sitini katika karne ya ishirini, kukapatikana ushawishi wa Marekani na Urusi (Muungano wa sovyeti) ndani ya hili bara kando na ushawishi wa nchi za kikoloni za Ulaya. Na kutokana na udhaifu wa Urusi, na kutopatikana mrithi wake wa kale wa ukoloni humo, ililazimika kutoka. Na hilo ni kwa kuondoka kwake huko Angola katika miaka ya themanini ya karne iliyopita. Pia nchi nyenginezo ndogo ndogo za kikoloni za Ulaya ziliondoka Afrika, ikawa hakuna waliobakia isipokuwa Uingereza na Ufaransa, hawa ndio waliobakisha ukoloni wao ndani ya mzunguko wa muungano wa common wealth ya Uingereza, na muungano wa Frankfone ya Ufaransa. Na Marekani nayo ikaingia kwa nguvu zake zote kwenye mashindano makali dhidi ya Uingereza na Ufaransa, ili iweze kuidhibiti Afrika. Jambo lililopekea Waingereza na Wafaransa kutetea maslahi ya Ulaya kupitia njia ya kushirikiana katika misimamo yao, na kupanga ziara za pamoja za mawaziri wao wa kigeni kwa nchi tofauti tofauti za kiafrika.

Na bado mivutano kati ya hizo nchi tatu yaendelea ndani ya Afrika, na bado yadhihirika katika vita vya kikabila ambavyo vyazidi ishirini, Na nyanja wazi zaidi za hiyo mivutano mpaka sasa ni yanayoendelea huko: Seralion, Liberia, Cote'd Ivoire, Somalia, Uganda, Congo, Rwanda, Burundi, na Sudan.

Hili bara jeusi limepatwa na balaa kutokana na hii mivutano ya kikoloni kupitia mapigano ya umwagaji damu, na idadi yake hivi karibuni imezidi mizozo 26 ambayo hushiriki ndani yake zaidi ya nchi 30. Na hii mizozo iliyobuniwa imechangia madeni ya Afrika kuzidi dolari bilioni 360, ambayo huwakilisha 65% ya uzalishaji jumla wa bara hili, na kwa sababu yake yamezikwa ardhini mabomu zaidi ya milioni 30 ndani ya nchi 18, ambayo yawakilisha zaidi ya robo ya mabomu yaliyozikwa ardhini ulimwenguni kote.

Na ni muhimu kutaja kwamba, hii mivutano baina ya nchi za kikoloni juu ya Afrika wakati mwengine hugeuka na kuwa makubaliano na mikataba baina ya nchi kubwa, kama ilivyotokea

Marekani na Uingereza kukubaliana kuganya Sudan ikawa Kusini na Kaskazini, na kama Marekani ilivyokubaliana na Ufaransa huko Cote'd Ivoire. Lakini mashindano ya kiuchumi na kisiasa kati ya hizi nchi aghalabu ndio alama wazi zaidi katika mivutano yao.

Hivi ndivyo mivutano ya kimataifa ya kikoloni yalivyohamia Afrika, kadhia yake ikawa pia ni kadhia ya kiulimwengu na bado iko hivyo, kwa sababu ingawa Uingereza, Marekani, na Ufaransa wamekubaliana kukusanya nchi za kiafrika chini ya muungano walioupatia jina la "shirika la kongamano la kiafrika" na kisha wakaliita "Umoja wa Afrika" lakini mivutano baina mataifa bado yaendelea ndani na nje ya huu Umoja na shirika, hasa baina ya Uingereza na Marekani.

Baada ya kumalizika kwa kambi mbili za Mashariki na Magharibi, na Marekani kuwa na msimamo wa kuzifukuza nchi zote za Ulaya hasa Uingereza kutoka kwenye koloni zao zote hasa ndani ya Afrika, hakika kinachoshuhudiwa ni kwamba Marekani yajaribu kupenya ndani ya Afrika kwa kisingizio cha **"Vita dhidi ya Ugaidi"** kwa kuwa na mawasiliano na majeshi ya hizo nchi, na imeweka – na bado yajaribu kuweka – kambi zake za kijeshi ndani ya Afrika Kaskazini, Magharibi, na Mashariki yake. Ili kupitia kwake iweze kuzitilia nguvu harakati za uwasi na ziwe mbinu za kuzibana serikali za hayo maeneo kwa lengo la kuzifukuza nchi zote za Ulaya hasa Uingereza kutoka katika koloni zao zilizosalia. Lakini kwa sababu ya maslahi ya Ulaya kushikana ndani ya Afrika, basi kipindi hiki kitakuwa na sifa ya ukali na umwagikaji damu, hasa kwa kuwa ndani ya Afrika hakuna kinachotiwa maanani isipokuwa maslahi ya kimada na utajiri wa maliasili.

Kwa hivyo, kadhia ya Afrika ni katika kadhia za kimataifa.

Hayo ndio maswala makubwa ambayo ndani hufanyika matendo ya kisiasa, lakini hii haina maana kwamba matendo ya kisiasa hayafanyiki isipokuwa ndani ya hayo maswala tu, bali yamaanisha kwamba mivutano baina ya mataifa hudhirika zaidi ndani ya hizo kadhia.

Katika hali ya amani mivutano baina ya nchi huwa kwa matendo ya kisiasa, na huwenda yakaandamana na matendo ya kijeshi kama ilivyokuwa katika hali ya Vietnam na kama hali ilivyo kwa sasa huko Mashariki ya Kati (Kuwait, Iraq, na Afhanistan...) na wakati mwengine hayaandamani na matendo ya kijeshi kama hali ilivyokuwa ndani ya Afrika huko Rudisya na Afrika Kusini huko nyuma, na kwa sasa huko Tunisia na Libya. Na kwa kuwa hii mivutano hutokea kwa ajili ya kadhia na mambo fulani, basi ndio maana hizi kadhia sita zikawa ndio kadhia muhimu zaidi zinazosababisha misuguano baina ya nchi, ndio sababu tukazileta kama mifano juu ya matendo ya kisiasa, lakini hata hivyo matendo ya kisiasa hufanyika katika kadhia nyenginezo pia, bali wakati mwengine hufanyika bila ya kuwepo mvutano. Na maadamu kuna nchi kubwa zinazoshindana na kufanyiana vitimbi na njama, basi hapan budi zitafanyiana matendo ya kisiasa, ima kwa ajili ya kuwekeana mitego ili nchi zengine zianguke ndani yake, au ima kwa ajili ya kuidhoofisha nchi nyengine, au kwa ajili ya kujiongezea nguvu yenyewe, au kwa ajili ya malengo mengine. Na mifano juu ya hayo ni mingi, kwa mfano: fikra ya kuvuliwa silaha ilipoingizwa kwenye muungano wa mataifa, Uingereza iliitumia kama mbinu ya kuidhoofisha Ufaransa, ikaanza kuibana Ufaransa ili itekeleze hiyo fikra, na yenyewe ikawa yajionyesha eti imeanza kupunguza silaha zake, Ufaransa ikaisadiki na kuanza kupunguza silaha zake kivitendo na kujiwekea mipaka katika kujiwekea silaha. Na hii ilikuwa ni njama ya Uingereza ili kuidhoofisha Ufaransa kwa upande wake na upande wa Ujerumani pia. Kwa sababu hiyo Ufaransa haikuweza kuthubutu mbele ya Ujerumani katika vita vya pili vya dunia, na ikaporoka vibaya sana na kwa haraka, na kutabanni kwake fikra ya kupunguza silaha ndio iliyokuwa na athari katika hayo.

Na kwa mfano: wakati vita vya pili vya dunia vilipotokea, Urusi (Muungano wa usovieti) ilichangamka ndani ya China, ikabuni chama cha kikomonisti chenye nguvu na ikakiunga mkono ili kichukuwe utawala humo, na Marekani ilikuwa ikiunga mkono utawala uliokuwa madarakani, kisha ikawa yamuunga mkono Shan

Kai Chek, mwanzoni ikamruhusu kushirikiana na wakomonisti mpaka wakawa na nguvu, kisha wakajitenga naye na kuanza kumpiga vita. Marekani ikawa yamuunga mkono Shan Kai Chek wazi na kumtia nguvu kwa mali na silaha lakini kwa kiasi kidogo. Na ikawa pia yakishajiisha chama cha kikomonisti kwa siri na kumdhibiti Shan Kai Chek, hivyo ikawa yafuata hatua za kisiri, lakini kwa hatua makini zilizopelekea ushindi wa wakomonisti na kuchukuwa utawala ndani ya China yote na kumfukuza Shan Kai Chek na kumfungia katika kisiwa cha Furmoza (Taiwan ya sasa). Shan Kai Chek akawa anayaona hayo na kushangaa, kwani alikuwa hatarajii kuwa Marekani yafanya kazi ya kuifanya China kuwa nchi ya kikomonisti. Lakini yeye alikuwa akinisabisha hili kwa ujinga wa Marekani, na kwamba wao hawajui uhalisia wa msimamo, lakini ilibainika baadae kwamba Marekani iliweka mpango wa kuifanya China kuwa nchi ya kikomonisti ili iweze kuwa kikwazo mbele ya Urusi, kwa lengo la kusambaratisha kambi ya Ukoministi na kuitawanya. Na mpango wa Marekani ulifanikiwa kivitendo ingawa ni baada ya takriban miaka ishirini. Hiki ni kitendo cha kisiasa kilichofanywa na Marekani na chazingatiwa kuwa ni miongoni mwa mitego mikubwa ya kimataifa.

Na mfano: baada ya vita vya pili vya dunia, Ulaya ilitoka ikiwa imevunjwa-vunjwa, maskini, na ikiwa yatishiwa na Urusi, hivyo ikajitupa mapajani mwa Marekani na kuiomba iikowe, nayo ikafanya haraka kuikoa, na ikaweka mradi wa Marshall, misaada ya Marekani ikawa yamiminika Ulaya, lakini ilikuwa ni misaada ya kiuchumi, silaha, na wataalamu. Na kupitia hii misaada Marekani ikaingia katika ushirika wa mashirika, na ikawashajiisha wasomi kuhamia Marekani, na ikafungamanisha uchumi wa Ulaya na uchumi wa Marekani, na baada ya miaka michache tu Ulaya ikawa yaifuata Marekani na kuwa chini yake, na viwanda vya Ulaya takriban vyote vikawa kiujumla vyamilikiwa na mashirika ya kimarekani. Kwa hivyo misaada ya Marekani kwa Ulaya ikawa ni njama ya kuifungamanisha Ulaya na Marekani, na kwa lengo la

kuchukua wasomi wake, na kwa lengo la kushirikiana nayo katika uchumi wake.

Mfano mwengine: Ujerumani ilitoka katika vita vya pili vya dunia ikiwa na majeraha mabaya, na ikiwa viwanda vyake vimeharibiwa, Marekani ikafanya haraka kuisaidia. Na Marekani ilikuwa yatambua umuhimu wa kuanzisha viwanda ndani ya nchi, kwani nchi haiwi nchi ya kiviwanda kwa maana ya kimataifa ila itakapofanya msingi wa viwanda vyake kuwa ni viwanda vya kivita na kujenga viwanda vyake vyote juu ya msingi wa viwanda vya kivita. Na Ujerumani itakaporudishiwa viwanda juu ya huo msingi basi ni kwa haraka sana itarudi tena kuwa nchi kubwa kwa mara nyengine. Ndio maana Marekani ikaitangulia Ujerumani na kutabanni kupangilia viwanda vya Ujerumani kwa kwa msingi wa kiuchumi na ukuzaji visiwe kwa msingi wa kivita. Basi viwanda vya kimarekani vikaingizwa Ujerumani na viwanda vikaundwa humo kwa mali za Marekani. Hivyo Ujerumani ikawa imepata pigo kama nchi ya kijeshi, ndani yake kukapatikana viwanda vikubwa, na uchumi wake ukawa mzuri. Basi ikawa kwa upande wa kiuchumi ina utajiri zaidi kuliko ilivyokuwa kabla ya vita vya pili vya dunia, ikawadhihirikia walimwengu jinsi Ujerumani ilivyorudisha viwanda vyake kwa haraka sana.

Lakini kiuhakika, Ujerumani kutokana na hivi viwanda ilikuwa imejinyonga, wala haitosimama tena ila ikiwa itarudi kuangalia upya viwanda vyake na kuvibomoa kwanzia msingi na kuvijenga juu ya msingi wa kivita, na wala pia haitoendelea kiuchumi ila ikiwa itavitoa viwanda vya kimarekani humo. Kwa hiyo, misaada ya Marekani kwa Ujerumani kwa hiyo namna ni kitendo cha kisiasa kilichoipa Ujerumani pigo badala ya kuisaidia, na hivyo basi chazingatiwa kuwa ni mtego wa kimataifa.

Mfano mwengine: Kasrto ambaye ni kiongozi wa Cuba alipowasiliana na kambi ya kikomonisti na kuiomba msaada Urusi (Muungano wa kisovieti) Marekani haikubabaika, licha ya kuwa msingi wa Monrow ulikuwa unaharamisha nchi zote kufikiria

kuipiga vita Marekani, na Urusi ilipoanza kumsaidia Kasrto kwa silaha Marekani ilinyamazia hilo pamoja na kuwa kulingana na ada ya kimataifa hilo lachukuliwa kuwa ni kuingilia Marekani kisilaha moja kwa moja. Lakini kunyamaza huku kwa Marekani haikuwa ni uoga, wala kutokujua, na Cuba iko hatua kadhaa tu kutoka kwake, bali ilikuwa ni njama ya kuivuta Urusi kwenye ulimwengu mpya ili iweze kutanuka sana kiasi cha Urusi kushindwa kuihami na hilo kudhoofisha msimamo wake, na Marekani kupata nafasi juu yake. Ndio maana hata baadhi ya wanasiasa wa Urusi yenyewe walikuwa wanaona kuwa kitendo kilichofanywa na Urusi huko Cuba ni ujinga, na lau kama sio ule mkataba wa mapatano kati ya hawa wababe wawili huko Vienna basi utanuzi wa Urusi ungelikuwa maangamivu kwake.

Wala haifai kusemwa kwamba Marekani ilibabaika, na kukaribia kuingia vitani kwa ajili ya hilo lau kama sio Urusi kutumia akili na kuondoa makombora ya kinuklia iliyokuwa imeweka huko Cuba, haifai kusemwa hivyo kwa sababu, kitendo cha Kenedy kuitishia Urusi kwa sababu ya hayo makombora, na Kharchev kuyaondoa, hiki kilikua kitendo cha kujifanyisha kilichofanywa kwa maafikiano ya pande zote mbili, kwa sababu miongoni mwa waliyokubaliana hao wawili ni Marekani kuondoa kambi yake ya kinuklia huko Uturuki, na Urusi nayo kuondoa yake huko Cuba. Na Marekani ilikuwa yaweza kuondoa kambi yake Uturuki bila kelele kwa sababu Uturuki isingeathirika kwa hilo, na wala kuondolewa kwake hakungeleta suitafahum kati ya Marekani na Uturuki, lakini Urusi kuondoa makombora yake huko Cuba tena kwa hiyari yake, ilikuwa na maana ya kuacha kuitetea Cuba, na hili lingechemsha nchi zote za kikomonisti, na kuichemsha Cuba hasa na kusababisha suitafahum kati ya Urusi na Cuba. Kwa hivyo ikawa hakuna budi kutumike mbinu ya kuondoa hii kambi kwa namna ambayo haitoathiri uhusiano kati Urusi na nchi zengine za kikomonisti, ndipo wakakubaliana kwamba Marekani ibuni sababu ya kuleta hamaki ya kimataifa itakayopelekea kuondolewa kwa hiyo kambi. Na Kenedy alitegea wakati munasaba na kuitumia hii mbinu kwa

maslahi yake, kwa sababu alipoona jinsi Uingereza ilivyokusanya nguvu zake kule Aden na Baihan ili kuingilia Yemen dhidi ya jeshi la Misri kwa lengo la kuitoa humo, na akaona kweli Uingereza imeanza kulisumbua jeshi la Misri kivitendo na kujaribu kulivamia kutokea upande wa Baihan, - Kenedy alipoyaona hayo – ndipo akaibua suala la makombora ya kinuklia huko Cuba, na kusababisha hamaki ya kimataifa, hadi Uingereza na Ufaransa zikahofia kuibuka kwa vita vya kidunia, hapo Uingereza ikaghairi mpango wa kuingilia Yemen, na Kharchev naye akajifanya ameghairi na kujifanya eti yuko tiyari kuondoa kambi yake huko Cuba ikiwa Marekani nayo itaondoa yake kule Uturuki. Kennedy akajifanya kuwa atafilikiria hilo, halafu kambi kambi ya kinuklia ikaondoshwa Uturuki. Huu ndio uhalisia wa yaliyotokea, ilikuwa ni vitendo vya kubuniwa ili kupatikane sababu ya Urusi kuondoa kambi yake Cuba, na hiyo ikafanywa kuwa mbinu ya kuitishia Uingereza.

Na dalili ya kwamba kimya cha Marekani kuhusu Urusi kuweka kambi yake ya kinuklia kule Cuba kuwa kilikua ni njama na mtego wa kimataifa, ni yale yaliyotokea Ugiriki baada ya vita vya pili vya dunia, kulipoibuka mapinduzi ya kikomonisti Titto alipendekeza kwa Stalin kwamba Yugoslavia iingilie dhidi ya Ugiriki na ibuni nchi ya kikomonisti humo ambayo itaunganishwa na kambi ya kikomonisti. Lakini Stalin alitambua hatari iliyo ndani ya haya mapendekezo, akamwambia Titto kwa uwazi: *“Hivi wataka tuweke kambi kwenye bahari nyeupe ya kati dhidi ya nchi yenye nguvu zaidi na tajiri zaidi duniani?! na je sisi kweli tutaweza kuilinda hiyo kambi? kikubwa tunachoweza kufanya ni kuitatiza tu Marekani, ama kuichukua Ugiriki kutoka kwa Marekani hilo hatuwezi na wala hatutolifikiria”*.

Na mfano: wakati vilipoibuka vita vya pili vya dunia, Hitla alihofia isije Uturuki ikaingia vitani ikiwa upande wa Uingereza, yaani upande wa washirika, naye alijua kwamba kipote cha Mustafa Kamal kilicho madarakani kinachoitwa Hizb Ash’ab ni kipote kinachofuata Uingereza na kukubali fadhila zake juu yao, hivyo ni rahisi sana kwa Uingereza kuwaingiza vitani wakiwa pambizoni

mwake, alikuwa akilijua hili ndipo akahofia Uturuki kuingia vitani dhidi ya Ujerumani, hivyo akataka kuifanya iwe kati na kati, kwa kuwa alijua Uturuki kuingia vitani kutamdhuru kwa pande tatu: Kwanza: kwa sababu waturuki ni mashujaa, na wana ushujaa zaidi kuliko Uingereza, kuliko wafansa, na kuliko warusi, kwa hiyo hawa kuingia vitani wakiwa upande wa washirika kutawapa nguvu yenye uzito wake katika vita. Pili: ni kwamba waturuki ni Waislamu, kwa hiyo kuingia kwao vitani kutamaanisha kuwa hisia za Waislamu – waarabu na wasiokuwa waarabu – zitakua dhidi ya Ujerumani, na hili litakuwa na athari yake katika propaganda ya kimataifa. Tatu: kwa sababu Uturuki ipo mahala muhimu sana kistratejia, hivyo ikiwa haitoegemea upande wowote basi itakuwa ngome katika upande wa vikosi vya Kaskazini-Magharibi na kuzuia wale washirika wasiingie Ulaya, na itakuwa kizuizi cha nguvu kitakachozuia Ujerumani isivamiwe kwa nyuma. Kwa sababu hizi ndipo akawa na pupa ya kuifanya Uturuki kuwa kati na kati, ndio maana akamtuma mmoja kati ya watu wake aliyekuwa mjanja sana, ambaye ni Fone Babon awe balozi wa Ujerumani ndani ya Uturuki, ili atekeleze kazi ya kuifanya Uturuki kutoegemea upande wowote, na kuizuia isiingizie vitani ikiwa upande wa washirika, kwa sababu ilikuwa haitarajiwi wala hakuna matumaini Uturuki kuingia vitani dhidi yao, kwa hivyo hamu ya Hitla ilikuwa ni kupata dhamana ya Uturuki kutoingia vitani ikiwa upande wa washirika ikawa dhidi ya Ujerumani, ndio maana akamtuma mtu wake mjanja zaidi kwa jukumu hili.

Lakini ili kuficha lengo lake hili, alifanya jukumu la Fone liwe ni kujaribu kuivuta Uturuki upande wa Ujerumani, na kujaribu kuikinaisha iingie vitani ikiwa upande wake dhidi ya washirika, ndio maana na washirika nao kwa upande wao pia wakawa na pupa ya kuifanya Uturuki kutoegemea upande wowote, mabalozi wao wakawa wanalishughulikia hili kwa bidii, na Fone Babon akawa anashughulika "kidhahiri" kuivuta Uturuki upande wa Ujerumani, hilo likazifanya nchi washirika kufanya bidii sana ili Uturuki ibaki kati kati bila kuegemea upande wowote.

Kupitia huu mchezo wa kisiasa na kutokana na ujanja wa Fone, Hitla alifanikiwa kuifanya Uturuki kuwa kati na kati ndani ya kipindi chote cha vita, licha ya kwamba ilikuwa rahisi sana kwa washirika kuishambulia Ujerumani kupitia kwa Uturuki kwa kuivuta upande wao. Lakini hawakufanya hivyo kwa kuhofia kufungua huo upande, na kwa ajili ya pupa yao kuwa Uturuki ibaki bila kuegemea kokote ili iweze kulinda hiyo sehemu kwa kuwa kwake kati na kati. Kwani kitendo kama hiki cha kisiasa huzingatiwa kuwa ni katika vitendo vyenye athari katika hali ya kivita.

Hiyo ndio mifano ya vitendo vya kisiasa ambavyo nchi tofauti-tofauti hufanyiana katika mivutano na maisha ya kimataifa, ima kuwekeana mitego ya kimataifa, au kwa ajili ya kudhoofisha nchi zengine, au kwa ajili ya uchokozi wa kisiasa, au kwa malengo mengine yasiyokuwa hayo. Na hayo matendo kama yanavyofanyika katika maisha ya kimataifa kwa ujumla, pia hufanyika ndani ya mvutano uliopo kwenye zile kadhia sita kuu. Lakini wakati hayo yanapofanyika huwa yamefungika katika nukta moja na baina ya nchi mbili au zaidi zinazovutana, lakini yakifanyika kwa ujumla basi athari yake ya kimataifa huwa kubwa zaidi. Kwa hivyo haitakiwi kwa mwanasiasa kufunga akili yake katika kadhia muhimu peke yake na matendo ya kisiasa yanayofanyika humo, bali anapaswa kutanua mtizamo wake na kuangalia kitendo chochote cha kisiasa kinachofanywa na nchi yoyote kubwa. Na miongoni mwa yanayowajibika kuangaliwa hapa ni kwamba, mwanasiasa wakati anapoyatizama matendo ya kisiasa basi ni lazima ayaepushe na utenganishaji na uwenezaji jumla, kila kitendo akifungamanishe na dhurufu zake na mazingira yake makhsusi yaliyokizunguka. Hivyo haifai kukichukua kitendo kikiwa kimetanganishwa na mazingira yake, wala haifai kueneza maudhui kiujumla, kama ambavyo pia haifai kufanyia makisio matendo mengine juu ya kitendo maalumu, pia haifai kupangilia matukio mpangilio wa kimantiki na kufikia natija ya kimantiki, bali ni wajibu ajiepushe na hayo kabisa, kwani hakuna jambo hatari zaidi juu ya ufahamu wa kisiasa kama kama

mantiki na kufanya qiyas (kukisia). Kwa sababu matukio ya maisha yanatofautiana wala hayafanani, bali kila kitendo kina mazingira na hali yake tofauti. Kwa hivyo ni wajibu kwake kuunganisha kila kitendo na maalumati ya kisiasa aliyo nayo kukihusu, na akichukuwe kikiwa ndani ya dhurufu na hali zake, hapo atakuwa na ufahamu ulio karibu zaidi na usahihi. Na mifano juu ya hayo ni mengi hayana hisabu, kwani matukio ya kila siku katika maisha ya kimataifa na matendo ya mataifa makubwa yote ni mifano tosha, kwa sharti ifahamike kuwa kila kitendo kina fungamano na msingi wake fulani wenye uhusiano na sera ya nchi, au msimamo wa kimataifa, au hali za nchi mbali-mbali, na kwa sharti kwamba kila kitendo kina dhurufu zake makhsusi na mazingira yake ambayo hayana ushirikiano na vitendo vyengine.

Kwa mfano: mwaka wa 1969 Korea ilipiga Ndege ya kijasusi ya Marekani huko Mashariki ya mbali, Marekani ikatikisika, kukawekwa mkao wa ulinzi wa nchi, kisha Rais Nikson akatoka na uwamuzi kuwa Marekani haina niya ya kulipiza kisasi kwa kuangushwa Ndege yake, na kikubwa kilichofanyika ni kwamba itakuwa Ndege na meli za kijasusi zikilindwa zisifanyiwe uwadui. Lakini mwaka wa 1968 Korea ilipoiteka Meli ya kijasusi Marekani ikatikisika, kukawa na mkao wa usalama, kisha Rais Johnson akatoa maneno makali na vitisho vikali, na Manuwari ya 7 ikaanza kuelekea upande wa Korea. Marekani ilipoona vitisho vyake na vita vya kihisia havikuathiri chochote ikarudia mbinu ya ulaini na kufanya majadiliano hadi meli yake na manahodha wakaachiliwa.

Haya ni matukio ya aina moja, nchi ndogo kama Korea kuichokoza nchi kubwa kama Marekani kwa kuipiga Ndege yake na kuwaua Marubani, na kuteka Meli na manahodha wake, basi ni kwanini ikawa na msimamo tofauti katika kila tukio? je ni kwa kuwa watawala ni tofauti? hilo lawezekana, au ni kwa kuwa vitisho havikuwa na matunda? pia hili lawezekana. Lakini inavyodhihirika ni kwamba dhurufu ya Meli ilikuwa ni ya kawaida au yafanana na ya kawaida, na China ilikuwa imeshughulishwa na mapinduzi ya kithaqafa, hivyo vitisho havitopelekea kutokea kwa uwezekano wa

hatari. Lakini dhurufu ya Ndege haikuwa ya kawaida, kwani Urusi ilikuwa ikikusanya wanajeshi wake wengi wa nchikavu na wa angani huko katikati ya Ulaya, na wakikusanya wanajeshi wake wa Baharini katika Bahari nyeupe ya kati, na China iko katika hali ya kutaka kujionyesha kwa ulimwengu baada ya kutenga kwa mda wa mapinduzi ya kithaqafa, nayo yaisumbua Urusi kwa lengo la kutaka kujionyesha. Kwa hivyo lau kama Nickson angeitishia Korea basi yatarajiwa Uchina kujibu, na hili lingepeleka msuguwano na kuzidisha wasiwasi, na huenda Uingereza nayo ingetumia hii fursa kama mbinu na kuchochea dhidi ya kambi ya Mashariki. Hivyo basi haikuwa sawa kwa Marekani kutoa vitisho wala kufanya vita vya kihisia, ndipo Nickson akaamua kunyamaza. Kwa kuwa dhurufu za haya matukio mawili zilikuwa tofauti basi ikawa hakuna budi pia maamuzi kuwa tofauti.

Na kwa mfano: Baada tu ya Nickson kuwa Rais alifanya ziara Ulaya haraka, na kudai kuwa ataka kurudia kwa washirika wake ili kuchukua rai zao kabla ya kuwasiliana na Urusi (Sovieti) kwa ajili ya tatizo la Mashariki ya kati. Kauli yake hii ingesadikiwa lau kama kusingelikuwa na dhurufu zengine zilizo karibu zaidi kuwa ndio sababu hasa. Lakini kwa uchunguzi wa kina ilibainika kwamba Uingereza ilikuwa ikifanya mawasiliano na nchi za Ulaya kwa lengo la kuwakunya kando yake katika tatizo la Mashariki ya kati, na yataka kuwakinaisha ili ziwe upande wake dhidi ya Urusi hata kama ingepelekea vita vya dunia dhidi ya kambi ya Mashariki. Dhurufu hizi zilikuwa hatari, na ndio iliyomfanya Nickson kuzuru nchi za Ulaya haraka baada tu ya kuwa Rais kabla ya kufanya kitendo chengine chochote. Kwa hiyo safari yake Ulaya ilikuwa kwa lengo la kuzitawanya nchi za huko pambizoni mwa Uingereza.

Na mfano mwengine: Mwishoni mwa mwaka wa 1968 Urusi iliivamia Slovakia kwa kushirikiana na muungano wa Warsaw, wote wakashiriki isipokuwa Romania. Majeshi ya muungano yakaingia Slovakia kwa kisingizio cha kulinda Ukoministi, Serikali, na Chama cha kikomonisti dhidi ya uwadui unaowezekana kutoka Ulaya. Yawezekana kulikuwa na kitu kati ya hayo, lakini dhurufu ambazo

hili tukio lilipatikana ndani yake ilikuwa hatari zaidi kuliko madai ya kulinda Ukoministi na chama cha kikomonisti, hasa kwa kuwa hakukuwa na kitu isipokuwa ijtihadi za viongozi wa chama cha kikomonisti katika kufasiri huo Ukoministi. Na kwa kuangalia kiundani dhurufu yabainika kwamba, Manuwari za Urusi zilizopo katika pwani ya Misri zilikuwa zatishiwa na Uingereza, kwani Uingereza imekuwa ikiwakusanya wanajeshi wake kwenye bahari nyeupe ya kati, na huenda (Israil) ikaishambulia Misri, hivyo Urusi kulazimika kuingilia kati kwa hoja ya kulinda Ukoministi, na hapo kutakuwa na Uingereza nayo kuipiga Urusi, hivyo basi ikawa hakuna budi kujiandaa na vita, na pia kutayarisha mbinu za kuongezea nguvu.

Na hizo mbinu za kuongezea nguvu kuja kutoka Urusi kupitia mlima Tariq katika hali ya vita haitokuwa sahali mbali na kuwa ni njia ndefu. Kwa hiyo ikawa hakuna budi kutengeneza mapitio katika bahari nyeupe ya kati, yatakayokuwa karibu na Misri. Ndipo Urusi ikawakusanya wanajeshi milioni mbili, Ndege (3,000) na silaha za kinuklia ndani ya Ulaya ya kati, na ikatayarisha muungano wa Warsaw kushiriki vitani, basi muungano huu ukaingia Slovakia kwa uwazi kwa ajili ya kuitishia Uingereza, kwa kukusanya kwake nguvu zake katikati ya Ulaya, ikiwa imejiandaa kupasua Yugoslavia na Albania ili kufikia bahari nyeupe ya kati endapo Urusi itapambana vitani na Uingereza. Kwa hivyo, kuingia Slovakia kwa madai ya kulinda nchi ya kikoministi makusudio yake ilikuwa ni kuitishia Uingereza na kujiandaa kwa vita, na kutayarisha muungano wa Warsaw kwa ajili ya kuingia vitani.

Hivi ndivyo matukio ya kisiasa yanavyounganishwa na msingi wake, na kuwekwa ndani ya dhurufu na mazingira yake, na kufahamika ndani ya siku yake tofauti na jana yake, pamoja na kutia maanani mabadiliko na maendeleo yaliyotokea ndani ya hiyo siku moja, bali hata ndani ya saa moja. Wala haifai mtu kubaki kwenye zama zilizopita, wala hata saa iliyopita au madakika, bali aende na wakati na ayafahamu mambo na matukio kulingana na kipindi cha

mwisho kabisa kutokana na mambo au matukio yanayotokea katikati ya hicho kipindi.

Hayo ndio masuala nyeti ya ulimwengu, na hayo ndio mataifa makubwa yanayoathiri katika sera/siasa za kiulimwengu, na hivyo ndivyo tulivyobainisha jinsi ya kufungamanisha kati ya matendo ya kisiasa na msingi wake, na kuyaweka ndani ya mazingira na dhurufu zake, na kuyafahamu kulingana na siku yake, bali ndani ya saa yake, kutokana na matukio yanavyobadilika kwa kasi.

****

## [7] SABABAU ZA MATATIZO YA ULIMWENGU

Hakuna shaka kwamba matatizo ya ulimwengu yanatokana na mataifa makubwa, tangu yalipoanza kuudhibiti kwa sifa yake ya kuwa nchi kubwa duniani. Pia ulimwengu umepata shida kwa sababu ya fikra waliyobuni ya "jamii ya kimataifa". Kadhalika ulimwengu umetaabika kwa sababu ya ukoloni tangu ulipopatikana mfumo wa kibepari, yaani tangu ulipopatikana ukoloni. Na ulimwengu utaendelea kuteseka maadamu uongo wa "jamii ya kimataifa" utakuwepo, maadamu nchi kubwa zitaendelea kuushindania ulimwengu na kuudhibiti, na maadamu ukoloni utaendelea kuwepo bila kujali utakavyobadilika muundo wake na mbinu zake kuwa mpya. Kwa hivyo, haiwezekani kuuokoa ulimwengu na kuutoa katika hili shimo uliotumbukia na kuuweka katika njia ya furaha, isipokuwa pale hayo matatizo mmatatu yatakapotibiwa, yaani kuondoshwa haya majanga matatu: uongo wa jamii ya kimataifa, udhibiti wa nchi kubwa na kutawala kwake, na ukoloni na ukiritimba.

**Ama kuhusu jamii ya kimataifa:** Msingi ambao ulisimama juu yake na kuasisiwa ulikuwa batili mwanzoni. Kwani mwanzoni kabisa iliundwa juu ya msingi wa jamii ya nchi za kikristo ndani ya Ulaya Magharibi, ili ziwe muungano utakaosimama mbele ya serikali ya kiislamu, kisha zikaunganishwa nchi za kikristo zitokazo

Ulaya Mashariki, hivyo ikawa ni "jamii ya wakristo wa nchi za Ulaya" na ikaendelea kuwa hivyo tangu karne ya kumi na sita, yaani tangu ilipokuwa serikali ya kiislamu ni nguvu inayofagia Ulaya, hadi nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa, yaani hadi mwaka wa 1856, wakati serikali ya kiislamu ilipofikia kiwango kibaya cha udhaifu mpaka kuitwa "mtu mgonjwa" na ikawa njama yaendelea kupangwa kuhusu namna ya kugawana milki zake. Basi kwa mda wote huo wa takriban karne tatu jamii ya kimataifa ilikuwa yamaanisha jamii ya kikristo, na likimaanisha uwadui dhidi ya serikali ya kiislamu.

Pamoja na kwamba ilikuwa ni kwa ajili ya nchi za kikristo tu, na ni ya nchi za Ulaya peke yake, hairuhusiwi nchi zisizokuwa za kikristo kujiunga, pamoja na hayo wakaiita eti ni jamii ya kimataifa, ili hii peke yake ndio iwe na sifa ya kimataifa na peke yake ndio iwe yadajili mambo ya kimataifa bila kuwahusisha wengine, na mambo yangekuwa sahali lau kama wangetosheka tu na mkusanyiko wa Wakristo na kuifanya ni ya Wakristo dhidi ya Waislamu, lakini wakaifanya ni ya kimataifa. Hilo ni kwa kuwa fikra ya jamii ya kimataifa iliasisiwa juu ya msingi wa nchi za kikristo, yakawa mambo ya kimataifa ni yale yanayohusiana na hii jamii, na kadhia ya kimataifa ikawa ni yale yanayohusu hii jamii, na ili kupangilia hayo na kuyadumisha milele kukawekwa kanuni za kidesturi ambazo baadae zikaitwa sheria za kimataifa. Kwani walichukua ile mikataba iliyokuwa imefungwa baina ya nchi za kikristo, na wakachukua pia mila na desturi zilizokuwa zimeenea ndani ya jamii za kikristo kwa sifa yake ya mikusanyiko, ndio wakaunda misingi kutokana na hayo halafu wakazifanya kuwa ndio misingi ya kimataifa au kile kinachoitwa sheria za kimataifa.

Kwa hivyo, kuziita nchi za Ulaya za kikristo kuwa ndio jamii ya kimataifa ni upotoshaji, kwa sababu ulimwengu sio hizo nchi peke yake. Na mikataba yao na mila na tamaduni zao kuitwa kuwa ndio sheria za kimataifa hilo pia upotoshaji na uchakachuaji, kwa sababu fikra zinazofaa kuwa kanuni za kimataifa sio mikataba na

desturi za nchi za kikristo peke yake, bali inayofaa ni mkusanyiko wa desturi jumla zinazopatikana baina ya mikusanyiko ya watu ulimwenguni, na mikataba jumla inayofungwa kati ya wanadamu kote duniani. Kwa hivyo, mafhumu ya “jamii ya kimataifa ilikuwa ni ya makosa kwanzia kuasisiwa kwake, na pia “sheria za kimataifa” kwanzia kuasisiwa kwake ni makosa. Na ilikuwa yawezekana kuepuka hayo lau kama hizi nchi zingekubali nchi zengine duniani kujiunga nazo, lakini kiuhalisia ni kwamba hii jamii haizitambua nchi zengine bali ilikuwa hakubali nchi yoyote kuungana nayo ila kama ni ya kikristo, hadi ilipofika nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa ndipo ikakubali baadhi ya nchi zisizokuwa za kikristo kujiunga na kuzingatiwa kuwa ni katika jamii ya kimataifa, lakini hawakukubali misingi isiyokuwa ile waliyoiweka kwa msingi kuwa ni ya Ulaya ya kikristo, ndio maana wakataka kwa serikali ya kiuthmani iache kuhukumu kwa sheria ya kiislamu na wakashurutisha hilo, na wala hawakukubali ijiunge nao ila baada yake kukubali hilo sharti na kunyenyekea misingi ya desturi za nchi za Ulaya za kikristo. Hii ikiwa na maana kuwa hii jamii iliziruhusu baadhi ya nchi kujiunga nayo, lakini haikuruhusu kamwe misingi na desturi nyenginezo kuwepo katika mahusiano ya kimataifa. Hali ikaendelea hivyo hadi vilipomalizika vita vya kwanza vya dunia, na kumalizwa kwa serikali ya kiislamu. Na kulikuwa na uwezekano wa kuepuka kuendelea kwa hiyo hali baada ya hivi vita kukoma, kwa sababu yule adui ambaye hii jamii iliundwa kwa ajili yake, na sheria za kimataifa zikawekwa kwa ajili ya kupambana naye tiyari ameshatoweka, lakini mambo hayakuwa hivyo, bali hizi nchi ziliendelea kushikamana na ule msingi na sheria ambazo hii jamii iliasisiwa juu yake, ndipo zikakubaliana kuunda shirika la kimataifa litakalowakilisha hii jamii, lakini hawakulifanya kwa ajili ya nchi zote, zikakubaliwa baadhi ya nchi zisizokuwa za kikristo na zisizokuwa za Ulaya, lakini zile sheria na desturi za nchi za kikristo zilibaki kama zilivyo, wala hawakujali desturi na fikra za nchi nyenginezo.

Kisha ilipokuja taasisi ya umoja wa mataifa, ilitakiwa wanachama wawe ni zile nchi tu zilizoingia vitani dhidi ya Ujerumani, yaani zile nchi za kikristo na nchi zinazozifuata, lakini Marekani ikatanua wanachama wa umoja wa mataifa na kuruhusu nchi zengine kujiunga, kwa lengo kutanua ushawishi wa Marekani ulimwenguni na kuziingiza hizo nchi chini ya kivuli chake. Lakini hata hivyo, Marekani na nchi zote za kikristo hazikuruhusu misingi yoyote kupenya katika sheria za kimataifa wala katika nidhamu ya umoja wa mataifa, bali ile misingi ya nchi za kikristo zilibaki kuwa ndio msingi wa sheria za kimataifa, na hizo zenyewe ndio sheria za kimataifa, na ndio nidhamu ya umoja wa mataifa. Hata kambi ya Mashariki ikiongozwa na Urusi licha ya kuamini kwake aqeeda ya ukoministi ambayo inagongana na nidhamu ya kiraslimali, na ambayo pia yagongana na misingi ya nchi za kikristo, lakini pamoja na hayo haikuweza kubadilisha chochote katika msingi wa nidhamu ya kimataifa, wala haikuweza kupenyeza fikra yoyote humo. Kwa hivyo misingi ya nchi za kikristo/nchi za kibepari na tamaduni zao pekee ndio bado ziliendelea kudhibiti wanadamu ulimwenguni, na kupuuza fikra na desturi za nchi zengine, na wakati huohuo "jamii ya kimataifa" kiuhalisia wake iliendelea kumaanisha nchi za kikristo au nchi za kibepari, japo nchi nyingi ziliruhusiwa kujiunga. Hivyo hakuna budi maana ya "jamii ya kimataifa" kuangaliwa upya, pia hakuna budi "sheria za kimataifa" kuangaliwa upya.

Na kilichoharibu mambo zaidi, ni kuwa hizi nchi za kikristo au za kibepari hazikuacha suala la utekelezaji wa hizo desturi zao ambazo baadae zikawa sheria za kimataifa, liwe ni kwa msukumo wa "kimaanawiya" kama ilivyo hali katika desturi za kimataifa, pia hazikuacha zitekelezwe tu kwa zile nchi zilizojifunga nazo, bali zikafanya zitekelezwe kwa nguvu ya silaha, na zikalazimisha zitekelezwe na nchi zote duniani, zilizojifunga nazo na ambazo hazikujifunga nazo pia! Basi zamani zile nchi kubwa zikajifanya kuwa wao ndio walinzi wa amani na nidhamu katika mujtama wa kimataifa, hivyo zikawa zaingilia mambo ya nchi zengine kila zinapohisi kuna tishio kwa usalama au kuharibu nidhamu. Na ikawa

hakuna jambo lolote linalowazuia wao kuingilia mambo ya nchi zengine yaani kutekeleza zile sheria za kale walizokubaliana, isipokuwa ikiwa hizo nchi zinazoingiliwa zina nguvu, au ikiwa hizo nchi kuu zimeshindwa kukabiliana nazo.

Kabla ya vita vya kwanza vya dunia, zile nchi za Ulaya za kikristo kwa pamoja au mmoja wao ndizo zilizokuwa zikijifanya kuwa polisi wa kimataifa ulimwenguni kwa ajili ya kutekeleza nidhamu ya kimataifa, hata baada ya kuundwa kwa umoja wa mataifa. Halafu ilipoundwa taasisi ya umoja wa kimataifa, nchi za kiraslimali ziliendelea kujifanya polisi wa kutekeleza sheria na nidhamu, na mifano ya hayo ni Marekani na Uingereza kuingilia Mashariki ya kati mwaka wa 1958. majeshi ya Marekani yakiwa ndani ya Lebanon huku majeshi ya Uingereza yakiwa Jordan, na kuvamia kwao Iraq mwaka wa 2003. Hiyo ni mifano ya hizi nchi za kibepari kujifanya polisi wa kimataifa kwa ajili ya kutekeleza kile wanachokiita nidhamu ya ulimwengu. Kitendo kikawa miongoni mwa vitendo viovu zaidi, vilivyosababisha mateso kwa ulimwengu kutokana na jamii ya kimataifa kwa ufahamu wake wa kiulaya, na kutokana na sheria za kimataifa. Kwa hivyo hakuna budi kutibu haya matatizo ili kuukomboa ulimwengu kutokana na hizi dhiki.

Ama kuhusu tiba ya hili tatizo ni kwamba, ikiwa hakuna budi kuwepo kwa jama’ah ya kimataifa ndani ya jamii ya kimataifa, basi ni lazima hii jamii (mujtama) isifanyiwe makisio kwa jamii ya kawaida. Kwani jamii ya kawaida huwa ni lazima iwe na chombo cha kuondosha dhulma na uhasama na kuamua mizozo baina ya watu, ndio maana ni lazima kila jamii iwe na serikali, na hapana budi iwe na mamlaka, pia ni lazima kuwe na kanuni, kama ambavyo pia hapana budi kutekelezwa kinguvu juu ya watu. Lakini mujtama wa kimataifa ni mikusanyiko ya wanaadamu ambao kuna mahusiano baina yao, wala sio mikusanyiko ya watu binafsi ambayo hujengeka mahusiano kati yao. Na kila mkusanyiko kati hiyo mikusanyiko una haki ya ubwana na haki ya matakwa moja kwa moja bila kufungwa, kwa hivyo utenzaji nguvu wowote kutoka nje juu ya mkusanyiko

wowote au nchi basi humaanisha kuwapokonya ubwana, na huo ndio utumwa, ukoloni, na udhibiti wa utenzaji nguvu, na kuwakataza kutekeleza maamuzi yao humaanisha kuwafunga minyororo na kuwalemaza. Kwa hivyo sio sahihi kuwepo kwa nguvu fulani juu ya mikusanyiko ya wanaadamu ambayo itakuwa ni kama utawala juu ya mujtama mmoja. Kwa maana nyengine: sio sahihi jamii ya kimataifa kuwa jamii moja inayosimamiwa na utawala mmoja wenye haki ya kuchunga mambo, yaani haisihi kuwepo serikali ya kiulimwengu inayotawala nchi zote duniani, wala isiruhusiwe kuwepo kwake. Bali ni lazima mikusanyiko ya wanaadamu iendelee kubaki ikiwa na ubwana wao na matakwa yao. Na ikiwa hakuna budi kuundwa jama'ah ya kimataifa kutokana na hayo makundi ya watu, basi ni lazima kusiwe na serikali ya kiulimwengu, na ni lazima hiyo jama'ah iasisiwe kwa hiyari ya wanaotaka kuiunda, sio kuundwa na nchi maalumu yenye ufahamu maalumu, au nchi moja kuwa na nguvu zaidi ya zengine. Bali jamii ya kimataifa iasisiwe na wote wanaotaka kwa hiyari yao, bila kujali aina ya fahamu zao, wala kiwango cha nguvu au ushawishi, na nchi yoyote ambayo haikushiriki katika kuasisi ipewe uhuru wa kushiriki wakati wowote ikitaka, nayo iwe na haki na wajibu sawa na waasisi, na wote wawe na haki kujitoa wakati wowote ikitaka, pia nchi yoyote isitenzwe nguvu kutekeleza maamuzi. Hapo ndio itakuwa jamii ya kimataifa kwa haki, sio familia maalumu ya kimataifa ambayo imeitwa jamii ya kimataifa kiuzushi na kiuongo, na sio serikali ya kiulimwengu ambayo imeitwa kwa jina la umoja wa kimataifa kiuzushi na uongo.

Hayo ni kuhusiana na jamii ya kimataifa, ama kuhusu kanuni: jamii ya kimataifa na nchi za dunia hazitakiwi kuwa na sheria za kimataifa, bali jamii ya kimataifa iwe na kanuni za kimpangilio zinazopangilia mambo kiidara peke yake, na kubainisha namna ya kuendesha matendo, ziundwe kwa rai ya wengi na kubadilishwa au kurekebishwa pia kwa rai ya wengi kulingana na matukio na mahitaji yake.

Ama kile kinachoitwa “kanuni za kimataifa” hazifai kuwepo wala haifai kutungwa, hilo ni kwa sababu kanuni huwa ni amri ya mtawala, na hakuna serikali ya wala mamlaka ya kiulimwengu, bali haifai kuwepo na serikali inayotawala nchi zengine, kwa sababu hilo haliwezekani, na madai ya uwepo wake kutamaanisha kupatikana kwa vita na mizozo ya umwagi damu, kwa hiyo haifai kuwepo kwa serikali ya kiulimwengu wala mamlaka ya kiulimwengu. Hivyo basi twasisitiza tena haisihi kupatikana wala kuwekwa kanuni za kimataifa, kwa sababu tatu zifuatazo:

1. Kanuni maana yake ni amri ya mtawala, na hakuna mwenye utawala jumla juu ya nchi zote duniani, wala juu ya jamii ya kimataifa. Hivyo kiasili kamwe hakuna kanuni za kimataifa.
2. Kanuni huwa ni lazima zitekelezwe, basi hapana budi kuwepo kwa mamlaka ya utekelezaji, na haisihi kuwepo kwa mamlaka yenye kutekeleza maamuzi yake kwa nguvu juu ya nchi zote duniani, kwa sababu hilo litapelekea vita na mizozo ya umwagaji damu.
3. Kanuni hupangilia mahusiano, na mahusiano ya kimataifa hupatikana baina ya makundi ya wanaadamu kwa hiyari, seikali mbili au zaidi zikapangilia mahusiano baina yao kulingana na maslahi yao na kwa ridhaa zao, tofauti na mahusiano ya nchi zengine. Hivyo kinachopangilia mahusiano kati yao huwa ni mikataba wala sio kanuni, na mafungamano yanayotokea kivitendo hayapangiliwi isipokuwa kwa mikataba. Kwa hivyo hakuna kanuni za kimataifa zinazopangilia mahusiano ya nchi zote. Kutokana na sababu zote hizo haisihi kuwepo kanuni za kimataifa.

Pamoja na kwamba watu wengi – hata wamagharibi – walipinga kuwepo kwa kanuni jumla za kimataifa, na pia wakakemea suala la nchi zengine kulazimishwa kwa nguvu kuzitekeleza hizo kanuni. Kwani kulijitokeza ikhtilafu baina ya wanasheria wa Ulaya tangu kudhihiri kwa hii fikra ya kanuni za kimataifa kuhusu uhalisia wa misingi yake, na wengi wao wakatilia shaka nguvu yake ya kulazimisha. Wasomi wa huko Ujerumani kama vile Kant na

Haigel, na Horboz na Austin pamoja na wafuasi wao huko Uingereza wote walipinga kuwepo kwa kanuni za kimataifa wakiungwa mkono na wanasheria wengi wa Ulaya. Na hata hao wanasheria wa Ulaya waliozikubali hawasemi ziwe kama kanuni ambazo ni wajibu kutekelezwa, bali wamezizingatia kama msingi wa kiakhlaqi tu, ambayo haina jukumu lolote la kikanuni.

Hata wale wanaojaribu kufanya hila ili kufasiri maana ya kanuni za kimataifa, hizo tafsiri zao zajulisha kwamba hakuna kanuni za kimataifa, bali kilichopo na kinachoweza kuthibitishwa ni desturi ya kimataifa, wala sio kanuni za kimatafia, ndio maana wakawa ni mufakirina wachache – hata huko Ulaya kwenyewe – wanaoamini kuwepo kwa kanuni za kimataifa.

Kunazo desturi (*urfu*) ambazo makundi ya wanaadamu wamekubaliana nazo, na miongoni mwazo kuna desturi jumla ambazo zilipatikana kwa wanaadamu tangu zama za kale hadi leo, kama vile kutokuuliwa kwa mabalozi kati ya nchi au kinachojulikana kama kinga ya mabalozi, na kati yazo zipo ambazo ni desturi (*urfu*) makhsusi baina ya makundi fulani, kama vile ilivyokuwa yajulikana kwa waarabu kwamba hazuiliwi yeyote kuzuru Al-baitul-Haraam. Hizo desturi bila shaka zipo, lakini nazo sio kanuni, bali ni “istilahi” ambazo watu wanakubaliana juu yake kutokana na matukio maalumu kujirudiarudia kwa watu wote au makundi maalumu. Kwa hiyo, desturi za kimataifa (urfu) zipo, lakini kanuni jumla ya kimataifa hakuna.

Limebakia suala la kuwatekelezea watu kanuni za kimataifa kwa nguvu: utekelezaji huu wa kinguvu au kuwatenza nguvu watu juu ya utekelezaji hili halifai, kwa sababu huo utekelezaji kama utafanywa na serikali ya kiulimwengu: basi hilo ni muhali, kwa kuwa hakuna serikali ya kiulimwengu. Na kama utafanywa na mkusanyiko wa nchi kubwa mbili au zaidi: basi huo utakuwa ni uwadui wala sio utekelezaji wa kanuni, kwa sababu lau kama moja kati ya nchi mbili au zaidi zinazotekeleza hizo kanuni nazo zikikhalifu kanuni, basi nchi zengine haziwezi kutekeleza kanuni

juu yao, kwa kuwa hilo litamaanisha kuzuka kwa vita. Na lau hizo nchi zinazotekeleza zitaenda kinyume na kanuni basi ni nani atawatekelezea? bila shaka hakuna, hivyo basi nchi zenye nguvu kutekeleza kanuni juu ya nchi ndogo au dhaifu itakuwa ni uwadui wala sio utekelezaji wa kanuni za kimataifa. Kwa hiyo yabainika wazi kwamba hakuna utekelezaji wa kanuni jumla za kimataifa juu ya nchi zote, hivyo basi sio sahihi hata kuwaza kuhusu fikra ya kutekeleza kanuni za kimataifa kwa nguvu, kwa sababu hilo halitakuwa isipokuwa ni uwadui.

Kutokana na hayo yote, yabainika kwamba hakuna kanuni za kimataifa, bali haiwezekani kuwepo kivitendo, lakini kilichopo ni mikataba kati ya nchi mbali mbali, na desturi wanazoafikiana juu yake kuhusina na hiyo mikataba, na kuhusiana na mahusiano ya kivita na mahusiano ya amani baina ya makundi ya wanaadamu. Kwa hivyo ikiwa hakuna budi kuundwa kwa jamii ya kimataifa, basi itakuwa tu na kanuni za kiidara, na kazi yake itakuwa ni kuangalia katika desturi za kimataifa na wanaozikiuka, na desturi zinazohusiana na mikataba ya kimataifa pia zitaingizwa humo: kuhusu kufungwa kwake, utekelezaji, na kujitoa, na mfano wa hayo, kwa sharti zisichukuliwe desturi zote za kimataifa, bali zichukuliwe tu zile zinatokea ndani ya kundi linalounda jamii ya kimataifa, na hizi desturi haziundwi kwa maamuzi yanayowekwa na nchi, hili ni kosa na lina madhara mengi sana, bali desturi hizi hutokea kutokana na nchi mbali mbali kuzifuata kwa mda mrefu hadi zikamakinika. Na hapo nchi zitaamini kwa msukumo wa kibinafsi kwamba hizi desturi ni wajibu kufuatwa.

Ama kuhusu maudhui ya nchi kuzifuata desturi: hilo huwa kutokana na msingi au amri au mafhumu kurudiwa-rudiwa ili izingitiwe kuwa ni desturi (urfu). Kwa sababu kitendo cha watu na kukubaliana kwao tu juu ya kitu hakufanyi kitu hicho au kitendo kuwa desturi, bali hapana budi kupatikane kurudiwa-rudiwa mara kwa mara mpaka kupatikane desturi jumla. Hii ndio desturi jumla ambayo huangaliwa na jamii ya kimataifa wakati inapotaua mizozo

ya kimataifa au uhalifu uliofanywa na nchi zinaunda hiyo jamii. Kwa hiyo, desturi ya kimataifa kwa maana yake ya kihakika, ndio ambayo kwamba huangaliwa wakati wa kuondoa mizozo ya kimataifa. Lakini hii desturi haifai hata kufikiriwa kwamba utekelezaji wake uwe kwa mabavu juu ya nchi, bali hutekelezwa kupitia rai jumla (Public opinion) na msukumo wa kindani, kwa sababu nchi wanachama katika jamii ya kimataifa hazikuamua kuwa msingi au jambo fulani liwe desturi ya kimataifa ila baada ya kuhakikisha kwamba limeshakuwa desturi, wakati huo itakua ishapatikana itikadi kwa hizo nchi kwamba hii desturi ni wajibu kufuatwa, kwa hiyo itakuwa hakuna haja ya kutekelezwa kinguvu. Mbali na hayo, hakika nguvu ya rai jumla dhidi ya nchi inayokhalifu desturi (hii nguvu) yatosha kuilazimisha hiyo nchi/serikali kwa hiyari na kindani zaidi kuliko nchi hiyo kulazimishwa kutoka nje kwa nguvu za kushikika. Na kundi la wanaadamu kuhofia kuaibishwa kutokana na kuhalifu desturi hili linaliathiri zaidi kuliko kuhofia kwao kutekelezewa kimabavu kwa nguvu za kimada. Kwa hiyo iachwe rai jumla na msukumo wa kindani zisimamie utekelezaji wa maamuzi ya jamii, na hii ndio njia ya utekelezaji wake.

**Ama kuhusu suala la ulimwengu kuteseka kwa sababu ya zile nchi kubwa:** tatizo hasa sio nchi fulani kuwa nchi kubwa, bali hayo mateso yanatokana na kuungana kwa hizo nchi, na kushikamana kwao ili kugawana maslahi na faida baina yao, huku kuungana kwao ndio msingi wa balaa. Kwa hiyo suluhisho yapaswa kuelekezwa kwenye huko muungano wenyewe wa hizo nchi kuu, na sio kwenye nchi tu kuwa kubwa. Kwani “muungano mtakatifu” ambao ndio uliokuwa muungano wa kwanza wa nchi kubwa, uliundwa kwa ajili ya nchi kuu kugawana maslahi, na ili kutetea viti vya hawa wafalme walioungana, na kwa lengo la kukandamiza harakati yoyote ya mapinduzi ya kiraia dhidi ya hao wafalme, au kwenda kinyume na matendo yao, na ili kuweza kuingilia nchi yoyote duniani kwa kisingizio cha kutishia amani au nidhamu. Basi huu muungano ukawa maangamivu kwa ulimwengu hasa Ulaya.

Ndio, ni kweli kwamba raia wa Ulaya waliweza kuvunja athari ya huo muungano na kulemaza nguvu zake, wakafanya mapinduzi na kuvunja maamuzi ya wafalme, lakini fikra ya nchi kubwa kuungana iliendelea kutawala dunia hadi leo hii. Wafaransa walifanya mapinduzi ya kiraia na kuondoa ufalme na kutangaza jamhuri, Ubelgiji ilifanya mapinduzi ikajitenga na Uholanzi na kuwa huru, wajerumani nao walifanikiwa kumaliza vijinchi vilivyokuwa vimegawanywa na kuunda Ujerumani moja, hayo yote yalikuwa ni mapinduzi dhidi ya muungano wa wafalme watano. Lakini hizi nchi kubwa baada ya kubadilisha nidhamu zao za utawala, ziliendelea kushikamana na fikra ya miungano ya kimataifa, na hiyo miungano ndio iliyosababisha vita vya kwanza vya dunia na vya pili pia.

Ndio, ni kweli kwamba mapatano kati ya Marekani na Urusi (muunga wa kisovieti) yaliondoa miungano miwili, yaani kambi mbili za Ujamaa na Uraslimali, na kuweka mbali uwezekano wa kuzuka kwa vita vya tatu vya dunia, baada ya Khrushchov na Kennedy mwaka wa 1961 huko Vienna, lakini wao walibadilisha miungano kwa muungano wao mpya. Hivyo hawazingatiwi kwamba walitibu fikra ya muungano wa nchi kubwa, bali walibadilisha tu sura ya miungano kwa kubuni muungano mwengine mpya kwa maslahi yao na kusababisha hatari mpya, nayo ni nchi mbili kuu kugawana ulimwengu baina yao, na kudhuru msimamo wa kimataifa. Kwa hiyo badala ya wao kutatua tatizo la muungano wa kimataifa walizidi kuufanya mgumu na wakautilia nguvu zaidi, na kuweka mbali uwezekano wa nchi ndogo ndogo kufaidika kutokana na nchi kubwa kukhtalifiana na hizo nchi kunusuru kadhia zao, basi kwa sababu ya mapatano ya hao wababe wawili kukawa na hatari kubwa kwa siasa za kimataifa.

Hivyo basi, miungano huhatarisha amani, bali huwa hatari kwa nchi zengine ziwe kubwa ama ndogo, haijalishi ikiwa ni miungano kama ya zamani, yaani nchi zilizoungana zenye uwezo sawa kugawana ngawira baina yao kwa usawa, au ikawa ni miungano kwa

sura yake ya kisasa, yaani nchi kubwa ya kwanza (ambayo ni Marekani kwa sasa) kuzitumia nchi zengine ili kufikia maslahi yake kwa daraja ya kwanza, na kuidhibiti ngawira yote au sehemu yake kubwa, na nchi zengine katika muungano hazipati isipokuwa kitu kidogo tu. Kama ilivyotokea katika muungano wa kimataifa kwenye vita vya pili vya Ghuba (Khalij) wakati Iraq ilipoinyakua Kuwait, kisha Marekani ikamimina mashambulizi yake ya kinyama juu ya Iraq mwanzoni mwa miaka ya tisaini katika karne iliyopita, na kuunganisha takriban nchi thelathini pamoja nayo. Na vilevile uwadui uliofanywa na Marekani dhidi ya Iraq mwanzoni mwa mwaka wa 2003 ilipokusanya takriban nchi thelathini ndani ya Iraq chini ya miito ya miungano mbali-mbali.

Miungano yote hata ikiwa na sura tofauti-tofauti husababisha shari za kuendelea katika ulingo wa kimataifa. Kwa hivyo hakuna budi kupatikana tiba ya haraka kuhusu fikra ya miungano ya kimataifa, bila kujali ikiwa nchi zilizoungana ni nchi kubwa ama nchi kubwa na ndogo.

Ama kuhusu hiyo tiba yenyewe: tunaloonelea ni kwamba, haiwezekani kupatikana tiba ila kwa **kubadilisha ufahamu (*mafhum*) kuanzia msingi wake**, kwa sababu mienendo ya mwanaadamu maishani huwa ni kulingana na ufahamu wake kuhusiana na hayo maisha, kwa hiyo hakuna budi kwanza kubadilishwa ufahamu wa raia ambao ndio huunda hizo nchi kubwa zenye kubeba fikra ya miungano ya kimataifa, kisha ifuatie hatua ya kutokomeza kabisa miungano ya kimataifa. Na maadamu huo ufahamu haujabadilishwa, basi ulimwengu utaendelea kuteseka, bali huenda mateso yakazidi.

Ama kuhusu njia ya kubadilisha huo ufahamu: hilo lifanywe kwa kutengeneza rai jumla (rai aam) ya kiulimwengu dhidi ya miungano, hii ndio itakuwa tiba bora zaidi ya hili gonjwa. Na dalili juu ya haya ni kwamba, katika karne ya kumi na tisa fikra ya kukoloni nchi dhaifu ilikuwa ndio fikra ambayo nchi kubwa na ndogo za kimagharibi zote zikijifakhiri na kujigamba nayo, na

zikashindana katika kuwakoloni watu na nchi mbali-mbali kwa sura ya wazimu! hakuna tofauti kati ya Uingereza na Uholanzi, wala baina ya Ujerumani na Ubelgiji, wala baina ya Ufaransa na Uhispania, nchi zote za Ulaya zilitoka ili kuwakoloni watu. Na wakati iliposimama serikali ya kikomonisti ndani ya Urusi baada ya vita vya kwanza vya ulimwengu, ilitabanni fikra ya kupiga vita ukoloni na ikaishambulia kwa ukali na nguvu, na ikawahimiza watu ulimwenguni kupambana nayo, na kuwachochea dhidi ya wakoloni. Na hadi kufika tu vita vya pili vya ulimwengu ikawa tiyari imeshapatikana rai jumla iliyoenea duniani dhidi ya ukoloni, ndio sababu kukawekwa vifungu katika mkataba wa umoja wa mataifa kuhusiana na kukomesha ukoloni ulimwenguni, na fikra ya kupata uhuru nayo ikaenea, ndipo nchi za kikoloni zikarudi nyuma na kauchana na ukoloni, na kutokana na mbano wa rai jumla zikalazimika kupeana uhuru kwa nchi walizozikoloni, ingawa baadhi ya nchi zilifanya hiyo ni *uslubu* mpya ya kubadilisha tu sura ya ukoloni. Lakini vyovyote itakavyokuwa, rai jumla ileweza kubadilisha mtazamo kuhusiana na ukoloni, basi ni hivyo hivyo pia kuhusiana na fikra ya miungano ya nchi kubwa. Kwa hiyo hakuna la zaidi kwa watu walio/wanaoteseka na kuumia kutokana na miungano ya nchi kubwa kubwa isipokuwa ni kujaribu sana kupambana na hii fikra kwa nguvu kali hadi kufikia kuitokomeza kabisa. Lakini huko kuitokomeza kabisa kunahitajia uwepo wa serikali yenye nguvu itakayotabanni fikra ya kupambana na hiyo miungano. Na kwakuwa nchi kubwa zilizopo sasa zaunga mkono hii fikra kwa pande tofauti tofauti kwa ajili ya kutumikia maslahi yao, basi ni vigumu sana kwa wanaoteseka na miungano yao kufanikiwa kuisambaratisha kabisa hii fikra, ila kama hao watu watafaulu kusimamisha serikali yenye nguvu itakayotabanni fikra ya kuangamiza miungano, na bila shaka kusimama kwa serikali ya kiislamu ndio tumaini pekee la watu waliofanywa wanyonge, ili waweze kujikomboa kutokana na hii fikra.

Limebakia suala la mataifa kukoloniwa, au uporaji wa raslimali zao na kuwadhalilisha: hii fikra ingawa walimwengu wamepiga

hatua nzuri katika kupambana nayo, lakini bado ukoloni ni katika matendo hatari zaidi yanayotesa mataifa dhaifu, na ndio inayotishia zaidi utulivu wa maeneo na ulimwengu kwa ujumla, na tatizo la Congo lililoendelea kwa miaka mingi na inayoendelea kukoloniwa mpaka leo, na matatizo ya Mashariki ya Kati yanayoendelea, yote hayo ni mifano hai ya jinsi ukoloni unavyotishia utulivu, kwa hiyo imekuwa ni lazima sana hili janga la ukoloni kupata tiba.

Hakika ukoloni ni uti wa mgongo wa mfumo wa kiraslimali na haiwezekani kutenganishwa, bali ukoloni ndio njia ya kutekelezwa fikra yake, kwa hiyo hakuna njia ya kutibu ukoloni kimsingi ila kwa kutumia juhudi zote katika kupambana na mfumo wa Uraslimali na kuumaliza kabisa. Na kwa hakika Ukomonisti umepiga hatua katika kutibu ukoloni na katika kupambana na uraslimali, lakini ulifuata fikra ya makosa na mapambano yenye kasoro, kwani Ukomonisti ulipambana na aqeeda ya kutenganisha dini na serikali kwa aqeeda ya maendeleo ya mada, na hii aqeeda ya maendeleo ya mada nayo ni ya makosa na yaenda kinyume na maumbile ya mwanaadamu, ndio maana haikupata kukubalika katika mujtamaa za kiraslimali, mbali na kwamba hata watu binafsi walioamini aqeeda ya mabadiliko ya mada hii aqeeda haikuwaathiri katika mienendo yao maishani, kwa sababu anayeamini mabadiliko ya mada hakuna kitakachomdhuru akitekeleza aqeeda ya dini kutenganishwa na serikali, kwa kuwa aqeeda ya kutenganisha dini na serikali yaweza kubebwa na mtu anayeamini kuwepo kwa Mungu, na pia anayekanusha uwepo wake, kwa sababu hii aqeeda haimaanishi kumkanusha Mungu, wala pia haimaanishi kumuamini, bali yamaanisha kwamba dini isifanywe muamuzi katika mambo ya serikali, na hili haliathiri mienendo ya anayebeba aqeeda ya mabadiliko ya mada, hii ndio maana twakuta kwamba aqeeda ya kikomonisti haikuathiri katika mujtamaa za kiraslimali wala haikuleta mabadiliko yoyote humo.

Ama kuhusu Ukomonisti kupambana na Uraslimali: hili lilianza na fikra za Karl Marix na wanafalsafa wa kikomonisti waliokuja baada yake, fikra zao zikajenga watu binafsi na makundi

walioziamini, lakini hazikuweza kujenga watu jumla wote kuzibeba kupitia kuzisoma tu na kuzitafiti. Mbali na hilo, njia yake ya kuzifanya zipatikane katika serikali ya kikomonisti ilikuwa njia ya kimakosa pia, na ilikuwa ni njia ya kimawazo tu. Njia ilikuwa ya kimakosa kwa sababu ya wao kufanya usimamishaji wa serikali kuwa ndio njia ya kufikia kuusambaratisha Uraslimali, na tumesema ilikuwa ya kimawazo kwa sababu ya kutaka mapinduzi yawe ya kiulimwengu, yatakayoanza na mataifa yaliyoendelea kiviwanda na kisha kuenea ulimwenguni, ndipo Lenin akalazimika kuikhalifu hii njia kwa kisingizio cha kuifasiri, akaunda serikali ya kikomonisti ndani ya Urusi peke yake, ambayo iliyokuwa nyuma kiviwanda ikilinganishwa na Ulaya. Kisha baada ya thuluthi ya karne waliokuja baada ya Lenin kufanya mapatano na Marekani ambayo ndio nchi kubwa zaidi ya kikoloni, yaani wakafanya mapatano na ukoloni! Natija yake ikawa ni Ukomonist wenyewe kuanguka kabisa, na nchi/serikali kiongozi ya kikomonisti pia ikasambaratika, hivyo basi Ukomonisti ukawa umefeli kufikia malengo yake.

Kwa hivyo imekua hakuna budi kutafutwa suluhisho lengine ili kupambana na Ubepari na kutokomeza ukoloni, na hakuna mfumo mwengine wenye uwezo wa kufanya hivyo isipokuwa Uislamu, bali ndio suluhisho pekee la kuondosha ukoloni na kuuvunja ubepari. Na msingi wa suluhisho ni kuleta fikra jumla (aqeeda) kuhusiana na ulimwengu, mwanaadamu, na uhai/maisha, kwenye uwanja wa mijadala ya kiulimwengu, na kuiingiza katika mkataba wa jamii ya kimataifa inayosimamia utekelezaji wa desturi ya kimataifa kwa ridhaa na hiyari. Hiyo mijadala ya kiulimwengu kuhusu fikra jumla ndio itakayobadilisha *mafahim* (ufahamu) na kuondosha fahamu potofu na kusahihisha desturi za kimataifa. Kwa sababu ukoloni ni mtazamo maalumu katika maisha, na ukoloni hautomalizwa ikiwa huu mtazamo hautabadilishwa. Ndio, ni kweli kwamba rai jumla iliyopo ulimwenguni dhidi ya ukoloni iliuathiri lakini haikuumaliza kabisa ukoloni, kikubwa kilichofanyika ni kubadilisha mbinu zake, nchi zilizokoloniwa huko Afrika, Asia, na Marekani ya kilatini zote zimekoloniwa ingawa zimewekwa katika mbinu ya nchi huru, na

hizi nchi hazikuwa huru ila kwa mapinduzi ya kiraia, vita vya kikanda na vya kiulimwengu.

Lakini maadamu nchi kubwa kubwa zilizopo ulimwenguni zimeshikamana na ukoloni kama fikra na kutumia nguvu zao zote kwa ajili yake, basi hakuna namna ya kuumaliza ukoloni duniani ila kwa kung'oa hiyo fikra katika nyoyo za wanaoiamini kama mtizamo wao maalumu maishani. Ndio, ni sahihi kwamba ni lazima kupambana na ukoloni kwa mapambano ya kimada (kivitendo), na huku rai jumla kuendelea kuwa dhidi yake, na juhudi ziongezwe katika hayo, lakini hayo sio tiba bora zaidi, bali tiba na suluhisho bora zaidi ni kuuonyesha Uislamu katika ulingo wa mijadala ya kimataifa kama fikra jumla kuhusiana na ulimwengu, Mwanadaamu, na maisha, fikra hii iweze kujadiliwa na watu na mataifa yote, na iwe ndio kitu cha kutafitiwa na kujadiliwa kimataifa. Hii ndio tiba bora zaidi ya ukoloni, na haiwezekani kutekelezwa kivitendo ila kwa kuwepo serikali ya kiislamu yenye nguvu kwenye ulingo wa kimataifa.

Hayo tuliyoeleza ndio majanga matatu ambayo yameutesa ulimwengu na kuukwaza usifuate njia ya mafanikio, na pia hii namna ya kutibu hizo balaa tatu. Lakini kutibiwa kwake hakumaanishi kukosekana kwa vita wala kukosekana kwa wasiwasi na misukosuko, na wala pia haina maana kwamba mitego ya kimataifa, uchokozi wa siasa, na mbinu chafu zitakoma, hapana haina maana hiyo, bali itamaanisha kuondoshwa kwa zimwi la miungano ya pamoja ambalo lilikua limeshindikana. Lakini mivutano baina ya nchi ni jambo la kimaumbile, na baadhi ya nchi kukimbilia vita ni la kimaumbile pia, kadhalika kupatikana uchokozi ni la kawaida, lakini hayo yatakuwa ni ya nchi moja moja kibinafsi au yatakuwa ni mambo yenye mipaka fulani wala haivuta umwengu wote kwenye vita kama ilivyokuwa katika vita viwili vya dunia vilivyopita, wala ufikiriaji wa mataifa hautofungika kwenye kunyonya tu damu za mataifa kama hali ilivyo kwa sasa, bali yatakuwa kama ilivyo tabia ya mwanaadamu: uongofu na upotofu, kheri na shari, uzuri na ubaya, nchi zitakuwa na hili au lile wala zote

hazitokuwa na shari kama ilivyo tangu ilipozuka fikra ya muungano wa nchi kubwa-kubwa, na fikra ya "jamii ya kimataifa" na fikra ya ukoloni iliyopo sasa. **Kwa hivyo, hakuna budi kuikomesha hii shari iliyotawala ulimwengu kwa karne nyingi, na hakuna budi kuundwa serikali yenye uwezo wa kuikomesha, nayo ni serikali ya kiislamu ya Khilafah.**

********

## [8] NAMNA YA KUATHIRI KATIKA SIASA ZA KIMATAIFA

Huenda kukaulizwa: itawezekanaje kwa watu binafsi kuathiri katika siasa za kimataifa? bali yawezekana vipi vyama kuathiri katika mwelekeo wa nchi? hasa na kwa kuwa huo mwelekeo ni mkongwe na kuendelea kwa karne kadhaa! Jibu ya hayo ni kwamba: Watu binafsi au vyama wakati wanapofuatilia matendo ya kisiasa na kufahamu siasa za kimataifa, hawafanyi hivyo kwa ajili tu ya starehe ya kiakili na israfu ya kifikra, wala sio kwa lengo la kujifundisha na kuzidisha maalumati, **bali huyafuatilia ili kusimamia mambo ya ulimwengu, na kwa lengo la kuweza kufikiria kwa njia ambayo watauathiri ulimwengu, yaani ili wawe wanasiasa,** na haiwezekani kusudio la mwanasiasa liwe ni kustarehesha akili hata kama atakuwa ni miongoni mwa wenye akili kubwa, na haiwezekani kwake kuegemea kufanya israfu ya kifikra tu hata kama atakuwa miongoni mwa wenye fikra za kina sana. Hivyo basi yeye anapofuatilia siasa, anapofahamu msimamo na hali ya kimataifa, na anapofuatilia siasa za kimataifa, hufanya yote hayo kwa sababu tu yeye ni mwanasiasa, wala sio kwa kuwa ni mwenye akili au mfikiriaji.

Na maana ya huyu mtu kuwa mwanasiasa ni kwamba anafanya kazi ili kusimamia mambo ya ulimwengu, yaani ili kuathiri katika siasa za kimataifa. Hili ni kwa upande mmoja, na kwa upande mwengine yeye hafanyi kazi kama mtu binafsi, bali kama sehemu ya Ummah na kama aliye ndani ya serikali. Naye ingawa – kwa sasa - sio katika wanaopanga sera wala katika watekelezaji, lakini ana

hamu ya kuwa miongoni mwa wenye kutoa maamuzi au watekelezaji au mwenye kuwawajibisha wenye maamuzi na watekelezaji. Basi kwa hayo ataathiri kimataifa hata kama atakuwa mtu binafsi asiyekuwa haki ya maamuzi wala utekelezaji, akiwa na hizo sifa atakuwa na athari, kwa sababu nchi ambayo yeye yumo ndani yake huathiri kupitia watu kama yeye, au yeye na mfano wake wataenda mbio ili kuifanya iathiri katika siasa na msimamo wa kimataifa, na hapa ndio huja kinachokusudiwa katika matunda ya fahamu za kisiasa, nayo ni kuifanya nchi iathiri katika siasa/sera na msimamo wa kimataifa, kupitia kuwajenga watu binafsi wenye uelewa wa kisiasa, wanaotambua matendo ya kisiasa yanayotendeka ulimwenguni hasa yanayofanywa na nchi kubwa kubwa.

Kwa hiyo, hatua ya kwanza ya kuathiri katika siasa na msimamo wa kimataifa ni kuwa na ufahamu makini wa kisiasa, na jiwe la msingi ni kuwahimiza watu binafsi kufuatilizia matendo ya kisiasa na kufahamu siasa za kimataifa, yaani kuwaunda wanasiasa katika siasa za kimataifa, basi hapo serikali itaathiri katika siasa za kimataifa na msimamo wake kimaumbile. Imebainika kupitia hayo kiwango cha ulazima wa fahamu za kisiasa na thamani yake.

Lakini ni lazima ijulikane kwamba nchi haiwi na uwepo wa kimataifa isipokuwa kwa mahusiano yake na nchi zengine, kwani hata mtu binafsi hawi na uwepo katika jamii yake ila kwa mahusiano na watu wengine na daraja yake ndani ya jamii huwa kulingana na hayo mahusiano na kulingana na kuathiri kwake katika mahusiano baina ya watu, basi hivyo hivyo nchi pia uwepo wake hutokana na mahusiano yake na nchi zengine, na daraja yake hupanda na kushuka kulingana na hayo mahusiano na kulingana na namna inavyoathiri katika mahusiano ya kimataifa. Serikali ya kiislamu ni serikali ya kimfumo na mfumo ndio kazi yake ya kimsingi, yaani wadhifa wake ni kubeba ulinganizi wa kiislamu kuwapelekea walimwengu, hivyo ni lazima kwake – bali ni sehemu ya muundo wake – kuwa na cheo cha kimataifa, na ni lazima iathiri katika mahusiano ya kimataifa.

Kwa hivyo, fahamu za kisiasa walizonazo wanasiasa ni lazima ziwe ni fahamu za siasa za kimataifa, sio fahamu za siasa za kieneo au za kikanda. Yaani hakuna budi kwa wanasiasa – kwa sifa yao ya kuwa Waislamu – wawe na ufahamu wa kisiasa kwa upande wa kimataifa, sio tu kwa kufahamu siasa za nchi au kikanda, kwa kuwa serikali ni ya kiislamu basi ni lazima wawe na uelewa kamili wa kisiasa. Kwa sababu Uislamu wao, na serikali yao kuwa ya kiislamu, na wadhifa wake msingi kuwa ni kupeleka ujumbe wa Uislamu kwa walimwengu, yote hayo yanawalazimisha kuwa na uelewa wa kisiasa, na huo uelewa uwe kamili.

****

## [9] UFAHAMU WA KISIASA

Kuelewa siasa haimaanishi kujua hali ya kisiasa, au msimamo wa kimataifa, au matukio ya kisiasa, au kufuatilia siasa na matendo ya kimataifa, ingawa hayo ni katika mambo yanayolazimiana na ukamilifu wake. Bali kuelewa siasa ni kuuangalia ulimwengu kwa mtizamo maalumu, nao kulingana na sisi ni kwa mtizamo wa aqeeda ya kiislamu, mtizamo wa ***(laa ilaaha illa-llah, Muhammadur-Rasulullah) "Nimeamrishwa kuwapiga vita watu mpaka waseme: laa ilaaha illa-llah, Muhammadur-Rasulullah, wakishasema hivyo basi watakuwa wamelinda nafsi zao na mali zao isipokuwa kwa haki ya Uislamu",*** Huu ndio uelewa wa siasa. Basi kuuangalia ulimwengu bila mtizamo maalumu hili huzingatiwa kuwa ni uelewa wa kijuujuu tu, wala sio uelewa wa kisiasa. Kuangalia maeneo ya ulipo au upande wa ukanda fulani pia ni ujinga tu wala sio kufahamu siasa, kwani uelewa wa kisiasa haukamiliki mpaka yatimie mambo mawili: kuangalia ulimwengu wote, na kuangalia huko kuwe ni kwa upande wa mtizamo maalumu bila kujali huo upande: uwe ni wa kimfumo fulani maalumu, au fikra maalumu, au maslahi fulani maalumu, au upande wowote mwengine.

Hayo ni kuhusu uhalisia wa uelewa wa kisiasa kama ulivyo, nao kulingana na Muislamu bila shaka ni kwa upande wa aqeeda ya kiislamu. Huu ndio ufahamu wa siasa, na maadamu huu ndio

uhalisia wake, basi hili lamlazimisha mwanasiasa kimaumbile kujitosa katika mapambano ya kujenga ufahamu maalumu kuhusu maisha kwa mwanaadamu kama mwanaadamu popote alipo, na kujenga huo ufahamu ndio jukumu la kwanza katika mabega ya mwanasiasa, jukumu ambalo hapati raha ila kwa kusumbuka katika kulibeba na kulifikisha kwa wengine.

Muelewa wa siasa hana budi kuingia kwenye mapambano dhidi ya mielekeo yote inayogongana na muelekeo wake, na dhidi ya fahamu zote zinazokinzana na ufahamu wake, wakati anapopambana ili kukitisha ufahamu wake na muelekeo wake. Kwa hiyo yeye hufanya kazi mbili kwa wakati mmoja, mojawapo haitengani na nyengine hata kidogo kwa sababu ni kitu kimoja: yeye huvunja na kutengeneza, hubomoa na kujenga, huondoa kiza na huwasha mwangaza, yeye huwa kama ilivyosemwa: "Ni moto unaoteketeza uharibifu, na ni nuru inayoangaza njia ya uongofu". Kama anavyopambana ili kukita fahamu zake na mielekeo yake kwa kuyaowanisha na matukio pamoja na kujiweka mbali na utenganishaji (wa matukio yanayohusiana) na kujiweka mbali na kanuni za mantiki, kadhalika hupambana dhidi ya mielekeo mengine, hupambana dhidi ya hujuma zinazoelekezwa dhidi ya ufahamu wake kuhusu maisha, hupambana dhidi ya "*mafahimul a'maaq"* (fahamu zilizokita ndani yake) zilizokuja kutoka zama za mporomoko, hupambana ili asiathiriwe na upotoshaji wa maadui unaoenezwa kuhusu fikra na vitu, hakubali kufuata njia za mkato ili kufikia malengo ya juu zaidi na malengo ya mbali kwa kupata malengo ya kivipande na ya mda mfupi. Kwa hiyo daima hupambana katika sehemu mbili: nje na ndani, na pia hupambana katika mielekeo miwili: mwelekeo wa kubomoa na wa kujenga, kadhalika hufanya kazi ndani ya viwanja viwili: uwanja wa siasa na uwanja wa fikra.

Kiufupi: muelewa wa siasa huingia katika mapambano ya maisha katika nyanja zake zilizo bora zaidi na zilizo juu kabisa. Kwa hiyo wajuzi wa kadhia katika kusuguana kwao na hali halisi na watu na matatizo ya maisha, wao kugongana katika hayo ni jambo

lisiloepukika, hakuna tofauti baina ya uwanja wa kindani wa pale walipo au uwanja wa kinje wa kimataifa. Na katika huko kugongana ndio hudhihirika uwezo wa kufanya ujumbe alioubeba, na upande wake maalumu ambao huutumia kuangalia nao ulimwengu kulingana na ufahamu aliotabanni, (hudhihirika uwezo wa kufanya haya kuwa) ndio msingi, hakimu, na ndio lengo analoliendea mbio na kusumbuka ili kulifanikisha.

Lakini kwa kuwa amejifunga na upande maalumu wa kuangalia nao ulimwengu, na kwa sababu ana dhauku yake na muelekeo (muyul) maalumu, iwe ni ya kimaumbile au ya kimfumo: (kwa sababu hizo) yahofiwa – asipojichunga – asije akayapaka matukio rangi anayopenda yeye, na kuyafasiri (kufanya ta'wil) fikra kwa namna anayotaka yeye, na kuzifahamu habari kulingana na natija anayotaka yeye kufikia. Kwa hiyo ni lazima awe na tahadhari *muyul* zake zisije zikatawala maoni na habari, kwani matakwa ya nafsi kwa kitu fulani, au chama, au mfumo huenda yakamfanya akatafsiri rai fulani kuwa ni kweli kumbe ni uongo, au akadhani kuwa ni uongo kumbe ni kweli, hivyo basi muelewa ni lazima achunguze maneno yanayosemwa na matendo yanayofanywa.

Ama kuhusiana na uhalisia: iwe ni uhalisia wa vitu au matukio, basi ni lazima autambue huo uhalisia kwa namna ya kuhisika, auhisi kimantiki lakini kama ulivyo uhalisia wenyewe, sio kama anavyopenda yeye uwe. Ama kuhusiana na fikra (*afkaar*): pia ni wajibu zifahamike kama zilivyo katika uhalisia wake, zitoke ubongoni mwake kwenda nje, na kwa moyo wake aone uhalisia unaeleza kuhusu fikra, na aifahamu hiyo fikra kulingana na anavyoiona hali halisi inayojulisha hiyo fikra kama ilivyo, sio kama inavyokubaliana na anavyotaka yeye. Ndio, ni kweli kwamba wakati mwengine maneno yawezekana yakawa ni ya *kimajazi*, na pia yawezekana yakawa ni *isti'aara*, au yakawa ni *kinayah*, na yawezekana sentensi ikafahamika kulingana na mririko wake wala sio kulingana na matamshi yaliyounda hiyo sentensi. Lakini hayo hayamzuilii kwenda nje na kuona uhalisia inayojulisha kulingana na lugha inavyojulisha na kama wenye lugha walivyosema.

Kwa hivyo, muelewa wa siasa ni lazima afuate haki lakini kulingana muelekeo wa mtazamo wake ambao ameuchukua kwa yakini na kukatikiwa, na aone uhakika kama ulivyo, lakini kulingana na muono wake wa kihisia au kifikra, kwa kufanya hivyo ndio uelewa wake utakamilika, kwa kuwa ana nyenzo na mbinu za kuzingatia. Lakini ni lazima msingi wa kila kitu – mtizamo, kuhisi, na kufahamu – uwe ni kuangalia ulimwengu kwa upande wa mtizamo maalumu.

Hapa huibuka swali: hali ya mwanasiasa muelewa kujifunga na haki na kuona uhalisia kama ulivyo, hali hii itaafikiana vipi na hali ya yeye kuangalia ulimwengu kupitia upande maalumu? likiibuka swali kama hili basi huwa ni kutokana na kuyaangalia mambo kijuujuu, lakini akiingia ndani zaidi katika kutafiti basi hatouliza swali kama hili, kwa sababu kuna tofauti baina uhalisia wa vitu na kuvitolea hukumu, kwani watu hawatofautiani kuhusu uhalisia wa vitu. Vikiwa vyahusiana na kuviona kwa macho, basi kila mwenye macho sahihi ataviona vitu kama vilivyo, labda kama atahadaiwa au kupotoshwa. Na ikiwa uhalisia wahusiana na kuhisi, basi yeyote atakayehisi kitu iwe ni kuhisi kwa kuonja chenye ladha chungu au tamu, au kuhisi kwa kukigusa kiwe ni laini au kigumu, au kuhisi kwa kusikia sauti, au kuhisi kwa kunusa vyenye harufu, basi watu watahisi vitu kama vilivyo vyovyote watakavyo tofautiana, lakini kutoa hukumu juu ya vitu ndio watu hutofautiana. Kwa hivyo basi, kuutizama ulimwengu kupitia upande maalumu hili lahusiana na kuvitolea hukumu vitu na vitendo, na kuona uhalisia kama ulivyo hili lauhusiana na kuhisi na kudiriki. Kwa hivyo hakuna budi kwa muelewa wa siasa kuyaona mambo kama yalivyo na kujifunga na upande wa haki, na hana budi kuangalia ulimwengu, matukio, na vitu kupitia upande maalumu wa aqeeda yake.

Ama kuhusu jinsi hayo yanavyoambatana na siasa za kiulimwengu: tukieleza baadhi ya mifano itatuonyesha ni vipi tutayaangalia matukio kupitia upande maalumu, hebu tutaje baadhi ya mifano kutokana siasa ya Mtume (saw), na baadhi ya mifano

kutokana siasa za karne za kati, na baadhi ya mifano kutokana na siasa za zama hizi.

Mtume (saw) upande ambao alikuwa akiangalia ulimwengu kupitia kwake ulikuwa ni wa kueneza Ulinganizi, na kwa kuwa Maquraish walikuwa ndio nchi kubwa ndani ya *Aljazirah*, na ndio waliokuwa kichwa cha ukafiri katika kusimama mbele ya ulinganizi, basi ndio maana Mtume (saw) akayafunga matendo yake yote ya kisiasa na ya kivita kwa Maquraish, akawa anawatumia majajusi kuwachunguza, akivamia biashara zao, na kupambana nao katika viwanja vya vita, na alikuwa akitosheka kwa nchi zengine – yaani makabila – wakibakia wakiyaangalia mambo tu, au kama inavyosemwa: kubakia bila kuegemea upande wowote. Kwa hivyo, vitendo vyake vya kisiasa na vya kijeshi vilikuwa vikitokana na kuangalia ulimwengu kupitia upande maalumu.

Na Mtume (saw) alipojua kwamba watu wa Khaibar wanajadiliana na Maquraish kuhusu kufunga mkataba wa kuungana ili kuivamia Madinah na kummaliza Muhammad (saw) na kuufuta Uislamu, basi Mtume (saw) akafanya upande maalumu wa vitendo ni kufunga mkataba wa amani na kufanya sulhu na Maquraish, ili apate nafasi nzuri ya kuimaliza Khaibar, hivyo basi kutokana na upande huu akafanya sera ya amani ndio msingi wa vitendo vyake vinavyofuata, maadamu vitafanikisha malengo yake. Basi vitendo vyake vyote: kwenda Umra, kuridhia kupuuzwa na Maquraish, kuwa laini mbele ya inadi zao, kuwakhalifu maswahaba wake... vitendo vyote vikawa vyaenda kulingana na sera ya amani. Kwa hiyo, namna anavyoyatizama vitendo ya kisiasa anavyoelekeza dhidi ya adui wake vikawa ni kutokana na upande maalumu, na kuendana na mahitaji ya huo upande maalumu.

Hiyo ni mifano miwili katika matendo ya Mtume (saw): moja ni kitendo jumla: kuelekeza juhudi na akili kwa nchi kubwa ambayo ndio kichwa cha maadui zake kwa msingi wa upande maalumu. Na cha pili ni kitendo makhsusi: kuelekeza juhudi na akili kwenye lengo maalumu, akafanya huo ndio upande maalumu, akawa anayatizama matendo ya kisiasa na ya kijeshi kupitia huu upande

maalumu. Hivi ndivyo inavyoshuhudiwa namna ambavyo kuangalia matendo ya kisiasa kupitia upande maalumu kunavyotawala juu ya matendo, na lau kama sio huo mtizamo kupitia upande maalumu basi matendo hayangekuwa na maana yoyote.

Baada ya kongamano la Barlin nchi kubwa zilifanya upande wake maalumu ni kupora miliki za serikali ya kiislamu ya kiuthmani, wala sio kuimaliza, ingawa zilijadiliana kuhusu hayo mawili kwa pamoja, zikaamua kukubaliana juu ya lengo la pili, lakini hazikufanya kuwa ndio upande maalumu, ndio maana vitendo vyao vyote vikajipanga kulingana na huu upande, zikaingia kwenye mivutano ya kisiasa wenyewe kwa wenyewe iliyoendelea zaidi ya karne, nayo japo ilikoma kwa kuondoka serikali ya kiislamu, lakini hilo halikuwa upande wake maalumu ambao hizi nchi zilikuwa zikiangalia nayo matukio na matendo ya kisiasa. Kwani upande wao maalumu ndio uliotawala na kudhibiti siasa zao na mtizamo wao kwa matendo ya kisiasa.

Marekani baada ya vita vya pili vya dunia ilisema: dunia ni shirika, na Marekani ndio yenye hisa nyingi zaidi ndani ya hili shirika, hivyo ni lazima uendeshaji wa mambo ya shirika uwe mikononi mwake, na ikafanya hii kauli ndio upande wake maalumu ambao itaangalia ulimwengu kupitia kwake, basi matendo yake yanapangwa kulingana na huu upande, na ikawa yaangalia vitendo vya kisiasa vinavyoendelea ulimwenguni kupitia upande huu. Kuangalia mambo kwa jicho hili ndio kuliifanya Marekani kupata bali kuungana na muungano wa kisovieti, na kuipuuzia Uingereza na Ufaransa. Na baada ya muungano wa kisovieti kuanguka mtizamo wa Marekani ukabadilika, ikawa haipuuzi Uingereza na Ufaransa pekee, bali ikawa yazipuuza nchi zote ulimwenguni, na ikafika mbali zaidi ikawa yapuuza hata mikataba ya kimataifa ambayo nchi zimekubaliana juu yake, ikajitoa katika mkataba wa Kyoto, ikadinda kuingia kwenye mkataba wa kuondoa mabomu ya ardhini, na kwenye mkataba wa kuasisiwa kwa mahakama ya jinai ya kimataifa, na mikataba mengine. Ukawa upande maalumu inayoangalilia ulimwengu nao umesimama juu ya msingi kwamba

hakuna nchi inayolingana nayo ili iungane nayo kwa usawa, basi ikaamua kuendesha mambo peke yake, na ikawa yaamiliana na nchi kubwa zengine kwa mbinu ya ubabe na kiburi.

Kuangalia matukio ya kisiasa yanayotokea ulimwenguni kupitia upande maalumu huwa ni hivi, sawa sawa huo upande maalumu uwe ni jumla kama vile kufanya uenezaji wa ulinganizi kuwa ndio msingi wa sera za kigeni, yaani upande maalumu ambao huangalilia nao ulimwengu, au uwe ni makhsusi kama vile kufunga uwadui kwa nchi maalumu ambayo ushindi dhidi yake utatuwezesha kutokea ulimwenguni, au uwe ni makhsusi zaidi kama vile kupambana katika mapambano maalumu ya kisiasa ili nchi zengine zione mfano wa mapambano yetu ya kisiasa.

Kwa hiyo, kuangalia matukio na matendo ya kisiasa kuafikiana na upande maalumu ni jambo rahisi, hakuna cha zaidi kinachohitajika isipokuwa kushughulika na siasa yenyewe kivitendo, bali pia kuyaangalia matukio ya kisiasa kiundani yatosha kuyafahamu. Kwa hiyo yamabainika kutokana na hayo kwamba, kufuatilia siasa na kujua fahamu za kisiasa ni lazima yapelekee kuundika kwa uwelewa wa kisiasa (al-wa'yus- siyasi), na kwamba huu uwelewa wa kisiasa ni jambo lisilo na budi katika kazi ya kisiasa, bali hapana budi kuwa nao ili kuweza kuathiri katika matukio ya kisiasa.

Ikiwa uwelewa wa kisiasa umeshakuwa jambo la kawaida kabisa kwa nchi kubwa kubwa, na kujua siasa za kiulimwengu imekua ndio mkate wa kila siku kwa wanasiasa, basi yapaswa kwa wana wa Ummah wa kiislamu – ambao ndio wana wa serikali ya kiislamu – iwe uwelewa wa kisiasa ndio jambo la mwanzo kabisa ambalo ni wajibu kwao kujipamba nalo katika fahamu za kisiasa, na uwe ndio msingi wa kutenda kwao vitendo vya kisiasa, na wafanye kazi ili huo uwelewa uenee baina ya watu na uwe ni jambo la kawaida kabisa ndani ya jamii, uwe ndio mkate wa kila siku kwa wanasiasa. Kwa sababu jukumu lao kubwa na wadhifa wao wa kiasili ni kubeba ulinganizi wa kiislamu kwa ulimwengu na kueneza uongofu baina ya watu, na hayo hayawezekani isipokuwa kama

watakuwa wanasiasa, ila kama watauangalia ulimwengu kupitia upande maalumu, na ila kama watakuwa na uwelewa kamili wa kisiasa.

Na ili suala la uwelewa wa kisiasa lisiwe kubwa sana kwao, na ili wasidhanie kwamba hilo ni jambo la ajabu sana ambalo huwezwa tu na wale watu wajanja kupindukia au wasomi pekee, basi ni lazima wajue kwamba uwelewa wa kisiasa ni rahisi sana, na watu wote – hata wale wa kawaida tu na wasiojua kusoma wala kuandika– wanaweza kuwa nao. Kwa sababu kuelewa siasa haimaanishi kuujua Uislamu wote kwa pande zote, wala sio kujua kitu ambacho ni lazima kufanywa kuwa ndio upande maalumu wa kuangalia nao ulimwengu, hapana, bali kuelewa siasa yamaanisha tu kwamba mtizamo uwe ni kwa ulimwengu wote, bila kujali kiwango cha ujuzi wake ni kingi au kichache, na huu mtizamo uwe ni kupitia upande maalumu. Kwa hiyo kinachozingatiwa ni mtizamo uwe wa kiulimwengu hata kama ni kitendo kimoja tu cha kisiasa, na huo mtizamo wa kiulimwengu uwe ni kwa upande makhsusi na maalumu. Yakipatikana hayo mawili basi yatosha kuwa dalili juu ya uwelewa wa kisiasa.

Ndio, ni sahihi kwamba huo uwelewa wa kisiasa watofautiana nguvu na udhaifu kwa sababu ya kutofautiana katika kujua ulimwengu na matukio ya kisiasa, na pia kwa sababu ya kutofautiana katika kuwa na maarifa kuhusu huo upande maalumu, lakini hata hivyo yote ni uwelewa wa kisiasa, na hata ukitofautiana vipi yote hupelekea natija moja tu: kutokuwa na ufahamu wa kijuujuu katika siasa, na kutokua na mtizamo wa kipuuzi katika kuangalia mambo. Kwa hivyo uwelewa wa kisiasa sio makhsusi kwa wanasiasa na wenye fikra (*mufakkirin)* peke yao, wala haifai kuwa makhsusi kwao tu, bali ni wa wote na ni lazima uwe wa watu wote, na yawezekana uwelewa wa kisiasa kujengwa kwa wasiojua kusoma na kuandika (*Ummiyyin*) na watu wa kawaida (*Awaam*) kama inavyowezekana kujengwa kwa wasomi na wanafunzi, bali ni lazima kujengwa ndani ya Ummah japo kwa ujumla wao, kwa sababu Ummah ndio mchanga ambao **Wanaume** humea humo, basi

hapana budi huo mchanga uwe ni mchana wa uwelewa wa kisiasa, ili **Wanaume wa kikweli** waweze kumea humo, na ili Ummah uweze kuwahisabu (kuwawajibisha) watawala, kuwathamini Wanaume wa kweli, na ili uweze kukabiliana na hatari za nje wakiwa na uwelewa sahihi.

Ama kuhusu njia ya kujenga huu uwelewa wa kisiasa kwa watu binafsi na ndani ya Ummah: hilo huwa kupitia kuwapa thaqafa ya kisiasa kwa maana ya kisiasa, sawa sawa iwe ni kuwapa thaqafa ya fikra za kiislamu na hukmu zake, au iwe ni kwa kufuatilizia matukio ya kisiasa. Wapewe thaqafa ya fikra za kiislamu na hukmu zake sio kama nadharia tu, bali kwa kuzifungamanisha na matukio. Na matukio ya kisiasa yafuatiliwe sio kama anavyofualia mwanahabari ili kujua tu habari, au kama anavyofuatilia Mwalimu ili kuzidisha maalumati, la! bali kwa kuyaangalia kupitia upande maalumu kwa ajili ya kuyatolea hukmu anayoona, au ili ayaunganishe na matukio mengine au fikra zengine, au ili ayaunganishe na hali halisi ya vitendo vya kisiasa vinavyoendelea mbele yake. Ujengaji huu wa kisiasa kupitia mfumo na siasa yenyewe ndio njia ya kujenga uwelewa wa kisiasa ndani ya Ummah na watu binafsi, na ndio utakaofanya Ummah wa kiislamu kubeba jukumu lake la kimsingi na wadhifa wake wa kiasili, nao ni kubeba ulinganizi wa kiislamu kwa ulimwengu na kueneza uongofu kwa watu wote. Kwa hiyo njia ya kujenga uwelewa wa kisiasa ni kufunza thaqafa ya kisiasa. Hivyo basi hakuna budi kueneza thaqafa ya kisiasa ndani ya Ummah wa kiislamu kwa upana zaidi, kwa sababu ndio itakayojengea ufahamu wa kisiasa na kuufanya uzalishe **wanasiasa hodari** wengi zaidi.

Jumaadal Thani / 1425H.
Agosti / 2004M.

****